# Kiswahili 2

## Mwongozo wa Mwalimu



**Tusome Early Literacy programme**

# Yaliyomo

Utangulizi ........ ii
Dibaji ........ ii
Maelezo ........ iii
Sauti na majina ya herufi za Kiswahili ........ iv
Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo ........ v
Kamusi ya Kiswahili ........ vii
Wiki ya 1 ........ 1
Wiki ya 2 ........ 11
Wiki ya 3 ........ 21
Wiki ya 4 ........ 31
Wiki ya 5 ........ 36
Wiki ya 6 ........ 41
Wiki ya 7 ........ 46
Wiki ya 8 ........ 51
Wiki ya 9 ........ 56
Wiki ya 10 ........ 61
Wiki ya 11 ........ 66
Wiki ya 12 ........ 71
Wiki ya 13 ........ 76
Wiki ya 14 ........ 81
Wiki ya 15 ........ 86
Wiki ya 16 ........ 91
Wiki ya 17 ........ 96
Wiki ya 18 ........ 101
Wiki ya 19 ........ 106
Wiki ya 20 ........ 111
Wiki ya 21 ........ 116
Wiki ya 22 ........ 121
Wiki ya 23 ........ 126
Wiki ya 24 ........ 131
Wiki ya 25 ........ 136
Wiki ya 26 ........ 141
Wiki ya 27 ........ 146
Wiki ya 28 ........ 151
Wiki ya 29 ........ 156
Wiki ya 30 ........ 161

## Utangulizi

Tangu kupata uhuru, serikali ya Kenya imetambua elimu kama mojawapo ya haki za kimsingi za binadamu; kwa hivyo imejitolea kuwapa wananchi wake wote elimu bora. Raslimali nyingi zimewekezwa ili kuimarisha upatikanaji, umuhimu, usawa na ubora, vipengee ambavyo vimeboresha miundomsingi na kuongeza idadi ya wanaohudhuria masomo katika nyanja tofauti za elimu na mafundisho.

Serikali inatambua ya kwamba ili kuweza kushindana katika nyanja za kimataifa na kuimarika kiuchumi, taifa linahitaji elimu inayowawezesha wananchi kuwa wabunifu, kupata elimu ya kudumu maishani na wanaoweza kufanya kazi zilizo tata na zenye changamoto. Elimu pia inafaa kuwawezesha wananchi kutatua shida katika jamii, kukata shauri, kufanya kazi bila kufuatiliwa, kuwajibika na pia waweze kusoma, kupiga mambomsasa na kupata ujuzi wa kujidhihirisha. Maendeleo ya kudumu yanahitaji kila binadamu apate maarifa ya karne ya 21, ujuzi, mtazamo na maadili yanayohitajika kudumisha maisha ya siku za usoni. Mkazo unatiliwa kwenye elimu inayowezesha kusoma na kufanya hesabu. Nchi ya Kenya imefanya maendeleo katika kuhakikisha ubora wa elimu. Miradi mbalimbali imewekwa ili kuangazia ubora wa elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi.

Kitabu hiki cha Tusome, bila shaka, kitaimarisha masomo kuanzia darasa la 1 na la 2 ya shule za msingi kwenye somo la kujua kusoma na kuandika. Mpangilio wa masomo unahakikisha ya kwamba wanafunzi wote nchini Kenya wanaweza kusoma na kuelewa ifikapo mwisho wa mwaka. Kwa hivyo, nawahimiza washirika wetu waendelee kusaidia sekta ya elimu katika utekelezaji wa mikakati na mbinu ili kuboresha elimu.

**Prof. Jacob T. Kaimenyi**, PhD, FICD, EBS

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

## Dibaji

Lengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote bila kuzingatia hali yao ya kuichumi na kijamii. Mabadiliko yamefanywa ili kuimarisha sekta ya elimu. Mabadiliko haya yana mtazamo wa kuifanya nchi ishindane kimataifa. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa na Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki mwa Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) inaonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuboresha mafanikio katika uwezo wa kusoma na kufanya hesabu.

Maendeleo yaliyofanyika hivi karibuni katika nchi ya Kenya yalionyesha kuwa kuna haja zaidi ya kuwa na mfumo wenye kina wa kuhakikisha ubora wa elimu. Mabadiliko haya yamo katika Katiba ya Kenya (2010) na Ruwaza ya Kenya ya 2030. Katiba ya Kenya inahakikishia kila mtoto nchini masomo ya msingi yasiyo na malipo. Vilevile, Ruwaza ya Kenya ya 2030 inatarajia kuhakikisha kuwa kuna mabadiliko ya kimaendeleo nchini na pia ushindani katika nyanja za kimataifa ifikapo mwaka wa 2030. Kati ya matarajio ni kutoa elimu bora na mafundisho ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi wa hali ya juu. Mfumo uwe wa kupatia wanafunzi ujuzi wa kazi utakaounganisha nchi na soko la kimataifa. Nakala ya Kikao Cha Bunge Nambari 14 ya 2012 inaonyesha njia mwafaka na wanafunzi asilimia mia moja waweze kukamilisha masomo katika elimu ya msingi bila kuathiri ubora wa elimu.

Wizara ya elimu inatazamia kuboresha elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi hasa ikizingatia uwezo wa kusoma na kuandika na kufanya hesabu. Mradi wa Kitaifa wa Tusome unaodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika (USAID) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), unakusudia kuboresha matokeo ya kuweza kusoma na kuandika katika madarasa ya 1 na ya 2. Mradi huu unalenga kuboresha uwezo wa walimu wa kuelekeza darasani, kuhakikisha wanafunzi wamepata vitabu sahihi vya kusoma na vya ziada, na kuwaelekeza walimu kupitia kwa wakufunzi wa mashauri ya walimu (TAC Tutors) na walimu wakuu. Halikadhalika, utaanzisha njia mwafaka za kufuatilia na kutathmini matokeo ambayo itaunganisha mafunzo na matokeo katika kujifunza kusoma na kuandika. Mradi huu utatumia teknolojia ili kuimarisha mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na kuongeza uwezo wa sekta ya elimu kuboresha matokeo ya masomo.

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu, ninawasihi washikadau wote kushirikiana ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Tusome umefua dafu.

**Dkt. Belio R. Kipsang**

Katibu Mkuu,

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia: Idara ya Elimu

# Maelezo

Mpangilio wa masomo katika kitabu hiki cha mwalimu uliandikwa ukizingatia mwongozo shupavu wa washauri wa kusoma na lugha kutoka hapa nchini Kenya na kimataifa. Katika warsha ya kwanza maafisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST) na Taasisi ya Maandalizi ya Mitaala (KICD), walisimamia uandishi wa mwongozo wa masomo ambao umekuwa kielelezo cha mpangilio wa masomo hayo. Mwongozo huo unaeleza kwa kina vipengele vyote vinavyostahili kuwekwa kwenye mpangilio wa masomo haya. Katika warsha hiyo, uamuzi ulifanywa kuhusu vile herufi za lugha ya Kiswahili na Kiingereza zitafunzwa na mbinu zile zitatumika kufundisha watoto jinsi ya kusoma.

Mpangilio wa lugha ya Kiswahili unazingatia sauti za herufi zinazotumika mara nyingi katika lugha hiyo. Kwa hivyo herufi zinazotumika mara nyingi hufundishwa kwanza ili kuwawezesha wanafunzi kuanza kusoma maneno na sentensi kwa muda wa wiki mbili hivi. Hadithi pia zimeandikwa kwa makini zikizingatia sauti za herufi ambazo wanafunzi wamezisoma tayari. Hadithi hizi pia zinazingatia mada za silabasi ya Taasisi ya Maandalizi ya Mitaala (KICD) pamoja na msamiati wa kiwango cha mwanafunzi ili waweze kusoma na kuelewa maneno na hadithi.

Kila mpangilio wa somo una mbinu mbalimbali zinazotoa mwelekeo wa kipekee wa kufunza kusoma kwa lugha ya Kiswahili. Mbinu hizi pia zinazingatia vipengele vinne vya lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika.) Pia zinafunza waziwazi na kwa mfululizo maalum unaozingatia vipengele vitano muhimu vya kusoma: Utambuzi wa fonimu, utambuzi wa herufi, utambuzi wa maneno, kusoma kwa mtiririko unaozingatia shada na kiimbo na kusoma kwa ufasaha na kuelewa unachokisoma. Vipengele hivi vinazingatia mambo yote muhimu kwa kumsaidia mwanafunzi apate ujuzi wa kujua kusoma mapema.

Mpangilio huu pia unasisitiza wazo kuu kwamba maneno huundwa kwa sauti, na kila herufi ina sauti na sauti hizi zinapounganishwa huunda neno. Wazo lingine ni kuwa maneno yana maana. Maneno yanapounganishwa hutengeneza sentensi, na sentensi huunda taarifa ama hadithi. Kila siku wanafunzi hufanya mazoezi ya herufi, maneno, kusoma hadithi na ufahamu. Siku ya tano ya kila wiki, huwa ya marudio na mazoezi ili walimu waweze kutathmini jinsi wanafunzi wanavyoendelea katika masomo yao.

Kila kipengele kinafunzwa kwa kuzingatia hatua tatu maalum: Ninafanya–Tunafanya–Unafanya. Kwenye hatua ya kwanza (Ninafanya), mwalimu anatoa maelezo na kielelezo cha kipengele kinachofunzwa. Kwenye hatua ya pili (Tunafanya), mwalimu anawahusisha wanafunzi kufanya mazoezi ya hicho kipengele pamoja naye. Kwenye hatua ya tatu (Unafanya), mwanafunzi anapewa nafasi kufanya mazoezi ya kile ambacho amejifunza. Mwanafunzi ataweza kuhusisha yale ambayo amesoma katika maisha yake ya kila siku. Upimaji wa uelewa wa mwanafunzi umepewa kipaumbele kwenye mpangilio huu, kwani unafanyika katika kila kipengele, kila siku, kila juma na kila muhula.

Tunawashauri walimu wajitayarishe kabla ya somo. Ni vyema kutambua msamiati unaoweza kuwatatiza wanafunzi na kutumia kamusi ili kupata maelezo na maana halisi ya maneno.

# Sauti na majina ya herufi za Kiswahili

| Herufi ndogo | Herufi kubwa | Alama za fonetiki | Matamshi | Jina |
|---|---|---|---|---|
| m | M | /m/ | /m/ | Ma |
| a | A | /a/ | /a/ | A |
| u | U | /u/ | /u/ | U |
| k | K | /k/ | /k/ | Ka |
| t | T | /t/ | /t/ | Ta |
| l | L | /l/ | /l/ | La |
| n | N | /n/ | /n/ | Na |
| o | O | /ɔ: / | /o/ | Oo |
| w | W | /w/ | /w/ | Wa |
| e | E | /e/ | /e/ | Ee |
| i | I | /i/ | /i/ | Ii |
| h | H | /h/ | /h/ | Ha |
| s | S | /s/ | /s/ | sa |
| b | B | /b/ | /b/ | ba |
| y | Y | /y/ | /y/ | ya |
| z | Z | /z/ | /z/ | Za |
| g | G | /g/ | /g/ | Ga |
| d | D | /d/ | /d/ | Da |
| j | J | /ɟ/ | /j/ | Ja |
| r | R | /r/ | /r/ | ra |
| f | F | /f/ | /f/ | Fa |
| v | V | /v/ | /v/ | Va |
| sh | SH | /ʃ/ | /sh/ | Sha |
| ny | NY | /ɲ/ | /ny/ | Nya |
| dh | DH | /ð/ | /dh/ | Dha |
| th | TH | /θ/ | /th/ | Tha |
| ch | CH | /tʃ/ | /ch/ | Cha |
| gh | GH | /ɚ/ | /gh/ | Gha |
| ng' | NG' | /ŋ/ | /ng'/ | ng'a |
| ng | NG | /ng/ | /ng/ | Nga |

## Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo
## (Mwaka wa 2, Wiki ya 1-6)

| **Sehemu** | **Siku 1 na 3** | **Siku 2 na 4** | **Siku 5** |
|---|---|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | | | |
| Ufahamu wa herufi | 3 | 3 | 3 |
| Silabi | 4 | 4 | |
| Kusoma maneno kwa silabi | 4 | | |
| Kusoma maneno marefu | | 5 | |
| Sarufi | | 5 | 4 |
| jedwali la silabi | | | 5 |
| **Hadithi ya mwanafunzi** | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya mwanafunzi | 4 | 3 | |
| Wakati wa kusoma hadithi ya mwanafunzi | 6 | 5 | |
| Baada ya kusoma hadithi ya mwanafunzi | 6 | 4 | |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 5 |
| Wakati wa kusoma hadithi ya mwalimu | | | 5 |
| Baada ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 5 |
| Kuandika | 3 | 3 | 3 |
| | 30 | 30 | 30 |

# Mapendekezo ya mgawanyiko wa muda wa kila somo
# (Mwaka wa 2, Wiki ya 7-30)

| **Sehemu** | **Siku 1 na 3** | **Siku 2 na 4** | **Siku 5** |
|---|---|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | | | |
| Ufahamu wa herufi | | | |
| Silabi | | | |
| Kusoma maneno kwa silabi | 5 | | |
| Kusoma maneno marefu | | 5 | |
| Sarufi | | 5 | 5 |
| jedwali la silabi | | | 5 |
| **Hadithi ya mwanafunzi** | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya mwanafunzi | 6 | 3 | |
| Wakati wa kusoma hadithi ya mwanafunzi | 7 | 5 | |
| Baada ya kusoma hadithi ya mwanafunzi | 9 | 9 | |
| **Hadithi ya mwalimu** | | | |
| Kabla ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 4 |
| Wakati wa kusoma hadithi ya mwalimu | | | 6 |
| Baada ya kusoma hadithi ya mwalimu | | | 7 |
| Kuandika | 3 | 3 | 3 |
| | 30 | 30 | 30 |

# Kamusi ya Kiswahili

**Zingatia, Ilani, Tilia Maanani (TM)**: Maneno haya yameelezwa kulingana na jinsi yalivyotumika kwenye kitabu hiki.

| MSAMIATI | | MAANA |
|---|---|---|
| Adhuhuri | – | Muda ulioko baada ya saa sita ya mchana mpaka saa tisa jioni |
| Akateleza | – | Akaenda kwa ulaini hivi kwamba karibu aanguke |
| Ala..../ala za muziki | - | Vyombo vya muziki |
| Alama ya kugawanya | – | Ishara ya ÷ hutumiwa katika somo la hisabati. |
| Alama ya kutoa | - | Ishara ya – hutumiwa katika somo la hisabati. |
| Alama ya kuzidisha | – | Ishara ya + hutumiwa katika somo la hisabati. |
| Agiza | – | Itisha bidhaa ili kuzinunua |
| Alihofia | – | Alijawa na wasiwasi; alijawa na woga. |
| Alijihisi | – | Alijua moyoni au kudhania |
| Alinguruma | – | Alitoa sauti ya mvumo; toa sauti kama mlio wa simba |
| Alipaa | – | Aliienda angani; enda juu. |
| Alipaza | – | Alitoa sauti ya juu. |
| Alisita/ Sita | – | Kutokuwa na uhakika wa kufanya kitu. Aliacha kufanya jambo aghalabu kwa sababu fulani baada ya kutia nia ya kulifanya au kuacha kulifanya jambo baada ya kulianza. |
| Amewaahidi | – | Amesema atawafanyia jambo fulani. |
| Amkua/Kuamkua | – | Kusalimia, kutoa salamu. |
| Angani | – | Sehemu wazi iliyoko juu ya dunia; mbingu. |
| Arafa | – | Ujumbe mfupi unaotumiwa kwa simu. |
| Ardhi | - | Nchi |
| Babu | – | Baba ya mzazi wako. |
| Bandika | - | Tumia aina ya gundi ili kuweka kitu juu ya kingine kama vile karatasi huwekwa juu ya ukuta. |
| Bara | – | Sehemu za nchi ambayo iko mbali na bahari. |
| Baraka | - | Fanaka; Heri; Mambo mema. |
| Barua pepe | – | Barua inayotumwa kwa kupitia mtandao wa intaneti (email.) |
| Barubaru | - | Kijana wa umri wa miaka kama kumi na miwili kwenda juu. |
| Bata bukini | - | Bata mkubwa sana mwenye rangi nyeupe. |
| Bibi | - | Hutumiwa kwa mama mzaa baba / mama (pia huitwa nyanya.) Jina la heshima kwa mwanamke au mke wa mtu. |
| Binamu | – | Mtoto wa amu, mtoto wa mjomba au mtoto wa shangazi. |
| Buibui | – | Mdudu anayetengeneza utando (spider); Vazi jeusi linalovaliwa juu ya nguo za kawaida. Vazi hili huvaliwa na wanawake haswa wa kiislamu wakati wanapotoka nje ya nyumba. |
| Bundi | – | Namna ya ndege mkubwa atokaye usiku tu na mwenye macho makubwa yanayomwezesha kuona gizani; hudhaniwa kuwa ni ndege mbaya. |
| Bustani | – | Kiunga cha kupandia miti ya maua, matunda au mboga. Pia ni mahali pa kupumzika palipopandwa miti au maua. |

Bwawa – Eneo kubwa la maji yaliyokusanyika. Ni ndogo kuliko ziwa.

Changamoto – Shida fulani zinazomkabili au kumpata mtu.

Cheo – Daraja la mtu katika kazi, ukuu, ukubwa.

Chiriku – Ndege mdogo mwenye kelele sana. Hutumiwa kwa mtu apendaye kusemasema sana au mtu mwenye maneno mengi.

Chombo – Kifaa cha kufanyia kazi fulani.

Chomoza – Tokea. Kwa hivyo jua likichomoza ni wakati jua linapotokea asubuhi na mapema kutoka upande wa mashariki.

Dalili – Alama ya kuonyesha hali au kitendo fulani kitakachofanyika; ishara. Pia ni alama iliyowachwa na kitu.

Dawa usiwache ovyo - Dawa usiwache vibaya au kiholela.

Dawati – Chombo ambacho hutumiwa na wanafunzi kukalia na kuandikia. Pia huitwa deski.

Dhihaka – Maneno au vitendo vya kufanyia mzaha; mchezo au utani.

Dhuluma – Tendo lisilo la haki; Tendo baya. Jina lingine ni ukatili.

Duaradufu – Umbo lililozunguka kama vile yai.

Foleni – Piga mstari. Mlolongo wa watu.

Foronya – Mfuko wa kitambaa wa kutilia mto wa kulalia.

Friji – Chombo mfano wa kabati lakini kilichotengenezwa kwa madini na chenye mtambo wa kuleta baridi na kufanyia barafu; pia huitwa jokofu.

Fulana - Vazi linalovaliwa ndani ya shati au kanzu. Pia ni aina ya vazi lililofumwa kwa sufi au manyoya.

Gramu – Uzito wa kitu. Uzamu unaochukua miligramu 1000 au sentigramu 100.

Halaiki – Watu wengi sana. Umati mkubwa wa watu

Halisi – Ya kweli.

Hatari – Kitu kisicho salama.

Hekima – Kuwa mwerevu. Mwenye kutumia akili; busara; maarifa vyema.

Hisabati – Somo la hesabu.

Hitimu – Pata ujuzi unaofaa. Kukamilika katika ujuzi fulani.

Hodari - Mtu ambaye ana ujuzi wa kufanya jambo vizuri kuliko wengine.

Homa ya matumbo – Ugonjwa wa kuhara na kutapika unaoambatana na kuhara damu.

Huathiri – Husababisha matokeo mabaya baada ya jambo fulani kufanyika.

Huburudisha – Hufurahisha ama huleta raha.

Huchechemea – Huenda kwa miguu miwili lakini kwa namna isiyo kawaida; hasa hatua za mguu mmoja kutofautiana na za mguu mwingine.

Hudumia – Toa utumishi au msaada.

Hupungia mkono wa buriani – Huaga na kusema kwaheri.

Hurembesha – Fanya kitu kiwe cha kupendeza kwa kukipamba. Hutia mapambo katika kitu ili kipendeze machoni; pamba.

Ilipopusa – Ilipoisha kama vile mvua inapoacha kunyesha tunasema ‘mvua imepusa’.

Inapowadia – Inapofika.

| | | |
|---|---|---|
| Indigo | – | Rangi moja ya upinde wa mvua iliyo kama urujuani (Lugha ya kiingereza ni "purple") |
| Jamaa | – | Watu wa ukoo mmoja; ndugu. Pia watu wenye uhusiano fulani. |
| Jawabu | – | Jibu. |
| Jitahidi | – | Tia bidii; kujaribu sana ili kufaulu. |
| Jumla | – | Yote pamoja. |
| Kabambe | – | Kamilifu. |
| Kahawa | – | Kinywaji kinachotengenezwa kwa unga wa buni(mbegu za kahawa) zilizokaangwa na kutwangwa na kutiwa katika maji ya kuchemka. |
| Kalenda | – | Kitabu au karatasi inayoonyesha tarehe na miezi ya kila Siku ya mwaka. |
| Kanga | – | Aina ya ndege kama kuku mwenye rangi nyeusi na madoadoa meupe (guinea fowl.) |
| Kaptura | – | Suruali fupi ambayo urefu wake huishia magotini. |
| Kasi | – | Mwendo wa haraka sana. |
| Katiba | – | Jumla ya kanuni au sheria iliyowekwa ili kuwezesha serikali kuitawala nchi. |
| Kibinafsi | – | Kwa nafsi ya mtu mwenyewe; kwa manufaa ya mtu mwenyewe. |
| Kichuguu | – | Nyumba ya mchwa. Hujengwa kwa udongo na mchwa. |
| Kifyekeo | – | Kifaa cha kukata nyasi. |
| Kilemba | – | Kitambaa au nguo inayovaliwa kwa kuzungushwa kichwani. |
| Kinapaa | – | Kinaenda juu; enda angani. |
| Kinga | – | Kuzuia kitu fulani kufanyika. |
| Kinu | – | Chombo cha mti kinachotumiwa kutwangia nafaka, au kusindikia mafuta. Pia ni chombo cha chuma kinachoponda au kusaga. |
| Kipaji | – | Uwezo fulani alionao mtu unaomwezesha kufanya jambo kwa uzuri. |
| Kipawa | - | Kipaji. |
| Kisigino | – | Sehemu iliyotokeza iliyoko nyuma ya mguu/nyuma ya wayo. |
| Kitulizo | – | Kitu kinachoondoa uchungu au kufurahisha mtu. |
| Kivuko | – | Kitu cha kuvukia mto kutoka upande mmoja hadi mwingine; daraja. |
| Kivuli | – | Giza linalofanywa kwa kitu kuwa mbele ya mwanga. |
| Kiwavi | – | Aina ya mdudu mwenye miguu mingi. Manyoya yake huwasha sana. |
| kombamwiko | – | Mende. Mdudu anayependa kukaa pahali pachafu (cockroach.) |
| Kudumisha | – | Kuendelea na jambo kwa muda mrefu; fululiza; baki. |
| Kufana | – | Kutendeka jambo au kitu kwa namna nzuri na ya kuridhisha; faulu. |
| Kufilisika | – | Kumaliza pesa za mtu katika biashara au mashindano. |
| Kuhutubia | – | Kusoma hotuba au kutoa mawaidha. |
| Kuimarisha | – | Kufanya imara au iwe na nguvu au iwe madhubuti. Pia kufanya idumu au istawi. |
| Kujiajiri | – | Kufanya kazi yako mwenyewe bila kumfanyia mtu mwingine. |
| Kujivunia | – | Kufurahia kitu. Kuhisi kuwa u zaidi kuliko wengine; kujiona bora; ringa. |

| | | |
|---|---|---|
| Kukwea | – | Kupanda juu ya mti. |
| Kumbikumbi | – | Aina fulani ya mchwa wanaoota mabawa ambao huonekana wakati wa mvua nyingi. |
| Kumuadhibu | – | Kurekebisha makosa kwa kumchapa au kwa njia nyingine ile. |
| Kupakua | – | Kutoa chakula kwenye chombo kilimopikiwa na kukitia katika chombo kingine ili kuwa tayari kuliwa. |
| Kusanyika | – | Kuja pamoja kama vile watu au maji. |
| Kusawazisha | – | Kuweka kitu, tendo, jambo kama inavyopaswa kuwa; rekebisha. |
| Kusinzia | – | Kushikwa au kujawa na usingizi mwepesi; onyesha dalili ya kutaka kulala kwa kufumbafumba macho. |
| Kusubiri | – | Kukaa kwa muda kwa madhumuni ya kupata kitu au kungoja mtu. Pia kuwa na uvumilivu, subira. |
| Kutoathiri | – | Kutoharibu kitu hasa mazingira. |
| Kutuarifu | - | Kutueleza. |
| Kutumbuiza | – | Kuburudisha au starehesha kwa muziki, nyimbo, mashairi n.k. |
| Kuzidisha | – | Kurudia idadi mara zinazotakikana. |
| Kuzingatia | – | Kutia moyoni na kufikiria. |
| Lifti | – | Chombo kinachotumiwa kuwasafirisha watu kwenye nyumba za ghorofa kutoka orofa moja hadi nyingine. |
| Limetoweka | – | Limepotea machoni; limekosa kuonekana. |
| Lishe bora | – | Mchanganyiko wa vyakula vya aina mbalimbali vinavyoleta afya mwilini. |
| Lowesha | – | Fanya kitu kuwa maji maji.Weka kwenye maji. |
| Maadili | – | Mwenendo mwema;mambo ya haki. Pia ni mafundisho yatolewayo kwa njia ya hadithi au shairi na yenye nia ya kufundisha tabia njema. |
| Madaftari | – | Kitabu cha kuandikia. Hutumiwa na wanafunzi kuandika masomo mbalimbali. |
| Madhara | – | Uharibifu au athari mbaya. |
| Madoadoa | – | Alama au matone ambayo yana rangi tofauti na mwili wa kitu. |
| Mafuriko | – | Maji yanayojaa kwenye mto mpaka yakavuka kingo zake. |
| Maganda | – | Sehemu ya nje ya tunda kama ndizi, yai au hindi. |
| Magurudumu | – | Vitu vya duara vinavyotengenezwa kwa mpira na ambavyo hutumiwa kama miguu ya gari. |
| Maktaba | – | Mahali ambapo pana vitabu vingi watu wanapoenda kusomea. Mkusanyiko wa vitabu vingi. |
| Malishoni | – | Mahali wanapopelekwa wanyama au mifugo ili kula nyasi. |
| Manjano | – | Rangi kama ganda la ndimu au limau lililoiva (yellow.) |
| Manowari | – | Chombo cha baharini kilichoundwa kwa chuma na chenye silaha za kivita. |
| Maradhi | – | Ugonjwa au magonjwa. |
| Maridadi | – | Kinachopendeza macho; kitu cha ajabu. |
| Masafa marefu | – | Kiasi cha mwendo mrefu. |
| Mashavu | – | Nyama ya juu iliyoko kwenye sehemu ya kulia na kushoto ya uso. |

| | | |
|---|---|---|
| Mashua | – | Chombo maalumu kinachosafirisha watu na mizigo juu ya maji. |
| Mashuhuri | – | -Enye kujulikana, –enye sifa, maarufu. |
| Matibabu | – | Tibu ili kuponya maradhi. |
| Matini | – | Aina yoyote ya maneno yaliyoandikwa. Kwa mfano ujumbe mfupi utumiwao kwa simu. |
| Maumbile | – | Tabia ya asili ya kiumbe. |
| Mawaidha | – | Maneno ya kushauri mtu. |
| Mayowe | – | Kilio cha mtu aliye hatarini. |
| Mazingira | – | Hali au mambo yaliyomzunguka kiumbe katika sehemu au maisha yake. |
| Mbuga ya wanyama | – | Ardhi yenye nyasi isiyokuwa na miti mikubwa mingi; nyika ambapo wanyama huishi. |
| Mchi | – | Kipande maalum cha mti kinachotumiwa kupondea au kutwanga vitu katika kinu. |
| Mchwa | – | Mdudu mweupe anayejenga kichuguu na hula sana miti au vitu vilivyotengenezwa kwa mti. |
| Mhunzi | – | Mtu anayefanya kazi ya kufua madini ya chuma au bati. |
| Miayo | – | Kitendo cha kupanua mdomo kama alama ya uchovu (onyesha kitendo.) |
| Mihogo | – | Mimea inayozaa mizizi yenye kuhifadhi chakula ambacho huliwa. |
| Mila | – | Mambo yanayofanywa na sehemu kubwa ya jamii fulani yanayolingana na asili na utaratibu wa jamii hiyo. |
| Mitumbwi | – | Vyombo vilivyotengenezwa kutokana na gogo la mti ambavyo vinafanana na mashua au dau. |
| Mlingoti | – | Mti mrefu unaosimamishwa chini huwekewa vitu kama bendera. |
| Mola | – | Mungu; Maulana. |
| Mpishi | – | Mtu mwenye ujuzi wa kupika. |
| Msalani | – | Mahali pa kuenda haja; choo. |
| Msamaha | - | Tendo la kuwia mtu radhi kwa makosa aliyofanya. |
| Mshindo | – | Sauti kubwa na nzito inayosababishwa na mgongano. |
| Msingi | – | Mahali palipochimbwa kwa madhumuni ya kusimamishia jengo; asili. |
| Mstatili | – | Umbo lenye pembe nne. |
| Mtaa wa mabanda | - | Sehemu zilizojengwa nyumba za mabati bila mpangilio (informal settlement.) |
| Mtoto Sisherehekee | - | Mtoto usisherehekee au kufurahia sana. |
| Mviringo | – | Umbo lililo duara au mzunguko (onyesha umbo hilo.) |
| Mwanga | – | Mwangaza kutokana na jua, mwezi au kitu kinachowaka. |
| Nadhifu | – | Safi, -enye kupendeza, aliyevalia vizuri. |
| Ndoto | – | Maono anayoona mtu awapo usingizini. |
| Nitundie | – | Kutoa matunda kutoka mtini. |
| Nundu | – | Sehemu ya mnyama kv. Ng’ombe au ngamia iliyotokea mgongoni. |
| Nyeupe pepepe | – | Nyeupe sana. |

| | | |
|---|---|---|
| Nyuni | – | Kiumbe chenye mabawa kinachofanana na kuku; ndege. |
| Pacha | – | Watoto wawili waliozaliwa kutoka kwa mimba moja. |
| Pambwa | – | Rembeshwa. |
| Paredi | – | Mlolongo au mstari wa watu (wanafunzi, majeshi n.k.) |
| Pasi | – | Kifaa kinachotumia joto ili kunyorosha nguo. |
| Potovu | – | Kitu chenye sifa mbaya. |
| Rejesta | – | Kitabu kinachowekewa orodha ya majina ya watu pia huitwa sajala. |
| Runinga | – | Televisheni. |
| Rununu | – | Simu ya mkononi. |
| Sahihi | – | Sawa lisilo na kosa. |
| Sala | – | Ombi au dua. |
| Samawati | – | Rangi ya bluu; Rangi ya mbingu bila mawingu. |
| Sambusa | – | Aina ya andazi lililotiwa nyama, vitunguu, pilipili na viungo vinginevyo ambalo hupikwa kwa kuwekwa katika mafuta ya moto. |
| Seremala | – | Fundi wa kutengeneza vitu kutoka kwa mbao au miti. |
| Shangazi | – | Ndugu wa kike wa baba. |
| Shughuli | – | Kazi fulani ambazo mtu huzifanya. Jambo ambalo linamfanya mtu atumie nguvu, juhudi na akili yake ili kulitekeleza. |
| Sijiwezi sijitambui | – | Kuwa katika hali mbaya sana. |
| Siri | – | Jambo lililofichwa ili wengine wasilijue. |
| Spesheli | – | Maalumu, kitu chema na muhimu zaidi. |
| Stadi | – | Hodari; anayejua mambo. |
| Tamaduni | – | Mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. |
| Tapakaa | – | Kuwa kila mahali; enea; sambaa. |
| Tarakilishi | – | Kompyuta. |
| Teknolojia | - | Vitu au mbinu za kisasa kama vile kompyuta n.k. |
| Tiba | – | Kitu kinachoponya mtu awapo mgonjwa. |
| Trafiki | – | Kitu kinachohusu usafiri na barabara. |
| Trekta | – | Chombo kinachofanana na gari ambacho hutumika kulima au kubeba vitu. |
| Uchunguzi | – | Kutafuta ukweli wa kitu au jambo lililotendeka. Utafutaji wa jambo lililofichama na lisilojulikana na wengi ili kulidhihirisha. |
| Ugua | – | Kuwa na ugonjwa. |
| Uhuru | – | Hali ya kutotawaliwa na mtu mwingine; hali ya kufanya mambo bila ya kuingiliwa kati. |
| Ujanja | – | Hali ya kuwa na uongo au udanganyifu. |
| Ujumbe | - | Habari. |
| Ukoo | – | Kikundi cha watu wanaotokana na jamii moja. |
| Ukumbi | – | Sehemu katika nyumba. Chumba kikubwa maalum kwa kupokelea wageni au mazungumzo. |
| Umbo | – | Mkao wa kitu kilivyoundwa au kilivyoumbwa. |
| Ungedhani ni pilipili | - | Ungefikiri ni pilipili. |

Upele – Vidonda vidogo katika mwili ambavyo huwasha na hutoka usaha.
Urujuani – Rangi ya zambarau nyeupe.
Ushungi – Sehemu ya manyoya yaliyo kichwani mwa ndege.
Utosini - Sehemu ya juu katikati ya kichwa.
Uvumilivu – Hali ya kustahimili machungu; ustahimilivu.
Uzima huenda kwisha - Mtu atakufa, kufariki.
Viganja – Sehemu ya mbele ya mkono.
Vinywaji – Vyakula vya majimaji k.v. uji, chai n.k
Vitendawili – Maneno yanayoficha maana ya kitu ili kisijulikane kwa urahisi.
Viumbe - Vyenye kuumbwa na vyenye roho k.v. binadamu.
Waangalifu – Watu walio makini wakati wa kufanya jambo.
Wakilisha – Fanya jambo kwa niaba ya mtu mwingine.
Wakristo – Wafuasi wa dini ya Kikristo.
Walemavu – Watu walio na upungufu wa kimaumbile.
Walimtambua – Walimjua au walimgundua.
Waliwasili – Walifika.
Wamenisinya – Hawanifurahishi au wamenichukiza.
Wanariadha – Wanaoshiriki katika mashindano ya mbio mbalimbali.
Waridi – Aina ya ua ambalo huwa na rangi mbalimbali za kupendeza.
Wasili – fika.
Wazalendo – Watu wanaoipenda nchi yao na wako tayari kuipigania hata kuifia.
Woga – Hali ya kuogopa au hofu.
Yakachangia – Yakafanya kitu kitendeke.
Yakatanda – Yakaenea kila pahali.

## Nyenzo za kufundishia:

| Somo | Nyenzo za kufundisha |
|---|---|
| Ufahamu wa fonimu | Jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili |
| Ufahamu majina ya herufi na sauti | Kadi za herufi, jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili, mfuko wa herufi |
| Silabi | Chati za herufi na silabi, jedwali la sauti na majina ya herufi za Kiswahili |
| Kusoma maneno | Chati za herufi na silabi, kadi za maneno, kadi za silabi |
| Msamiati | Chati za picha na michoro, kadi za picha na michoro, Kamusi ya Kiswahili, vifaa halisi au ghushi, chati zenye msamiati |
| Ufahamu | Vitabu vya hadithi, magazeti na jarida |
| Maktaba | Vitabu vya hadithi, magazeti na jarida |

## Namna ya kushughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu

1. Endapo darasani kuna wanafunzi walio na mahitaji maalumu, mwalimu anapaswa kutafuta mbinu ya kushughulikia mahitaji haya kwa makini. Baadhi ya mahitaji hayo ni kama:
   a) matatizo ya kusikia.
   b) matatizo ya kuona vyema.
   c) udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo haraka.
   d) udhaifu wa kuwasiliana, kwa mfano mtoto aweza kuwa na hali ya kugugumiza na kadhalika.
   e) udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili.
   f) walio hodari katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani.
2. Ni muhimu kwa mwalimu kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya, wakati wa na baada ya somo. Kufanya hivi kutamwezesha kushughulikia mahitaji hayo kwa njia inayofaa ili yasiadhiri fanaka ya somo.
3. Mifano ya mahitaji maalumu na namna ya kuyashughulikia:

| Mahitaji maalumu | Baadhi ya mapendekezo na namna ya kushughulikia mahitaji maalumu |
|---|---|
| a) Matatizo ya kusikia | - Tumia lugha ya ishara inapowezekana<br>- Mwanafunzi aketi karibu na mwalimu au pale anapoweza kusikia vizuri<br>- Himiza matumizi ya vifaa vya kuongezea sauti<br>- Matumizi ya vifaa halisi kunahimizwa |
| b) Matatizo ya kuona vyema | - Mwanafunzi aketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake<br>- Himiza matumizi ya braille inapofaa<br>- Jadili na wazazi au walezi matumizi ya miwani au vioo vya kukuza kimo cha maandishi<br>- Epuka vifaa vinavyoathiri uwezo wa kuona<br>- Mwanafunzi aketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake<br>- Matumizi ya vifaa halisi kunahimizwa |
| c) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa haraka | - Wape wanafunzi muda mwingi wa ziada kuliko wanafunzi wengine<br>- Watengewe muda maalumu wa kurejelea waliyosoma baada ya somo<br>- Gawa somo kwa hatua fupi fupi kuanzia nyepesi hadi hatua tatanishi<br>- Wape mazoezi ya ziada<br>- Mwalimu awakinge wanafunzi walio dhaifu dhidi ya kudunishwa kwa njia yoyote ile |
| d) Udhaifu wa kuwasiliana | - Wape wanafunzi muda wa kuwasilisha mawazo yao<br>- Mwalimu aepukane na vitendo vinavyoweza kuathiri hisia au maono ya mwanafunzi<br>- Mwalimu atumie mbinu tofauti za mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi |
| e) Udhaifu au ulemavu wa viungo vya mwili | - Mwanafunzi apewe muda wa ziada ili kukidhia upungufu (ulemavu) wake<br>- Wapewe vifaa vya teknolojia ikiwezekana au vya kubuniwa kulingana na hali ya ulemavu ili kuongeza uwezo wa utenda kazi wao<br>- Mwalimu anaweza kushauriana na wahudumu wa walemavu kwa usaidizi zaidi |
| f) Walio hodari katika kuelewa mambo haraka kuliko wale wa wastani | - Wanafunzi wapewe kazi ya ziada ili watumie muda wao vyema<br>- Wanafunzi wapewe nafasi za kukuza vipawa vyao<br>- Wanafunzi wapewe kazi zenye changamoto zaidi ili kufanyisha kazi akili zao na kuwapa fursa ya kutumia uhodari wao. |

Wiki ya 1: Siku ya 1 na 2 — **Ukoo/Jamaa**

Tamka sauti.

■ **M m** **A a** **U u**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

● **ma** **maa** **mu** **muu**

Soma silabi na maneno.

▬ bi na mu — **binamu**; sha nga zi — **shangazi**

m jo mba — **mjomba**; a ta m pa — **atampa**

Tamka sauti.

▲ **K k** **T t** **L l**

Soma sehemu za neno na neno lote.

⬬ hu m tembelea — **humtembelea**; a ka wa peleka — **akawapeleka**

a ka m kumbuka — **akamkumbuka**; a ka mwambia — **akamwambia**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|---|---|
| **m**jomba | — | **wa**jomba | **m**jukuu | — | **wa**jukuu |
| **m**zazi | — | **wa**zazi | **m**zee | — | **wa**zee |

1

**Wiki ya 1: Siku ya 1**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** za herufi zifuatazo: **m, a, u**. (*Andika herufi ndogo m, a na u ubaoni.)*

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* (*Onyesha herufi m kisha useme*), jina la herufi hii ni *ma*. Sauti ya herufi hii ni **/m/**.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tutaje sote. Jina la herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi: ma*
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* **/m/**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Tajeni peke yenu. Jina la herufi hii ni?
*Wanafunzi: ma*
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Wanafunzi:* **/m/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza herufi a na u.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *1.*

● **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. /**m** /, /**a**/ - **ma.** Silabi hii ni **ma**.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome silabi hii pamoja.
*Mwalimu na Wanafunzi:* /**m**/ /**a**/- **ma**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hii peke yenu.
*Wanafunzi:* /**m** / /**a**/- **ma.**
*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi mu, maa na muu.)*

**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ma** ubaoni. Nitazame. /**m**/ /**a**/ - **ma.** Silabi hii ni **ma**.

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **ma** kwenye madaftari.
*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaiandika silabi ma.)*

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **muu** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi: (Wanaiandika silabi muu.)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *1.*

● **Kusoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi**

Tutatumia silabi kusoma na kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame: **a ta m pa - atampa**. Neno hili ni **atampa.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome pamoja.
*Mwalimu na Wanafunzi:* **a ta m pa - atampa**.

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni wakati wenu sasa someni peke yenu.
*Wanafunzi:* **a ta m pa - atampa**.
*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza neno: binamu, mjomba, shangazi.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 1.**


**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Sasa nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **binamu** ubaoni. Nitazame. **bi na mu - binamu**

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Sasa tutatamka kila silabi la neno **binamu** huku tukiliandika kwenye daftari. Daftari ni jina lingine la kitabu unachotumia kuandikia shuleni.
*Mwalimu na Wanafunzi:* **bi na mu - binamu**.

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **mjomba** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi:* **m jo mba - mjomba**.

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 1: Siku ya 1 na 2 — **Ukoo/Jamaa**



**Okitoi**

Okitoi, babu na nyanya wanaishi katika kijiji cha Makutano. Dada yake Pendo anaishi na baba na mama katika jiji la Kisumu. Shule zikifungwa, Okitoi humtembelea shangazi yao Amina. Shangazi humsalimia, "Hujambo Okitoi karibu nyumbani." Naye humjibu, "Sijambo shangazi asante sana." Akiwa kwa shangazi, yeye hucheza na binamu zake, Karimu na Sila.

Siku moja, Pendo na binamu zake walienda kwa mjomba. Wakamwamkua mjomba, "Shikamoo mjomba." Mjomba alijibu kwa furaha, "Marahaba wanangu." Mjomba akawapeleka kwenye mbuga ya wanyama. Mara Pendo akamkumbuka kaka yake Okitoi akasema, "Okitoi angefurahia sana kuwaona wanyama hawa."

Mjomba akamwambia Pendo atampa picha ya wanyama ili ampelekee Okitoi. Pendo akatabasamu na kusema, "Asante mjomba."

2

**Kabla ya kusoma hadithi:**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **binamu.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **binamu**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **binamu** ni **mtoto wa mjomba au shangazi**.)

(Tumia hatua hii kufunza **shangazi - shangazi ni dada wa baba. Mjomba ni kaka wa mama**.)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na picha):* Tutazame kichwa cha hadithi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 2. Kichwa cha hadithi ni "**Okitoi"**. Je, tunajua nini kuhusu "**Okitoi"**? (*Wanafunzi 3 - 4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* *Tutazame picha.* Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 - 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wa kikundi chao.)*

**Wakati wa kusoma:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 2 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiliza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja kwa sauti huku mkiifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la.) Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* "**Okitoi"**. Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. *Okitoi anaishi na nani?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye hadithi.**Anaishi na babu na nyanya.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome sentensi hiyo pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Wanasoma*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Binamu za Okitoi ni nani?*

*Wanafunzi:* (*Wajibu. Hakikisha wanarejelea hadithi na kuisoma tena ili kulipata jibu.Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watambue sentensi yenye jibu na wasome sentensi hiyo.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Mjomba alisema angempa Pendo nini? (picha))*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **shangazi, mjomba, binamu, babu, nyanya.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 1: Siku ya 1*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

______________________________

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kipindi cha somo la Kiswahili kina urefu wa dakika 30. Hakikisha unafunza kwa utaratibu ndio uweze kumaliza kufunza somo kwa muda uliopewa. Ukurasa wa v una mpangilio wa kila sehemu na vile unavyostahili kufunza na muda wake.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 1: Siku ya 1 na 2 **Ukoo/Jamaa**

Tamka sauti.

■ **M m** **A a** **U u**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

● **ma** **maa** **mu** **muu**

Soma silabi na maneno.

▬ bi na mu **binamu** sha nga zi **shangazi**

m jo mba **mjomba** a ta m pa **atampa**

Tamka sauti.

▲ **K k** **T t** **L l**

Soma sehemu za neno na neno lote.

⬬ hu m tembelea **humtembelea** a ka wa peleka **akawapeleka**

a ka m kumbuka **akamkumbuka** a ka mwambia **akamwambia**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|---|---|
| **m**jomba | — | **wa**jomba | **m**jukuu | — | **wa**jukuu |
| **m**zazi | — | **wa**zazi | **m**zee | — | **wa**zee |

1

**Wiki ya 1: Siku ya 2**

### ■ Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **k, t, l**. (*Andika herufi ndogo k, t, l ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi k kisha useme*), jina la herufi hii ni **ka**. Sauti ya herufi hii ni **/k/**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ka**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/k/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **ka**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/k/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza t na l)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *1.*

### ● Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. /**k** / /**u**/ - **ku.** Silabi hii ni **ku**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome silabi pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* /**k** / /**u**/ - **ku**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hii peke yenu.

*Wanafunzi:* /**k** / /**u**/ - **ku.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi kuu, te, lo.)*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **ku** ubaoni. Nitazame. /**k** / /**u**/ - **ku.** Silabi hii ni **ku**.

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **ku** kwenye madaftari.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaiandika silabi ku.)*

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **kuu** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaiandika silabi kuu.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 1**.

### ▬ Kusoma maneno marefu

Tutajifunza jinsi ya kusoma neno kwa kutumia sehemu ya neno yenye maana. Sehemu hii wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (andika neno **humtembelea** kisha sema)

Nitazame. **hu m tembelea-humtembelea.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja. Neno ni **humtembelea.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **hu m tembelea - humtembelea.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Sasa mtafanya peke yenu. Neno ni **humtembelea.**

*Wanafunzi:* **hu m tembelea - humtembelea**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno haya: a ka wa peleka- akawapeleka; a ka m kumbuka- akamkumbuka, a ka mwambia- akamwambia)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *1.*

### ◆ Sarufi Umoja na wingi wa maneno

Leo tutajifunza umoja na wingi. *(Andika maneno haya ubaoni jinsi yalivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**mjomba, mzazi, mjukuu, mzee**

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno **mjukuu** liko katika hali ya umoja. Yaani ni mjukuu mmoja. Wakiwa wengi, wao huitwa **wajukuu.**

**mjukuu – wajukuu**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja katika hali ya umoja na wingi.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **mjukuu – wajukuu**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu katika hali ya umoja na wingi.


*Wanafunzi:* **mjukuu – wajukuu**.

*(Tumia hatua ya 3 kufunza umoja na wingi wa maneno yaliyosalia: mjomba - wajomba, mzazi - wazazi, mjukuu - wajukuu, mzee - wazee.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *1.*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 1: Siku ya 1 na 2 — Ukoo/Jamaa



**Okitoi**

Okitoi, babu na nyanya wanaishi katika kijiji cha Makutano. Dada yake Pendo anaishi na baba na mama katika jiji la Kisumu. Shule zikifungwa, Okitoi humtembelea shangazi yao Amina. Shangazi humsalimia, "Hujambo Okitoi karibu nyumbani." Naye humjibu, "Sijambo shangazi asante sana." Akiwa kwa shangazi, yeye hucheza na binamu zake, Karimu na Sila.

Siku moja, Pendo na binamu zake walienda kwa mjomba. Wakamwamkua mjomba, "Shikamoo mjomba." Mjomba alijibu kwa furaha, "Marahaba wanangu." Mjomba akawapeleka kwenye mbuga ya wanyama. Mara Pendo akamkumbuka kaka yake Okitoi akasema, "Okitoi angefurahia sana kuwaona wanyama hawa."

Mjomba akamwambia Pendo atampa picha ya wanyama ili ampelekee Okitoi. Pendo akatabasamu na kusema, "Asante mjomba."

2

**Kabla ya kusoma hadithi:**

Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana. Kabla ya kusoma hadithi tutajikumbusha maana ya maneno: **binamu, shangazi** na **mjomba**. *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma:**

*Mwalimu:* Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja huku tukiifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **Okitoi**.) Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. ***Ni jambo gani ambalo Okitoi hulifanya akiwa na shangazi yake?*** Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu halipatikani kwenye hadithi. Ni lazima tufikirie mambo ambayo watu hufanya wakati wametembelea shangazi. **Pengine yeye hucheza na binamu zake n.k.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe mambo mengine ambayo watoto hufanya wanapotembelea jamaa zao.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Kwa nini Pendo alitabasamu?*

*Wanafunzi:* (*Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie ubunifu ili wapate jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Je, **mjomba wa Okitoi ni mtu wa aina gani?** (ni mtu mzuri, ni mtu mkarimu)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike kwenye vitabu vyao:

- **i. Huyu ni mjukuu - Hawa ni wajukuu.**
- **ii. Huyu ni mzazi wangu - Hawa ni wazazi wetu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 1: Siku ya 2*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

______________________________________________

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4 — **Ukoo/Jamaa**

Tamka sauti.

■ Nn Oo Ww

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

● no wo to noo

Soma silabi na maneno.

▬ ma ra fi ki — wa za zi — m sa a da — m ku bwa

**marafiki** **wazazi** **msaada** **mkubwa**

Tamka sauti.

▲ Ee Hh Ii

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ **he** **hi** **hee** **hii**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku ni letea — tu sherehekee

**kuniletea** **tusherehekee**

ni ta wa elezea — na wa heshimu

**nitawaelezea** **nawaheshimu**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Mti huu ni **mkubwa** | - | Mti huu ni **mdogo**. |
| Huu ndio **mwanzo** wa hadithi | - | Huu ndio **mwisho** wa hadithi. |
| Talia ni **rafiki** yangu | - | Talia ni **adui** yangu. |
| Chai hii ni **tamu** | - | Chai hii ni **chungu**. |

3

**Wiki ya 1: Siku ya 3**

### ■ Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **n, o, w**. (*Andika herufi ndogo* **n, o, w** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* (*Onyesha herufi n kisha useme*), jina la herufi hii ni **na**. Sauti ya herufi hii ni **/n/**.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* **na**
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* **/n/**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?
*Wanafunzi:* **na**
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Wanafunzi:* **/n/**
*(Tumia hatua ya 3 kufunza o na w)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

### ● Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. **/n/, /o/ - no.** Silabi hii ni **no.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tutamke kila sauti tuisome silabi **no.**
*Mwalimu na Wanafunzi:* **/n/ /o/ - no**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti muisome silabi hii**.**
*Wanafunzi:* **/n/, /o/ - no**
*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi wo, to, noo.)*

**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **no** ubaoni**.** Nitazame. **/n/ /o/ - no.** Silabi hii ni **no.**

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **no** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **wo** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi: (Wanaandika silabi* **wo***)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3*

### ● Kusoma maneno kwa silabi

Tutatumia silabi ambazo tumejifunza kusoma na kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. **ma ra fi ki - marafiki.** Neno hili ni **marafiki.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome pamoja sasa.
*Mwalimu na Wanafunzi:* **ma ra fi ki - marafiki**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Someni peke yenu sasa.
*Wanafunzi:* **ma ra fi ki - marafiki.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo: wazazi, msaada, mkubwa)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Sasa nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **marafiki** ubaoni. Nitazame. **ma ra fi ki - marafiki.** Neno hili ni **marafiki**.

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Tutamke kila silabi huku tukiliandika neno **marafiki** kwenye madaftari.
*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **marafiki***.)*

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiiandika neno **binamu** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **binamu***.)*

**SHAIRI LA MWANAFUNZI**

Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4 **Ukoo/Jamaa**



Jamaa yangu

Hodi hodi marafiki, shairi nawaletea,
La baba na mama yangu, wazazi walonilea,
Majina ya jamaa yangu, wote nitawaelezea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Kaka, dada umenipa, ndugu zangu wa pekee,
Na marafiki umenipa, tucheze tusherehekee,
Binamu ni watoto, wa mjomba na shangazi,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Shangazi, amu na mjomba, ndugu za baba na mama,
Si lazima kuwaomba, msaada wanatumana,
Baba mdogo, mkubwa, Mungu ametuletea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Wa mwisho na wa muhimu, waliozaa wazazi wangu,
Wananipenda nawaheshimu, babu na bibi yangu,
Hadithi zilizo tamu, michezo hucheza yangu,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

4

**Kabla ya kusoma shairi:**

Ni wakati wa kusoma shairi. Lakini kabla ya kulisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye shairi hilo. Pia tutasoma kichwa cha shairi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kile kinachozungumziwa kwenye shairi hilo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **jamaa.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **jamaa**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **jamaa** ni **sawa na familia au watu mnaoishi pamoja nao**.)

(Tumia hatua hii kufunza **babu - baba ya mama au baba, bibi - mama ya baba au mama.**)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha shairi na picha kisha useme:* Tutazame kichwa cha shairi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 4. Kichwa cha shairi ni **"Jamaa yangu"**. Je, tunajua nini kuhusu **Jamaa**? (*Wanafunzi 3 -4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma shairi:**

*Mwalimu:* Leo tutasoma shairi. Hakikisha umefungua ukurasa wa 4 kwenye kitabu chako. Nitasoma shairi kisha tutalisoma pamoja. Baadaye, mtalisoma peke yenu. Fuatilia kwa makini ili muweze kulisoma peke yenu baadaye.

**Baada ya kusoma shairi:**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na shairi la* **"Jamaa Yangu"**. *Sema.)* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu.)* Tujibu maswali yafuatayo. Tutajifunza jinsi ya kujibu maswali kisha tutayajibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. ***Baba na mama pia huitwaje?*** Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye shairi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye ubeti wa kwanza mstari wa pili. Nitausoma mstari huo tena. (*Soma.)* Jina lingine la baba na mama ni **wazazi**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome mstari huo tena pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* *(Wanasoma.*)

*Mwalimu:* Je, baba na mama pia huitwaje?

*Mwalimu na Wanafunzi:* Wazazi

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mtatumia mbinu ambayo tumejifunza ya kutumia shairi kujibu swali hili. ***Watoto wa mjomba na shangazi pia huitwaje****?*

*Wanafunzi: (Wajibu. Hakikisha wanafunzi wanasoma tena shairi ili kutafuta jibu – ambalo ni binamu, na wausome mstari wenye jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili:* ***Babu ni nani? (Mzazi wa kiume wa mzazi wangu.)***

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi wandike sentensi zingine mbili kuhusu picha hiyo.

- Babu ameshika mtoto.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 1: Siku ya 3*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4 — **Ukoo/Jamaa**

Tamka sauti.

■ **N n** **O o** **W w**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

● **no** **wo** **to** **noo**

Soma silabi na maneno.

▬ ma ra fi ki — wa za zi — m sa a da — m ku bwa

**marafiki** **wazazi** **msaada** **mkubwa**

Tamka sauti.

▲ **E e** **H h** **I i**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ **he** **hi** **hee** **hii**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku ni letea — tu sherehekee

**kuniletea** **tusherehekee**

ni ta wa elezea — na wa heshimu

**nitawaelezea** **nawaheshimu**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Mti huu ni **mkubwa** | - | Mti huu ni **mdogo**. |
| Huu ndio **mwanzo** wa hadithi | - | Huu ndio **mwisho** wa hadithi. |
| Talia ni **rafiki** yangu | - | Talia ni **adui** yangu. |
| Chai hii ni **tamu** | - | Chai hii ni **chungu**. |

3

**Wiki ya 1: Siku ya 4**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **e, h** na **i**. (*Andika herufi ndogo* **e, h, i** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi e kisha useme*), jina la herufi hii ni **ee**. Sauti ya herufi hii ni **/e/**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ee**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/e/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **ee**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/e/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza h na i)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

● **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **/h/ /e/ -he.** Silabi hii ni **he.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Hebu tutamke sauti na tuisome silabi **he.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/h/ /e/ - he**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti na muisome silabi hii**.**

*Wanafunzi:* **/h/ /e/ - he.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi hi, hee, hii.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **he** ubaoni**.** Nitazame. **/h/ /e/ - he.** Silabi hii ni **he.**

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **he** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **hi** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaandika silabi* **hi***.)*

▬ **Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma maneno marefu kwa kutumia sehemu za maneno zenye maana. Sehemu hizo wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **ku ni letea - kuniletea.** Neno hili ni **kuniletea**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno hili pamoja. Tutatamka sehemu za neno hili kisha tuziunganishe na kusema neno hilo.

*Wanafunzi:* **ku ni letea - kuniletea**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni sehemu za neno hili kisha mziunganishe na kulisema neno hilo kwa sauti.

*Wanafunzi:* **ku ni letea - kuniletea.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo: ni ta wa elezea; - nitawaelezea; tu sherehekee - tusherehekee; na wa heshimu - nawaheshimu.)* **Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

**Sarufi Kinyume cha maneno**

Leo tutajifunza maneno na kinyume. *(Andika sentensi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii ni **mti huu ni mkubwa**. Kinyume chake ni **mti huu ni mdogo.** Neno **mkubwa** linabadilika kuwa **mdogo**.

**Mti huu ni mkubwa – Mti huu ni mdogo.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja sentensi hii na kinyume chake.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Mti huu ni mkubwa – Mti huu ni mdogo.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, someni sentensi hii peke yenu na kinyume chake.

*Wanafunzi:* **Mti huu ni mkubwa – Mti huu ni mdogo.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza kinyume cha sentensi zilizosalia: Huu ndio mwanzo wa hadithi-Huu ndio mwisho wa hadithi; Talia ni rafiki yangu-Talia ni adui yangu; Chai hii ni tamu – Chai hii ni chungu.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *3.*

**SHAIRI LA MWANAFUNZI**

**Wiki ya 1: Siku ya 3 na 4** — **Ukoo/Jamaa**



Jamaa yangu

Hodi hodi marafiki, shairi nawaletea,
La baba na mama yangu, wazazi walonilea,
Majina ya jamaa yangu, wote nitawaelezea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Kaka, dada umenipa, ndugu zangu wa pekee,
Na marafiki umenipa, tucheze tusherehekee,
Binamu ni watoto, wa mjomba na shangazi,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Shangazi, amu na mjomba, ndugu za baba na mama,
Si lazima kuwaomba, msaada wanatumana,
Baba mdogo, mkubwa, Mungu ametuletea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Wa mwisho na wa muhimu, waliozaa wazazi wangu,
Wananipenda nawaheshimu, babu na bibi yangu,
Hadithi zilizo tamu, michezo hucheza yangu,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

4

**Kabla ya kusoma shairi:**

*Mwalimu:* Tutasoma tena shairi tulilosoma jana. Kabla ya kusoma shairi: tutajikumbusha maana ya maneno yafuatayo: **jamaa, babu** na **bibi.** *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma shairi:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 4 kwenye kitabu chako. Nitasoma shairi kisha tutalisoma pamoja. Baadaye, mtalisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiliza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tulisome shairi hili pamoja huku tukilifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi:* *(Wanalisoma shairi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni shairi hili pamoja huku mkilifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi:* *(Wanalisoma shairi peke yao.)*

**Baada ya kusoma shairi:**

*Mwalimu:* (*Waongoze kujibu maswali kutokana na shairi la* **"Jamaa yangu"**.*)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. J*e, jamaa wana umuhimu gani?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu halipatikani kwenye hadithi. Ni lazima tufikirie umuhimu wa kuwa na jamaa. **Pengine umuhimu wa jamaa ni kama vile kusaidiana n.k.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe mambo mengine ambayo yanaonyesha umuhimu wa jamaa zao.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. J*e, ni baraka gani ambayo Mungu amekupa?*

*Wanafunzi:* (C*hagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie akili ili wapate jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Je, umewahi kutembelea jamaa gani? Jamaa yako wanaishi wapi? (Wanafunzi watoe majibu.)*

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni: Tumia neno kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi zao: jamaa, Mola, babu, bibi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 1: Siku ya 4*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

___

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kufunza msamiati, unaweza kutumia lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 1: Siku ya 5 **Ukoo/Jamaa**

Tamka sauti.

■ Ss Bb Yy

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ja ma a - jamaa**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ba | nga | ja | mba | a | Zi |
| sha | ma | bu | m | bi | jo |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Yule ni **m**jukuu wangu | — | Wale ni **wa**jukuu wetu. |
| **M**jomba amefika | — | **Wa**jomba wamefika. |
| **M**zazi ameenda kazini | — | **Wa**zazi wameenda kazini. |
| **M**ke wangu anapika | — | **Wa**ke wetu wanapika. |

Nyati na sungura



5

**Wiki ya 1: Siku ya 5**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **s, b** na **y**. (*Andika herufi ndogo* **s, b, y** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* (*Onyesha herufi s kisha useme*), jina la herufi hii ni **sa.** Sauti ya herufi hii ni **/s/.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* **sa**
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* /**s**/

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?
*Wanafunzi:* **sa**
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Wanafunzi:* **/s/**
*(Tumia hatua ya 3 kufunza herufi b na y)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *5.*

● **Silabi: kuandika**

Tutatumia silabi zilizo kwenye jedwali kuandika maneno halisi. Maneno halisi ni maneno yenye maana. Kabla ya kuunda maneno tutasoma silabi zote kwa pamoja bila sauti. Silabi ya kwanza ni **ba.** Tusome silabi nyingine *(wanafunzi na walimu wanasoma silabi kwenye jedwali.*) Vyema! Sasa tutatumia silabi hizi kuunda maneno.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame.
Naweza kutumia silabi **ja, ma** na **a** kuandika neno *jamaa.*

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome neno pamoja.
*Mwalimu na Wanafunzi:* **jamaa**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:*
Ni zamu yenu sasa. Tazameni jedwali hili kisha muunde maneno halisi.
*(Mwalimu aandike maneno ubaoni jinsi wanafunzi wanavyoyaunda. Mkimaliza myasome pamoja.)*

◆ **Sarufi Umoja na wingi wa maneno**

Leo tutajifunza umoja na wingi kutumia maneno yaliyo na –**angu** na -**etu**. *(Andika sentensi hizi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii ni **Yule ni mjukuu wangu** na iko katika hali ya umoja. Katika hali ya wingi itakuwa **wale ni wajukuu wetu.**
**Yule ni mjukuu wangu - Wale ni wajukuu wetu.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome sentensi hizi pamoja katika umoja na wingi.
*Mwalimu na Wanafunzi:* **Yule ni mjukuu wangu - Wale ni wajukuu wetu.**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu katika umoja na wingi.
*Wanafunzi:* **Yule ni mjukuu wangu - Wale ni wajukuu wetu.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza umoja na wingi wa sentensi zilizosalia.*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *5.*

**HADITHI YA MWALIMU**

📖 **Kabla ya kusoma hadithi:**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **nitundie.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **nitundie**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:*

Maana ya hili neno **kutunda** ni **ni kutoa matunda kutoka mtini**. Kwa hivyo **nitundie, maana yake ni nitolee matunda kutoka mtini**.)

(Tumia hatua hii kufunza **Kukwea-ni hali ya kupanda mti kwenda juu na ujanja - kuwa mwerevu**.)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na picha,* tutazame kichwa cha hadithi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 5. Kichwa cha hadithi ni **"Nyati na Sungura"**. Je, tunajua nini kuhusu **Nyati na Sungura**? *(Wanafunzi 3-4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 5 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi nanyi msikilize kwa makini. Baadaye nitawauliza maswali.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini.

**Nyati na Sungura**

Hapo zamani, Nyati na Sungura walikuwa marafiki. Sungura hakuwa na maziwa mengi kama nyati. Siku moja, Sungura akamwomba Nyati maziwa. Nyati akakataa. Sungura akarudi nyumbani kwa huzuni.

Siku iliyofuata, Sungura akakutana na Nyati. Akamwambia Nyati, "Tafadhali nitundie matunda kwenye mti." Nyati akakataa. Sungura akafanya ujanja na kusema, "Ukiwa hutaki kukwea mti, unaweza kuutikisa mti kwa kuugonga kwa pembe zako. Hivyo matunda yataanguka." Nyati akarudi nyuma, na kukimbia mbele kwa kasi na kuugonga mkuyu. Pembe zake zikakwama kwenye mti.

Sungura akakimbia nyumbani. Akawaleta watoto wake pamoja na vibuyu vya maziwa. Sungura akamkama nyati na kutoa maziwa yote. Watoto wa sungura wakanywa maziwa mpaka wakashiba. Baadaye walibeba maziwa kwenye vibuyu.

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la.) Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **"Nyati na Sungura"**. *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. *Sungura alimuomba Nyati nini?.* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye hadithi. **Sungura aliomba maziwa.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Ni kitu gani kingine ambacho Sungura alimwomba Nyati?

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Wanajibu.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. *Sungura alifanya ujanja gani kwa nyati?*

*Wanafunzi:* (*Wajibu. Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Je, unafikiri Nyati na Sungura ni marafiki wa kweli? Eleza jibu lako. Kama ungekuwa Nyati ungefanya nini?)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika: **wazazi, marafiki, mjukuu, binamu, mkubwa, mjomba.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 1: Siku ya 5*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kuunda maneno kutoka kwa jedwali, kumbusha wanafunzi kuwa wanaweza tu kutengeneza haya maneno wakitumia sauti au silabi zilizo kwenye jedwali. Maneno hayo ni sharti yawe maneno halisi yenye maana.

Tarehe: __________ Muda: __________ Idadi: __________

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 **Teknolojia**

Tamka sauti.

■ Z z D d G g

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **da** **zi** **gu** **ga**

Soma silabi na maneno.

▬ si mu ru nu nu vi fa a ta ra ki li shi
**simu** **rununu** **vifaa** **tarakilishi**

Tamka sauti.

▲ **J j** **R r** **F f**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ **je** **ro** **fo** **jo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku wasiliana wa li tumia
**kuwasiliana** **walitumia**
zi me rahisisha zi na weza
**zimerahisisha** **zinaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Simu **hii** ni **yangu** | - | Simu **hizi** ni **zetu.** |
| Kompyuta **hii** ni **yangu** | - | Kompyuta **hizi** ni **zetu.** |
| Printa **hii** ni **yangu** | - | Printa **hizi** ni **zetu.** |
| Tarakilishi **hii** ni **yangu** | - | Tarakilishi **hizi** ni **zetu.** |

6

**Wiki ya 2: Siku ya 1**

### ■ Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi

Tutajifunza tena **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **z, g, d**. (*Andika herufi ndogo z, g na d ubaoni.)*

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* (*Onyesha herufi z kisha useme*), jina la herufi hii ni *za*. Sauti ya herufi hii ni ***/z/***.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tutaje sote. Jina la herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi: za*
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Mwalimu na Wanafunzi:* ***/z/***

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Tajeni peke yenu. Jina la herufi hii ni?
*Wanafunzi: za*
*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?
*Wanafunzi:* ***/z/***

*(Tumia hatua ya 3 kufunza herufi g na d.)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *6.*

### ● Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. /**d** / /**a**/ - **da.** Silabi hii ni **da**.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome pamoja silabi hii.
*Mwalimu na Wanafunzi:* /**d** / /**a**/ - **da**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hii peke yenu.
*Wanafunzi:* /**d** / /**a**/ - **da**
*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi zi; gu; ga)*

**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Nitatamka kila silabi huku nikiiandika silabi **da** ubaoni. Nitazame. /**d** / /**a**/ - **da.** Silabi hii ni **da**.

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **da** kwenye madaftari.
*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaiandika silabi da.)*

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **gu** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi: (Wanaiandika silabi gu.)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 6**.

### ★ Maneno: Kutumia silabi kusoma na kuandika maneno

Ni wakati wa kusoma maneno sasa. Tutatumia silabi ambazo tumejifunza kusoma na kuandika maneno mengine.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nitazame. **ta ra ki li shi – tarakilishi.** Neno hili ni **tarakilishi.**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tusome pamoja sasa.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ta ra ki li shi – tarakilishi**

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sana. Hebu someni peke yenu.
*Wanafunzi:* **ta ra ki li shi – tarakilishi**
*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo: simu, rununu, vifaa.)*
**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *6.*

**Hatua ya 4:**
*Mwalimu:* Nitatamka kila silabi huku nikiandika neno **simu** ubaoni. Nitazame. **si mu – simu.** Neno hili ni **simu**.

**Hatua ya 5:**
*Mwalimu:* Tutamke kila silabi huku tukiliandika neno **simu** kwenye madaftari.
*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **simu***.)*

**Hatua ya 6:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **rununu** kwenye madaftari yenu.
*Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **rununu***.)*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 **Teknolojia**



**Vifaa vya ofisini**

Ofisi huwa na vifaa vya kufanyia kazi mbalimbali. Vifaa hivi hufanya kazi kuwa rahisi. Watu hutumia tarakilishi kutuma barua pepe. Hapo awali watu walitumia simu za waya pekee kuwasiliana. Sasa tuna simu za rununu pia ambazo zinaweza kutumika mahali popote. Njia za kisasa za kutuma ujumbe zimerahisisha mawasiliano.

7

**Kabla ya kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **tarakilishi.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **tarakilishi**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:)* Maana ya hili neno **tarakilishi** ni **kompyuta** (onyesha picha.)

(Tumia hatua hii kufunza maneno **barua pepe - barua inayotumwa kutumia kompyuta, simu za rununu au vipakatalishi** na **ujumbe - habari**.)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na picha)* Tutazame kichwa cha hadithi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 7. Kichwa cha hadithi ni **"Vifaa vya ofisini"**. Je, tunajua nini kuhusu **vifaa**? (*Wanafunzi 3 -4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 7 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja huku tukifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkiifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la.) Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya "***Vifaa vya ofisi"**. Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. *Vifaa vya ofisi vina umuhimu gani?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye hadithi. **Hufanya kazi za ofisi kuwa rahisi.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome sentensi hiyo pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Wanasoma.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Zamani watu walitumia simu za aina gani?*

*Wanafunzi:* (*Wajibu. Hakikisha wanarejelea hadithi na kuisoma tena ili kulipata jibu.Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watambue sentensi ambapo jibu lapatikana.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Sasa watu pia hutumia simu za aina gani? (simu za rununu))*

**Kuandika**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **simu, rununu, tarakilishi, vifaa, printa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 2: Siku ya 1*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

_______________________________________________

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2** **Teknolojia**

Tamka sauti.

Z z    D d    G g

Tamka sauti ya herufi na silabi.

da    zi    gu    ga

Soma silabi na maneno.

si mu    ru nu nu    vi fa a    ta ra ki li shi

**simu**    **rununu**    **vifaa**    **tarakilishi**

Tamka sauti.

J j    R r    F f

Tamka sauti ya herufi na silabi.

je    ro    fo    jo

Soma sehemu za neno na neno lote.

ku wasiliana    wa li tumia

**kuwasiliana**    **walitumia**

zi me rahisisha    zi na weza

**zimerahisisha**    **zinaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Simu **hii** ni **yangu** | - | Simu **hizi** ni **zetu.** |
| Kompyuta **hii** ni **yangu** | - | Kompyuta **hizi** ni **zetu.** |
| Printa **hii** ni **yangu** | - | Printa **hizi** ni **zetu.** |
| Tarakilishi **hii** ni **yangu** | - | Tarakilishi **hizi** ni **zetu.** |

6

**Wiki ya 2: Siku ya 2**

**Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajifunza tena **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **ja, ra** na **fa**. (*Andika herufi ndogo* **j, r, f** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi j kisha useme*): Jina la herufi hii ni **ja**. Sauti ya herufi hii ni **/j/**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ja**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/j/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **ja**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/j/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza r na f.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *6.*

**Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. /**j** / /**e**/ - **je.** Silabi hii ni **je**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja silabi hii.

*Mwalimu na Wanafunzi:* /**j** / /**e**/ - **je.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hii peke yenu.

*Wanafunzi:* /**j** / /**e**/ - **je**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi ro, fo, jo.)*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiandika silabi **je** ubaoni. Nitazame. /**j** / /**e**/ - **je.** Silabi hii ni **je**.

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **je** kwenye madaftari.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaiandika silabi je.)*

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **ro** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaiandika silabi ro.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 6**.

**Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma maneno marefu kwa kutumia sehemu za maneno zenye maana. Sehemu hizo wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **ku wa siliana - kuwasiliana.** Neno hili ni **kuwasiliana**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno hili pamoja. Tutatamka sehemu za neno hili kisha tuziunganishe na kusema neno hilo.

*Wanafunzi:* **ku wa siliana - kuwasiliana**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni sehemu za neno hili kisha mziunganishe na kulisema neno hilo.

*Wanafunzi:* **ku wa siliana - kuwasiliana**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo:* **zi me rahisisha (zimerahisisha), zi na weza (zinaweza), wa li tumia (walitumia)***)*

**Sarufi Umoja na wingi wa sentensi**

Leo tutajifunza hali ya umoja na wingi. *(Andika sentensi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii **simu hii ni yangu** iko katika umoja. Yaani ni simu moja na ni yangu. Zikiwa nyingi zitakuwa **simu hizi ni zetu.**

**Simu hii ni yangu – Simu hizi ni zetu.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja katika umoja na wingi.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Simu hii ni yangu – Simu hizi ni zetu.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu katika umoja na wingi.

*Wanafunzi:* **Simu hii ni yangu – Simu hizi ni zetu.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza umoja na wingi wa sentensi zilizosalia: Kompyuta hii ni yangu; Printa hii ni yangu – Printa hizi ni zetu; Tarakilishi hii ni yangu – Tarakilishi hizi ni zetu.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *6.*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 2: Siku ya 1 na 2 — **Teknolojia**



**Vifaa vya ofisini**

Ofisi huwa na vifaa vya kufanyia kazi mbalimbali. Vifaa hivi hufanya kazi kuwa rahisi. Watu hutumia tarakilishi kutuma barua pepe. Hapo awali watu walitumia simu za waya pekee kuwasiliana. Sasa tuna simu za rununu pia ambazo zinaweza kutumika mahali popote. Njia za kisasa za kutuma ujumbe zimerahisisha mawasiliano.

7

**Kabla ya kusoma hadithi:**

Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana. Kabla ya kusoma hadithi tutajikumbusha maana ya maneno yafuatayo: **tarakilishi, barua pepe** na **ujumbe.** *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 7 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi ya vifaa vya ofisi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja huku tukifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii pamoja huku mkifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu: (Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **Vifaa vya ofisi***.) Sema:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. J*e, unafikiri kabla ya kuja kwa simu za rununu watu waliwasiliana vipi?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu halipatikani kwenye hadithi. Ni lazima tufikirie mambo ambayo watu hufanya wakati wametembelea shangazi. **Waliandikiana barua n.k.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe mambo mengine ambayo watoto hufanya wanapotembelea jamaa zao.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Ni aina gani ya simu unayoijua?*

*Wanafunzi:* (*Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie akili ili wapate jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili:Tuambie kisa ambacho simu ilitumiwa kusaidia mtu? (Wanafunzi wajibu.)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

**i. Simu hii - simu hizi.**
**ii. Kompyuta hii - kompyuta hizi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 2: Siku ya 2*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

Tarehe: ____________ Muda: __________ Idadi: __________

**Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4** **Teknolojia**

Tamka sauti.

■ v sh dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● vo sha dhi dhu

Soma sehemu za neno na neno lote.

■ ku zu ngu m za **kuzungumza** ma wa si li a no **mawasiliano**
ku si ki za **kusikiza** ku ta za ma **kutazama**
ru ni nga **runinga** a ra fa **arafa**

Tamka sauti.

▲ ny ch ng'

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● nye cho cha ng'u

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku amini **kuamini** wa na wasiliana **wanawasiliana**
wa na weza **wanaweza** tu na weza **tunaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ Simu ya rununu iko **juu ya** meza.
Simu huwekwa **mbali na** maji.
Aliongea kwa simu **chini ya** mti.
Nyaya za simu huwekwa **juu ya** mti.

8

**Wiki ya 2: Siku ya 3**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **va, sha** na **dha.** (*Andika herufi ndogo* **v, sh, dh** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi v kisha useme*), jina la herufi hii ni **va**. Sauti ya herufi hii ni **/v/**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **va**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/v/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **va**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/v/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza sh na dh)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *8.*

● **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Wakati huu tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **/v/, /o/ - vo.** Silabi hii ni **vo.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti tuisome silabi **vo.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/v/, /o/ - vo**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti muisome silabi **vo.**

*Wanafunzi:* **/v/, /o/ - vo**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi sha, dhi, dhu.)*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **vo** ubaoni**.** Nitazame. **/v/ /o/ - vo.** Silabi hii ni **vo.**

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **vo** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **dhi** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaandika silabi* **dhi***.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 8**.

★ **Maneno: Kusoma na kuandika kwa kutumia silabi**

Ni wakati wa kusoma maneno. Tutasoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **ku zu ngu m za-kuzungumza.** Neno hili ni **kuzungumza.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutamke kila silabi tulisome neno **kuzungumza** pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ku zu ngu m za-kuzungumza**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi ili mlisome neno hili**.**

*Wanafunzi:* **ku zu ngu m za-kuzungumza**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo:* **mawasiliano, kusikiza, kutazama, runinga, arafa.***)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *8.*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **runinga** ubaoni**.** Nitazame. **ru ni nga-runinga.** Neno hili ni **runinga.**

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila silabi huku tukiliandika neno **runinga** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **kutazama** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaandika neno* **kutazama.***)*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4 **Teknolojia**



**Teknolojia**

Katika dunia ya leo, watu wengi wanawasiliana kwa kutumia simu za rununu. Simu ya rununu ni simu ya mkononi. Simu za rununu hutumika kwa kuzungumza, kutuma na kupokea ujumbe mfupi au arafa. Pia hutumiwa kutuma barua pepe. La ajabu ni kuwa siku hizi tunaweza kutuma pesa, kusikiza redio na hata kutazama runinga kwenye simu zetu. Pia kuna michezo tele katika simu za rununu. Siku hizi hata watoto wadogo wanaweza kutumia simu hizi. Ni vigumu kuamini kuwa kuna wakati simu za rununu hazikuwepo.

9

**Kabla ya kusoma taarifa:**

*Mwalimu:* Ni wakati wa kusoma taarifa. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye taarifa hiyo. Pia tutasoma kichwa cha taarifa na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye taarifa hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **arafa.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **arafa**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **arafa** ni **ujumbe mfupi unaotumwa kwa kutumia simu za rununu**.)

(*Tumia hatua hii kufunza* **runinga-televisheni. (Onyesha picha) Kuwasiliana-kubadilishana habari au kuzungumza.**)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha taarifa na picha kisha useme),* tutazame kichwa cha taarifa na picha iliyoko kwenye ukurasa wa 9. Kichwa cha taarifa ni **"Teknolojia"**. Je, tunajua nini kuhusu teknolojia? (*Wanafunzi 3 - 4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 - 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye taarifa hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma taarifa:**

*Mwalimu:* Nitasoma taarifa sasa. Sikiza kwa makini kwani tutajibu maswali baada ya kuisoma taarifa hiyo. Soma taarifa. Soma taarifa pamoja na wanafunzi. Wanafunzi waisome taarifa peke yao.

**Baada ya kusoma taarifa**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la. Waongoze kujibu maswali kutokana na taarifa ya* ***"Teknolojia".*** *Sema.)* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu.)* Tujibu maswali yafuatayo. Tutajifunza jinsi ya kujibu maswali kisha tutayajibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. ***Watu wengi wanatumia nini kuwasiliana siku hizi?*** Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye taarifa au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye mstari wa kwanza. Nitausoma mstari huo tena. (*Soma.)* **Watu wengi wanatumia simu za rununu kuwasiliana.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome mstari huo tena pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanasoma.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mtatumia mbinu ambayo tumejifunza ya kutumia taarifa kujibu swali hili. ***Mbali na kuzungumza, simu za rununu hutumiwa kufanya nini?***

*Wanafunzi: (Wajibu. Hakikisha wanafunzi wanasoma tena taarifa ili kutafuta jibu – wausome mstari ambao una jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili:* ***Ni nini jambo la ajabu? (simu hutumiwa kutuma pesa, kusikiza redio na kutazama runinga.****)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha hiyo. Wanafunzi waunde simu ya rununu wakitumia udongo.

1. Mtu ameshika simu.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 2: Siku ya 3*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4 **Teknolojia**

Tamka sauti.

■ v sh dh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● vo sha dhi dhu

Soma sehemu za neno na neno lote.

▬ ku zu ngu m za **kuzungumza** ma wa si li a no **mawasiliano**
ku si ki za **kusikiza** ku ta za ma **kutazama**
ru ni nga **runinga** a ra fa **arafa**

Tamka sauti.

▲ ny ch ng’

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● nye cho cha ng’u

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku amini **kuamini** wa na wasiliana **wanawasiliana**
wa na weza **wanaweza** tu na weza **tunaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ Simu ya rununu iko **juu ya** meza.
Simu huwekwa **mbali na** maji.
Aliongea kwa simu **chini ya** mti.
Nyaya za simu huwekwa **juu ya** mti.

8

**Wiki ya 2: Siku ya 4**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutarejelea kujifunza **jina** na **sauti** ya herufi zifuatazo: **ny, ch** na **ng’**. (*Andika herufi ndogo* **ny, ch, ng’** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi ny kisha useme*), jina la herufi hii ni **nya**. Sauti ya herufi hii ni **/ny/**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuseme sote. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **nya**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/ny/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **nya**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* /**ny/**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza ch na ng’.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *8.*

● **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Ni wakati wa kusoma silabi. Tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **/ny/ /e/ - nye.** Silabi hii ni **nye.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutamke sauti huku tukiisoma silabi **nye.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/ny/ /e/ - nye**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti muisome silabi hii**.**

*Wanafunzi:* **/ny/ /e/ - nye**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi cho, cha, ng’u)*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila sauti huku nikiiandika silabi **nye** ubaoni**.** Nitazame. **/ny/, /e/.** Silabi hii ni **nye.**

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila sauti huku tukiiandika silabi **nye** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila sauti huku mkiiandika silabi **ng’u** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaandika silabi* **ng’u***.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 8***.*

▬ **Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma maneno marefu kwa kutumia sehemu za maneno zenye maana. Sehemu hizo wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **ku amini - kuamini.** Neno hili ni **kuamini**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno hili pamoja. Tutatamka sehemu za neno hili kisha tuziunganishe na kusema neno hilo.

*Wanafunzi:* **ku amini - kuamini**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni sehemu za neno hili kisha mziunganishe na kulisema neno hilo kwa sauti.

*Wanafunzi:* **ku amini - kuamini**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo:* **wa na weza (wanaweza), wa na wasiliana (wanawasiliana), tu na weza (tunaweza.)**

**Sarufi Viashiria vya mahali**

Leo tutajifunza jinsi ya kuashiria mahali. *(Andika maneno haya ubaoni jinsi yalivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii ni, **simu ya rununu iko juu ya meza. Juu ya** inaashiria mahali palipowekwa simu.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja sentensi hii.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Simu ya rununu iko juu ya meza.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu sentensi hii.

*Wanafunzi:* **Simu ya rununu iko juu ya meza.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza sentensi zilizosalia: Simu huwekwa mbali na maji; Aliweka simu ndani ya mfuko; Nyaya za simu huwekwa juu ya mlingoti.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *8.*

**TAARIFA YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 2: Siku ya 3 na 4 — **Teknolojia**



**Teknolojia**

Katika dunia ya leo, watu wengi wanawasiliana kwa kutumia simu za rununu. Simu ya rununu ni simu ya mkononi. Simu za rununu hutumika kwa kuzungumza, kutuma na kupokea ujumbe mfupi au arafa. Pia hutumiwa kutuma barua pepe. La ajabu ni kuwa siku hizi tunaweza kutuma pesa, kusikiza redio na hata kutazama runinga kwenye simu zetu. Pia kuna michezo tele katika simu za rununu. Siku hizi hata watoto wadogo wanaweza kutumia simu hizi. Ni vigumu kuamini kuwa kuna wakati simu za rununu hazikuwepo.

9

**Kabla ya kusoma taarifa:**

*Mwalimu:* Tutasoma tena taarifa tuliyoisoma jana. Kabla ya kusoma hadithi tutajikumbusha maana ya maneno: **arafa, runinga** na **kuwasiliana/wanawasiliana.** *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma taarifa:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 9 kwenye kitabu chako. Nitasoma taarifa kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome taarifa hii pamoja huku tukifuatilia kwa kidole.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni taarifa hii pamoja huku mkifuatilia kwa kidole.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma taarifa**

*Mwalimu: (Waongoze kujibu maswali kutokana na taarifa ya "***Teknolojia"***.) Sema:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. ***Mbali na simu watu hutumia nini kuwasiliana?*** Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye taarifa au la. Jibu halipatikani kwenye taarifa. Ni lazima tufikirie njia zingine za kuwasiliana**.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe njia zingine ambazo hutumiwa kuwasiliana.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. **Je umewahi kutumia simu ya rununu? Eleza inavyotumika.**

*Wanafunzi:* (C*hagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie akili ili wapate jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: **Ni kipindi gani cha redio au runinga unachokisikiliza sana? (Wanafunzi watoe majibu))***

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni: Tumia neno moja kuunda sentensi. Eleza Wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi zao: wanawasiliana, runinga, arafa.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 2: Siku ya 4*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 2: Siku ya 5 **Teknolojia**

Tamka sauti.

■ **th** **gh** **ng**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: **si mu** - **simu**.

★

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ya | ta | a | hu | fa | ki | mu | li | fa |
| shi | wa | ru | ba | si | no | ra | nu | vi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Umoja -angu | Wingi -etu |
|---|---|
| Hii ni simu **yangu** | - Hizi ni simu **zetu.** |
| Hii ni tarakilishi **yangu** | - Hizi ni tarakilishi **zetu.** |
| Hii ni ofisi **yangu** | - Hizi ni ofisi **zetu.** |
| Hii ni runinga **yangu** | - Hizi ni runinga **zetu.** |

Teknolojia



10

**Wiki ya 2: Siku ya 5**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajifunza **jina** na **sauti** ya herufi **tha, gha** na **nga**. (*Andika herufi ndogo* **th, gh, ng** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi th kisha useme*), jina la herufi hii ni **tha.** Sauti ya herufi hii ni **/th/.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **tha**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/th/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **tha**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/th/**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *10.*

● **Silabi: Kuandika**

Tutatumia silabi zilizo kwenye jedwali kuandika maneno halisi. Maneno halisi ni maneno yenye maana. Kabla ya kuunda maneno tutasoma silabi zote kwa pamoja bila sauti. Silabi ya kwanza ni **ya.** Tusome silabi nyingine *(wanafunzi na walimu wanasoma silabi kwenye jedwali.*) Vyema! Sasa tutatumia silabi hizi kuunda maneno.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame.

Naweza kutumia silabi **si** na **mu** kuandika neno *simu.*

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **simu**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:*

Ni zamu yenu sasa. Tazameni jedwali hili kisha muunde maneno halisi.

*(Mwalimu aandike maneno ubaoni jinsi wanafunzi wanavyoyaunda. Mkimaliza myasome pamoja.)*

◆ **Sarufi Umoja na wingi wa maneno**

Leo tutajifunza umoja na wingi kutumia maneno yaliyo na –**angu** na **-etu**. *(Andika sentensi hizi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii ni; **hii ni simu yangu**, na iko katika hali ya umoja. Katika hali ya wingi itakuwa; **hizi ni simu zetu.**

**Hii ni simu yangu - Hizi ni simu zetu.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome sentensi hizi pamoja katika umoja na wingi.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Hii ni simu yangu – Hizi ni simu zetu.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu katika umoja na wingi.

*Wanafunzi:* **Hii ni simu yangu – Hizi ni simu zetu.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza umoja na wingi wa maneno yaliyosalia: **hii ni tarakilishi yangu – hizi ni tarakilishi zetu, hii ni ofisi yangu – hizi ni ofisi zetu; hii ni runinga yangu – hizi ni runinga zetu.**.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *10.*

**SHAIRI LA MWALIMU**

📖 **Kabla ya kusoma shairi:**

Ni wakati wa kusoma shairi. Shairi ni aina ya maandishi yanayofuata muundo maalum kueleza jambo au wazo fulani. Hebu kwanza tuzungumze kuhusu baadhi ya msamiati na vifungu vya maneno vinavyopatikana kwenye shairi hilo. Pia tutasoma kichwa cha shairi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye shairi hilo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Kifungu cha kwanza ni **teknolojia imeingia.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kukisikia hiki kifungu? *(Wanafunzi wanainua mikono.*) Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya kifungu hiki? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie*

*wajadiliane na wenzao kuhusu kifungu hicho. Ikiwa ni wachache wanaolielewa)* Maana ya hiki kifungu **teknolojia imeingia** ni kuwa **teknolojia ni kitu kipya ambacho kimepata sifa, au teknolojia imefika**.

*(Endelea kufunza maneno haya: **mawaidha – maneno ya mafunzo au maonyo au mashauri; zimetapakaa – kuenea kote, kufika kila pahali.**)*

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi picha ya* ***"Teknolojia"*** *kisha useme),* tazama kichwa cha shairi hili. Shairi linahusu ***"Teknolojia"***. Je, tunajua nini kuhusu teknolojia? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)* (*Eleza tofauti kati ya watu na vitu kwa kutumia mifano mbalimbali*.)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Sasa tutafikiria kitakachozungumziwa kwenye shairi. Kufikiria kitakachozungumziwa na kukisema pia huitwa kutabiri. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye shairi hili. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**TEKNOLOJIA**

Dunia imebadilika, teknolojia imeingia,
Bara, pwani imefika, wote wameitikia,
Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.

Redio nazo tunazo, nyumbani na kwenye simu,
Mawaidha na vitulizo, mafundisho yakuheshimu,
Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.

Tarakilishi twatumia, shuleni hata kazini,
Zina michezo ya kuvutia, zitumie kwa makini,
Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.

Runinga zimeenea, zaitwa televisheni,
Picha video kuonea, muziki pia sikizeni,
Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.

Simu zimetapakaa, kila pahali nchini,
Za rununu na za waya, twatuma hata matini,
Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.

**Baada ya kusoma shairi:**

*Mwalimu:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Kwanza, nitawaonyesha jinsi ya kujibu maswali hayo. Kisha tutashirikiana kuyajibu maswali hayo. Baadaye mtashirikiana kuyajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. *Taja vitu vitano vya teknolojia vilivyotajwa kwenye shairi.* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye shairi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye ubeti wa pili mstari wa kwanza. Nitausoma mstari huo tena. (*Soma.) Aina moja ya vitu vya teknolojia ni runinga.*

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutaje aina zingine za vitu vya teknolojia.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanataja. Mwalimu awasomee wanafunzi shairi tena: **redio, simu za rununu na za waya na tarakilishi.***)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. *Teknolojia imefika wapi na wapi?*

*Wanafunzi: (Wajibu. Hakikisha wanafunzi wanasoma tena shairi ili kutafuta jibu – ambalo ni **bara na pwani au kila mahali.**)*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Swali la tatu. *Eleza umuhimu wa tarakilishi.* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye shairi au la. Jibu la swali hili halijitokezi waziwazi kwenye shairi. Inabidi tusome sehemu mbalimbali za shairi kupata jibu. Lakini pia inabidi tutumie maarifa yetu kulijibu. Katika ubeti wa tano mstari wa mwisho tunasoma **kuwa tarakilishi zina michezo ya kuvutia**.

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutoe hoja zingine tena.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wajibu. Wanaweza kutaja: **kutuma barua pepe; kuandika matini na taarifa mbalimbali, kufanya hisabati; kuchora michoro mbalimbali n.k..**)*

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuchanganya taarifa na maarifa yetu kujibu swali lifuatalo. *Ungechagua kipi kati ya simu ya rununu na tarakilishi? Eleza jibu lako.*

*Wanafunzi: (Wajibu. Chagua wanafunzi wawili au watatu waeleze sababu zao.)*

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika **simu, rununu, runinga, arafa, tarakilishi, vifaa, printa, teknolojia, kusikiza.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 2: Siku ya 5*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Tarehe: ________________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2** — **Nyumbani**

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ■ | **i** | **e** | **u** | **e** |
| | **chi** | **che** | **pu** | **pe** |
| | **mchi** | **mche** | **mpu** | **mpe** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ● | m chi | m pu nga | m re fu |
| | **mchi** | **mpunga** | **mrefu** |
| | m ge ni | s ti ma | s ta re he |
| | **mgeni** | **stima** | **starehe** |

Tamka silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▲ | **e** | **e** | **i** | **a** |
| | **re** | **ge** | **ti** | **ta** |
| | **mre** | **mge** | **sti** | **sta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ⬬ | a ki twanga | a ka mwona | a ki wasili |
| | **akitwanga** | **akamwona** | **akiwasili** |
| | a li washa | a li nawa | ku m karibisha |
| | **aliwasha** | **alinawa** | **kumkaribisha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

★ Mchi umo **ndani ya** kinu.

Alilala **nyuma ya** nyumba.

Mgeni aliketi **juu ya** kiti.

Aliwasha taa na kuiweka **kando ya** birika.

11

**Wiki ya 3: Siku ya 1**

- **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Wakati huu tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. silabi hii ni **i**. Nitaongeza sauti **/ch/**. Sasa silabi hii ni **chi**. Nikiongeza sauti **/m/** mbele ya silabi **chi** sasa inasomeka **mchi**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome silabi hizi pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **i, chi, mchi**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hizi peke yenu.

*Wanafunzi:* **i, chi, mchi.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi* **e, che, mche, u, pu, mpu, e, pe, mpe, e, re, mre**.)

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 11**.

- **Maneno: Kutumia silabi kusoma na kuandika maneno**

Ni wakati wa kusoma maneno. Tutatumia silabi kusoma na kuandika maneno.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **m chi - mchi.** Neno hili ni **mchi.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **m chi – mchi**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Someni peke yenu.

*Wanafunzi:* **m chi – mchi.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza maneno yafuatayo:* **mpunga, mrefu, mgeni, stima, starehe.***)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *11.*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **mchi** ubaoni. Nitazame. **m chi - mchi.** Neno hili ni **mchi**.

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila silabi huku tukiliandika neno **mchi** kwenye madaftari.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **mchi***.)*

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **mgeni** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaliandika neno* **mgeni***.)*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**



Mgeni nyumbani

Rehema alikuwa akitwanga mpunga kwenye kinu kwa mchi mrefu. Akamwona mgeni akiwasili langoni. Rehema akamsalimia na kumkaribisha kwenye chumba cha wageni. Aliwasha taa na kufungua televisheni ili mgeni astarehe. Rehema aliwasha moto haraka haraka na kupika wali na nyama ya kukaanga. Aliandaa chakula na kumkaribisha mgeni mezani. Mgeni alinawa na kupakua chakula baada ya maombi. Rehema na mgeni wakala wali kwa nyama.

12

**Kabla ya kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **kinu.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **kinu**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **kinu ni chombo kinachotumiwa kutwangia mahindi, mpunga na nafaka zingine**.) (Onyesha picha.)

(Tumia hatua hii kufunza **mchi-mti unaotumiwa kutwanga kwenye kinu.** (Onyesha picha) **Wasili maana yake ni kufika.**)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na picha kisha useme:* Tutazame kichwa cha hadithi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 12. Kichwa cha hadithi ni **"Mgeni nyumbani"**. Je, tunajua nini kuhusu **Mgeni**?) (*Wanafunzi 3 -4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 12 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja sasa.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi peke yenu.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la.) Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **"Mgeni Nyumbani"**. *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wajibu.)* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. ***Rehema alikuwa akifanya nini?*** Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye hadithi. **Alikuwa akitwanga mpunga.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome sentensi hiyo pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Wanasoma sentensi.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Rehema alipoona mgeni akiwasili, alifanya nini?*

*Wanafunzi:* (*Wajibu. Hakikisha wanarejelea hadithi na kuisoma tena ili kulipata jibu. Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watambue sentensi ambako jibu linapatikana.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili:* **Rehema na mgeni walikula vyakula gani? (wali kwa nyama.)**

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika madaftari yao: **mpunga**, **kinu**, **mchi**, **kupakua**.


Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 3: Siku ya 1*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

____________________________________________

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: ______________



Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2 **Nyumbani**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **e** | **u** | **e** |
| **chi** | **che** | **pu** | **pe** |
| **mchi** | **mche** | **mpu** | **mpe** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m chi | m pu nga | m re fu |
| **mchi** | **mpunga** | **mrefu** |
| m ge ni | s ti ma | s ta re he |
| **mgeni** | **stima** | **starehe** |

Tamka silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **e** | **e** | **i** | **a** |
| **re** | **ge** | **ti** | **ta** |
| **mre** | **mge** | **sti** | **sta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a ki twanga | a ka mwona | a ki wasili |
| **akitwanga** | **akamwona** | **akiwasili** |
| a li washa | a li nawa | ku m karibisha |
| **aliwasha** | **alinawa** | **kumkaribisha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

Mchi umo **ndani ya** kinu.

Alilala **nyuma ya** nyumba.

Mgeni aliketi **juu ya** kiti.

Aliwasha taa na kuiweka **kando ya** birika.

11

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha kwamba umeangalia kazi ya ziada kabla ya kupeana kazi nyingine.

**Wiki ya 3: Siku ya 2**

**▲ Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Wakati huu tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. silabi hii ni **e**. Nitaongeza sauti **/r/**. Sasa silabi hii ni **re.** Nikiongeza sauti **/m/** mbele ya silabi **re** sasa inasomeka **mre**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome silabi hizi pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **e, re, mre**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hizi peke yenu.

*Wanafunzi:* **e, re, mre.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi e, ge, mge, i, ti, sti,a, ta, sta.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 11**.

**⬬ Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma maneno marefu kwa kutumia sehemu za maneno zenye maana. Sehemu hizo wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **A ki twanga-akitwanga.** Neno hili ni **akitwanga**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno hili pamoja. Tutatamka sehemu za neno hili kisha tuziunganishe na kusema neno hilo.

*Wanafunzi:* **a ki twanga - akitwanga.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni sehemu za neno hili kisha mziunganishe na kulisema neno hilo.

*Wanafunzi:* **a ki twanga - akitwanga.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno yafuatayo:* **a ka mwona (akamwona), a ki wasili (akiwasili), a li washa (aliwasha) a li nawa (alinawa), ku m karibisha (kumkaribisha)**

**Sarufi Viashiria vya mahali**

Leo tutajifunza jinsi ya kuashiria mahali. *(Andika sentensi hizi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii **mchi umo ndani ya kinu. Ndani ya** inaashiria mahali palipowekwa mchi.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja sentensi hii.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Mchi umo ndani ya kinu.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, someni sentensi hii peke yenu.

*Wanafunzi:* **Mchi umo ndani ya kinu.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza sentensi zilizosalia: **alilala nyuma ya nyumba; mgeni aliketi juu ya kiti; aliwasha taa na kuiweka kando ya birika.**)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *11.*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

**Wiki ya 3: Siku ya 1 na 2** **Nyumbani**



**Mgeni nyumbani**

Rehema alikuwa akitwanga mpunga kwenye kinu kwa mchi mrefu. Akamwona mgeni akiwasili langoni. Rehema akamsalimia na kumkaribisha kwenye chumba cha wageni. Aliwasha taa na kufungua televisheni ili mgeni astarehe. Rehema aliwasha moto haraka haraka na kupika wali na nyama ya kukaanga. Aliandaa chakula na kumkaribisha mgeni mezani. Mgeni alinawa na kupakua chakula baada ya maombi. Rehema na mgeni wakala wali kwa nyama.

**Kabla ya kusoma hadithi:**

Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana. Kabla ya kusoma hadithi tutajikumbusha maana ya maneno yafuatayo: **kinu, mchi** na **kupakua.** *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 12 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja sasa.
*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii peke yenu.
*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **"Mgeni nyumbani"**.*) Sema:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**
*Mwalimu:* Swali la kwanza. J*e, unafikiri mgeni aliwasili saa ngapi?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu halipatikani kwenye hadithi. Ni lazima tufikirie wakati ambao mgeni anaweza kufika nyumbani. **Jioni/usiku**

**Hatua ya 2:**
*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.
*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe sababu zinazofanya wafikirie ilikuwa jioni.)*

**Hatua ya 3:**
*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Kwa nini unafikiri ulikuwa usiku?*
*Wanafunzi:* (*Chagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie akili ili wapate jibu)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Unafikiri wazazi wa rehema walikuwa wapi wakati mgeni aliwasili? (Wanafunzi wajibu jibu lolote sahihi.)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao.

i. Mtoto amelala juu ya meza.
ii. Mpira uko ndani ya chungu.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 3: Siku ya 2*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

________________________________________

________________________________________

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ufahamu wa fonimu huzingatia kufunza sauti za herufi. Wakati wa kufunza sauti, mwalimu hapaswi kuziandika herufi hizi ubaoni.Kipindi hiki ni cha mazungumzo pekee.

Tarehe: __________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 — **Nyumbani**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **a** | **a** | **o** |
| **zi** | **za** | **da** | **do** |
| **nzi** | **nza** | **nda** | **ndo** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ku si n zi a | b la n ke ti |
| **kusinzia** | **blanketi** |
| a li a nza | fo ro nya |
| **alianza** | **foronya** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **e** | **i** | **e** | **i** |
| **ke** | **ki** | **se** | **si** |
| **mke** | **mki** | **mse** | **msi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li amua | a li imba | a li sinzia |
| **aliamua** | **aliimba** | **alisinzia** |
| a li nawa | a li washa | a li m sikia |
| **alinawa** | **aliwasha** | **alimsikia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **ali**amua | — | **haku**amua |
| **ali**imba | — | **haku**imba |
| **ali**anza | — | **haku**anza |
| **ali**sinzia | — | **haku**sinzia |

13

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka hatua tatu muhimu kwenye mtindo wa kufunza somo. Mtindo huu ni: Ninafanya, Tunafanya na Unafanya.

**Wiki ya 3: Siku ya 3**

■ **Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Wakati huu tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. silabi hii ni **i.** Nitaongeza sauti **/z/**. Sasa silabi hii ni **zi.** Nikiongeza sauti **/n/** mbele ya silabi **zi** sasa inasomeka **nzi**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome silabi hizi pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **i, zi, nzi**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hizi peke yenu.

*Wanafunzi:* **i, zi, nzi**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza silabi a, za,* **nza, a, da, nda, o, do, ndo***.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 13**.

● **Maneno: Kusoma na kuandika kwa kutumia silabi**

*Mwalimu:* Ni wakati wa kusoma maneno. Tutasoma na kuandika maneno kwa kutumia silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **ku si nzi a - kusinzia.** Neno hili ni **kusinzia.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutamke kila silabi tulisome neno **kusinzia** pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ku si nzi a - kusinzia.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi mlisome neno **kusinzia.**

*Wanafunzi:* **ku si nzi a - kusinzia.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza maneno haya:* **alianza, blanketi, alimsikia)**

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Nitatamka kila silabi huku nikiliandika neno **blanketi** ubaoni**.** Nitazame. **b la n ke ti - blanketi.** Neno hili ni **blanketi.**

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutamke kila silabi huku tukiliandika neno **blanketi** kwenye madaftari.

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni kila silabi huku mkiliandika neno **foronya** kwenye madaftari yenu.

*Wanafunzi: (Wanaandika neno* **foronya***.)*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 — **Nyumbani**



Kapendo

Jana jioni Kapendo aliamua kusikiliza redio. Redio ilikuwa ikicheza nyimbo tamutamu. Mara Kapendo alianza kusinzia. Mama yake akaja na kusema, "Kapendo, amka. Kumbuka kunawa miguu yako kabla ya kulala. Sitaki uchafue blanketi lako." Kapendo alijibu, "Ndio mama." Muda si muda, Kapendo alisinzia tena. Alianza kuota kuwa yuko kwenye kitanda chenye godoro zito na foronya nyororo. Kitanda hicho kilikuwa kinapaa angani. Alisikia sauti ikimwita. Hapo ndipo alimsikia mama yake akisema, "Mwanangu, amka. Nenda ukalale."

14

**Kabla ya kusoma hadithi:**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kabla ya kuisoma, tutazungumza kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno la kwanza ni **kusinzia.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kulisikia hili neno **kusinzia**? *(Wanafunzi wanainua mikono.)* Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu neno hilo. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **kusinzia** ni **ni kuhisi usingizi/onyesha kwa vitendo**.)

(Tumia hatua hii kufunza **kupaa-kwenda juu-kinapaa maana yake ni kwenda juu. Foronya-nguo nyepesi inayotumiwa kufunikia mto/onyesha picha au kitu halisi**.)

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* (*Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi na picha kisha useme),* tutazame kichwa cha hadithi na picha iliyo kwenye ukurasa wa 14. Kichwa cha hadithi ni **"Kapendo"**. Je, tunajua nini kuhusu **Kapendo**? (*Wanafunzi 3 -4 wapewe nafasi kujibu swali.)*

*Mwalimu:* Tutazame picha. Ni kitu gani unachokiona kwenye picha? *(Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi hii. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Wakati wa kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Nitasoma hadithi sasa. Sikiza kwa makini kwani tutajibu maswali baada ya kuisoma hadithi hiyo.

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* (*Waulize wanafunzi ikiwa utabiri wao ulitimia au la.) Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **"Kapendo".** *Sema:* Je, utabiri wenu ulitimia au la? *(Wanafunzi wanajibu.)* Tujibu maswali yafuatayo. Tutajifunza jinsi ya kujibu maswali kisha tutayajibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. *Redio ya akina Kapendo ilikuwa ikicheza nyimbo gani?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye shairi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye ubeti wa kwanza mstari wa pili. Nitausoma mstari huo tena. (*Soma.)* **Ilikuwa ikicheza nyimbo tamutamu.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome mstari huo tena pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanasoma.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Mtatumia mbinu ambayo tumejifunza ya kutumia taarifa kujibu swali hili. *Mamake Kapendo alimkumbusha Kapendo kufanya nini?*

*Wanafunzi: (Wajibu. Hakikisha wanafunzi wanasoma tena hadithi ili kutafuta jibu – ambalo ni kunawa miguu kabla ya kulala.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili: Kapendo alilala akiwa wapi? (kitini).)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waziandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

i. Kapendo amesuka nywele.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 3: Siku ya 3*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

---

**Vidokezo vya Mwalimu**

Mwalimu mzuri ni yule anayechukua muda kujiyatarisha kabla ya somo. Ni vizuri kuliangalia somo kabla ya kulifunza. Kujitayarisha vyema hufanya somo liwe zuri na la kupendeza.

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 — Nyumbani

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i | a | a | o |
| zi | za | da | do |
| nzi | nza | nda | ndo |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ku si n zi a | b la n ke ti |
| **kusinzia** | **blanketi** |
| a li a nza | fo ro nya |
| **alianza** | **foronya** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| e | i | e | i |
| ke | ki | se | si |
| mke | mki | mse | msi |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li amua | a li imba | a li sinzia |
| **aliamua** | **aliimba** | **alisinzia** |
| a li nawa | a li washa | a li m sikia |
| **alinawa** | **aliwasha** | **alimsikia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **ali**amua | — | **haku**amua |
| **ali**imba | — | **haku**imba |
| **ali**anza | — | **haku**anza |
| **ali**sinzia | — | **haku**sinzia |

13

**Wiki ya 3: Siku ya 4**

**Silabi: Kutumia sauti kusoma na kuandika silabi**

Wakati huu tutatumia sauti ambazo tumejifunza kusoma na kuandika silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. silabi hii ni **e.** Nitaongeza sauti **/k/.** Sasa silabi hii ni **ke.** Nikiongeza sauti **/m/** mbele ya silabi **ke** sasa inasomeka **mke.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome silabi hizi pamoja**.**

*Mwalimu na Wanafunzi:* **e, ke, mke**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni silabi hizi peke yenu.

*Wanafunzi:* **e, ke, mke.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza silabi i, ki,* **mki; e, se, mse; i, si, msi***.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 13**.

**★ Kusoma maneno marefu**

Tutajifunza jinsi ya kusoma maneno marefu kwa kutumia sehemu za maneno zenye maana. Sehemu hizo wakati mwingine huwa kubwa kuliko silabi.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. **a li amua - aliamua.** Neno hili ni **aliamua**.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno hili pamoja. Tutatamka sehemu za neno hili kisha tuziunganishe na kusema neno hilo.

*Wanafunzi:* **a li amua - aliamua.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tamkeni sehemu za neno hili kisha mziunganishe na kulisema neno hilo kwa sauti.

*Wanafunzi:* **a li amua - aliamua.**

*(Tumia hatua ya 1-3 kufunza maneno:* **a li imba (aliimba), a li sinzia (alisinzia), a li nawa (alinawa), a li washa (aliwasha), a li m sikia (alimsikia.)**

**¤ Sarufi Kukanusha maneno**

Leo tutajifunza maneno na ukanusho wake. *(Andika maneno haya ubaoni jinsi yalivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**aliamua, aliimba, alisinzia, alinawa, aliwasha, alimsikia.**

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Neno hili **aliamua**, ukanusho wake ni **hakuamua.** Sehemu ya neno **ali** inabadilika kuwa **haku**. Hebu nisome neno hili na kinyume chake.

**aliamua – hakuamua.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome pamoja neno hili na ukanusho wake.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **aliamua – hakuamua**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome neno hili peke yenu na kukanusha wake.

*Wanafunzi:* **aliamua-hakuamua.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza ukanusho wa maneno yaliyosalia: aliimba - hakuimba; alianza - hakuanza; alisinzia - hakusinzia.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *13.*

**HADITHI YA MWANAFUNZI**

Wiki ya 3: Siku ya 3 na 4 **Nyumbani**



Kapendo

Jana jioni Kapendo aliamua kusikiliza redio. Redio ilikuwa ikicheza nyimbo tamutamu. Mara Kapendo alianza kusinzia. Mama yake akaja na kusema, "Kapendo, amka. Kumbuka kunawa miguu yako kabla ya kulala. Sitaki uchafue blanketi lako." Kapendo alijibu, "Ndio mama." Muda si muda, Kapendo alisinzia tena. Alianza kuota kuwa yuko kwenye kitanda chenye godoro zito na foronya nyororo. Kitanda hicho kilikuwa kinapaa angani. Alisikia sauti ikimwita. Hapo ndipo alimsikia mama yake akisema, "Mwanangu, amka. Nenda ukalale."

14

**Kabla ya kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Tutasoma tena hadithi tuliyoisoma jana. Kabla ya kusoma hadithi tutajikumbusha maana ya maneno yafuatayo: **sinzia, kinapaa** na **foronya**. *(Wanafunzi waeleze maana ya maneno haya. Ikiwa hawakumbuki, wakumbushe maana.)*

**Wakati wa kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Hakikisha umefungua ukurasa wa 14 kwenye kitabu chako. Nitasoma hadithi kisha tutaisoma pamoja. Baadaye, mtaisoma peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nasoma sasa. Sikiza kwa makini. Tumia kidole kufuatilia jinsi ninavyosoma.

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome hadithi hii pamoja sasa.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi.)*

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Someni hadithi hii peke yenu.

*Wanafunzi: (Wanaisoma hadithi peke yao.)*

**Baada ya kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* (*Waongoze kujibu maswali kutokana na hadithi ya* **"Kapendo"**.) *Sema:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Nitawafunza jinsi ya kujibu maswali kisha tujibu pamoja. Baadaye mtayajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la kwanza. J*e, unafikiri ni nini kilimfanya Kapendo kulala haraka hivyo?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu halipatikani kwenye hadithi. Ni lazima tufikirie mambo ambayo yangemfanya kulala haraka. **Nyimbo redioni n.k.**

Hatua ya 2:

*Mwalimu:* Tutoe majibu mengine kwa swali hili.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Watoe sababu zingine ambazo hufanya mtu kulala kama vile uchovu n.k.)*

Hatua ya 3:

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuisoma tena hadithi kujibu swali lifuatalo. *Unafikiri nyumba ya akina Kapendo ilikuwa na vyumba vingapi?*

*Wanafunzi:* (C*hagua wanafunzi wawili au watatu wajibu swali. Wahimize watumie akili ili wapate jibu.)*

*(Tumia hatua ya 3 kufunza swali hili:* J*e, umewahi kuota ndoto? Tueleze ndoto yako (wanafunzi waeleze ndoto waliyowahi kuota.)*

**Kuandika**

Andika maneno haya. Tumia neno alisinzia kuunda sentensi. Wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

a) **aliimba** b) **hakuamua** c) **alianza**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 3: Siku ya 4*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

______________________________

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati unapouliza maswali ya ufahamu yenye majibu kwenye hadithi, hakikisha kuwa wanafunzi wanaangalia jawabu kwenye hadithi kabla ya kujibu swali.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 3: Siku ya 5 **Nyumbani**

Tamka sauti.

■ **ng' dh ny ng mb**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m chi - mchi**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ta | m | ki | do | mba | ra |
| mbo | wi | fo | nda | ti | ng'o |
| nya | ro | go | chi | pi | dha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● 

| Umoja -angu | | Wingi -etu |
|---|---|---|
| Huu ni mchi **wangu** | - | Hii ni michi **yetu.** |
| Huu ni mlingoti **wangu** | - | Hii ni milingoti **yetu.** |
| Huu ni mpira **wangu** | - | Hii ni mipira **yetu.** |
| Huu ni mti **wangu** | - | Hii ni miti **yetu.** |

Maina, kizee na ng'ombe



15

**Wiki ya 3: Siku ya 5**

■ **Ufahamu wa herufi: Majina na sauti za herufi**

Tutajikumbusha majina na sauti ya herufi **ny, ng** na **ng'** (*Andika herufi ndogo* **ny, ng, ng'** *ubaoni.*)

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* (*Onyesha herufi ng' kisha useme*), jina la herufi hii ni **ng'a.** Sauti ya herufi hii ni **/ng'/.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tutaje pamoja. Jina la herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **ng'a**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **/ng'/**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Jina la herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **ng'a**

*Mwalimu:* Sauti ya herufi hii ni?

*Wanafunzi:* **/ng'/**

*Mwalimu: (Endelea kuwafunza ny, ng.)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *15.*

★ **Jedwali la silabi Kuandika maneno**

Chora jedwali ubaoni.

*Mwalimu:* Tutatumia silabi zilizoko kwenye jedwali kuandika maneno halisi. Maneno halisi ni maneno yenye maana. Kabla ya kuunda maneno tutasoma silabi zote kwa pamoja bila sauti. Silabi ya kwanza ni **ta.** Tusome silabi nyingine *(wanafunzi na walimu wanasoma silabi kwenye jedwali.)* Vyema! Sasa tutatumia silabi hizi kuunda maneno.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame.

Naweza kutumia silabi **m** na **chi** kuandika neno *mchi.*

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome neno pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **mchi**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tazameni jedwali hili kisha muunde maneno halisi.

*(Mwalimu aandike maneno ubaoni jinsi wanafunzi wanavyoyaunda. Mkimaliza myasome pamoja.)*

● **Sarufi Umoja na wingi wa maneno**

Leo tutajifunza umoja na wingi kutumia maneno yaliyo na –**angu** na **-ao**. *(Andika sentensi ubaoni jinsi zilivyo katika kitabu cha mwanafunzi.)*

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Nitazame. Sentensi hii ni **huu ni mchi wangu** na iko katika umoja. Katika wingi itakuwa **hii ni michi yetu.**

**Huu ni mchi wangu – Hii ni michi yetu.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tusome sentensi hizi pamoja katika umoja na wingi.

*Mwalimu na Wanafunzi:* **Huu ni mchi wangu – Hii ni michi yetu.**

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa, msome peke yenu katika umoja na wingi.

*Wanafunzi:* **Huu ni mchi wangu – Hii ni michi yetu.**

*(Tumia hatua ya 3 kufunza umoja na wingi wa sentensi zilizosalia:* ***huu ni mlingoti wangu - hii ni milingoti yetu; huu ni mpira wangu - hii ni mipira yetu; huu ni mti wangu - hii ni miti yetu.****)*

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *15.*

**HADITHI YA MWALIMU**

📖 **Kabla ya kusoma hadithi:**

*Mwalimu:* Leo tutasoma hadithi ya **"Maina, Kizee na Ng'ombe".**

📖 **Kabla ya kusoma hadithi:**

Ni wakati wa kusoma hadithi. Lakini kwanza tuzungumze kuhusu baadhi ya maneno au msamiati unaopatikana kwenye hadithi hiyo. Pia tutasoma kichwa cha hadithi na kutazama picha. Kisha tutafikiria kuhusu kitakachotendeka kwenye hadithi hiyo.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Neno la kwanza ni **malishoni.** Ni wangapi kati yenu wamewahi kusikia neno hili? *(Wanafunzi wanainua mikono.)*
Ni wangapi kati yenu wanajua maana ya hili neno? *(Wanafunzi wanainua mikono. Ikiwa zaidi ya nusu ya idadi ya wanafunzi watainua mikono yao, waambie wajadiliane na wenzao kuhusu kifungu hicho. Ikiwa ni wachache wanaolielewa sema:* Maana ya hili neno **malishoni** ni kule wanakopelekwa ng'ombe kula nyasi.)

*(Endelea kuwafunza maneno haya: Kizee – mtu mzee sana na ambaye ana maumbile madogo mno; maarifa – ni hekima au akili nyingi; kilimsihi - kilimwomba; angemwadhibu – angemchapa.)*

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu: (Onyesha wanafunzi kichwa cha hadithi* **"Maina, Kizee na Ng'ombe"** *kisha useme):* Tazama kichwa cha hadithi hii. Hadithi hii inahusu **Maina, Kizee na Ng'ombe***.* Je, tunajua nini kuhusu **Maina, Kizee na Ng'ombe***?*

*Wanafunzi 3 – 4 wapewe nafasi wajibu.)* (*Eleza tofauti kati ya watu na vitu kwa kutumia mifano mbalimbali*.)

Je, kichwa kinataja watu, wanyama au vitu?

*Mwalimu na Wanafunzi:* **watu na wanyama**

*Mwalimu:* Sasa tutajibu swali la pili. Je, kichwa cha hadithi kinataja jambo linalotendeka?

*Mwalimu na Wanafunzi:* La

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Sasa tutafikiria kitakachotendeka kwenye hadithi hii kisha tukiseme. Kufikiria kitakachotendeka na kukisema pia huitwa kutabiri. Mgeukie mwenzako kisha umueleze kitu kimoja unachofikiria kitatendeka kwenye hadithi tutakayoisoma. (*Chagua mwanafunzi kutoka katika kila kikundi azungumze kuhusu utabiri wao.)*

**Maina, kizee na ng'ombe**

Siku moja, Maina aliwapeleka ng'ombe wao malishoni. Alipofika kule, aliketi kwenye mwamba na kuanza kuimba. Mara kilitokea kizee kimoja. Kilimuamkua Maina na kusema kiliitwa Maarifa. Kizee hicho kilimsihi Maina akipelekee maji ya kunywa kutoka kisimani. Maina alisita. Kizee kikamhakikishia kingemlindia ng'ombe wake.

Maina alifululiza moja kwa moja hadi kisimani. Alichota maji na kurudi haraka. Aliporudi alishangaa kuona yule kizee aligeuka akawa jitu. Maina aliogopa sana. Kwa haraka alichukua pembe aliyopewa na babu yake. Akapuliza lile pembe na wanakijiji wakasikia na kuja pale Maina alipokuwa. Mara lile jitu likatoweka kama upepo. Wanakijiji wakamsaidia Maina kuwapeleka ng'ombe nyumbani.

**Baada ya kusoma hadithi**

*Mwalimu:* Hebu sasa tujibu maswali yafuatayo. Kwanza, nitawaonyesha jinsi ya kujibu maswali hayo. Kisha tutashirikiana kuyajibu maswali hayo. Baadaye mtashirikiana kuyajibu peke yenu.

**Hatua ya 1:**

*Mwalimu:* Swali la Kwanza. *Maina aliwapeleka ng'ombe wao wapi?* Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu lapatikana moja kwa moja kwenye sentensi ya kwanza. Nitasoma sentensi hiyo tena. *(Soma.)* **Maina aliwapeleka ng'ombe wao malishoni.**

**Hatua ya 2:**

*Mwalimu:* Tuisome sentensi hiyo pamoja.

*Mwalimu na Wanafunzi:* (*Wanasoma.*)

**Hatua ya 3:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. *Kizee kilichomjia Maina kiliitwa nani?*

*Wanafunzi: (Wajibu. Hakikisha wanafunzi wanasoma tena hadithi ili kutafuta jibu – Maarifa), na waisome sentensi ambako jibu hilo lapatikana.*

**Hatua ya 4:**

*Mwalimu:* Swali la tatu. *Eleza kilichotendeka baada ya Kizee kuomba kiletewe maji kutoka kisimani?*

Hebu niangalie ikiwa jibu la swali hili liko kwenye hadithi au la. Jibu la swali hili lapatikana kwenye sentensi kadha za hadithi. Inabidi tuzisome sehemu hizo zote ili tupate jibu. Tukio la kwanza ni kwamba Maina alisita kwenda kuchota maji. Huenda alikuwa na wasiwasi kuhusu ng'ombe wake. Lakini kizee kilisema nini?

**Hatua ya 5:**

*Mwalimu:* Tutoe jibu.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wajibu.)*

*Mwalimu:* Tutoe matukio yaliyofuata.

*Mwalimu na Wanafunzi: (Wajibu.)*

**Hatua ya 6:**

*Mwalimu:* Ni zamu yenu sasa. Tumia mbinu ambayo tumejifunza ya kuchanganya hadithi na maarifa yetu kujibu swali lifuatalo. *Je, unafikiria hadithi hii ni ya kweli au la? Tetea hoja yako.*

*Wanafunzi: (Wawekwe kwenye vikundi viwili (upande mmoja wa la na mwingine wa ndio) ili wajadili.)*

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika **mchi, foronya, mgeni, amka, blanketi, alisinzia, nyimbo, mpunga, starehe, aliimba.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 3: Siku ya 5*

**Tathmini ya somo/MAONI YA MWALIMU**

______________________________________________

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha kuwasaidia watoto ambao hawajui kusoma. Wape mazoezi ya kusoma sauti, silabi na maneno mepesi. Baada ya muda mfupi wataanza kusoma kama wengine.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 4: Siku ya 1

**Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2** — **Darasani**

Tamka sauti.

**dh** **sh**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

**dha** **she** **dhi** **sho**

Soma silabi na maneno.

na dhi fu — **nadhifu**

dha ha bu — **dhahabu**

sa hi hi sha — **sahihisha**

m ko mbo zi — **mkombozi**

Tamka sauti.

**m** **k**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **o** | **i** | **a** | **a** |
| **ko** | **ki** | **wa** | **wa** |
| **mko** | **mki** | **mwa** | **twa** |

Soma silabi na maneno.

a na itwa — **anaitwa**

hu wa tuza — **huwatuza**

a na penda — **anapenda**


wa ki soma — **wakisoma**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja (ni) | | Wingi (tu) |
|---|---|---|
| **ni**natuzwa | - | **tu**natuzwa |
| **ni**naitwa | - | **tu**naitwa |
| **ni**napenda | - | **tu**napenda |
| **ni**nasoma | - | **tu**nasoma |

16

**Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2** — **Darasani**



Mwalimu wetu

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu anaitwa Kazamoyo. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Pia anapenda kuvaa saa ya dhahabu mkononi. Yeye hubeba kalamu mbili za wino. Moja ni ya kusahihishia madaftari yetu na nyingine ya kuandikia kazi zake. Mwalimu Kazamoyo hutufunza kusoma na kuandika kwa njia ya kipekee. Kila mara yeye hutumia chati za hisabati, herufi na picha za kufundishia maneno. Wanafunzi wakisoma vizuri yeye huwatuza kwa wimbo mtamu.

17

## Majina ya herufi na silabi

Eleza wanafunzi jina la herufi **dha (dh.**)

Tamka sauti ya herufi **/dh/**. Endelea na herufi **sh**.

## Kusoma silabi

Andika silabi **dha** ubaoni. N/T/U: Sema kila sauti **/dh/ /a/** kisha uunganishe na kusema silabi **dha**. **[U]** Endelea na silabi: **she, dhi, sho. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 16.

## Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **nadhifu** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **na dhi fu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **nadhifu**. **[U]** Endelea na maneno: **dhahabu, sahihisha, mkombozi. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 16.

## Kabla ya kusoma

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nadhifu, madaftari** na **hisabati**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Eleza wanafunzi wafungue vitabu vyao ukurasa wa 17. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mwalimu Wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

## Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja shule na darasa la Kajuzi. (Mkombozi, darasa la Pili)*
2. *Mwalimu alivalia saa ya aina gani? (dhahabu)*
3. *Mwalimu huwafanyia nini wanafunzi wake wanaposoma vizuri ? (huwatuza kwa wimbo mtamu)*

## Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **huvalia, nadhifu, dhahabu, madaftari, kufundishia.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 4: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati unapojitayarisha kwa somo, ni muhimu kusoma na kutafakari kuhusu vidokezo vya mwalimu kwenye mwongozo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 — Darasani

Tamka sauti.

■ dh sh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● dha she dhi sho

Soma silabi na maneno.

▬ na dhi fu — **nadhifu**; dha ha bu — **dhahabu**

sa hi hi sha — **sahihisha**; m ko mbo zi — **mkombozi**

Tamka sauti.

▲ m k

Soma silabi.

| o | i | a | a |
|---|---|---|---|
| ko | ki | wa | wa |
| mko | mki | mwa | twa |

Soma silabi na maneno.


★ a na itwa — **anaitwa**; hu wa tuza — **huwatuza**; a na penda — **anapenda**; wa ki soma — **wakisoma**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja (ni) | | Wingi (tu) |
|---|---|---|
| **ni**natuzwa | - | **tu**natuzwa |
| **ni**naitwa | - | **tu**naitwa |
| **ni**napenda | - | **tu**napenda |
| **ni**nasoma | - | **tu**nasoma |

16

Wiki ya 4: Siku ya 1 na 2 — Darasani



Mwalimu wetu

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu anaitwa Kazamoyo. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Pia anapenda kuvaa saa ya dhahabu mkononi. Yeye hubeba kalamu mbili za wino. Moja ni ya kusahihishia madaftari yetu na nyingine ya kuandikia kazi zake. Mwalimu Kazamoyo hutufunza kusoma na kuandika kwa njia ya kipekee. Kila mara yeye hutumia chati za hisabati, herufi na picha za kufundishia maneno. Wanafunzi wakisoma vizuri yeye huwatuza kwa wimbo mtamu.

17

### ▲ Majina ya herufi na sauti

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **m**. Tamka sauti ya herufi **/m/**. Endelea na herufi **k**.

### ⬬ Kusoma silabi

Andika silabi **o** ubaoni. N/T/U: Soma sauti hiyo **/o/.** Ongeza sauti **/k/** kisha uunganishe na kusema silabi **ko**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mko**. **[U]** Endelea na silabi: **o, ko, mko; i, ki, mki; a, wa, mwa; a, wa, twa. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 16.

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **anaitwa** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **a na itwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **anaitwa** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **hu wa tuza (huwatuza), a na penda (anapenda), wa ki soma (wakisoma.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 16**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U. Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **ni**natuzwa | - | **tu**natuzwa |
| **ni**naitwa | - | **tu**naitwa |
| **ni**napenda | - | **tu**napenda |
| **ni**nasoma | - | **tu**nasoma |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 16**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **nadhifu, madaftari** na **hisabati**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mwalimu wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiri kwa nini mwalimu alibeba kalamu mbili? (moja ya kusahihisha kazi za wanafunzi na nyingine ya kuandika kazi zake)*
2. *Je, unafikiria watoto walifurahia kazi ya mwalimu wao? (ndio)*
3. *Kwa nini unasema hivyo? (alikuwa nadhifu, alifanya kazi kwa njia ya kipekee, aliwatuza wanafunzi wake)*

### ✍ Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

i. **Mimi ninasoma kitabu - Sisi tunasoma vitabu.**
ii. **Mimi ninapenda kulima - Sisi tunapenda kulima.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 4: Siku ya 2*

# Wiki ya 4: Siku ya 3

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ■ | **a**<br>**ia**<br>**mia** | **a**<br>**ia**<br>**dhia** | **a**<br>**ia**<br>**tia** | **a**<br>**ia**<br>**lia** |

Soma silabi na maneno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ● | ku bwa<br>**kubwa** | re ji s ta<br>**rejista** | mi cho ro<br>**michoro** | ku hi fa dhi a<br>**kuhifadhia** |

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ⬬ | **a**<br>**wa**<br>**bwa** | **a**<br>**wa**<br>**mbwa** | **a**<br>**wa**<br>**kwa** | **a**<br>**wa**<br>**mwa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★
zi me bandikwa — **zimebandikwa**
hu tumia — **hutumia**
zi me pambwa — **zimepambwa**
ku onyesha — **kuonyesha**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (Hili)** | | **Wingi (Haya)** |
|---|---|---|
| **Hili** ni darasa langu | – | **Haya** ni **ma**darasa yetu. |
| **Hili** ni dawati langu | – | **Haya** ni **ma**dawati yetu. |
| **Hili** ni jina langu | – | **Haya** ni **ma**jina yetu. |
| **Hili** ni yai langu | – | **Haya** ni **ma**yai yetu. |

18

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Darasani**




### Darasa la akina Hamisi

Darasa la akina Hamisi linavutia sana. Hamisi analipenda darasa lake. Yeye na rafiki yake Karani hutumia dawati moja. Kuta za darasa lao zimepambwa kwa chati zenye michoro mizuri. Picha za wanyama na mimea zimebandikwa kwenye kuta hizo. Kuna kabati kubwa la kuhifadhia vitabu vya mwalimu na wanafunzi. Juu ya kabati kuna sajala au rejista yenye majina ya wanafunzi wote. Karibu na kabati kuna kalenda ya kuonyesha siku na tarehe.

19

■ **Kusoma silabi**

N/T/U: Andika herufi **a** ubaoni. Soma sauti hiyo **/a/**. Ongeza sauti **/i/** kisha uunganishe na kusema silabi **ia**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mia**. **[U]** Endelea na silabi: **a, ia, mia; a, ia, dhia; a, ia, tia; a, ia, lia.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 18**.

● **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **kuhifadhia** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ku hi fa dhi a** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kuhifadhia**. **[U]** Endelea na maneno: **kubwa, rejista, michoro.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 18**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **dawati, sajala, kalenda**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Darasa la akina Hamisi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Hamisi alitumia dawati na nani? (karani)*
2. *Picha zilizobandikwa ukutani zilikuwa za nini? (wanyama na mimea)*
3. *Kalenda darasani ilionyesha nini? (siku na tarehe)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Wanafunzi wameketi kwenye dawati.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 4: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Hakikisha umejiandaa vyema kabla ya kuenda darasani. Panga kadi za herufi utakazozitumia kwa mfuko wa herufi kabla ya kuanza kufunza. Hii itasaidia kuokoa wakati.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Darasani**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **ia** | **ia** | **ia** | **ia** |
| **mia** | **dhia** | **tia** | **lia** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku bwa | re ji s ta | mi cho ro | ku hi fa dhi a |
| **kubwa** | **rejista** | **michoro** | **kuhifadhia** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** | **wa** |
| **bwa** | **mbwa** | **kwa** | **mwa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ zi me bandikwa **zimebandikwa** — hu tumia **hutumia**


zi me pambwa **zimepambwa** — ku onyesha **kuonyesha**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (Hili)** | | **Wingi (Haya)** |
|---|---|---|
| **Hili** ni darasa langu | – | **Haya** ni **ma**darasa yetu. |
| **Hili** ni dawati langu | – | **Haya** ni **ma**dawati yetu. |
| **Hili** ni jina langu | – | **Haya** ni **ma**jina yetu. |
| **Hili** ni yai langu | – | **Haya** ni **ma**yai yetu. |

18

Wiki ya 4: Siku ya 3 na 4 **Darasani**




Darasa la akina Hamisi

Darasa la akina Hamisi linavutia sana. Hamisi analipenda darasa lake. Yeye na rafiki yake Karani hutumia dawati moja. Kuta za darasa lao zimepambwa kwa chati zenye michoro mizuri. Picha za wanyama na mimea zimebandikwa kwenye kuta hizo. Kuna kabati kubwa la kuhifadhia vitabu vya mwalimu na wanafunzi. Juu ya kabati kuna sajala au rejista yenye majina ya wanafunzi wote. Karibu na kabati kuna kalenda ya kuonyesha siku na tarehe.

19

**Kusoma silabi**

Andika herufi **a** ubaoni. N/T/U: Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/w/** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. Ongeza sauti **/b/** kisha uunganishe na kusema silabi **bwa**. **[U]** Endelea na silabi: **a, wa, mbwa; a, wa, kwa; a, wa, mwa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 18**.

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **zimebandikwa** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **zi me bandikwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **zimebandikwa**. **[U]** Endelea na maneno: **hutumia, zimepambwa** na **kuonyesha.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 18**.

◆ **Sarufi**

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U. Soma sentensi hizi.

| | **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| i. | **Hili** ni darasa langu | - | **Haya** ni **ma**darasa yetu. |
| ii. | **Hili** ni dawati langu | - | **Haya** ni **ma**dawati yetu. |
| iii. | **Hili** ni jina langu | - | **Haya** ni **ma**jina yetu. |
| iv. | **Hili** ni yai langu | - | **Haya** ni **mayai** yetu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 18**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dawati, sajala** na **kalenda**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Darasa la akina Hamisi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

**Maswali**

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiri zile chati darasani zilikuwa za nini? (wanafunzi kusoma mambo mbalimbali)*
2. *Je, nini hakikuwa katika darasa la akina Hamisi ambacho tunacho katika darasa letu? (wanafunzi wataje vitu mbalimbali)*
3. *Mwanafunzi anayesimamia darasa huitwaje? (kiranja)*

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno darasa kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

i) **darasa**
ii) **dawati**
iii) **majina**
iv) **mayai**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 4: Siku ya 4*

Wiki ya 4: Siku ya 5 **Darasani**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ka ya mba - kayamba**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ri | gi | ma | ya | a | ze |
| mbi | ngo | mba | ka | fi | ta |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| **Wakati** | **Kitenzi** |
|---|---|
| jana | **wali**tufunza |
| juzi | **wali**tufunza |
| leo | **wana**tufunza |
| kesho | **wata**tufunza |
| kesho kutwa | **wata**tufunza |

Ala za muziki



20

## Ala za muziki

Maria na Sarun ni pacha. Wana miaka saba. Wao husoma katika shule ya msingi ya Kilimambogo. Pacha hao wanapenda kuimba sana. Pia wanajua kucheza ala tofauti tofauti za muziki.

Juzi walikuja darasani kwetu na kutufunza jinsi ya kupiga baragumu na firimbi. Jana walitufunza kupiga gitaa na kayamba.

Leo wanatufunza kupiga kinubi na marimba. Kesho watatufunza kupiga ngoma na kucheza njuga. Kesho kutwa watatufunza kupiga piano na tari.

Mtondo watatufunza kupiga tarumbeta na ngoma. Mtondogoo watatufunza kupiga zeze na zumari. Wao huwafundisha watoto wengine kupiga ala hizo za muziki. Siku moja, wataunda bendi yao.

**★ Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. NTU: Soma silabi zote kwenye jedwali. Tumia silabi **ka, ya** na **mba** kuandika neno **kayamba**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

**● Sarufi**

Andika maneno ubaoni kisha yasome na kueleza jinsi yanavyobadilika kwa wakati. N/T/U**:**

**juzi walitufunza, leo wanatufunza, kesho watatufunza, kesho kutwa watatufunza.**

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **pacha** na **ala**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Ala za muziki"** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Maria na Sarun walikuwa na miaka mingapi? (saba)*
2. *Taja ala za muziki za Maria na Sarun. (baragumu na firimbi)*
3. *Unapenda nyimbo gani? Kwa nini? (wanafunzi wajibu)*
4. *Kwa nini ala ni muhimu kwa muziki? (hufanya muziki kuwa mtamu)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika.
**Nadhifu, dhahabu, madaftari, kuhifadhi, kubwa, hutumia.**
Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 4: Siku ya 5*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha wanafunzi wameongea na wenzao kuhusu utabiri kabla ya kuuliza wachache waelezee kuhusu utabiri.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — **Shuleni**

Soma silabi.

■

| | | |
|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** |
| **njwa** | **shwa** | **swa** |

Soma silabi na maneno.

●

| | |
|---|---|
| mwa li mu | m go njwa |
| **mwalimu** | **mgonjwa** |
| hu zu ni shwa | ke nge le |
| **huzunishwa** | **kengele** |

Soma silabi.

⬬

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **ea** | **ea** | **ua** | **ua** |
| **mea** | **lea** | **mua** | **lua** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| a ka amua | a li yo isoma |
| **akaamua** | **aliyoisoma** |
| wa ka kusanyika | tu li furahia |
| **wakakusanyika** | **tulifurahia** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **mwa**limu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **mwa**nafunzi | - | Hawa ni **wa**nafunzi. |
| Huyu ni **m**kuu wa shule | - | Hawa ni **wa**kuu wa shule. |
| Huyu ni **m**gonjwa | - | Hawa ni **wa**gonjwa. |

21

Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2 — **Shuleni**



**Darasani**

Kengele ilipolia, sote tulitulia darasani kusubiri mwalimu. Mwalimu mkuu, Bi. Fahamu, alikuja na kutuarifu kuwa mwalimu wetu alikuwa mgonjwa. Tulihuzunishwa na habari hiyo. Kiranja wetu, Galana, akaamua kutusomea hadithi tamu. Hadithi aliyoisoma Galana ilituchekesha sana. Tulifurahia kusoma hadithi tamutamu. Kengele ya pili ilipolia, wanafunzi wote na walimu wakakusanyika mbele ya ofisi ya mwalimu mkuu.

22

### ■ Kusoma silabi

Andika herufi **a** ubaoni. N/T/U: Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/w/** kisha uunganishe na kusema silabi **wa**. Ongeza sauti **/n/** na **/j/** kisha uunganishe na kusema silabi **njwa**. **[U]** Endelea na silabi: **a, wa, shwa; a, wa, swa. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 21.

### ● Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mwalimu** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **mwa li mu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mwalimu**. **[U]** Endelea na maneno: **mgonjwa, huzunishwa, kengele.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 21**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kusubiri, kutuarifu, kusanyika**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Darasani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Kengele ilipolia, wanafunzi walifanya nini?* (walitulia darasani wakisubiri mwalimu)
2. *Taja jina la kiranja wa darasa?* (galana)
3. *Wanafunzi na walimu walikusanyika wapi?* (nje ya ofisi ya mwalimu mkuu)

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mwalimu, huzunishwa, ugonjwa, kusanyika, mgonjwa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 5: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 5: Siku ya 2

**Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2** — **Shuleni**

Soma silabi.

| ■ | | |
|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** |
| **njwa** | **shwa** | **swa** |

Soma silabi na maneno.

| ● | |
|---|---|
| mwa li mu | m go njwa |
| **mwalimu** | **mgonjwa** |
| hu zu ni shwa | ke nge le |
| **huzunishwa** | **kengele** |

Soma silabi.

| ⬬ | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **ea** | **ea** | **ua** | **ua** |
| **mea** | **lea** | **mua** | **lua** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| ★ | |
|---|---|
| a ka amua | a li yo isoma |
| **akaamua** | **aliyoisoma** |
| wa ka kusanyika | tu li furahia |
| **wakakusanyika** | **tulifurahia** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **mwa**limu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **mwa**nafunzi | - | Hawa ni **wa**nafunzi. |
| Huyu ni **m**kuu wa shule | - | Hawa ni **wa**kuu wa shule. |
| Huyu ni **m**gonjwa | - | Hawa ni **wa**gonjwa. |

21

**Wiki ya 5: Siku ya 1 na 2** — **Shuleni**



## Darasani

Kengele ilipolia, sote tulitulia darasani kusubiri mwalimu. Mwalimu mkuu, Bi. Fahamu, alikuja na kutuarifu kuwa mwalimu wetu alikuwa mgonjwa. Tulihuzunishwa na habari hiyo. Kiranja wetu, Galana, akaamua kutusomea hadithi tamu. Hadithi aliyoisoma Galana ilituchekesha sana. Tulifurahia kusoma hadithi tamutamu. Kengele ya pili ilipolia, wanafunzi wote na walimu wakakusanyika mbele ya ofisi ya mwalimu mkuu.

22

### ⬬ Kusoma silabi

Andika herufi **a** ubaoni. Soma sauti hiyo **/a/.** Ongeza sauti **/e/** kabla ya **a** kisha uunganishe na kusema silabi **ea**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mea**. **[U]** Endelea na silabi: **a, ea, lea; a, ua, mua; a, ua, lua.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 21**.

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **akaamua** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **a ka amua** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **akaamua**. **[U]** Endelea na maneno: **a li yo i soma (aliyoisoma), wa ka kusanyika (wakakusanyika), tu li furahia (tulifurahia.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 21**.

### ◆ Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. Soma sentensi: Soma sentensi hizi na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**walimu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **m**wanafunzi | - | Hawa ni **wa**nafunzi. |
| Huyu ni **m**vuvi | - | Hawa ni **wa**vuvi. |
| Huyu ni **m**gonjwa | - | Hawa ni **wa**gonjwa. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 21**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kusubiri, kutuarifu, kusanyika.**

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Darasani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Wanafunzi wa darasa hili walikuwa na nidhamu. Je, ni kweli? (ndiyo)*
2. *Kwa nini unasema hivyo? (walitulia darasani n.k)*
3. *Kwa nini wanafunzi na walimu walikusanyika mbele ya ofisi ya mwalimu mkuu? (walifuata mwito wa kengele)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi hizi katika vitabu vyao.

**Mwalimu amesimama wima - Walimu wamesimama wima.**

**Mwanafunzi anakimbia - Wanafunzi wanakimbia.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 5: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 5: Siku ya 3

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **i** | **o** |
| **ta** | **ta** | **ti** | **to** |
| **kta** | **sta** | **sti** | **sto** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma k ta ba | m li ngo ti | bu s ta ni |
| **maktaba** | **mlingoti** | **bustani** |
| m ku bwa | m si ngi | m kuu |
| **mkubwa** | **msingi** | **mkuu** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **i** | **u** | **e** |
| **li** | **si** | **ku** | **ke** |
| **mli** | **msi** | **mku** | **mke** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma kubwa | m refu | ku pendeza | ku leta |
| **makubwa** | **mrefu** | **kupendeza** | **kuleta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Huu ni **m**lingoti **m**refu | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**refu. |
| Huu ni **m**lingoti **m**fupi | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**fupi. |
| Huu ni **m**lingoti **m**kubwa | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**kubwa. |
| Huu ni **m**lingoti **m**zuri | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**zuri. |
| Huu ni **m**kebe **m**dogo | - | Hii ni **mi**kebe **mi**dogo. |

23

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 — **Shuleni**



**Shule ya Msingi ya Tuigoin**

Shule ya Msingi ya Tuigoin ni shule kubwa sana. Ina madarasa makubwa ya mawe. Madarasa yana madirisha makubwa ya kuleta mwangaza na hewa safi. Shule hii pia ina ofisi ya mwalimu mkuu, maktaba na chumba cha walimu. Nje ya ofisi kuna bustani ya maua ya kupendeza. Pia kuna mlingoti mrefu wa bendera. Shule hii ina uwanja mkubwa. Kando ya uwanja kuna vyoo safi vya wanafunzi na walimu.

24

■ **Kusoma silabi**

Andika herufi **a** ubaoni. N/T/U: Soma sauti hiyo **/a/**. Ongeza sauti **/t/** kabla ya **a** kisha uunganishe na kusema silabi **ta**. Ongeza sauti **/k/** kisha uunganishe na kusema silabi **kta**. **[U]** Endelea na silabi: **a, ta, sta; i, ti, sti; o, to, sto.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 23**.

● **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **maktaba** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ma k ta ba** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **maktaba**. **[U]** Endelea na maneno: **mlingoti, bustani, mkubwa, msingi, mkuu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 23**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mlingoti, maktaba, bustani**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Shule ya msingi ya Tuigoin"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, shule ya msingi ya Tuigoin ni ya aina gani (ni kubwa sana)*
2. *Kwa nini shule ina madirisha makubwa? (ya kuleta mwangaza na hewa safi)*
3. *Nje ya ofisi kuna nini? (bustani)*

**Kuandika:**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Bendera inapepea kwenye mlingoti.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 5: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza huu mwaka. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ________________ Muda: ________________ Idadi: ________________

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 **Shuleni**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **i** | **o** |
| **ta** | **ta** | **ti** | **to** |
| **kta** | **sta** | **sti** | **sto** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma k ta ba | m li ngo ti | bu s ta ni |
| **maktaba** | **mlingoti** | **bustani** |
| m ku bwa | m si ngi | m kuu |
| **mkubwa** | **msingi** | **mkuu** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **i** | **u** | **e** |
| **li** | **si** | **ku** | **ke** |
| **mli** | **msi** | **mku** | **mke** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma kubwa | m refu | ku pendeza | ku leta |
| **makubwa** | **mrefu** | **kupendeza** | **kuleta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Huu ni **m**lingoti **m**refu | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**refu. |
| Huu ni **m**lingoti **m**fupi | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**fupi. |
| Huu ni **m**lingoti **m**kubwa | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**kubwa. |
| Huu ni **m**lingoti **m**zuri | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**zuri. |
| Huu ni **m**kebe **m**dogo | - | Hii ni **mi**kebe **mi**dogo. |

23

Wiki ya 5: Siku ya 3 na 4 **Shuleni**



**Shule ya Msingi ya Tuigoin**

Shule ya Msingi ya Tuigoin ni shule kubwa sana. Ina madarasa makubwa ya mawe. Madarasa yana madirisha makubwa ya kuleta mwangaza na hewa safi. Shule hii pia ina ofisi ya mwalimu mkuu, maktaba na chumba cha walimu. Nje ya ofisi kuna bustani ya maua ya kupendeza. Pia kuna mlingoti mrefu wa bendera. Shule hii ina uwanja mkubwa. Kando ya uwanja kuna vyoo safi vya wanafunzi na walimu.

24

### Kusoma silabi

Andika herufi **i** ubaoni. N/T/U: Soma sauti hiyo **/i/.** Ongeza sauti **/l/** kabla ya **i** kisha uunganishe na kusema silabi **li**. Ongeza sauti **/m/** kisha uunganishe na kusema silabi **mli**. **[U]** Endelea na silabi: **i, si, msi; e, ke, mke; u, ku, mku.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 23**.

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **makubwa** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **ma kubwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **makubwa**. **[U]**. Endelea na maneno: **mrefu, kupendeza** na **kuleta.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 23**.

### ◆ Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| **i.** | Huu ni **m**lingoti **m**refu | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**refu. |
| **ii.** | Huu ni **m**lingoti **m**fupi | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**fupi. |
| **iii.** | Huu ni **m**lingoti **m**kubwa | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**kubwa. |
| **iv** | Huu ni **m**kebe **m**dogo | - | Hii ni **mi**kebe **mi**dogo. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 23**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mlingoti, maktaba** na **bustani**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Shule ya msingi ya Tuigoin"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, uwanja mkubwa wa shule hii ulikuwa wa nini? (wanafunzi kuchezea)*
2. *Je, unafikiri shule hii ilikuwa na wanafunzi wengi au wachache? (wengi)*
3. *Toa sababu za jibu lako. (kwa sababu ilikuwa shule kubwa)*

### Kuandika


Andika maneno haya ubaoni.

Tumia maneno: **mlingoti mrefu, mkebe mdogo, mikebe midogo, milingoti mirefu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 5: Siku ya 4*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________


Wiki ya 5: Siku ya 5 — Shuleni

Tamka sauti.
■ ms sh aa

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **bu sta ni - bustani**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| sta | da | ni | ma | u | sa |
| na | ba | kta | wa | bu | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.
● **Kuakifisha**
Mlingoti huu ni mrefu.
Mfupa huu ni mkubwa.
Mkebe huu ni mdogo.
Mchoro huu ni mbaya.

Shule yangu

25

**★ Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote na wanafunzi. Tumia silabi **bu s ta** na **ni** kuandika neno **bustani**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

**● Sarufi - Kuakifisha**

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U: Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia alama ya kituo (**.**) Alama hii inatumiwa katika **mwisho** wa sentensi.

Mlingoti huu ni mrefu.
Mfupa huu ni mkubwa.
Mkebe huu ni mdogo.
Mchoro huu ni mbaya.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 25**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **msingi, mashuhuri, maadili na jitahidi**. Soma kichwa cha shairi. Waonyeshe wanafunzi picha. *Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.*

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **Shule yangu** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Baada ya kusoma**

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

i. *Waalimu huwafundisha nini wanafunzi? (maadili.)*
ii. *Ni mambo yapi mazuri yaliyo katika shule yao? (masomo, michezo.)*
iii. *Je, mwanafunzi huyu alipenda shule yake? (ndio.)*
iv. *Vitu gani vingekufanya wewe kuipenda shule hii? (masomo, michezo, walimu, marafiki.)*

**Kuandika - Kuakifisha**

Andika sentesi hizi ubaoni bila alama ya kikomo (**.**) Wanafunzi waziandike kwenye madaftari yao wakiakifisha.

1. Mti huu umevunjika
2. Mkate huu ni mtamu
3. Mpira huu ni wangu

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 5: Siku ya 5*

## Shule yangu

Naisifu shule yangu, hii ni msingi wangu,
Mwalimu rafiki yangu, wanafunzi ndugu zangu,
**Asubuhi na mapema, furaha hujaa tele.**

Shuleni mengi mazuri, masomo nayo michezo,
Masomoni tu mashuhuri, michezoni sio mchezo,
**Mchana jua kichwani, furaha hujaa tele.**

Walimu wamenilea, maadili kunifundisha,
Werevu kanitolea, Upumbavu ukaisha,
**Jioni inapofika, furaha hujaa tele.**

Tamati nimeshafika, lakini utakumbuka,
Jitahidi utainuka, kote utasifika,
**Usiku uingiapo, furaha hujaa tele.**

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Tamka sauti.

■ **ny** **ng**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **nye** **nya** **ngi** **ngo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u koo<br>**ukoo** | sha nga zi<br>**shangazi** | m ku bwa<br>**mkubwa** |
| bi na mu<br>**binamu** | nya nya<br>**nyanya** | za ngu<br>**zangu** |

Soma silabi.

| | | |
|---|---|---|
| o | o | u |
| **do** | **jo** | **ku** |
| **mdo** | **mjo** | **mku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ni eleza<br>**alinieleza** | a ka endelea<br>**akaendelea** |
| a ka ni eleza<br>**akanieleza** | ni ta mu ita<br>**nitamuita** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja –angu** | | **Wingi –etu** |
|---|---|---|
| **Huyu** ni nyanya **yangu** | - | **Hawa** ni nyanya **zetu**. |
| **Huyu** ni babu **yangu** | - | **Hawa** ni babu **zetu**. |
| **Huyu** ni shangazi **yangu** | - | **Hawa** ni shangazi **zetu**. |
| **Huyu** ni binamu **yangu** | - | **Hawa** ni binamu **zetu**. |

26





### Ukoo wetu

Siku moja nyanya yangu alinieleza kuhusu ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye alikuwa na watoto watano. Nyanya akanieleza kuwa kaka za baba yangu nitawaita amu. Nyanya akaendelea kusema kuwa dada za baba yangu ni shangazi zangu. Nao watoto wao wote nitawaita binamu. Nyanya akanieleza kuwa kaka wa mama yangu ni mjomba. Dada mkubwa wa mama yangu nitamuita mama mkubwa.

27

■ **Majina ya herufi na sauti**

N/T/U: Eleza wanafunzi jina la herufi **ny**. Tamka sauti ya herufi **/ny/**. Endelea na (**ng**.)

● **Kusoma silabi**

Andika silabi **nye** ubaoni. N/T/U: Sema kila sauti **/ny/ /e/** kisha uunganishe na kusema silabi **nye**. **[U]** Endelea na silabi**: nya, ngi, ngo. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 26.

▬ **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **ukoo** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **u koo** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ukoo**. **[U]** Endelea na maneno: **shangazi, mkubwa, binamu, nyanya, zangu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 26**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **shangazi, mjomba** na **binamu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Ukoo wetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Nyanya alisema shangazi ni nani? (dada ya baba)*
2. *Amu ni nani? (kaka za baba)*
3. *Mjomba ni nani? (kaka ya mama)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili. Wanafunzi wayanakili kwenye madaftari yao: **nyanya, shangazi, mjomba, binamu, mkubwa**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 6: Siku ya 1*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 — Familia/Ukoo

Tamka sauti.

ny ng

Tamka sauti ya herufi na silabi.

nye nya ngi ngo

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u koo<br>**ukoo** | sha nga zi<br>**shangazi** | m ku bwa<br>**mkubwa** |
| bi na mu<br>**binamu** | nya nya<br>**nyanya** | za ngu<br>**zangu** |

Soma silabi.

| | | |
|---|---|---|
| o | o | u |
| do | jo | ku |
| mdo | mjo | mku |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ni eleza<br>**alinieleza** | a ka endelea<br>**akaendelea** |
| a ka ni eleza<br>**akanieleza** | ni ta mu ita<br>**nitamuita** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja –angu** | | **Wingi –etu** |
|---|---|---|
| **Huyu** ni nyanya **yangu** | - | **Hawa** ni nyanya **zetu**. |
| **Huyu** ni babu **yangu** | - | **Hawa** ni babu **zetu**. |
| **Huyu** ni shangazi **yangu** | - | **Hawa** ni shangazi **zetu**. |
| **Huyu** ni binamu **yangu** | - | **Hawa** ni binamu **zetu**. |

26

Wiki ya 6: Siku ya 1 na 2 — Familia/Ukoo



### Ukoo wetu

Siku moja nyanya yangu alinieleza kuhusu ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye alikuwa na watoto watano. Nyanya akanieleza kuwa kaka za baba yangu nitawaita amu. Nyanya akaendelea kusema kuwa dada za baba yangu ni shangazi zangu. Nao watoto wao wote nitawaita binamu. Nyanya akanieleza kuwa kaka wa mama yangu ni mjomba. Dada mkubwa wa mama yangu nitamuita mama mkubwa.

27

### Kusoma silabi

N/T/U: Andika herufi **o.** Soma sauti **/o/.** Ongeza herufi **d.** Soma silabi yote **do.** Ongeza herufi **m,** sasa soma silabi yote kwa pamoja **mdo**. **[U]** Endelea na silabi: **o, jo, mjo; u, ku, mku.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 26**.

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **alinieleza** ubaoni. Tamka sehemu za neno **a li ni eleza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **alinieleza**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **akanieleza, akaendelea** na **nitamuita.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 26**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma sentensi hizi.

| **Umoja –angu** | | **Wingi –etu** |
|---|---|---|
| Huyu ni nyanya yangu | - | Hawa ni nyanya zetu. |
| Huyu ni babu yangu | - | Hawa ni babu zetu. |
| Huyu ni shangazi yangu | - | Hawa ni shangazi zetu. |
| Huyu ni binamu yangu | - | Hawa ni binamu zetu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 26**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **shangazi, mjomba** na **binamu**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **ukoo wetu** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Dada ya baba yangu huitwaje? (shangazi.)*
2. *Binamu ni nani? (watoto wa mjomba au shangazi.)*
3. *Andika majina ya binamu zako wawili kama unao.*
   *(Kila mwanafunzi aandike. Kama kuna wale ambao hawana binamu waulize waandike majina ya jamaa wengine.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

**i. Huyu ni nyanya wangu - Hawa ni nyanya zetu.**
**ii. Huyu ni binamu wangu - Hawa ni binamu zetu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 6: Siku ya 2*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 **Familia/Ukoo**

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ■ | **e** | **i** | **o** | **u** |
| | **ze** | **zi** | **zo** | **zu** |
| | **mze** | **mzi** | **mzo** | **mzu** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ● | a ja bu | ma do a do a | m zo ga |
| | **ajabu** | **madoadoa** | **mzoga** |
| | hu mu u a | bwa wa | ng'o mbe |
| | **humuua** | **bwawa** | **ng'ombe** |

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ⬬ | **o** | **i** | **o** | **e** |
| | **to** | **ti** | **mo** | **me** |
| | **mto** | **mti** | **mmo** | **mme** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | | |
|---|---|---|
| ★ | wa na po mwona | wa ka m shauri |
| | **wanapomwona** | **wakamshauri** |
| | wa li shangaa | ya li yo fanana |
| | **walishangaa** | **yaliyofanana** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ◆ | mama mmoja | 1 | — | mama watatu | 3 |
| | dada mmoja | 1 | — | dada wawili | 2 |
| | babu mmoja | 1 | — | babu wanne | 4 |
| | shangazi mmoja | 1 | — | shangazi watano | 5 |

28

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 **Familia/Ukoo**



**Boma la Wakoli**

Katika kijiji cha Serere paliishi Mzee Wakoli. Mzee huyu alikuwa na ng'ombe wengi sana. Siku moja, ng'ombe wao mmoja alizaa ndama wa ajabu. Ndama huyu alikuwa na madoadoa yaliyofanana na ya chui. Watu wa Serere wakamshauri Wakoli amuue yule ndama. Wakoli na jamaa yake wakakataa. Kesho yake wanakijiji wa Serere walishangaa kuona boma lote la Wakoli limetoweka. Mahali pake palikuwa na bwawa la maji. Tangu siku hiyo, watu wa Serere wanapomwona ngo'mbe wa madoadoa, hutaka kumuua mara moja na kutupa mzoga wake msituni. Lakini wao hushangaa na kuogopa wanapokumbuka kisa hiki.

29

### ■ Kusoma silabi

Andika herufi **e** ubaoni**.** N/T/U: Soma sauti **/e/.** Ongeza sauti **z** kisha uunganishe na kusema silabi yote **ze.** Ongeza sauti **/m/,** sasa unganisha na kusoma silabi yote **mze**. **[U]** Endelea na silabi: **i, zi, mzi; o, zo, mzo; u, zu, mzu. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 28.

### ● Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **ajabu** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **a ja bu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ajabu**. **[U]** Endelea na maneno: **madoadoa, mzoga, bwawa, humuua, ng'ombe. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 28**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **madoadoa, limetoweka, ndama, mzoga** na **bwawa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Boma la Wakoli"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mzee wakoli aliishi wapi?* (Kijiji cha Serere)
2. *Kwa nini ndama alikuwa wa ajabu? (alikuwa na madoadoa kama chui)*
3. *Kwa nini wanakijiji walishangaa? (boma la Wakoli lilitoweka)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Ndama huyu ni wa madoadoa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 6: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni muhimu kutathmini kila mwanafunzi mara mbili kila muhula. Hii itakuwezesha kufahamu jinsi mwanafunzi anavyoendelea. Kusudi ni kuimarisha ufasaha wake wa kusoma na kufahamu. Kwa hivyo, ni bora kutathmini wanafunzi watatu kila siku.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — **Familia/Ukoo**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **e** | **i** | **o** | **u** |
| **ze** | **zi** | **zo** | **zu** |
| **mze** | **mzi** | **mzo** | **mzu** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a ja bu | ma do a do a | m zo ga |
| **ajabu** | **madoadoa** | **mzoga** |
| hu mu u a | bwa wa | ng'o mbe |
| **humuua** | **bwawa** | **ng'ombe** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **o** | **i** | **o** | **e** |
| **to** | **ti** | **mo** | **me** |
| **mto** | **mti** | **mmo** | **mme** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa na po mwona | wa ka m shauri |
| **wanapomwona** | **wakamshauri** |
| wa li shangaa | ya li yo fanana |
| **walishangaa** | **yaliyofanana** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mama mmoja | **1** | — | mama watatu | **3** |
| dada mmoja | **1** | — | dada wawili | **2** |
| babu mmoja | **1** | — | babu wanne | **4** |
| shangazi mmoja | **1** | — | shangazi watano | **5** |

28

Wiki ya 6: Siku ya 3 na 4 — **Familia/Ukoo**



**Boma la Wakoli**

Katika kijiji cha Serere paliishi Mzee Wakoli. Mzee huyu alikuwa na ng'ombe wengi sana. Siku moja, ng'ombe wao mmoja alizaa ndama wa ajabu. Ndama huyu alikuwa na madoadoa yaliyofanana na ya chui. Watu wa Serere wakamshauri Wakoli amuue yule ndama. Wakoli na jamaa yake wakakataa. Kesho yake wanakijiji wa Serere walishangaa kuona boma lote la Wakoli limetoweka. Mahali pake palikuwa na bwawa la maji. Tangu siku hiyo, watu wa Serere wanapomwona ngo'mbe wa madoadoa, hutaka kumuua mara moja na kutupa mzoga wake msituni. Lakini wao hushangaa na kuogopa wanapokumbuka kisa hiki.

29

### Kusoma silabi

Andika herufi **o** ubaoni**.** N/T/U: Soma sauti **/o/.** Ongeza sauti **/t/** kisha uunganishe na kusema silabi yote **to.** Ongeza sauti **/m/,** sasa unganisha na kusoma silabi yote **mto**. **[U]** Endelea na silabi: **i, ti, mti, o, mo, mmo, e, me, mme.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 28**.

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **wanapomwona** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa na po mwona** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanapomwona** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **wa li shangaa (walishangaa); wa ka m shauri (wakamshauri); ya li yo fanana (yaliyofanana.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 28**.

### Sarufi

Andika maneno ubaoni. N/T/U**:** Soma katika umoja na wingi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mama mmoja | 1 | — | mama watatu | 3 |
| dada mmoja | 1 | — | dada wawili | 2 |
| babu mmoja | 1 | — | babu wanne | 4 |
| shangazi mmoja | 1 | — | shangazi watano | 5 |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 28**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **madoadoa, limetoweka** na **bwawa**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **Boma la Wakoli** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.** Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiri ni kwa nini jamaa ya Mzee Wakoli walikataa kumuua ndama? (Walimpenda, waliogopa)*
2. *Chui ana madoadoa ya aina gani? (Meusi)*
3. *Je, umewahi kuona mnyama mwenye maumbile ya ajabu? (Kuku mwenye mguu mmoja, mbuzi mwenye pembe moja, nk)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **ndama wengi, chui mmoja, mtoto mmoja, ng'ombe wengi**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 6: Siku ya 4*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 6: Siku ya 5 — Familia/Ukoo

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno
Kwa mfano: ba bu - babu

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ba | nya | bi | mba | sha | wa |
| zi | m | go | da | ma | mu |
| bwa | do | ku | nga | bu | jo |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **m**kulima | - | **wa**kulima |
| **m**zazi | - | **wa**zazi |
| **m**jomba | - | **wa**jomba |
| **m**tawa | - | **wa**tawa |
| **m**vuvi | - | **wa**vuvi |

Mali shambani



30

## Mali shambani

Hapo zamani za kale paliondokea Mzee aliyeitwa Sila. Sila alikuwa na watoto wanne. Mtoto wa kwanza alikuwa msichana jina lake Katheu. Wale wavulana watatu walikuwa Kyalo, Katende na Mutinda.

Mzee Sila alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu sana. Siku moja alimwita Katheu na Kusema, “Mimi ni mgonjwa sana. Mle shambani mna mali na utajiri mwingi sana.” Kabla ya kusema kule utajiri huo ulikokuwa, Mzee Sila akafa.

Watoto wote walihuzunika sana. Baada ya **mazishi**, Katheu akawaambia ndugu zake, “Twendeni shambani. Baba alisema kuna mali na utajiri.” Wote walienda shambani wakatafuta kila mahali lakini hawakupata mali. Walilima shamba lote, lakini hawakupata kitu. Baadaye wakaona **afadhali** wapande mimea mbalimbali.

Mvua iliponyesha, mimea **ilimea vizuri** sana. **Walivuna** mazao mengi sana. Waliuza mazao hayo na wakatajirika. Hapo ndipo walipojua kuwa shamba ni mali.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ba** na **bu** kuandika neno **babu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika maneno ubaoni kisha usome peke yako. Yasome pamoja na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **m**kulima | – | **wa**kulima |
| **m**zazi | – | **wa**zazi |
| **m**jomba | – | **wa**jomba |
| **m**tawa | – | **wa**tawa |
| **m**vuvi | – | **wa**vuvi |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 30**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mazishi, afadhali, ilimea** na **walivuna**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mali shambani".**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja majina ya watoto wa mzee Sila.* (Katheu, Kyalo, , Katende na Mutinda)
2. *Mzee Sila alimwambia nini Katheu?* *(Mimi ni mgonjwa sana. Mle shambani mna mali na utajiri mwingi sana.)*
3. *Unafikiri ni mimea gani waliyoipanda mle shambani?* *(Wanafunzi wataje mimea mbalimbali.)*
4. *Unafikiri watoto wa mzee Sila walitumia pesa kufanya nini?* *(Wanafunzi watoe hoja zao.)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika katika daftari zao: **shangazi, mkubwa, binamu, madoadoa, mzoga, bwawa**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 6: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 7: Siku ya 1

Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2 — **Sehemu za mwili**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku pu mu li a | ku si ki li zi a | ku o ne a |
| **kupumulia** | **kusikilizia** | **kuonea** |
| ku li a | ku nywe a | ma a lu mu |
| **kulia** | **kunywea** | **maalumu** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma cho | m do mo | ki pa ji | vi si gi no |
| **macho** | **mdomo** | **kipaji** | **visigino** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu m peleka | ya me oshwa |
| **humpeleka** | **yameoshwa** |
| ku hakikisha | zi me katwa |
| **kuhakikisha** | **zimekatwa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **–ako** | | **–angu** |
|---|---|---|
| macho **yako** | - | macho **yangu** |
| masikio **yako** | - | masikio **yangu** |
| mikono **yako** | - | mikono **yangu** |
| magoti **yako** | - | magoti **yangu** |

31

Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2 — **Sehemu za mwili**



**Sehemu za mwili**

Kila sehemu ya mwili wako ni muhimu. Pua hutumiwa kupumulia, masikio kusikilizia na macho kuonea. Mikono hufanya kazi mbalimbali. Mdomo nao hutumiwa kwa kulia na kunywea. Miguu humpeleka mtu kokote atakako kwenda. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa kila sehemu ya mwili wetu ni safi kuanzia utosini hadi wayoni. Pia hakikisha kichwa, kipaji, macho, pua na masikio yameoshwa vizuri. Tumia jiwe maalum kusugua visigino na nyayo. Hakikisha kucha zako zimekatwa. Ukifanya hivyo, utakuwa na afya bora.

32

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **kupumulia** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ku pu mu li a** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kupumulia**.
**[U]** Endelea na maneno: **kusikilizia, kuonea, kulia, kunywea** na **maalumu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 31**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kipaji, utosini** na **visigino**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Sehemu za mwili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Pua hutusaidia kufanya nini? (kupumua)*
2. *Ni jukumu letu kuhakikisha nini kuhusu miili yetu? (ni safi kuanzia utosini)*
3. *Visigino husuguliwa kwa kutumia nini? (jiwe maalum)*

### Kuandika.

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyanakili kwenye madaftari yao. **Kipaji, utosini, visigino, kunywea, mdomo**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 7: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kuandika herufi kwa ubao, hakikisha usiandike hivi: **/e/** au **/sh/**, lakini uziandike hivi: **e** au **sh**.

**Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2** — **Sehemu za mwili**

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku pu mu li a | ku si ki li zi a | ku o ne a | |
| **kupumulia** | **kusikilizia** | **kuonea** | |
| ku li a | ku nywe a | ma a lu mu | |
| **kulia** | **kunywea** | **maalumu** | |
| ma cho | m do mo | ki pa ji | vi si gi no |
| **macho** | **mdomo** | **kipaji** | **visigino** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| hu m peleka | ya me oshwa |
| **humpeleka** | **yameoshwa** |
| ku hakikisha | zi me katwa |
| **kuhakikisha** | **zimekatwa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

◆

| **–ako** | | **–angu** |
|---|---|---|
| macho **yako** | - | macho **yangu** |
| masikio **yako** | - | masikio **yangu** |
| mikono **yako** | - | mikono **yangu** |
| magoti **yako** | - | magoti **yangu** |

31

**Wiki ya 7: Siku ya 1 na 2** — **Sehemu za mwili**



Sehemu za mwili

Kila sehemu ya mwili wako ni muhimu. Pua hutumiwa kupumulia, masikio kusikilizia na macho kuonea. Mikono hufanya kazi mbalimbali. Mdomo nao hutumiwa kwa kulia na kunywea. Miguu humpeleka mtu kokote atakako kwenda. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa kila sehemu ya mwili wetu ni safi kuanzia utosini hadi wayoni. Pia hakikisha kichwa, kipaji, macho, pua na masikio yameoshwa vizuri. Tumia jiwe maalum kusugua visigino na nyayo. Hakikisha kucha zako zimekatwa. Ukifanya hivyo, utakuwa na afya bora.

32

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **humpeleka** ubaoni. Tamka sehemu za neno **hu m peleka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **humpeleka**. N/T/U: Endelea na maneno: **ku hakikisha (kuhakikisha), ya me oshwa (yameoshwa), zi me katwa (zimekatwa.) Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 31.

### ◆ Sarufi

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U**:** Soma maneno ukitumia yako na yangu.

| **–ako** | | **–angu** |
|---|---|---|
| macho **yako** | - | macho **yangu** |
| masikio **yako** | - | masikio **yangu** |
| mikono **yako** | - | mikono **yangu** |
| magoti **yako** | - | magoti **yangu** |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 31**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kipaji, utosini** na **visigino**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Sehemu za mwili** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Unafikiri kila sehemu ya mwili ni muhimu? Kwa nini? (ina kazi maalum)*
2. *Unawezaje kuweka mwili wako kuwa safi kila mara? (kuoga, kunawa, kuchana nywele, kukata makucha, nk)*
3. *Unapaswa kufanya nini ili kuhakikisha kuwa una afya bora? (kutunza mwili vilivyo)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni:

- **i. Haya ni macho yetu.**
- **ii. Haya ni masikio yetu.**

Waagize wanafunzi waziandike katika vitabu vyao katika umoja: Kisha wachore sehemu za mwili kama: uso, kisigino, kipaji

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 7: Siku ya 2*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4** — **Sehemu za mwili**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mwi li | m do mo | ki chwa |
| **mwili** | **mdomo** | **kichwa** |
| ki de vu | ma sha vu | shi ngo |
| **kidevu** | **mashavu** | **shingo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li kubaliana | ya ka ongezeka |
| **walikubaliana** | **yakaongezeka** |
| ya ka changia | hu wa shikilia |
| **yakachangia** | **huwashikilia** |

Sarufi. Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mtoto ana **m**guu mfupi | - | Watoto wana **mi**guu mifupi. |
| Mvulana ana **m**kono mrefu | - | Wavulana wana **mi**kono mirefu. |
| Mzee ana **m**fupa mgumu | - | Wazee wana **mi**fupa migumu. |
| Mzazi ana **m**gongo mpana | - | Wazazi wana **mi**gongo mipana. |

33

**Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4** — **Sehemu za mwili**



**Wanakijiji wa mwili**

Wanakijiji wa Mwili walikutana kuzungumzia maisha yao. Mikono ikasema, "Sisi hufanya kazi zote za kusaidia mwili." Miguu ikakatiza, "Nasi huubeba mwili mzima." Macho yakachangia, "Sisi huhitajika kwa kuona." Masikio yakaongezea, "Nasi huhitajika kusikia." Mdomo ukasema, "Kwa nini mnadhani ni ninyi peke yenu mnaofanya kazi? Sote tuna kazi maalum. Shingo hukibeba kichwa. Vidole husaidia mikono. Kucha husaidia vidole. Shavu hurembesha uso. Kidevu hushikilia Mashavu na Mdomo." Wote kijijini Mwili walikubaliana naye kuwa kila mmoja wao ni muhimu.

34

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **mwili** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **mwi** na **li** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mwili**. **[U]** Endelea na maneno: **mdomo, kichwa, kidevu, mashavu, shingo.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 33**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **yakachangia, hurembesha** na **mashavu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Wanakijiji wa mwili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni wanakijiji wa wapi walikutana kuzungumzia maisha yao? (mwili.)*
2. *Miguu ilisema inafanya kazi ipi? (huubeba mwili.)*
3. *Nani alisababisha wote kijijini kukubaliana? (kidevu.)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mwili wangu una sehemu mbalimbali**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 7: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufunza kwa utaratibu katika wiki ya kwanza: Sio haraka sana wala polepole sana.

# Wiki ya 7: Siku ya 4

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 — **Sehemu za mwili**

Soma silabi na maneno.

| mwi li | m do mo | ki chwa |
|---|---|---|
| **mwili** | **mdomo** | **kichwa** |
| ki de vu | ma sha vu | shi ngo |
| **kidevu** | **mashavu** | **shingo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| wa li kubaliana | ya ka ongezeka |
|---|---|
| **walikubaliana** | **yakaongezeka** |
| ya ka changia | hu wa shikilia |
| **yakachangia** | **huwashikilia** |

Sarufi. Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mtoto ana **m**guu mfupi | - | Watoto wana **mi**guu mifupi. |
| Mvulana ana **m**kono mrefu | - | Wavulana wana **mi**kono mirefu. |
| Mzee ana **m**fupa mgumu | - | Wazee wana **mi**fupa migumu. |
| Mzazi ana **m**gongo mpana | - | Wazazi wana **mi**gongo mipana. |

33

Wiki ya 7: Siku ya 3 na 4 — **Sehemu za mwili**



**Wanakijiji wa mwili**

Wanakijiji wa Mwili walikutana kuzungumzia maisha yao. Mikono ikasema, "Sisi hufanya kazi zote za kusaidia mwili." Miguu ikakatiza, "Nasi huubeba mwili mzima." Macho yakachangia, "Sisi huhitajika kwa kuona." Masikio yakaongezea, "Nasi huhitajika kusikia." Mdomo ukasema, "Kwa nini mnadhani ni ninyi peke yenu mnaofanya kazi? Sote tuna kazi maalum. Shingo hukibeba kichwa. Vidole husaidia mikono. Kucha husaidia vidole. Shavu hurembesha uso. Kidevu hushikilia Mashavu na Mdomo." Wote kijijini Mwili walikubaliana naye kuwa kila mmoja wao ni muhimu.

34

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **walikubaliana** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li kubaliana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walikubaliana**. **[U]** Endelea na maneno **yakaongezeka, yakachangia** na **huwashikilia.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 33**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno ubaoni. N/T/U**:** Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mtoto ana **m**guu mfupi | - | Watoto wana **mi**guu mifupi. |
| Mvulana ana **m**kono mrefu | - | Wavulana wana **mi**kono mirefu. |
| Mzee ana **m**fupa mgumu | - | Wazee wana **mi**fupa migumu. |
| Mzazi ana **m**gongo mpana | - | Wazazi wana **mi**gongo mipana. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 33**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **yakachangia, hurembesha** na **mashavu**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Wanakijiji wa mwili"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Taja sehemu moja ya mwili ambayo haikutajwa katika hadithi.* (mdomo, mgongo, kichwa nk)
2. *Eleza umuhimu wa sehemu hiyo ya mwili.* (mdomo - kula nk)
3. *Kwa nini ni muhimu kulinda mwili?* (ili kuwa na afya bora n.k)

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni:

**mguu mfupi, mdomo safi, mkono mrefu** na **mfupa mgumu**. Tumia maneno **mguu mfupi** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno mengine kuunda sentensi zao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 7: Siku ya 4*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 7: Siku ya 5

Wiki ya 7: Siku ya 5 **Sehemu za mwili**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m do mo - mdomo**

★


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | si | a | do | o | gu |
| mo | cho | ki | pu | u | m |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Neno | | Wingi |
|---|---|---|
| shavu | - | **ma**shavu |
| sikio | - | **ma**sikio |
| goti | - | **ma**goti |
| bega | - | **ma**bega |

Binti wa mfalme



35

**Binti wa Mfalme**

Paliishi Binti Mfalme aliyesifika kwa urembo na werevu wake. Aliishi kwenye kasri nzuri. Simba wawili wa dhahabu walimlinda usiku na mchana. Wana wa wafalme wa nchi saba wakamletea posa. Akawaambia atakayejibu maswali matatu angemuoa. Hakuna aliyepata jibu sawa.

Siku moja akaja maskini kuleta posa. Binti mfalme akacheka lakini akampa nafasi ajibu maswali yake. Akauliza, "Ni kitu gani kidogo kuliko vyote duniani?" Yule maskini akajibu, "Kitu kidogo kwa vyote ni funza ambaye humuoni wewe. Ni funza aliye ndani ya funza.

Akauliza swali la pili, "Ni kitu gani kikubwa mno kuliko vyote duniani?" Yule maskini akafikiria na kusema, "Kuna hewa kila mahali duniani. Lazima ndiyo kubwa zaidi ya zote."

Binti mfalme akauliza swali la mwisho, "Ni kitu gani kilicho na sura nzuri zaidi duniani?"

Yule maskini akaomba aletewe kioo. Akamwonyesha Binti Mfalme na kusema, "Huyu ndiye mrembo zaidi."

Binti mfalme akaangua kicheko **kikubwa**. Akasema yule maskini alifaulu. Akaagiza harusi kubwa ifanywe. Wakafanya harusi ya **kufana** na kuishi raha **mustarehe**.

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **m, do** na **mo** kuandika: neno **mdomo**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika maneno haya ubaoni. Soma maneno. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| **Neno** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| shavu | - | **ma**shavu |
| sikio | - | **ma**sikio |
| goti | - | **ma**goti |
| bega | - | **ma**bega |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 35**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kasri, posa** na **akaangua kicheko.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Binti ya Mfalme"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole.

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Binti Mfalme alisifika kwa kitu gani? (urembo na werevu)*
2. *Ni watu gani walileta posa kwake? (wana wa mfalme wa nchi saba)*
3. *Ungekuwa mwenye posa, ungetoa jibu gani kwa swali la tatu? (kila mwanafunzi atoe jawabu kwa kila swali)*
4. *Unafikiri Binti Mfalme alitumia njia bora kupata mchumba? Kwa nini? (Ndio, la.)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **kipaji, utosini, visigino, yakachangia, hurembesha** na **mashavu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 7: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | ki fye ke o | t re k ta |
| **mkulima** | **kifyekeo** | **trekta** |
| ma sha mba | a li ng'o a | mbe gu |
| **mashamba** | **aling'oa** | **mbegu** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ho da ri | sho ka | ma za o | ti nga ti nga |
| **hodari** | **shoka** | **mazao** | **tingatinga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi li zo m patia | a li po taka |
| **zilizompatia** | **alipotaka** |
| a li ya uza | li li kuwa |
| **aliyauza** | **lilikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Shamba hili ni kubwa | - **Ma**shamba haya ni **ma**kubwa. |
| Shamba hili ni dogo | - **Ma**shamba haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni dogo | - **Ma**jembe haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni kubwa | - **Ma**jembe haya ni **ma**kubwa. |
| Tingatinga hili ni dogo | - **Ma**tingatinga haya ni **ma**dogo. |
| Tingatinga hili ni kubwa | - **Ma**tingatinga haya ni **ma**kubwa. |

36





### Mkulima hodari

Katika kijiji cha Nguvumali, kulikuwa na mkulima hodari sana. Aliitwa Mzee Bidii. Yeye alikuwa na mashamba makubwa na madogo. Alipotaka kukata nyasi katika shamba dogo alitumia kifyekeo, kisha akalima kwa jembe. Kama shamba lilikuwa kubwa, alitumia shoka kukatia miti mikubwa. Pia aling'oa mizizi ya miti kwa uma. Baadaye alitumia trekta au tingatinga kulima shamba hilo. Alipanda mbegu nzuri zilizompatia mazao mengi. Aliyauza mazao hayo na kuwa tajiri.

37

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **mkulima** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **m ku li ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mkulima**. **[U]** Endelea na maneno: **mashamba, kifyekeo, aling'oa, trekta** na **mbegu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 36**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hodari, kifyekeo** na **trekta**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Mkulima hodari** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mzee Bidii alifanya kazi gani katika kijiji cha Nguvumali? (Ukulima.)*
2. *Mzee bidii alitumia vifaa vipi kwa kazi yake? (kifyekeo, jembe , trekta.)*
3. *Mzee Bidii alipata vipi mazao mengi? (alipanda mbegu nzuri.)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **kifyekeo, trekta, shoka, uma, mazao, mbegu**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 8: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kabla ya wanafunzi kutabiri, hakikisha wamesoma kichwa cha hadithi na kueleza wanachokiona kwenye picha iliyo kwenye hadithi.

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 — Shambani

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | ki fye ke o | t re k ta |
| **mkulima** | **kifyekeo** | **trekta** |
| ma sha mba | a li ng'o a | mbe gu |
| **mashamba** | **aling'oa** | **mbegu** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ho da ri | sho ka | ma za o | ti nga ti nga |
| **hodari** | **shoka** | **mazao** | **tingatinga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi li zo m patia | a li po taka |
| **zilizompatia** | **alipotaka** |
| a li ya uza | li li kuwa |
| **aliyauza** | **lilikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Shamba hili ni kubwa | - | **Ma**shamba haya ni **ma**kubwa. |
| Shamba hili ni dogo | - | **Ma**shamba haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni dogo | - | **Ma**jembe haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni kubwa | - | **Ma**jembe haya ni **ma**kubwa. |
| Tingatinga hili ni dogo | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**dogo. |
| Tingatinga hili ni kubwa | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**kubwa. |

36

Wiki ya 8: Siku ya 1 na 2 — Shambani



### Mkulima hodari

Katika kijiji cha Nguvumali, kulikuwa na mkulima hodari sana. Aliitwa Mzee Bidii. Yeye alikuwa na mashamba makubwa na madogo. Alipotaka kukata nyasi katika shamba dogo alitumia kifyekeo, kisha akalima kwa jembe. Kama shamba lilikuwa kubwa, alitumia shoka kukatia miti mikubwa. Pia aling'oa mizizi ya miti kwa uma. Baadaye alitumia trekta au tingatinga kulima shamba hilo. Alipanda mbegu nzuri zilizompatia mazao mengi. Aliyauza mazao hayo na kuwa tajiri.

37

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **zilizompatia** ubaoni. Tamka sehemu za neno **zi li zo m patia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **zilizompatia**. N/T/U**:** Endelea na maneno **aliyauza, alipotaka** na **lilikuwa**.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 36**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1. | Shamba hili ni kubwa | - | **Ma**shamba haya ni **ma**kubwa. |
| 2. | Shamba hili ni dogo | - | **Ma**shamba haya ni **ma**dogo. |
| 3. | Jembe hili ni dogo | - | **Ma**jembe haya ni **ma**dogo. |
| 4. | Jembe hili ni kubwa | - | **Ma**jembe haya ni **ma**kubwa. |
| 5. | Tingatinga hili ni dogo | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**dogo. |
| 6. | Tingatinga hili ni kubwa | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**kubwa. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 36**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **hodari, kifyekeo** na **trekta**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Mkulima hodari"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Kwa nini mzee huyu aliitwa Mzee Bidii? (alikuwa na bidii kazini.)*
2. *Je, Mzee Bidii alikuwa na nguvu au la? Kwa nini? (alikuwa na nguvu, alifanya kazi nyingi n.k.)*
3. *Mzee Bidii alipanda mimea gani? (mahindi, ngano nk.***)**

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| **i.** | **Shamba hili ni kubwa** | **-** | **Mashamba haya ni makubwa.** |
| **ii.** | **Jembe hili ni dogo** | **-** | **Majembe haya ni madogo.** |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 8: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — **Shambani**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki bi na f si | mi ho go | mi me a |
| **kibinafsi** | **mihogo** | **mimea** |
| ma tu mi zi | ma hi ndi | ma ja ni |
| **matumizi** | **mahindi** | **majani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| i na yo pandwa | u ku lima |
| **inayopandwa** | **ukulima** |
| wa ku lima | ki bi nafsi |
| **wakulima** | **kibinafsi** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**zee huyu anatembea | - | **Wa**zee hawa wanatembea. |
| **M**tu huyu ni mgeni | - | **Wa**tu hawa ni wageni. |
| **M**tumishi huyu ni mcheshi | - | **Wa**tumishi hawa ni wacheshi. |

38

Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4 — **Shambani**



**Ukulima**

Ukulima ni kazi muhimu sana kwa ufanisi wa nchi. Kuna aina mbili za wakulima. Baadhi ya wakulima hulima ili wapate mazao kwa matumizi yao ya kibinafsi. Wakulima wengine hulima ili wauze mazao na kupata fedha. Mimea inayopandwa kwa matumizi ya nyumbani ni kama vile: mahindi, mboga, mihogo, ndizi na viazi vitamu. Mimea inayopandwa kwa ajili ya kuuza ni kama vile: kahawa, maua, majani chai na miwa.

39

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **kibinafsi** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ki bi na f si** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kibinafsi**. **[U]** Endelea na maneno: **matumizi, mihogo, mahindi, mimea, majani.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 38**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kibinafsi, mihogo** na **kahawa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **ukulima** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Kuna aina ngapi za wakulima? (mbili)*
2. *Taja aina za mimea za kuuzwa? (kahawa, maua, chai, miwa)*
3. *Ni mimea gani hutumiwa nyumbani? (mihogo, ndizi, viazi vitamu)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mkulima anapalilia mboga.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 8: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kumbuka hatua tatu muhimu kwenye mtindo wa kufunza somo. Mtindo huu ni: Ninafanya, Tunafanya na Unafanya.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4** **Shambani**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki bi na f si | mi ho go | mi me a |
| **kibinafsi** | **mihogo** | **mimea** |
| ma tu mi zi | ma hi ndi | ma ja ni |
| **matumizi** | **mahindi** | **majani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★ i na yo pandwa — **inayopandwa**; u ku lima — **ukulima**; wa ku lima — **wakulima**; ki bi nafsi — **kibinafsi**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| ◆ Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**zee huyu anatembea | - | **Wa**zee hawa wanatembea. |
| **M**tu huyu ni mgeni | - | **Wa**tu hawa ni wageni. |
| **M**tumishi huyu ni mcheshi | - | **Wa**tumishi hawa ni wacheshi. |

38

**Wiki ya 8: Siku ya 3 na 4** **Shambani**



**Ukulima**

Ukulima ni kazi muhimu sana kwa ufanisi wa nchi. Kuna aina mbili za wakulima. Baadhi ya wakulima hulima ili wapate mazao kwa matumizi yao ya kibinafsi. Wakulima wengine hulima ili wauze mazao na kupata fedha. Mimea inayopandwa kwa matumizi ya nyumbani ni kama vile: mahindi, mboga, mihogo, ndizi na viazi vitamu. Mimea inayopandwa kwa ajili ya kuuza ni kama vile: kahawa, maua, majani chai na miwa.

39

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **inayopandwa** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **I na yo pandwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **inayopandwa** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno **wakulima, ukulima** na **kibinafsi.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 38**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma katika umoja na wingi. N/T/U**:**

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**zee huyu anatembea | - | **Wa**zee hawa wanatembea. |
| **M**tu huyu ni mgeni | - | **Wa**tu hawa ni wageni. |
| **M**tumishi huyu ni mcheshi | - | **Wa**tumishi hawa ni wacheshi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 38**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kibinafsi, mihogo** na **kahawa**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Ukulima"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Mimea hutusaidia nini? (chakula, pesa, kivuli n.k.)*
2. *Kwa nini mkulima ni muhimu? (hutupatia chakula, pesa n.k.)*
3. *Je, mimea ina faida gani kwako? (kula, kupata karo, n.k.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno **darasa** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **mkulima yule**
2. **mtumishi huyu**
3. **mzee huyu**
4. **mtu yule**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 8: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Iwapo kuna wanafunzi wasioweza kujibu maswali ya ufahamu, waelekeze kwenye mbinu zitakazowapatia jibu kwa urahisi. Usiwapatie jibu papo hapo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 8: Siku ya 5 **Shambani**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m be gu - mbegu**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mbe | pe | go | a | sho |
| je | ho | me | ndi | ma |
| mi | hi | gu | ra | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● 

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**toto huyu si mtukutu | - | **Wa**toto hawa si watukutu. |
| **M**zazi huyu ana bidii | - | **Wa**zazi hawa wana bidii. |
| **M**jukuu huyu anafanya kazi | - | **Wa**jukuu hawa wanafanya kazi. |

Wema hauozi



40

## Wema hauozi

Katika kijiji cha Ramali, paliishi dada kwa jina Agatha. Agatha alifanya kazi katika duka la m-pesa mjini Oloitoktok. Kila mara alipofunga duka, alibeba kiasi kikubwa cha pesa zilizosalia. Siku moja alipokuwa akisafiri kutoka mjini Oloitoktok kwenda Ramali, alisahau kibeti chake kwenye matatu.

Dereva alikiona kile kibeti na kukichukua. Alitazama kibetini na kuona noti nyingi za pesa. Dereva huyo alikichukua kibeti na kukiweka mahali pazuri na salama. Alijua kwamba siku moja mwenye kibeti angetokea.

Baada ya siku chache, Agatha alipanda matatu iyo hiyo kwenda kituo cha polisi kuripoti. Dereva yule alipomuona Agatha akamkumbuka. Alipompa kile kibeti, Agatha alishukuru na kumpa nusu ya pesa zilizokuwemo kibetini humo. Dereva alimshukuru lakini hakuchukua pesa zile. Alimuambia Agatha, "Asante lakini mimi hutendea watu wote wema na najua wema hauozi."

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **mbe** na **gu** kuandika: neno **mbegu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma sentensi. Zisome pamoja na wanafunzi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari |
| **M**toto huyu si mtukutu | - | W**a**toto hawa si watukutu. |
| **M**zazi huyu ana bidii | - | **Wa**zazi hawa wana bidii. |
| **M**jukuu huyu anafanya kazi | - | **Wa**jukuu hawa wanafanya kazi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 40**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **maovu, cheo, kufilisika** na **msamaha**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya "**Wema hauozi"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali:**

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Agatha alifanya kazi gani? (kutoa huduma za M-Pesa)*
2. *Ndani ya kibeti dereva aliona nini? (noti za pesa)*
3. *Kwa nini dereva aliweka pesa pahali pazuri na salama? (alijua mwenye pesa angekuja)*
4. *Ungekuwa wewe dereva ungefanya nini? (watoto watoe maoni)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **shamba, wema, nyasi, msamaha, cheo, trekta, mazao, panga, tingatinga, kifyekeo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 8: Siku ya 5*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wadudu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m chwa | gha la ni | vi gi ngi |
| **mchwa** | **ghalani** | **vigingi** |
| u ha ri bi fu | ki chu guu | m du du |
| **uharibifu** | **kichuguu** | **mdudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu fananishwa | wa na m jua |
| **hufananishwa** | **wanamjua** |
| wa na o fanya | i ta wa letea |
| **wanaofanya** | **itawaletea** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mchwa ni **m**dudu **m**dogo | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**dogo. |
| Mchwa ni **m**dudu **m**haribifu | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**haribifu. |
| Mchwa ni **m**dudu mwenye bidii | - | Mchwa ni **wa**dudu wenye bidii. |
| Mchwa huyu ni **m**kali | - | Mchwa hawa ni **wa**kali. |

41



**Wadudu**



### Mchwa

Mchwa ni mdudu ambaye ana sifa nyingi. Watu wanamjua mchwa kwa uharibifu wake. Kwa mfano mchwa anaweza kuharibu mazao ghalani na kula miti na vigingi vya nyumba. Mbali na uharibifu, mchwa ana sifa nzuri kutokana na bidii yake. Je, wajua kwamba mchwa hujenga nyumba yake kwa mate? Nyumba hii huitwa kichuguu. Watu wanaofanya kazi kwa bidii hufananishwa na mchwa. Mara nyingi watu wanaofanya kazi kwa bidii hupata manufaa.

42

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **mchwa** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **m chwa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mchwa**. **[U]** Endelea na maneno: **uharibifu, ghalani, kichuguu, vigingi, mdudu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 41**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mchwa, kichuguu** na **manufaa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Mchwa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mchwa anajulikana sana kwa nini? (uharibifu wake)*
2. *Mchwa hujenga nyumba yake vipi? (kwa kutumia mate)*
3. *Kwa nini watu wanaofanya kazi kwa bidii hufananishwa na mchwa? (kwa sababu mchwa hufanya kazi kwa bidii)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mchwa, mdudu, kichuguu, vigingi, uharibifu**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 9: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kabla ya kusoma hadithi mwalimu huzungumza kuhusu msamiati, husoma kichwa cha hadithi, huzungumza kuhusu picha na wanafunzi hatimaye hutoa utabiri.

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m chwa | gha la ni | vi gi ngi |
| **mchwa** | **ghalani** | **vigingi** |
| u ha ri bi fu | ki chu guu | m du du |
| **uharibifu** | **kichuguu** | **mdudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| hu fananishwa | wa na m jua |
| **hufananishwa** | **wanamjua** |
| wa na o fanya | i ta wa letea |
| **wanaofanya** | **itawaletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mchwa ni **m**dudu **m**dogo | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**dogo. |
| Mchwa ni **m**dudu **m**haribifu | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**haribifu. |
| Mchwa ni **m**dudu mwenye bidii | - | Mchwa ni **wa**dudu wenye bidii. |
| Mchwa huyu ni **m**kali | - | Mchwa hawa ni **wa**kali. |







Mchwa

Mchwa ni mdudu ambaye ana sifa nyingi. Watu wanamjua mchwa kwa uharibifu wake. Kwa mfano mchwa anaweza kuharibu mazao ghalani na kula miti na vigingi vya nyumba. Mbali na uharibifu, mchwa ana sifa nzuri kutokana na bidii yake. Je, wajua kwamba mchwa hujenga nyumba yake kwa mate? Nyumba hii huitwa kichuguu. Watu wanaofanya kazi kwa bidii hufananishwa na mchwa. Mara nyingi watu wanaofanya kazi kwa bidii hupata manufaa.



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **hufananishwa** ubaoni. Tamka sehemu za neno **hu fananishwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **hufananishwa**. N/T/U**:** Endelea na maneno **wanaofanya, wanamjua** na **itawaletea.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 41**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Zisome katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mchwa ni **m**dudu **m**dogo | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**dogo. |
| Mchwa ni **m**dudu **m**haribifu | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**haribifu. |
| Mchwa ni **m**dudu mwenye bidii | - | Mchwa ni **wa**dudu wenye bidii. |
| Mchwa huyu ni **m**kali | - | Mchwa hawa ni **wa**kali. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 41**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mchwa, kichuguu** na **manufaa**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mchwa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mchwa anaweza kumfaidi vipi mwanadamu? (Ni chakula, anatengeneza mbolea, anaharibu taka)*
2. *Je, unafikiri mchwa hubebea wapi chakula chake? (mdomoni, miguuni, tumboni)*
3. *Ni manufaa gani ambayo tunaweza kupata kutokana na bidii yetu masomoni? (kazi, maarifa)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

i. **Huyu ni mchwa mdogo - Hawa ni mchwa wadogo.**
ii. **Huyu ni mchwa mkali - Hawa ni mchwa wakali.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 9: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 9: Siku ya 3

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — **Wadudu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ko mba mwi ko<br>**kombamwiko** | ki wa vi<br>**kiwavi** | ku mbi ku mbi<br>**kumbikumbi** |
| n zi<br>**nzi** | ki ro bo to<br>**kiroboto** | vi nywa ji<br>**vinywaji** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa ka sameheana<br>**wakasameheana** | ku wa alika<br>**kuwaalika** |
| wa li hudhuria<br>**walihudhuria** | a me chafua<br>**amechafua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Ki**pepeo **m**dogo **a**napepea | - | **Vi**pepeo **wa**dogo **wa**napepea. |
| **Ki**wavi **m**dogo **a**nakula | - | **Vi**wavi **wa**dogo **wa**nakula. |
| **Ki**roboto **m**dogo **a**meniuma | - | **Vi**roboto **wa**dogo **wa**meniuma. |
| **Ki**vunjajungu **m**dogo **a**naruka | - | **Vi**vunjajungu **wa**dogo **wa**naruka. |

43

Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4 — **Wadudu**



### Sherehe ya wadudu

Katika shamba la Ngomeni kulizuka vita kali kati ya kombamwiko na kiwavi. Kombamwiko alikuwa amechafua vazi la kiwavi ambalo lilikuwa maridadi sana. Kiroboto aliona ni heri aandae sherehe na kuwaalika wadudu wote. Mwendo wa saa nne, wadudu walianza kuingia. Viwavi, siafu, nyuki, nzi, panzi na kumbikumbi walihudhuria. Wadudu wakala vyakula na kunywa vinywaji vitamu. Mwishowe wakasameheana. Tangu siku hiyo wadudu waliishi kwa umoja.

44

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U Andika neno **kombamwiko** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ko mba mwi ko** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kombamwiko**. **[U]** Endelea na maneno: **nzi, kiwavi, kiroboto, kumbikumbi, vinywaji.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 43**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **kombamwiko, kiwavi,** na **kumbikumbi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Sherehe ya wadudu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Vita kati ya kombamwiko na kiwavi vilitokana na nini? (Kombamwiko alichafua vazi la Kiwavi)*
2. *Wadudu hawa waliishi wapi? (Katika shamba la Ngomeni)*
3. *Taja majina ya aina tatu za wadudu? (kumbikumbi, kiwavi, kombamwiko)*

**Kuandika**

Andika sentensi moja ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili.

Wadudu wengi wanakula chakula.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 9: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Fuatilizia kwa kidole unaposoma sauti ili uunde silabi au wakati unasoma silabi zinazotengeneza neno. Baadaye pitisha kidole chini ya silabi au neno zima.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 9: Siku ya 4

**Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4** **Wadudu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ko mba mwi ko<br>**kombamwiko** | ki wa vi<br>**kiwavi** | ku mbi ku mbi<br>**kumbikumbi** |
| n zi<br>**nzi** | ki ro bo to<br>**kiroboto** | vi nywa ji<br>**vinywaji** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ★ wa ka sameheana<br>**wakasameheana** | ku wa alika<br>**kuwaalika** |
| wa li hudhuria<br>**walihudhuria** | a me chafua<br>**amechafua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| ◆ **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Ki**pepeo **m**dogo **a**napepea | - | **Vi**pepeo **wa**dogo **wa**napepea. |
| **Ki**wavi **m**dogo **a**nakula | - | **Vi**wavi **wa**dogo **wa**nakula. |
| **Ki**roboto **m**dogo **a**meniuma | - | **Vi**roboto **wa**dogo **wa**meniuma. |
| **Ki**vunjajungu **m**dogo **a**naruka | - | **Vi**vunjajungu **wa**dogo **wa**naruka. |

43

**Wiki ya 9: Siku ya 3 na 4** **Wadudu**



### Sherehe ya wadudu

Katika shamba la Ngomeni kulizuka vita kali kati ya kombamwiko na kiwavi. Kombamwiko alikuwa amechafua vazi la kiwavi ambalo lilikuwa maridadi sana. Kiroboto aliona ni heri aandae sherehe na kuwaalika wadudu wote. Mwendo wa saa nne, wadudu walianza kuingia. Viwavi, siafu, nyuki, nzi, panzi na kumbikumbi walihudhuria. Wadudu wakala vyakula na kunywa vinywaji vitamu. Mwishowe wakasameheana. Tangu siku hiyo wadudu waliishi kwa umoja.

44

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **wakasameheana** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa ka sameheana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wakasameheana** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno **walihudhuria, kuwaalika** na **amechafua.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 43**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Zisome katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Ki**pepeo mdogo **a**napepea | - | **Vi**pepeo wadogo **wa**napepea. |
| **Ki**wavi mdogo **a**nakula | - | **Vi**wavi wadogo **wa**nakula. |
| **Ki**roboto mdogo **a**meniuma | - | **Vi**roboto wadogo **wa**meniuma. |
| **Ki**vujanjungu mdogo **a**naruka | - | **Vi**vujanjungu wadogo **wa**naruka. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 43**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **kombamwiko, kiwavi,** na **kumbikumbi**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Sherehe ya wadudu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiria kiwavi alikuwa amevalia vazi la aina gani? (hakuwa amevaa hii ni hadithi tu)*
2. *Je, mdudu gani alikosa katika sherehe hii? (jina la mdudu yeyote asiye kwenye hadithi)*
3. *Kati ya wadudu hawa nani alikuwa na hekima? Kwa nini? (kiroboto)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno **kiwavi** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **kipepeo mdogo**
2. **viwavi wadogo**
3. **kiroboto mdogo**
4. **vivujanjungu**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 9: Siku ya 4*

Wiki ya 9: Siku ya 5 **Wadudu**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nyi gu** - **nyigu**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| bo | si | nyu | vi | gu | pe |
| chwa | chu | o | ngu | zi | nyi |
| ro | m | to | du | n | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** - **Wingi**
Mchwa **huyu** ni **m**dogo - Mchwa **hawa** ni **wa**dogo.
Mbu **huyu** ni **m**baya - Mbu **hawa** ni **wa**baya.
Nyigu **huyu** ni **m**kubwa - Nyigu **hawa** ni **wa**kubwa.
Nzi **huyu** ni **m**chafu - Nzi **hawa** ni **wa**chafu.

Wadudu



45

## Wadudu

Katika mazingira yetu kuna wadudu wa aina nyingi. Wadudu wengine hupatikana kwa urahisi, na wengine huwa vigumu kupatikana. Wanaopatikana kwa urahisi ni kama vile: vipepeo, chungu, nyuki, nyigu, nzi na kombamwiko.

Wadudu huishi mahali kama vile: msituni, jangwani, mitoni, mchangani pia kwenye miili ya wanyama na binadamu.

Ijapokuwa wadudu wengi ni wadogo wao huwa na uwezo wa ajabu. Kwa mfano, parare au panzi anaweza kuruka urefu zaidi ya mara arobaini ya mwili wake.

Chungu naye, ana uwezo wa kubeba vitu vilivyo na uzito zaidi yake mara mia moja. Kuna aina ya mbu ambao wanaweza kupiga mabawa yao mara mia sita kwa sekunde moja.

Je, wajua kwamba nzi huonja vitu kwa miguu yake?

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **nyi** na **gu** kuandika: neno **nyigu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno au majina halisi ya wadudu kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome na kueleza jinsi maneno yanavyobadilika katika umoja na wingi pia. N/T/U:

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| 1. Mchwa **huyu** ni **m**dogo | - | Mchwa **hawa** ni **wa**dogo. |
| 2. Mbu **huyu** ni **m**baya | - | Mbu **hawa** ni **wa**baya. |
| 3. Nyigu **huyu** ni **m**kubwa | - | Nyigu **hawa** ni **wa**kubwa. |
| 4. Nzi **huyu** ni **m**chafu | - | Nzi **hawa** ni **wa**chafu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 45**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **parare, nyigu** na **sekunde**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **wadudu** huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Wadudu huishi wapi? (msituni, jangwani)*
2. *Je, viumbe wengine huonja vitu kwa kutumia nini? (ulimi)*
3. *Mbu hupiga mabawa wakifanya nini? (wakiruka)*
4. *Kwa nini ni jambo la ajabu kwa mbu kupiga mabawa yao mara mia sita kwa sekunde? (mbu ni mdudu mdogo sana)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **kichuguu, kumbikumbi, mdudu, nzi, kiwavi, kiroboto**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 9: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma wi ngu | ngu ru mo | ra di |
| **mawingu** | **ngurumo** | **radi** |
| mbi ngu | m cha che | mwa nga za |
| **mbingu** | **mchache** | **mwangaza** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu ki ruka ruka | ya ka tanda |
| **tukirukaruka** | **yakatanda** |
| i ka badilika | i li yo funikwa |
| **ikabadilika** | **iliyofunikwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Tuli**ona mwalimu | - | **Hatu**kuona mwalimu. |
| **Tuli**kuwa darasani | - | **Hatu**kuwa darasani. |
| **Tuli**chezea kwao | - | **Hatu**kuchezea kwao. |
| **Tuli**sikia sauti | - | **Hatu**kusikia sauti. |

46

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 **Anga**



**Anga**

Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukirukaruka na kucheza. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yakatanda angani. Mbingu ilionekana kama iliyofunikwa kwa blanketi jeusi. Muda mfupi baadaye, tukaona mwangaza mkali. Kisha tukasikia mingurumo ya radi. Kwa woga, sote tulitorokea darasani. Punde si punde, mvua nyingi ikaanza kunyesha. Maji yakajaa kila mahali. Mvua ilipopusa sote tulirudi uwanjani tukachezea maji ya mvua.

47

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **mawingu** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ma wi ngu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mawingu**. **[U]** Endelea na maneno **mbingu, ngurumo, mchache, radi, mwangaza.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 46**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **tulivu, yakatanda** na **ilipopusa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Anga** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Hali ya anga ilikuwa vipi? (tulivu)*
2. *Mawingu yaliyotanda angani yalikuwa rangi gani? (meusi)*
3. *Mvua ilipopusa wanafunzi walifanya nini? (walirudi uwanjani)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mawingu, mbingu, ngurumo, radi, mwangaza, kupusa**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 10: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wanafunzi wanaposoma, tembea darasani ndio uweze kujua wale ambao hawajui kusoma. Utawasaidia hao wanafunzi kusoma.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 **Anga**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma wi ngu | ngu ru mo | ra di |
| **mawingu** | **ngurumo** | **radi** |
| mbi ngu | m cha che | mwa nga za |
| **mbingu** | **mchache** | **mwangaza** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ★ tu ki ruka ruka | ya ka tanda |
| **tukirukaruka** | **yakatanda** |
| i ka badilika | i li yo funikwa |
| **ikabadilika** | **iliyofunikwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Tuli**ona mwalimu | - | **Hatu**kuona mwalimu. |
| **Tuli**kuwa darasani | - | **Hatu**kuwa darasani. |
| **Tuli**chezea kwao | - | **Hatu**kuchezea kwao. |
| **Tuli**sikia sauti | - | **Hatu**kusikia sauti. |

46

Wiki ya 10: Siku ya 1 na 2 **Anga**



**Anga**

Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukirukaruka na kucheza. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yakatanda angani. Mbingu ilionekana kama iliyofunikwa kwa blanketi jeusi. Muda mfupi baadaye, tukaona mwangaza mkali. Kisha tukasikia mingurumo ya radi. Kwa woga, sote tulitorokea darasani. Punde si punde, mvua nyingi ikaanza kunyesha. Maji yakajaa kila mahali. Mvua ilipopusa sote tulirudi uwanjani tukachezea maji ya mvua.

47

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **tukirukaruka** ubaoni. Tamka sehemu za neno **tu ki ruka ruka** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **tukirukaruka**. N/T/U: Endelea na maneno **ikabadilika, yakatanda** na **zilizofunikwa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 46**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno yafuatayo ubaoni. Soma katika hali ya kukanusha. N/T/U: Soma na wanafunzi kisha wasome peke yao.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Tuli**ona mwalimu | - | **Hatu**kuona mwalimu. |
| **Tuli**kuwa darasani | - | **Hatu**kuwa darasani. |
| **Tuli**chezea kwao | - | **Hatu**kuchezea kwao. |
| **Tuli**sikia sauti | - | **Hatu**kusikia sauti. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 46**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **tulivu, yakatanda** na **ilipopusa**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Anga"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mwangaza mkali ambao watoto waliona unaitwaje? (Radi)*
2. *Mbona watoto waliogopa? (radi ingewapiga)*
3. *Je, kuna madhara/hatari gani watoto kucheza mvuani? (watakuwa wagonjwa, watachafua nguo, watapigwa na radi)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i.** | **Tulikuwa uwanjani** | **-** | **Hatukuwa uwanjani.** |
| **ii.** | **Tulicheza mpira** | **-** | **Hatukucheza mpira.** |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 10: Siku ya 2*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma nu faa | hu bu ru di sha |
| **manufaa** | **huburudisha** |
| she re he ke a | ba fu ni |
| **sherehekea** | **bafuni** |
| ma go njwa | ku o ge le a |
| **magonjwa** | **kuogelea** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku tapika | ya ta chafuka |
| **kutapika** | **yatachafuka** |
| hu ya tamani | hu tu letea |
| **huyatamani** | **hutuletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| Pika viazi | - | **Usi**pike viazi. |
| Cheza kandanda | - | **Usi**cheze kandanda. |
| Elea juu ya maji | - | **Usi**elee juu ya maji. |
| Chafua ukuta | - | **Usi**chafue ukuta. |







**Maji**

Maji ya manufaa, mvua hutuletea,
Yaweza leta balaa, usije sherehekea,
Siyaone yatapakaa, ukaanza kutegemea,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Bila maji hakika, viumbe tutasumbuka,
Chakula sitakipika, wala vyombo kusafishika,
Majumba yatachafuka, magonjwa ya kutapika,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Twapenda kuyachezea, njiani hata bafuni,
Kuogelea na kuelea, kama samaki majini,
Wanyama nayo mimea, maji huyatamani,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**



### ▬ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **manufaa** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **ma nu faa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **manufaa**. **[U]** Endelea na maneno: **sherehekea, magonjwa, huburudisha, bafuni, kuogelea. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 48**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **bafuni, huburudisha** na **sherehekea**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri **"Shairi la maji"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mvua hutuletea manufaa gani? (maji, kuotesha mimea)*
2. *Bila maji viumbe tutafanya nini? (tutasumbuka, tutakufa kiu)*
3. *Twapenda kuchezea maji wapi? (njiani, kwenye kidimbwi cha kuogelea)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mvua inanyesha**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 10: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufanya utabiri na wanafunzi Siku ya kwanza, ya tatu na ya tano pekee. Hakuna utabiri: Siku ya 2 na ya 4. Wanafunzi watarejelea msamiati.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 10: Siku ya 3 na 4 **Anga**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ▬ | ma nu faa<br>**manufaa** | hu bu ru di sha<br>**huburudisha** |
| | she re he ke a<br>**sherehekea** | ba fu ni<br>**bafuni** |
| | ma go njwa<br>**magonjwa** | ku o ge le a<br>**kuogelea** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ★ | ku tapika<br>**kutapika** | ya ta chafuka<br>**yatachafuka** |
| | hu ya tamani<br>**huyatamani** | hu tu letea<br>**hutuletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| Pika viazi | - | **Usi**pik**e** viazi. |
| Cheza kandanda | - | **Usi**chez**e** kandanda. |
| Elea juu ya maji | - | **Usi**ele**e** juu ya maji. |
| Chafua ukuta | - | **Usi**chafu**e** ukuta. |

48

Wiki ya 10: Siku ya 3 na 4 **Anga**



**Maji**

Maji ya manufaa, mvua hutuletea,
Yaweza leta balaa, usije sherehekea,
Siyaone yatapakaa, ukaanza kutegemea,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Bila maji hakika, viumbe tutasumbuka,
Chakula sitakipika, wala vyombo kusafishika,
Majumba yatachafuka, magonjwa ya kutapika,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Twapenda kuyachezea, njiani hata bafuni,
Kuogelea na kuelea, kama samaki majini,
Wanyama nayo mimea, maji huyatamani,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

49

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **kutapika** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **ku tapika** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **kutapika**. **[U]** Endelea na maneno **huyatamani, yatachafuka** na **hutuletea.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 48**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma sentensi. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| Pika viazi | - | **Usi**pik**e** viazi. |
| Cheza kandanda | - | **Usi**chez**e** kandanda. |
| Elea juu ya maji | - | **Usi**ele**e** juu ya maji. |
| Chafua ukuta | - | **Usi**chafu**e** ukuta. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 48**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **bafuni, huburudisha** na **sherehekea**.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **maji** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, maji mengi yanaweza kuleta balaa gani? (mafuriko)*
2. *Nini kitatendeka kwa mimea na wanyama mvua isiponyesha kwa mda mrefu? (watafariki, mimea itakauka)*
3. *Je, kuna hatari gani kukosa kuoga miili yetu? (tutakuwa wagonjwa, tutakuwa wachafu, tutapatwa na magonjwa)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia maneno **pika, usicheze, elea, usichafuke** kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 10: Siku ya 4*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 10: Siku ya 5

Wiki ya 10: Siku ya 5 **Anga**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ku sa fi sha - kusafisha**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| pi | ku | o | sa | sha | ka |
| fu | ga | nywa | fi | a | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| M**wa**nadamu **yu**ko wapi? | - | **Wa**nadamu **wa**ko wapi? |
| Mnyama **yu**ko wapi? | - | **Wa**nyama **wa**ko wapi? |
| Mdudu **yu**ko wapi? | - | **Wa**dudu **wa**ko wapi? |

**Maji**



50

## Maji

Maji ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe. Wanadamu, wanyama, wadudu, miti na mimea hutegemea maji kwa uhai wao. Maji safi hayana harufu.

Maji hukusanyika kwenye mito, maziwa, na bahari. Binadamu anaweza kukaa kwa muda mrefu bila chakula, lakini siku chache sana bila maji.

Mbali na kunywa, maji hutumika kwa njia mbalimbali kama vile kupika, kuoga, kufua nguo na hata kusafishia nyumbani.

Chanzo kikuu cha maji ni mvua. Miti huleta mvua. Ukataji wa miti na utumizi mbaya wa maji unaweza kuleta madhara kwa maisha ya mwanadamu.

Mamba, kiboko, papa, na samaki wote hutegemea maji. Ni lazima tuhifadhi mazingira yetu. Njia moja ya kuhifadhi mazingira ni kupanda miti.

Upungufu wa maji kwenye mito na maziwa pia huathiri wanyama wa majini. Kumbuka maji ni uhai.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **ku, sa, fi** na **sha** kuandika: neno **kusafisha**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma sentensi. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Mwa**nadamu **yu**ko wapi? | - | **Wa**nadamu **wa**ko wapi? |
| **M**nyama **yu**ko wapi? | - | **Wa**nyama **wa**ko wapi? |
| **M**dudu **yu**ko wapi? | - | **Wa**dudu **wa**ko wapi? |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 50**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **viumbe, huathiri** na **madhara.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Maji".**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Maji safi hayana nini? (harufu)*
2. *Mbali na kunywa, maji hutumiwa kwa kazi gani? (kupika, kuoga n.k.)*
3. *Mbali na kupanda miti, tunaweza kuhifadhi vipi mazingira yetu? (kuokota taka, kuchimba mitaro)*
4. *Kwa nini tunasema "maji ni uhai"? (kwa sababu bila maji hatuwezi kuishi)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno yafuatayo mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika daftari zao. **mbingu, ngurumo, mchache, radi, mwangaza, bafuni, kuogelea.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 10: Siku ya 5*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha kwamba umeangalia kazi ya ziada kabla ya kupeana kazi nyingine.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 11: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| te k no lo ji a | ru nu nu |
| **teknolojia** | **rununu** |
| ta ra ki li shi | vi tu li zo |
| **tarakilishi** | **vitulizo** |
| te le vi she ni | ru ni nga |
| **televisheni** | **runinga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i me badilika | wa me itikia |
| **imebadilika** | **wameitikia** |
| zi me tapakaa | zi me enea |
| **zimetapakaa** | **zimeenea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Tarakilishi **hii** ni kubwa | - | Tarakilishi **hizi** ni kubwa. |
| Runinga **hii** ni nzuri | - | Runinga **hizi** ni nzuri. |
| Simu **hii** ni mpya | - | Simu **hizi** ni mpya. |
| Rununu **hii** ni nyeupe | - | Rununu **hizi** ni nyeupe. |

51

**Wiki ya 11: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**



Teknolojia

Dunia imebadilika, teknolojia imeingia,
Bara, pwani imefika, wote wameitikia,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Redio nazo tunazo, nyumbani na kwenye simu,
Mawaidha na vitulizo, mafundisho ya kuheshimu,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Tarakilishi twatumia, shuleni hata kazini,
Zina michezo ya kuvutia, zitumie kwa makini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Runinga zimeenea, zaitwa televisheni,
Picha video kuonea, muziki pia sikizeni,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Simu zimetapakaa, kila pahali nchini,
Za rununu na za waya, twatuma hata matini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

52

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **teknolojia** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **te k no lo ji a** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **teknolojia**. **[U]** Endelea na maneno: **tarakilishi, televisheni, rununu, vitulizo, runinga.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 51**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **rununu, vitulizo, tarakilishi, na matini**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **"Teknolojia"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja vifaa vya mawasiliano vilivyotajwa kwenye shairi. (redio, simu, tarakilishi, runinga, video, simu za rununu n.k.)*
2. *Redio tunazo wapi? (nyumbani, kwenye simu)*
3. *Runinga pia zinaitwaje? (televisheni)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **simu, rununu, tarakilishi, matini, televisheni**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 11: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kuwa kusoma hadithi kuna vipengele vitatu. Kusoma maneno vizuri, kwa mwendo mzuri na kuonyesha hisia na kuzingatia alama za uakifishaji.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 11: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| te k no lo ji a | ru nu nu |
|---|---|
| **teknolojia** | **rununu** |
| ta ra ki li shi | vi tu li zo |
| **tarakilishi** | **vitulizo** |
| te le vi she ni | ru ni nga |
| **televisheni** | **runinga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| i me badilika | wa me itikia |
|---|---|
| **imebadilika** | **wameitikia** |
| zi me tapakaa | zi me enea |
| **zimetapakaa** | **zimeenea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Tarakilishi **hii** ni kubwa | - | Tarakilishi **hizi** ni kubwa. |
| Runinga **hii** ni nzuri | - | Runinga **hizi** ni nzuri. |
| Simu **hii** ni mpya | - | Simu **hizi** ni mpya. |
| Rununu **hii** ni nyeupe | - | Rununu **hizi** ni nyeupe. |

51

**Wiki ya 11: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**



**Teknolojia**

Dunia imebadilika, teknolojia imeingia,
Bara, pwani imefika, wote wameitikia,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Redio nazo tunazo, nyumbani na kwenye simu,
Mawaidha na vitulizo, mafundisho ya kuheshimu,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Tarakilishi twatumia, shuleni hata kazini,
Zina michezo ya kuvutia, zitumie kwa makini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Runinga zimeenea, zaitwa televisheni,
Picha video kuonea, muziki pia sikizeni,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Simu zimetapakaa, kila pahali nchini,
Za rununu na za waya, twatuma hata matini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

52

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **imebadilika** ubaoni. Tamka sehemu za neno **i me badilika** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **imebadilika**. N/T/U: Endelea na maneno **zimetapakaa, wameitikia** na **zimeenea.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 51**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma sentensi ya kwanza. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Tarakilishi **hii** ni kubwa | - | Tarakilishi **hizi** ni kubwa. |
| Runinga **hii** ni nzuri | - | Runinga **hizi** ni nzuri. |
| Simu **hii** ni mpya | - | Simu **hizi** ni mpya. |
| Rununu **hii** ni nyeupe | - | Rununu **hizi** ni nyeupe. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 51**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **rununu, vitulizo, tarakilishi** na **matini**.

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu "**Teknolojia"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

[N/T/U] Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Tarakilishi hutumiwa kwa kazi gani? (kuandikia, kutuma ujumbe)*
2. *Taja kipindi chochote cha runinga unachokijua. (wanafunzi wataje vipindi mbalimbali)*
3. *Kwa nini mwandishi anasema "zitumie kwa makini" (kila teknologia itumiwe kwa uangalifu)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i.** | **Redio hii ni kubwa** | **-** | **Redio hizi ni kubwa.** |
| **ii.** | **Picha hii ni nzuri** | **-** | **Picha hizi ni nzuri.** |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 11: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 11: Siku ya 3 na 4 **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u hu nzi | u vu mi li vu | Ki bye go |
| **uhunzi** | **uvumilivu** | **Kibyego** |
| ku a ji ri | bi ri ka | m hu nzi |
| **kuajiri** | **birika** | **mhunzi** |
| su fu ri a | ka ra i | vyu ma |
| **sufuria** | **karai** | **vyuma** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu tengeneza | ku tengeneza |
| **hutengeneza** | **kutengeneza** |
| wa me tengeneza | i na hitaji |
| **wametengeneza** | **inahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**hunzi | - | Hawa ni **wa**hunzi. |
| Huyu ni **m**walimu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **m**susi | - | Hawa ni **wa**susi. |
| Huyu ni **m**bunge | - | Hawa ni **wa**bunge. |

53

Wiki ya 11: Siku ya 3 na 4 **Marejeleo**



Mzee Kibyego

Watu wengi siku hizi hutegemea sana kazi za kuajiriwa. Ni vyema pia kutafuta kazi ambazo unaweza kujiajiri wewe mwenyewe.
Kwa njia hii watu wengi watatengeneza kazi na kuwaajiri wengine.
Kwa mfano, Mzee Kibyego hufanya kazi ya uhunzi. Yeye hutengeneza vitu kama karai, sufuria na birika za vyuma.
Mzee Kibyego alifundishwa kazi hii na babake. Kwa kawaida, kazi hii inahitaji nguvu nyingi sana. Pia inahitaji uvumilivu. Mhunzi ni lazima atumie moto mkali na ujuzi mwingi sana. Kazi hii humletea mzee Kibyego manufaa makubwa.

54

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **uhunzi** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **u hu nzi** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **uhunzi**. **[U]** Endelea na maneno: **kuajiri, uvumilivu, birika, Kibyego, mhunzi.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 53**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mhunzi, kujiajiri** na **uvumilivu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Mzee Kibyego"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Watu wengi hutegemea kazi gani? (kazi za ofisi)*
2. *Mzee Kibyego anafanya kazi gani? (kazi ya uhunzi)*
3. *Taja vitu ambavyo Mzee Kibyego hutengeneza. (karai, sufuria, birika)*

**Kuandika**

Andika sentensi moja kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili.

**Mzee Kibyego ameshika nyundo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 11: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kiswahili ni lugha ya kupendeza sana. Mwalimu lazima ajifunze kutamka maneno sawasawa ili aweze kuongoza wanafunzi kuyatamka vyema.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 11: Siku ya 4



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u hu nzi | u vu mi li vu | Ki bye go |
| **uhunzi** | **uvumilivu** | **Kibyego** |
| ku a ji ri | bi ri ka | m hu nzi |
| **kuajiri** | **birika** | **mhunzi** |
| su fu ri a | ka ra i | vyu ma |
| **sufuria** | **karai** | **vyuma** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| hu tengeneza | ku tengeneza |
| **hutengeneza** | **kutengeneza** |
| wa me tengeneza | i na hitaji |
| **wametengeneza** | **inahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**hunzi | - | Hawa ni **wa**hunzi. |
| Huyu ni **m**walimu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **m**susi | - | Hawa ni **wa**susi. |
| Huyu ni **m**bunge | - | Hawa ni **wa**bunge. |







**Mzee Kibyego**

Watu wengi siku hizi hutegemea sana kazi za kuajiriwa. Ni vyema pia kutafuta kazi ambazo unaweza kujiajiri wewe mwenyewe.
Kwa njia hii watu wengi watatengeneza kazi na kuwaajiri wengine.
Kwa mfano, Mzee Kibyego hufanya kazi ya uhunzi. Yeye hutengeneza vitu kama karai, sufuria na birika za vyuma. Mzee Kibyego alifundishwa kazi hii na babake. Kwa kawaida, kazi hii inahitaji nguvu nyingi sana. Pia inahitaji uvumilivu. Mhunzi ni lazima atumie moto mkali na ujuzi mwingi sana. Kazi hii humletea mzee Kibyego manufaa makubwa.



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **hutengeneza** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **hu tengeneza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hutengeneza** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno **wametengeneza, kutengeneza** na **inahitaji.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 53**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma sentensi. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**hunzi | - | Hawa ni **wa**hunzi. |
| Huyu ni **m**walimu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **m**susi | - | Hawa ni **wa**susi. |
| Huyu ni **m**bunge | - | Hawa ni **wa**bunge. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 53**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mhunzi, kujiajiri** na **uvumilivu**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mzee Kibyego"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni kazi gani zingine tunazojua?*
2. *Unafikiri Mzee Kibyego alitumia pesa kufanya nini?*
3. *Je, ukiwa mtu mzima, ungependa kufanya kazi gani?*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **mhunzi, wahandisi, msusi, watangazaji**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia neno mhunzi kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 11: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kipindi cha somo la Kiswahili kina urefu wa dakika 30. Hakikisha unafunza kwa utaratibu ndio uweze kumaliza kufunza somo kwa muda uliopewa. Ukurasa wa (v) na (vi) una mpangilio wa kila sehemu na vile unavyostahili kufunza na muda wake.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 11: Siku ya 5 **Marejeleo**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma ji - maji**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a | ma | mu | ji | nywa |
| nga | ki | ru | si | ku |
| li | ni | vu | m | me |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Wakati uliopo** **Wakati ujao**

Walimu **wana**cheka - Walimu **wata**cheka.
Wananchi **wana**msalimia - Wananchi **wata**msalimia.
Wanyama **wana**enda - Wanyama **wata**enda.
Wanafunzi **wana**pata - Wanafunzi **wata**pata.

Mwalimu ni malaika



55

**MWALIMU NI MALAIKA**

Nianze nianze vipi, shairi la buriani
Huenda likawa fupi, ni wimbo toka moyoni
Tufunge basi mshipi, matatu iko mbioni
**Kama mzazi Mungu wa pili, mwalimu ni malaika**

Nilipokuja shuleni, sikuwa na marafiki
Wala wa kuamini, mwalimu kanibariki
Akanipa tumaini, ufahamu akahakiki
**Kama mzazi Mungu wa pili, mwalimu ni malaika**

Mwalimu si kama funza, yeye ni malaika
Jamani amenifunza, kusoma na kuandika
Hakika alinitunza, wakati nilitapika
**Kama mzazi Mungu wa pili, mwalimu ni malaika**

Malaika husaidia, wakati wa matatizo
Mwalimu hunipangia, kuimba nayo michezo
Kazi hutugawia, kwa upole wa maelezo
**Kama mzazi Mungu wa pili, mwalimu ni malaika**

Yananilenga machozi, na moyo wadundadunda
Ni heri nipige pozi, ukuta nimeudunda
Sitaki muanze dozi, najua mmetupenda
**Kama mzazi Mungu wa pili, mwalimu ni malaika**

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **ma** na **ji** kuandika: neno **maji**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi wakitumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Uzisome sentensi na kueleza jinsi zinavyobadilika kwa wakati.

| **Wakati uliopo** | | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| Walimu **wana**cheka | - | Walimu **wata**cheka |
| Wananchi **wana**msalimia | - | Wananchi **wata**msalimia |
| Wanyama **wana**enda | - | Wanyama **wata**enda |
| Wanafunzi **wana**pata | - | Wanafunzi **wata**pata |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 55**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno **buriani, akahakiki** na **wadundadunda**. Soma kichwa cha shairi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri shairi la **"Mwalimu ni Malaika"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni maneno gani yanayorudiwa kwenye shairi? (kama mzazi mungu wa pili, mwalimu ni malaika)*
2. *Eleza alichofunza mwalimu. (kusoma na kuandika)*
3. *Malaika husaidia wakati gani? (wakati wa matatizo)*
4. *Ni kitu gani kizuri unakumbuka kuhusu mwalimu wako? (watoto wajibu)*

**Kuandika - Imla**

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **karai, radi, mbingu, anga, sufuria, mwangaza, mbirika, mhunzi, ulimwengu, vyuma.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 11: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 **Haki za watoto**

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▬ | a | a | a | a |
| | wa | wa | wa | wa |
| | zwa | pwa | ndwa | swa |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ● | dhu lu ma | ku si ki zwa | ku fu ra hi a |
| | **dhuluma** | **kusikizwa** | **kufurahia** |
| | ku li pwa | ku li ndwa | a na pa swa |
| | **kulipwa** | **kulindwa** | **anapaswa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ★ | ha wa ruhusiwi | i na m linda |
| | **hawaruhusiwi** | **inamlinda** |
| | a me fikisha | wa na paswa |
| | **amefikisha** | **wanapaswa** |


Sarufi: Soma maneno haya.

**Maneno ya kuamuru na ukanusho**

| ◆ | Neno | Kukanusha | Neno | Kukanusha |
|---|---|---|---|---|
| | linda | **usi**linde | fanya | **usi**fanye |
| | saidia | **usi**saidie | chapa | **usi**chape |

56

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 **Haki za watoto**



**Haki za watoto**

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto kutokana na dhuluma za kila aina. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Watoto wanapaswa kufanya kazi za kuwasaidia wazazi nyumbani. Ni hatia kwa mtu yeyote kumuadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa, kupata matibabu yanayofaa na haki ya kusikizwa. Ni haki ya watoto kucheza na kufurahia maisha yao.

57

### ▬ Kusoma silabi

Andika herufi **a.** Soma sauti **/a/.** N/T/U: Ongeza herufi **w.** Soma silabi yote **wa.** Ongeza herufi **z,** sasa soma silabi yote kwa pamoja **zwa**. **[U]** Endelea na silabi: **a, wa, pwa; a, wa, ndwa; a, wa, swa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 56**.

### ● Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **dhuluma** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **dhu lu** na **ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **dhuluma**. **[U]** Endelea na maneno: **kulipwa, kusikizwa, kulindwa, kufurahia, anapaswa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 56**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **katiba**, **dhuluma, kumuadhibu** na **matibabu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Haki za watoto"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Kulingana na katiba ya Kenya, mtoto mwenye umri wa miaka sita anapaswa kufanya nini? (kuanza masomo shuleni)*
2. *Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya aina gani? (kazi ya kulipwa)*
3. *Watoto wanapaswa kufanya kazi gani? (kusaidia kwa kazi za nyumbani)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **katiba, dhuluma, wazazi, matibabu, kulindwa, kulipwa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 12: Siku ya 1*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 **Haki za watoto**

Soma silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▬ | a | a | a | a |
| | wa | wa | wa | wa |
| | **zwa** | **pwa** | **ndwa** | **swa** |

Soma silabi na maneno.

● dhu lu ma — **dhuluma**; ku si ki zwa — **kusikizwa**; ku fu ra hi a — **kufurahia**

ku li pwa — **kulipwa**; ku li ndwa — **kulindwa**; a na pa swa — **anapaswa**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ha wa ruhusiwi — **hawaruhusiwi**; i na m linda — **inamlinda**

a me fikisha — **amefikisha**; wa na paswa — **wanapaswa**


Sarufi: Soma maneno haya.

**Maneno ya kuamuru na ukanusho**

| ◆ | Neno | Kukanusha | Neno | Kukanusha |
|---|---|---|---|---|
| | linda | **usi**linde | fanya | **usi**fanye |
| | saidia | **usi**saidie | chapa | **usi**chape |

56

Wiki ya 12: Siku ya 1 na 2 **Haki za watoto**



**Haki za watoto**

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto kutokana na dhuluma za kila aina. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Watoto wanapaswa kufanya kazi za kuwasaidia wazazi nyumbani. Ni hatia kwa mtu yeyote kumuadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa, kupata matibabu yanayofaa na haki ya kusikizwa. Ni haki ya watoto kucheza na kufurahia maisha yao.

57

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **hawaruhusiwi** ubaoni. Tamka sehemu za neno **ha wa ruhusiwi** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **hawaruhusiwi**. N/T/U: Endelea na maneno **amefikisha, inamlinda** na **wanapaswa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 56**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno ubaoni. Soma katika hali ya kukanusha. N/T/U**:**

| **Neno** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| linda | - | **usi**linde |
| saidia | - | **usi**saidie |
| fanya | - | **usi**fanye |
| chapa | - | **usi**chape |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 56**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **dhuluma, kumuadhibu** na **matibabu**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **haki za watoto** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Wewe hufanya kazi gani nyumbani? (kupika, kufagia, kuosha vyombo)*
2. *Kwa nini kufanya kazi hiyo ni muhimu kwako? (mimi hujifunza kufanya kazi, hurahisisha kazi nyumbani)*
3. *Ni michezo ipi unayofurahia kucheza? (watoto wataje michezo: kucheza mpira, kukimbia, kuruka n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Kisha wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

1. Katiba inamlinda mtoto.
2. Usifanye kazi ya kulipwa.
3. Ni muhimu kusaidia wazazi nyumbani.
4. Usichape mtoto kwa fimbo.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 12: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 **Haki za watoto**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| wa le ma vu | ma gu ru du mu |
| **walemavu** | **magurudumu** |
| wa si o o na | ki ma u mbi le |
| **wasioona** | **kimaumbile** |
| wa si o si ki a | bi na da mu |
| **wasiosikia** | **binadamu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa na o zaliwa | wa na hitaji |
| **wanaozaliwa** | **wanahitaji** |
| ku wa saidia | hu chechemea |
| **kuwasaidia** | **huchechemea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mama **a**siyeona anakuja | - | Mama **wa**sioona wanakuja. |
| Nyanya **a**siyesikia analala | - | Nyanya **wa**siosikia wanalala. |
| Baba **a**siyetembea anacheka | - | Baba **wa**siotembea wanacheka. |
| Shangazi **a**siyezungumza anasoma | - | Shangazi **wa**siozungumza wanasoma. |

58

Wiki ya 12: Siku ya 3 na 4 **Haki za watoto**



**Ulemavu**

Binadamu huzaliwa au hupatwa na hali tofauti za kimaumbile. Wengine huzaliwa na ulemavu. Kuna walemavu wasioona na wale wasiosikia wala kuzungumza. Walemavu wengine huchechemea na wengine hutumia viti vya magurudumu. Wakati mwingine walemavu huhitaji usaidizi. Kwa mfano, tunaweza kuwasaidia kuvuka barabara na kwa kuwasomea hadithi. Ulemavu sio kutojiweza. Walemavu wamefanikiwa sana maishani mwao.

59

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **walemavu** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **wa le ma vu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **walemavu**. **[U]** Endelea na maneno: **wasioona, wasiosikia, magurudumu, kimaumbile, binadamu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 58**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **walemavu, huchechemea** na **magurudumu**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Ulemavu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja aina mbali mbali za ulemavu. (wasioona, wasiosikia, wasiozungumza, akili punguani n.k.)*
2. *Tunaweza kuwasaidia walemavu kwa njia gani? (kuvuka barabara, kuwasomea hadithi)*
3. *Ulemavu haumaanishi nini? (kutojiweza)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Watoto wanacheza uwanjani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 12: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni muhimu kutathmini kila mwanafunzi mara mbili kila muhula. Hii itakuwezesha kufahamu jinsi mwanafunzi anavyoendelea. Kusudi ni kuimarisha ufasaha wake wa kusoma na kufahamu. Kwa hivyo, ni bora kutathmini wanafunzi watatu kila siku.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| wa le ma vu<br>**walemavu** | ma gu ru du mu<br>**magurudumu** |
| wa si o o na<br>**wasioona** | ki ma u mbi le<br>**kimaumbile** |
| wa si o si ki a<br>**wasiosikia** | bi na da mu<br>**binadamu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ★ wa na o zaliwa<br>**wanaozaliwa** | wa na hitaji<br>**wanahitaji** |
| ku wa saidia<br>**kuwasaidia** | hu chechemea<br>**huchechemea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| ◆ Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Mama **a**siyeona anakuja | - | Mama **wa**sioona wanakuja. |
| Nyanya **a**siyesikia analala | - | Nyanya **wa**siosikia wanalala. |
| Baba **a**siyetembea anacheka | - | Baba **wa**siotembea wanacheka. |
| Shangazi **a**siyezungumza anasoma | - | Shangazi **wa**siozungumza wanasoma. |







**Ulemavu**

Binadamu huzaliwa au hupatwa na hali tofauti za kimaumbile. Wengine huzaliwa na ulemavu. Kuna walemavu wasioona na wale wasiosikia wala kuzungumza. Walemavu wengine huchechemea na wengine hutumia viti vya magurudumu. Wakati mwingine walemavu huhitaji usaidizi. Kwa mfano, tunaweza kuwasaidia kuvuka barabara na kwa kuwasomea hadithi. Ulemavu sio kutojiweza. Walemavu wamefanikiwa sana maishani mwao.



### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **wanaozaliwa** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa na o zaliwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanaozaliwa** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno **kuwasaidia, wanahitaji** na **huchechemea.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 58**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno ubaoni. Soma katika umoja na wingi. N/T/U:

| **umoja** | | **wingi** |
|---|---|---|
| Mama **a**siyeona anakuja | - | Mama **wa**sioona wanakuja. |
| Nyanya **a**siyesikia analala | - | Nyanya **wa**siosikia wanalala. |
| Baba **a**siyetembea anacheka | - | Baba **wa**siotembea wanacheka. |
| Shangazi **a**siyezungumza anasoma | - | Shangazi **wa**siozungumza wanasoma |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 58**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **walemavu, huchechemea** na **magurudumu**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Ulemavu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Taja njia zingine ambazo tunaweza kuwasaidia walemavu. (kuchanga pesa kwa miradi ya walemavu, kujenga shule za walemavu)*
2. *Je, mlemavu akiingia garini bila kiti cha ziada utafanya nini? (nitampa changu)*
3. *Walemavu wanaweza kucheza michezo ya kawaida? (ndio)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno **kimaumbile** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. mlemavu
2. wasioona
3. asiyesikia
4. wasiojiweza

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 12: Siku ya 4*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 12: Siku ya 5 **Haki za watoto**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **u le ma vu - ulemavu**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | nu | ha | u | o | le |
| ka | ndu | ba | dhi | wa | si |
| ma | ki | vu | chwa | ti | na |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| **Neno** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| cheza | - | **usi**cheze |
| adhibu | - | **usi**adhibu |
| sikiza | - | **usi**sikize |
| ficha | - | **usi**fiche |
| fichua | - | **usi**fichue |

Nandutu



60

**Nandutu**

Hapo zamani paliishi msichana aliyeitwa Nandutu. Alikuwa na sura ya kupendeza sana na alikuwa mtu wa kuaminika. Nandutu alikuwa na nundu mgongoni.

Siku moja dadake, kwa jina Jelimo, alipanga harusi. Wageni waliwasili bila kuchelewa. Nandutu alikuwa amejificha ili wageni wasijue ana ulemavu. Nandutu aliwachungulia akiwa kwenye chumba cha kulala.

Walipopewa chakula, bwana harusi alimeza chakula chote pamoja na sahani. Wale waliokuwa naye walisema, "Unataka bibi harusi ajue hali yetu halisi? Rudisha sahani haraka!" Bwana harusi alitapika chakula na sahani alizokuwa amemeza. Kumbe Bwana harusi na watu wake walikuwa majitu! Nandutu alishangazwa sana na jambo hilo.

Mara moja, Nandutu alimwambia dadake kuwa bwana harusi alikuwa jitu. Jelimo aliamini aliyoyasema dadake. Alipotoka chumbani, aliwaita watu na kuwaeleza siri na mambo yote yaliyotendeka.

Bwana harusi na rafiki zake walipojua siri imefichuka, waligeuka kuwa majitu na wakapotea hewani.

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **u, le, ma** na **vu** kuandika neno **ulemavu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi waliyoyasoma wiki hii kutumia Jedwali la silabi:

● **Sarufi**

Andika maneno yafuatayo ubaoni kisha uyasome na kueleza jinsi yanavyobadilika. N/T/U**:**

| **Neno** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| cheza | - | **usi**cheze |
| adhibu | - | **usi**adhibu |
| sikiza | - | **usi**sikize |
| ficha | - | **usi**fiche |
| fichua | - | **usi**fichue |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 60**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nundu, waliwasili, halisi, siri, imefichuka**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Nandutu".**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Nandutu alikuwa na ulemavu wa aina gani? (alikuwa na nundu mgongoni)*
2. *Nandutu alimsaidia Jelimo kwa njia gani? (Alifichua siri ya Bwana harusi ambaye alikuwa jitu)*
3. *Je, ulemavu unaleta shida gani? (ukosefu wa uwezo wa kuona, kutoweza kutembea kwa miguu n.k.)*
4. *Eleza jinsi unavyoweza kumsaidia mtu ambaye hana uwezo wa kuona. (Kumsaidia kuvuka barabara n.k.)*

✍ **Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao. **jitu, katiba, dhuluma, kulindwa, binadamu, kulipwa, wasioona, ulemavu, wasiosikia, nundu**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 12: Siku ya 5*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Afya na usafi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma a gi zo | lo we sha | ku na wa |
| **maagizo** | **lowesha** | **kunawa** |
| ku gu sa | vi ga nja | se ku nde |
| **kugusa** | **viganja** | **sekunde** |
| vi do le | m sa la ni | sa bu ni |
| **vidole** | **msalani** | **sabuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| u ji panguse | ku dumisha |
| **ujipanguse** | **kudumisha** |
| ku nawa | u ki tumia |
| **kunawa** | **ukitumia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-angu** | | **-ako** |
|---|---|---|
| Afya **yangu** ni nzuri | - | Afya **yako** ni nzuri. |
| Sabuni **yangu** ni nyeupe | - | Sabuni **yako** ni nyeupe. |
| Maji **yangu** ni safi | - | Maji **yako** ni safi. |
| Taulo **yangu** imezeeka | - | Taulo **yako** imezeeka. |

61

Wiki ya 13: Siku ya 1 na 2 **Afya na usafi**



### Maagizo ya kunawa mikono

Kunawa mikono ni muhimu kwa afya yako. Ni muhimu kunawa mikono kabla ya kula au kugusa chakula, baada ya kwenda msalani, na baada ya kucheza. Fuata hatua hizi:

1. Hakikisha unatumia maji safi na sabuni.
2. Lowesha mikono kwa maji, kisha paka sabuni.
3. Tengeneza povu kisha lieneze kwenye viganja na katikati ya vidole.
4. Sugua mikono kwa muda wa sekunde kumi na tano.
5. Nawa kwa maji safi kisha ujipanguse kwa taulo safi.

Usafi ni mojawapo ya njia za kudumisha afya bora.

62

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **maagizo** ubaoni. Tamka silabi **ma a gi zo** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno upesi **maagizo**.
**[U]** Endelea na maneno: **kugusa, lowesha, viganja, kunawa, sekunde.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 61**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno: **maagizo, msalani, lowesha, viganja**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Maagizo ya kunawa mikono"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, tunafaa kunawa mikono wakati gani? (kabla ya kula, baada ya kuenda msalani, baada ya kucheza)*
2. *Taja hatua ya tatu ya kunawa mikono. (hatua ya 3 ya kunawa - tengeneza povu)*
3. *Utatumia nini baada ya kunawa kwa maji safi? (Taulo safi)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **kunawa, msalani, viganja, lowesha, vidole, povu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 13: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kufunza msamiati, unaweza kutumia lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma a gi zo | lo we sha | ku na wa |
| **maagizo** | **lowesha** | **kunawa** |
| ku gu sa | vi ga nja | se ku nde |
| **kugusa** | **viganja** | **sekunde** |
| vi do le | m sa la ni | sa bu ni |
| **vidole** | **msalani** | **sabuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| u ji panguse | ku dumisha |
| **ujipanguse** | **kudumisha** |
| ku nawa | u ki tumia |
| **kunawa** | **ukitumia** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| -angu | | -ako |
|---|---|---|
| Afya **yangu** ni nzuri | - | Afya **yako** ni nzuri. |
| Sabuni **yangu** ni nyeupe | - | Sabuni **yako** ni nyeupe. |
| Maji **yangu** ni safi | - | Maji **yako** ni safi. |
| Taulo **yangu** imezeeka | - | Taulo **yako** imezeeka. |







**Maagizo ya kunawa mikono**

Kunawa mikono ni muhimu kwa afya yako. Ni muhimu kunawa mikono kabla ya kula au kugusa chakula, baada ya kwenda msalani, na baada ya kucheza. Fuata hatua hizi:

1. Hakikisha unatumia maji safi na sabuni.
2. Lowesha mikono kwa maji, kisha paka sabuni.
3. Tengeneza povu kisha lieneze kwenye viganja na katikati ya vidole.
4. Sugua mikono kwa muda wa sekunde kumi na tano.
5. Nawa kwa maji safi kisha ujipanguse kwa taulo safi.

Usafi ni mojawapo ya njia za kudumisha afya bora.



### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **ujipanguze** ubaoni. Tamka sehemu za neno **u ji panguze** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **ujipanguze**. **[U]** Endelea na maneno **kunawa, kudumisha** na **ukitumia.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 61**.

### ◆ Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi ukizingatia **-angu** na **-ako**.

| -angu | | -ako |
|---|---|---|
| Afya **yangu** ni nzuri | - | Afya **yako** ni nzuri. |
| Sabuni **yangu** ni nyeupe | - | Sabuni **yako** ni nyeupe. |
| Maji **yangu** ni safi | - | Maji **yako** ni safi. |
| Taulo **yangu** imezeeka | - | Taulo **yako** imezeeka. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 61**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **maagizo, msalani, lowesha, viganja.**

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Maagizo ya kunawa mikono"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiri usiponawa mikono ni kitu gani kitafanyika? (Husababisha magojwa)*
2. *Kwa nini tunawe mikono baada ya kucheza? (Mikono yetu huwa chafu)*
3. *Je, unafikiri kunawa mikono kunasaidia kupunguza magonjwa? Taja magonjwa hayo. (Kuhara, kipindupindu, homa ya matumbo)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi za sarufi wakitumia **-angu** na **-ako**.

1. **Afya yangu ni nzuri - Afya yako ni nzuri.**
2. **Taulo yangu ni safi - Taulo yako ni safi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 13: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 13: Siku ya 3

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Afya na usafi**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma zi ngi ra<br>**mazingira** | ku u mwa<br>**kuumwa** |
| ki pi ndu pi ndu<br>**kipindupindu** | ma tu mbo<br>**matumbo** |
| ma go njwa<br>**magonjwa** | wa li zi bu a<br>**walizibua** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li zungumza<br>**alizungumza** | a li endelea<br>**aliendelea** |
| a li tu shauri<br>**alitushauri** | a li tu shukuru<br>**alitushukuru** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

**Kuakifisha**

Kwa nini chakula kiliungua?

Kwa nini tunawe mikono kabla ya kula?

Kwa nini tunavaa sweta wakati wa baridi?

Kwa nini tunapaswa kula chakula safi?

63

Wiki ya 13: Siku ya 3 na 4 **Afya na usafi**



**Usafi wa mazingira**

Ijumaa asubuhi Mwalimu Mkuu, Bibi Kulamo, alizungumza kuhusu usafi wa mazingira ya shule yetu. Alisema mazingira yakiwa machafu tunaweza kupatwa na magonjwa. Alitushauri tusicheze kwenye nyasi ndefu kwani tunaweza kuumwa na nyoka au wadudu wabaya. Nyasi huficha wadudu kama mbu ambao huleta malaria. Aliendelea kusema kuwa kutupa takataka ovyoovyo pia ni hatari. Taka na maji machafu mitaroni yanaweza kutuletea magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo. Baadaye, Bibi Kulamo alitupa kazi ya kufyeka nyasi na kuokota takataka. Baadhi ya wanafunzi walizibua mitaro iliyokuwa imezibika. Bibi Kulamo alitushukuru kwa kazi nzuri.

64

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U Andika neno **mazingira** ubaoni. Tamka silabi **ma zi ngi ra** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno kwa upesi **mazingira**. **[U]** Endelea na maneno: **kipindupindu, magonjwa, kuumwa, matumbo, walizibua.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 63**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mazingira, alitushauri** na **homa ya matumbo.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Usafi wa mazingira** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mwalimu mkuu aliitwa nani? (Bibi Kulamo)*
2. *Alisema mazingira chafu yanaweza kuleta nini? (magonjwa)*
3. *Baada ya kazi zote Bi. Kulamo alifanya nini? (alitushukuru)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Wanafunzi wanazoa taka.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 13: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kuunda maneno kutoka kwa jedwali, kumbusha wanafunzi kuwa wanaweza tu kutengeneza haya maneno wakitumia sauti au silabi zilizo kwenye jedwali. Maneno hayo ni sharti yawe maneno halisi yenye maana.

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma zi ngi ra<br>**mazingira** | ku u mwa<br>**kuumwa** |
| ki pi ndu pi ndu<br>**kipindupindu** | ma tu mbo<br>**matumbo** |
| ma go njwa<br>**magonjwa** | wa li zi bu a<br>**walizibua** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li zungumza<br>**alizungumza** | a li endelea<br>**aliendelea** |
| a li tu shauri<br>**alitushauri** | a li tu shukuru<br>**alitushukuru** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ **Kuakifisha**

Kwa nini chakula kiliungua?

Kwa nini tunawe mikono kabla ya kula?

Kwa nini tunavaa sweta wakati wa baridi?

Kwa nini tunapaswa kula chakula safi?







**Usafi wa mazingira**

Ijumaa asubuhi Mwalimu Mkuu, Bibi Kulamo, alizungumza kuhusu usafi wa mazingira ya shule yetu. Alisema mazingira yakiwa machafu tunaweza kupatwa na magonjwa. Alitushauri tusicheze kwenye nyasi ndefu kwani tunaweza kuumwa na nyoka au wadudu wabaya. Nyasi huficha wadudu kama mbu ambao huleta malaria. Aliendelea kusema kuwa kutupa takataka ovyoovyo pia ni hatari. Taka na maji machafu mitaroni yanaweza kutuletea magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo. Baadaye, Bibi Kulamo alitupa kazi ya kufyeka nyasi na kuokota takataka. Baadhi ya wanafunzi walizibua mitaro iliyokuwa imezibika. Bibi Kulamo alitushukuru kwa kazi nzuri.



### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **alizungumza** ubaoni. Tamka sehemu za neno **a li zungumza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alizungumza** kwa upesi. **[U].** Endelea na maneno **alitushauri, aliendelea** na **alitushukuru.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 63**.

### ◆ Sarufi Kuakifisha (?)

Andika sentensi hizi ubaoni bila kuakifisha N/T/U. Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia alama ya kuuliza (?.) Alama hii inatumika wakati tunapouliza swali. Ikiwa sentensi imeanza kwa **kwa nini**, tunatumia alama ya (?.)

Kwa nini chakula kiliungua?

Kwa nini tunawe mikono kabla ya kula?

Kwa nini tunavaa sweta wakati wa baridi?

Kwa nini tunapaswa kula chakula safi?

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 63**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mazingira, alitushauri, homa ya matumbo.**

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Usafi wa mazingira"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, mitaro yenye maji chafu huwa na wadudu gani? (mbu, nzi n.k.)*
2. *Je, ni wadudu gani hatari ambao hujificha kwenye nyasi ndefu? (siafu, mbung'o)*
3. *Je, unafikiri wanafunzi walimpenda Bi. Kulamo. (ndio) Kwa nini unafikiri hivyo? (wanafunzi waeleze)*

### Kuandika - Kuakifisha

Andika sentensi hizi ubaoni wanafunzi waakifishe.

1. **Kwa nini tulichelewa shuleni**
2. **Kwa nini mama hakuenda jikoni**
3. **Kwa nini mwalimu alimtuza Njoki**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 13: Siku ya 4*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 13: Siku ya 5 **Afya na usafi**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m ku ki - mkuki**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mi | ma | ta | ri | pi |
| jo | ja | ba | chu | to |
| di | ka | vu | ku | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| -angu | | -ako |
|---|---|---|
| Afya **yangu** imeimarika | - | Afya **yako** imeimarika. |
| Maji **yangu** ni moto | - | Maji **yako** ni moto. |
| Mwalimu **wangu** ni mpole | - | Mwalimu **wako** ni mpole. |
| Mtoto **wangu** amefika | - | Mtoto **wako** amefika. |

Ugonjwa wa kipindupindu



65

### Ugonjwa wa kipindupindu

Wakati wa likizo iliyopita, Anyango alikuwa mgonjwa. Alianza kutapika na tumbo likawa linamuuma sana. Mamake alimuuliza, "Maumivu yako wapi?" Anyango alijibu huku akilia, "Joto la mwili liko juu japo nahisi baridi.  Tumbo langu linauma sana. Ninahisi maumivu kwenye viungo vyote.  Kichwa changu pia kimeanza kuuma sana."

Mama alimpeleka Anyango kwenye zahanati. Daktari alimfanyia uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi yalipotoka, Daktari alisema kuwa Anyango ana ugojwa wa kipindupindu. Ugonjwa huu husababishwa na uchafu wa aina mbalimbali.

Ili tujiepushe na magonjwa kama haya ni muhimu kudumisha usafi. Pia ni lazima tutumie maji yaliyo safi au yaliyochemshwa. Daktari alimhudumia mara moja bila kupoteza wakati.

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **m, ku** na **ki** kuandika neno **mkuki**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentesi hizi ubaoni.  N/T/U. Soma sentensi hizi.

| **-angu** | | **-ako** |
|---|---|---|
| Afya **yangu** imeimarika | - | Afya **yako** imeimarika. |
| Maji **yangu** ni moto | - | Maji **yako** ni moto. |
| Mwalimu **wangu** ni mpole | - | Mwalimu **wako** ni mpole. |
| Mtoto **wangu** amefika | - | Mtoto **wako** amefika. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 65**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno **nahisi, dalili** na **hudumia**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Ugonjwa wa Kipindupindu"**  kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Anyango alihisi vipi? (joto mwilini, baridi, maumivu ya tumbo, kuumwa viungo na kichwa)*
2. *Dalili za Anyango zilikuwa za ugonjwa gani? (Kipindupindu)*
3. *Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na nini? (Uchafu wa aina mbalimbali)*
4. *Je, unafikiri nini kilimponya Anyango? (Dawa alizopewa)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **maagizo, lowesha, kudumisha, kunawa, matumbo, aliendelea, takataka, kipindupindu, mgonjwa** na **viungo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 13: Siku ya 5*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| m cha nga nyi ko<br>**mchanganyiko** | mi ho go<br>**mihogo** |
| mbo ga<br>**mboga** | ma tu nda<br>**matunda** |
| ma ha ra gwe<br>**maharagwe** | ku je nga<br>**kujenga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku hakikisha<br>**kuhakikisha** | i na pata<br>**inapata** |
| ku imarisha<br>**kuimarisha** | vya kula<br>**vyakula** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Chakula** hiki ni **kitamu** | - | **Vyakula** hivi ni **vitamu**. |
| **Chuma** hiki ni **kikubwa** | - | **Vyuma** hivi ni **vikubwa**. |
| **Choo** hiki ni **kichafu** | - | **Vyoo** hivi ni **vichafu**. |
| **Chombo** hiki ni **kizuri** | - | **Vyombo** hivi ni **vizuri**. |
| **Chungu** hiki ni **kidogo** | - | **Vyungu** hivi ni **vidogo**. |

66





### Lishe bora

Vyakula ni muhimu sana katika mwili wa binadamu. Ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kuwa jamii yake inapata lishe bora. Lishe bora ni mchanganyiko wa vyakula vya kujenga mwili, vya kuupa mwili nguvu na vile vya kuimarisha kinga mwilini. Vyakula vya kujenga mwili ni kama vile nyama, maharagwe na mayai. Vile vya kuupa mwili nguvu ni kama mihogo, mchele na ugali. Vyakula vya kusaidia kuzuia magonjwa ni kama mboga na matunda.

67

**Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U Andika neno **mchanganyiko** ubaoni. Tamka silabi **m cha nga nyi ko** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mchanganyiko**. **[U]** Endelea na maneno: **mboga, maharagwe, mihogo, matunda, kujenga.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 66**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **lishe bora, kuimarisha** na **mihogo**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Lishe bora"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni jukumu la nani kuhakikisha kuwa jamii inapata lishe bora. (mzazi).*
2. *Lishe bora ni mchanganyiko wa vyakula gani? (kujenga mwili, kuupa mwili nguvu, kuimarisha kinga mwilini).*
3. *Ni vyakula gani hujenga mwili? (nyama, maharagwe, mayai).*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **maharagwe, mayai, mihogo, mboga, matunda**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 14: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Sauti za herufi ni muhimu kwa kusaidia mwanafunzi kusoma kwa haraka. Ni wajibu wako kuhakikisha umefanya mazoezi ya kusema sauti za herufi kabla ya kuzifunza na kuzisema darasani.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 14: Siku ya 2

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 — **Vyakula**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| m cha nga nyi ko<br>**mchanganyiko** | mi ho go<br>**mihogo** |
| mbo ga<br>**mboga** | ma tu nda<br>**matunda** |
| ma ha ra gwe<br>**maharagwe** | ku je nga<br>**kujenga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku hakikisha<br>**kuhakikisha** | i na pata<br>**inapata** |
| ku imarisha<br>**kuimarisha** | vya kula<br>**vyakula** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Chakula** hiki ni **kitamu** | - | **Vyakula** hivi ni **vitamu**. |
| **Chuma** hiki ni **kikubwa** | - | **Vyuma** hivi ni **vikubwa**. |
| **Choo** hiki ni **kichafu** | - | **Vyoo** hivi ni **vichafu**. |
| **Chombo** hiki ni **kizuri** | - | **Vyombo** hivi ni **vizuri**. |
| **Chungu** hiki ni **kidogo** | - | **Vyungu** hivi ni **vidogo**. |

66

Wiki ya 14: Siku ya 1 na 2 — **Vyakula**



### Lishe bora

Vyakula ni muhimu sana katika mwili wa binadamu. Ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kuwa jamii yake inapata lishe bora. Lishe bora ni mchanganyiko wa vyakula vya kujenga mwili, vya kuupa mwili nguvu na vile vya kuimarisha kinga mwilini. Vyakula vya kujenga mwili ni kama vile nyama, maharagwe na mayai. Vile vya kuupa mwili nguvu ni kama mihogo, mchele na ugali. Vyakula vya kusaidia kuzuia magonjwa ni kama mboga na matunda.

67

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **kuhakikisha** ubaoni. Tamka sehemu za neno **ku hakikisha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **kuhakikisha**. N/T/U: Endelea na maneno **kuimarisha, vyakula,** na **inapata.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 66**.

### ◆ Sarufi

Soma sentensi hizi. Soma pamoja na wanafunzi kisha wape nafasi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Chakula** hiki ni **kitamu** | - | **Vyakula** hivi ni **vitamu**. |
| **Chuma** hiki ni **kikubwa** | - | **Vyuma** hivi ni **vikubwa**. |
| **Choo** hiki ni **kichafu** | - | **Vyoo** hivi ni **vichafu**. |
| **Chombo** hiki ni **safi** | - | **Vyombo** hivi ni **safi**. |
| **Chungu** hiki ni **kidogo** | - | **Vyungu** hivi ni **vidogo**. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 66**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **lishe bora, kuimarisha** na **mihogo**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **lishe bora** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mtu asipokula kwa siku nzima atahisi nini? (njaa)*
2. *Vyakula hununuliwa wapi? (sokoni, dukani)*
3. *Taja vyakula uvipendavyo. (wanafunzi wataje vyakula mbalimbali)*

### Kuandika

Eleza wanafunzi waorodheshe vyakula:

**Vyakula vya kujenga mwili:**

_______________, _______________, _______________.

**Vyakula vya kuupa mwili nguvu:**

_______________, _______________, _______________.

Kisha wawasomee wazazi au walezi wao.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 14: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4** — **Vyakula**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| go do ro | fo ro nya | m pi shi |
| **godoro** | **foronya** | **mpishi** |
| m si cha na | m ku li ma | nyo ro ro |
| **msichana** | **mkulima** | **nyororo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ni nunulia | ni ji tayarishe |
| **alininunulia** | **nijitayarishe** |
| ni ka badilika | ni li kuwa |
| **nikabadilika** | **nilikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja - ake** | | **Wingi - ao** |
|---|---|---|
| Mkulima **wake** ana bidii | - | Wakulima **wao** wana bidii. |
| Mwashi **wake** amemaliza kazi | - | Waashi **wao** wamemaliza kazi. |
| Mpishi **wake** anapika vizuri | - | Wapishi **wao** wanapika vizuri. |
| Mwandishi **wake** anapendeza | - | Waandishi **wao** wanapendeza. |

68

**Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4** — **Vyakula**



**Ndoto na kazi**

Siku chache zilizopita baba yangu alininunulia godoro na foronya nyororo. Jana usiku nilipolala niliota ndoto. Ndoto yangu ilikuwa hivi: Nilikuwa msichana mkubwa. Nilikuwa nimepata kazi ya ualimu. Baada ya kufanya kazi hiyo kwa muda, nilibadilika kuwa mkulima. Kwenye shamba langu kulikuwa na mboga nzuri za kijani na nyanya zilizoiva. Mbuzi wakaja na kula mboga zote. Nililia mpaka nikabadilika kuwa mpishi. Baadaye nilipika chakula kitamu sana. Watu walikula na kufurahi sana.
Hapo ndipo mama alipokuja na kuniamsha ili nijitayarishe kwenda shuleni.

69

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **godoro** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **go do** na **ro** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **godoro**. **[U]** Endelea na maneno **msichana, foronya, mkulima, mpishi** na **nyororo.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 68**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **foronya, ndoto** na **mpishi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi "**Ndoto na kazi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja kazi mbalimbali zinazotajwa kwenye hadithi (ualimu, ukulima, upishi)*
2. *Baba alinunua vitu gani? (godoro, foronya nyororo)*
3. *Ni kitu gani kilifurahisha watu? (chakula kitamu)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mbuzi wanakula mboga.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 14: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Mwalimu mzuri ni yule anayechukua muda kujiyatarisha kabla ya somo. Ni vizuri kuliangalia somo kabla ya kulifunza. Kujitayarisha vyema kunafanya somo liwe zuri na la kupendeza.

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4 — **Vyakula**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| go do ro | fo ro nya | m pi shi |
| **godoro** | **foronya** | **mpishi** |
| m si cha na | m ku li ma | nyo ro ro |
| **msichana** | **mkulima** | **nyororo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ni nunulia | ni ji tayarishe |
| **alininunulia** | **nijitayarishe** |
| ni ka badilika | ni li kuwa |
| **nikabadilika** | **nilikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja - ake** | | **Wingi - ao** |
|---|---|---|
| M**kulima** **wake** ana bidii | - | **Wa**kulima **wao** wana bidii. |
| **M**washi **wake** amemaliza kazi | - | **Wa**ashi **wao** wamemaliza kazi. |
| **M**pishi **wake** anapika vizuri | - | **Wa**pishi **wao** wanapika vizuri. |
| **M**wandishi **wake** anapendeza | - | **Wa**andishi **wao** wanapendeza. |

68

Wiki ya 14: Siku ya 3 na 4 — **Vyakula**



### Ndoto na kazi

Siku chache zilizopita baba yangu alininunulia godoro na foronya nyororo. Jana usiku nilipolala niliota ndoto. Ndoto yangu ilikuwa hivi: Nilikuwa msichana mkubwa. Nilikuwa nimepata kazi ya ualimu. Baada ya kufanya kazi hiyo kwa muda, nilibadilika kuwa mkulima. Kwenye shamba langu kulikuwa na mboga nzuri za kijani na nyanya zilizoiva. Mbuzi wakaja na kula mboga zote. Nililia mpaka nikabadilika kuwa mpishi. Baadaye nilipika chakula kitamu sana. Watu walikula na kufurahi sana.

Hapo ndipo mama alipokuja na kuniamsha ili nijitayarishe kwenda shuleni.

69

★ **Kusoma maneno marefu**

N/T/U Andika neno **alininunulia** ubaoni. Tamka sehemu za neno **a li ni nunulia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alininunulia** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno **nikabadilika, nijitayarishe** na **nilikuwa.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 68**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizo.

| **Umoja - ake** | | **Wingi - ao** |
|---|---|---|
| **M**kulima **wake** ana bidii | - | **Wa**kulima **wao** wana bidii. |
| **M**washi **wake** amemaliza kazi | - | **Wa**ashi **wao** wamemaliza kazi. |
| **M**pishi **wake** anapika vizuri | - | **Wa**pishi **wao** wanapika vizuri. |
| **M**wandishi **wake** anapendeza | - | **Wa**andishi **wao** wanapendeza. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 68**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **foronya, ndoto** na **mpishi**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Ndoto ya kazi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**Maswali**

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Watu huota wakati gani? (wakati wanapolala).*
2. *Kwa kifupi, eleza ndoto ambayo unaikumbuka. (kila mwanafunzi anaeleza ndoto yake kwa ufupi).*
3. *Je, unafikiri hadithi hii ni ya kweli? (ndio, la - wanafunzi watetee majibu yao).*

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni: **msichana wake, wavulana wao, mbuzi wake, wapishi wao**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia maneno **msichana wake** kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 14: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Hakikisha kuwasaidia watoto ambao hawajui kusoma. Wape mazoezi ya kusoma sauti, silabi na maneno mepesi. Baada ya muda mfupi wataanza kusoma kama wengine.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 14: Siku ya 5** **Wanyama**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m bu ni - mbuni**

★

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| pu | ta | de | wa | nya | u | twi |
| si | ni | mbu | ma | ga | me | nda |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** - **Wingi**

Twiga **huyu** ni **m**refu - Twiga **hawa** ni **wa**refu.
Punda **huyu** ni **m**nono - Punda **hawa** ni **wa**nono.
Tausi **huyu ana** maringo - Tausi **hawa wa**na maringo.
Mbuni **huyu ana**furahisha - Mbuni **hawa wa**nafurahisha.

Wanyama dukani



70

## Wanyama dukani

Siku moja kundi la wanyama na ndege waliamua kwenda kutembea jijini. Walipofika jijini waliona maduka na hoteli iliyokuwa na vyakula mbalimbali. Twiga, pundamilia, tausi, na mbuni wakaingia hotelini.

Mwenye hoteli aliwapa chakula. Wakala huku wakitazama runinga na wengine wakisikiliza redio. Baada ya kushiba wanyama walicheza densi hadi wakatokwa na jasho.

Watu wengi walikuja kuwatazama wanyama wakicheza densi. Wengine waliona kana kwamba vilikuwa vioja, kwa sababu ilikuwa mara ya kwanza kuona wanyama wa mwituni wakicheza densi ndani ya duka.

Baadaye walipanga mlolongo wakarudi msituni. Wakaacha watu wakistaajabu.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **mbu** na **ni** kuandika neno **mbuni**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi waliyoyasoma wiki hii kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi. N/T/U: Soma sentensi. Soma sentensi pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Twiga **huyu** ni **m**refu | - | Twiga **hawa** ni **wa**refu. |
| Punda **huyu** ni **m**nono | - | Punda **hawa** ni **wa**nono. |
| Tausi **huyu ana** maringo | - | Tausi **hawa wa**na maringo. |
| Mbuni **huyu ana**furahisha | - | Mbuni **hawa wa**nafurahisha. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 70**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **runinga, pundamilia** na **densi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Wanyama dukani".**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Wanyama gani waliingia hotelini? (twiga, pundamilia)*
2. *Kwa nini watu walikuja kuwatazama wanyama wakicheza densi? (ilikuwa mara ya kwanza kuona wanyama wa mwituni wakicheza densi)*
3. *Mwenye hoteli aliwapa wanyama chakula gani? (majibu yanaweza kujumuisha ndizi, kabeji)*
4. *Ni ndege gani wawili walikosa katika safari hii? (wanafunzi kutaja ndege wawili wanaowajua)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno yafuatayo mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kisha wawasomee wazazi au walezi wao **maharagwe, mayai, mihogo, mboga** na **matunda**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 14: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 15: Siku ya 1

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 — **Ndege na wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| nde ge | ba ta m zi nga |
| **ndege** | **batamzinga** |
| ma nyo ya | f la mi ngo |
| **manyoya** | **flamingo** |
| ma ba wa | m si tu ni |
| **mabawa** | **msituni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa me changia | wa na po zuru |
| **wamechangia** | **wanapozuru** |
| wa na o fugwa | hu tu letea |
| **wanaofugwa** | **hutuletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-haya** | **-yale** |
|---|---|
| Mabawa **haya** ni mapana | - Mabawa **yale** ni mapana. |
| Manyoya **haya** ni marefu | - Manyoya **yale** ni marefu. |
| Mayai **haya** ni madogo | - Mayai **yale** ni madogo. |
| Mapato **haya** ni machache | - Mapato **yale** ni machache. |

71

Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2 — **Ndege na wanyama**



### Umuhimu wa ndege

Ndege au nyuni ni kiumbe chenye mabawa na manyoya. Ndege wengine hupatikana nyumbani na wengine msituni. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama kuku, bata na batamzinga. Ndege hawa hutupatia nyama na mayai. Ndege wa msituni ni kama vile mbuni, tausi na kanga. Ndege wanaoishi majini ni kama vile bata bukini na flamingo au heroe. Ndege hawa wamechangia sana katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Watalii wengi huja kuwaona ndege na wanyama.Wanapozuru nchi yetu wao hutuletea pesa za kigeni.

72

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **ndege** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **nde ge** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **ndege**. **[U]** Endelea kwa maneno **manyoya, mabawa, batamzinga, flamingo** na **msituni.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 71**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nyuni, bata bukini** na **wanapozuru**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Umuhimu wa ndege"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja jina lingine la ndege? (nyuni.)*
2. *Taja ndege wa nyumbani au wakufugwa. (kuku, bata, batamzinga)*
3. *Ndege wameimarisha vipi uchumi wetu? (watalii huja kuwaona)*

**Kuandika:**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **nyuni, mabawa, manyoya, flamingo, uchumi, heroe**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 15: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ufahamu wa fonimu huzingatia kufunza sauti za herufi. Wakati wa kufunza sauti, mwalimu hapaswi kuziandika herufi hizi ubaoni.Kipindi hiki ni cha mazungumzo pekee.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2** — **Ndege na wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| nde ge | ba ta m zi nga |
| **ndege** | **batamzinga** |
| ma nyo ya | f la mi ngo |
| **manyoya** | **flamingo** |
| ma ba wa | m si tu ni |
| **mabawa** | **msituni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa me changia | wa na po zuru |
| **wamechangia** | **wanapozuru** |
| wa na o fugwa | hu tu letea |
| **wanaofugwa** | **hutuletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-haya** | | **-yale** |
|---|---|---|
| Mabawa **haya** ni mapana | - | Mabawa **yale** ni mapana. |
| Manyoya **haya** ni marefu | - | Manyoya **yale** ni marefu. |
| Mayai **haya** ni madogo | - | Mayai **yale** ni madogo. |
| Mapato **haya** ni machache | - | Mapato **yale** ni machache. |

71

**Wiki ya 15: Siku ya 1 na 2** — **Ndege na wanyama**



**Umuhimu wa ndege**

Ndege au nyuni ni kiumbe chenye mabawa na manyoya. Ndege wengine hupatikana nyumbani na wengine msituni. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama kuku, bata na batamzinga. Ndege hawa hutupatia nyama na mayai. Ndege wa msituni ni kama vile mbuni, tausi na kanga. Ndege wanaoishi majini ni kama vile bata bukini na flamingo au heroe. Ndege hawa wamechangia sana katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Watalii wengi huja kuwaona ndege na wanyama.Wanapozuru nchi yetu wao hutuletea pesa za kigeni.

72

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **wamechangia** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa me changia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **wamechangia**. N/T/U: Endelea na maneno **wa na o fugwa (wanaofugwa), wa na po zuru (wanapozuru), hu tu letea (hutuletea.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 71**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Zisome pamoja na wanafunzi. Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao.

| **-haya** | | **-yale** |
|---|---|---|
| Mabawa **haya** ni mapana | - | Mabawa **yale** ni mapana. |
| Manyoya **haya** ni marefu | - | Manyoya **yale** ni marefu. |
| Mayai **haya** ni madogo | - | Mayai **yale** ni madogo. |
| Mapato **haya** ni machache | - | Mapato **yale** ni machache. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 71**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **nyuni, bata bukini** na **wanapozuru**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Umuhimu wa ndege"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ndege wengi huruka angani. Ni ndege gani hawaruki? (mbuni)*
2. *Ni ndege gani hajatajwa kwenye hadithi? (njiwa, n.k.)*
3. *Watalii wengi ambao huja nchini hutoka wapi? (ulaya)*

### ✍ Kuandika

Soma sentensi zifuatazo mara mbili huku wanafunzi wakiziandika kisha wawasomee wazazi au walezi wao:

1. **Hili ni bawa** - **Haya ni mabawa.**
2. **Hili ni yai** - **Haya ni mayai.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 15: Siku ya 2*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapojitayarisha kwa somo, ni muhimu kusoma na kutafakari kuhusu vidokezo vya mwalimu kwenye mwongozo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 15: Siku ya 3



## Ndege na wanyama

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| tu mbi li | ma ga nda | so kwe |
| **tumbili** | **maganda** | **sokwe** |
| nge de re | mi a yo | m nya ma |
| **ngedere** | **miayo** | **mnyama** |
| mi me a | ma tu nda | wa du du |
| **mimea** | **matunda** | **wadudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a na ye patikana | wa na o fanana |
| **anayepatikana** | **wanaofanana** |
| a na ye karibia | wa na po tafuta |
| **anayekaribia** | **wanapotafuta** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Wakati uliopita (jana) | Wakati uliopo (sasa) | Wakati ujao (kesho) |
|---|---|---|
| Mbwa a**li**patikana | a**na**patikana | a**ta**patikana |
| Mgeni a**li**karibia | a**na**karibia | a**ta**karibia |
| Babu a**li**ishi | a**na**ishi | a**ta**ishi |
| Mwalimu a**li**tafuta | a**na**tafuta | a**ta**tafuta |





## Ndege na wanyama



### Tumbili

Je, wajua kwamba tumbili ni mnyama anayepatikana sehemu nyingi za dunia? Jina lingine la tumbili ni ngedere au kima. Tumbili ni mnyama anayekaribia mwanadamu kimaumbile na kwa tabia. Baadhi ya tabia hizi ni kama kula ndizi baada ya kuambua na kutupa maganda yake. Vilevile tumbili huishi na kusafiri pamoja. Wao hushirikiana wanapotafuta chakula. Tumbili hula vyakula kama vile: matunda, mimea ya majani na wadudu. Wanyama wengine wanaofanana na tumbili ni nyani na sokwe. Tumbili anapopiga miayo huwa amechoka au amekasirika.



### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **tumbiri** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **tumbiri** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **tumbiri**. **[U]** Endelea na maneno: **ngedere, maganda, miayo, sokwe** na **mnyama.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 73**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **maganda, miayo** na **maumbile**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya "**Tumbiri"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni mnyama yupi anayepatikana kila sehemu ya nchi? (tumbiri)*
2. *Tumbiri hukaribiana vipi na binadamu?* (kimaumbile na tabia)
3. *Wanyama gani wanafanana na tumbiri?* (nyani, sokwe)

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Tumbiri amebeba ndizi**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 15: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kusoma hadithi (zamu yangu), hakikisha kuwa unasoma kwa mwendo wako na sio mwendo wa wanafunzi ili waweze kuelewa. Ni kwa njia hii pia wanafunzi watajua jinsi ya kusoma kwa haraka.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 15: Siku ya 3 na 4 **Ndege na wanyama**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| tu mbi li | ma ga nda | so kwe |
| **tumbili** | **maganda** | **sokwe** |
| nge de re | mi a yo | m nya ma |
| **ngedere** | **miayo** | **mnyama** |
| mi me a | ma tu nda | wa du du |
| **mimea** | **matunda** | **wadudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| a na ye patikana | wa na o fanana |
| **anayepatikana** | **wanaofanana** |
| a na ye karibia | wa na po tafuta |
| **anayekaribia** | **wanapotafuta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Wakati uliopita (jana) | Wakati uliopo (sasa) | Wakati ujao (kesho) |
|---|---|---|
| Mbwa a**li**patikana | a**na**patikana | a**ta**patikana |
| Mgeni a**li**karibia | a**na**karibia | a**ta**karibia |
| Babu a**li**ishi | a**na**ishi | a**ta**ishi |
| Mwalimu a**li**tafuta | a**na**tafuta | a**ta**tafuta |

73

Wiki ya 15: Siku ya 3 na 4 **Ndege na wanyama**



**Tumbili**

Je, wajua kwamba tumbili ni mnyama anayepatikana sehemu nyingi za dunia? Jina lingine la tumbili ni ngedere au kima. Tumbili ni mnyama anayekaribia mwanadamu kimaumbile na kwa tabia. Baadhi ya tabia hizi ni kama kula ndizi baada ya kuambua na kutupa maganda yake. Vilevile tumbili huishi na kusafiri pamoja. Wao hushirikiana wanapotafuta chakula. Tumbili hula vyakula kama vile: matunda, mimea ya majani na wadudu. Wanyama wengine wanaofanana na tumbili ni nyani na sokwe. Tumbili anapopiga miayo huwa amechoka au amekasirika.

74

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **anayepatikana** ubaoni. Tamka sehemu za neno **a na ye patikana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **anayepatikana**. **[U]** Endelea na maneno **anayekaribia, wanaofanana** na **wanapotafuta.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 73**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

1. Mbwa a**li**patikana - a**na**patikana - a**ta**patikana
2. Mgeni a**li**karibia - a**na**karibia - a**ta**karibia
3. Babu a**li**ishi - a**na**ishi - a**ta**ishi
4. Mwalimu a**li**tafuta - a**na**tafuta - a**ta**tafuta.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 73**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **maganda, miayo** na **maumbile**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Tumbiri"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Tumbiri huishi wapi? (mwituni)*
2. *Tumbiri hupenda chakula gani? (ndizi n.k.)*
3. *Ni wadudu gani huliwa na tumbiri? (mchwa, panzi, kumbikumbi)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni **kuandika, alipatikana, anakaribia, ataishi, alitafuta**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia neno **kuandika** kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 15: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 15: Siku ya 5 **Ndege na wanyama**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nde ge - ndege**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ta | nde | tu | nya | ba |
| ki | i | fa | ku | ri |
| mbi | ni | wa | ge | du |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Wakati uliopita | Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|---|
| a**li**fanana | a**na**fanana | a**ta**fanana |
| a**li**zuru | a**na**zuru | a**ta**zuru |
| a**li**taga | a**na**taga | a**ta**taga |
| a**li**kimbia | a**na**kimbia | a**ta**kimbia |
| a**li**hama | a**na**hama | a**ta**hama |

Ndege



75

## Ndege

Ndege ni viumbe ambao wana manyoya na hutaga mayai. Pia ndege wana miguu miwili na mabawa mawili. Kuna ndege ambao huruka kwa mabawa na wengine hutembea kwa miguu.

Kuna aina zaidi ya elfu kumi za ndege duniani. Mbuni ndiye ndege mkubwa zaidi duniani. Yeye hutaga mayai makubwa na hukimbia kwa kasi zaidi, kama mwendo wa gari.

Ndege mdogo zaidi ni ndege mvumaji. Urefu wake ni inchi mbili na ana uzito wa gramu ishirini. Cha kushangaza ni kuwa ndege huyu ana uwezo wa kuruka kinyumenyume.

Kuku ndiye ndege anayepatikana sehemu nyingi za dunia. Ndege hula vyakula tofauti kama vile: nafaka, mbegu, matunda na wadudu wa kila aina. Kila mwaka, zaidi ya asilimia ishirini ya ndege huhama kutoka sehemu moja hadi nyingine.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nde** na **ge** kuandika: neno **ndege**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika maneno ubaoni kisha yasome na kueleza jinsi yanavyobadilika kwa wakati. N/T/U:

| | wakati uliopita -li | | wakati uliopo -na | | wakati ujao -ta |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | a**li**fanana | - | a**na**fanana | - | a**ta**fanana |
| 2. | a**li**zuru | - | a**na**zuru | - | a**ta**zuru |
| 3. | a**li**taga | - | a**na**taga | - | a**ta**taga |
| 4. | a**li**kimbia | - | a**na**kimbia | - | a**ta**kimbia |
| 5. | a**li**hama | - | a**na**hama | - | a**ta**hama |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 75**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **viumbe, kasi** na **gramu**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Ndege"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ndege ni viumbe wa aina gani? (ndege ni viumbe ambao hutaga mayai, wana miguu miwili, ndege ni viumbe wenye manyoya/mabawa)*
2. *Ndege hula nini? (nafaka, mbegu, matunda na wadudu mbalimbali)*
3. *Je, ndege ana manufaa gani kwa binadamu? (hutupatia chakula, nyama, mayai)*
4. *Taja majina ya ndege unaowajua. (Majibu yanaweza kujumuisha: kuku, bata, mbuni, heroe n.k.)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **nyuni, msitu, tausi, kanga, maganda, kima, nyoka, mnyama, sokwe, flamingo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 15: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2

## Maumbo

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma u mbo | pe mbe ta tu | du a ra du fu |
| **maumbo** | **pembetatu** | **duaradufu** |
| du a ra | m s ta ti li | m ra ba |
| **duara** | **mstatili** | **mraba** |

Aina ya maumbo




Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ya na pendeza | hu onekana |
| **yanapendeza** | **huonekana** |
| ya na staajabisha | zi ki meta meta |
| **yanastaajabisha** | **zikimetameta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| Maumbo haya ya**na**pendeza | - Maumbo yale ya**li**pendeza. |
| Maumbo haya ya**na**staajabisha | - Maumbo yale ya**li**staajabisha. |
| Maumbo haya ya**na**patikana | - Maumbo yale ya**li**patikana. |
| Maumbo haya ya**na**metameta | - Maumbo yale ya**li**metameta. |

76

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2

## Maumbo



### Maumbo

Maumbo yako kila mahali. Maumbo mengine yanapendeza na mengine yanastaajabisha. Zawadi inaweza kuwekwa katika sanduku lenye umbo la mraba. Tairi za baiskeli yangu na magurudumu ya gari ni ya umbo la duara. Meza na mlango wetu una umbo la mstatili. Mayai nayo yana umbo la duaradufu. Baadhi ya pakiti za maziwa zina umbo la pembetatu. Nyota ambazo huonekana usiku zikimetameta huwa na pembe nyingi.

77

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **maumbo** ubaoni. Tamka silabi **ma u mbo** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **maumbo**. **[U]** Endelea na maneno: **duara, pembetatu, mstatili, duaradufu, mraba. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 76.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mstatili, duaradufu** na **yanastaajabisha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Maumbo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Maumbo hupatikana wapi? (kila mahali)*
2. *Taja mfano wa umbo la mraba ambao umetolewa kwenye hadithi. (kisanduku/kisanduku cha zawadi)*
3. *Umbo la pembe tatu linaweza kupatikana wapi katika hadithi? (pakiti za maziwa)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno yafuatayo mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika kwenye madaftari yao: **mraba, baiskeli, duara, pembetatu, mstatili, duaradufu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 16: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Iwapo kuna wanafunzi wasioweza kujibu maswali ya ufahamu, waelekeze kwenye mbinu zitakazowapatia jibu kwa urahisi. Usiwapatie jibu papo hapo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 — **Maumbo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma u mbo | pe mbe ta tu | du a ra du fu |
| **maumbo** | **pembetatu** | **duaradufu** |
| du a ra | m s ta ti li | m ra ba |
| **duara** | **mstatili** | **mraba** |

Aina ya maumbo




Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ya na pendeza | hu onekana |
| **yanapendeza** | **huonekana** |
| ya na staajabisha | zi ki meta meta |
| **yanastaajabisha** | **zikimetameta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo** | **Wakati uliopita** |
|---|---|
| Maumbo haya ya**na**pendeza | - Maumbo yale ya**li**pendeza. |
| Maumbo haya ya**na**staajabisha | - Maumbo yale ya**li**staajabisha. |
| Maumbo haya ya**na**patikana | - Maumbo yale ya**li**patikana. |
| Maumbo haya ya**na**metameta | - Maumbo yale ya**li**metameta. |

76

Wiki ya 16: Siku ya 1 na 2 — **Maumbo**



Maumbo

Maumbo yako kila mahali. Maumbo mengine yanapendeza na mengine yanastaajabisha. Zawadi inaweza kuwekwa katika sanduku lenye umbo la mraba. Tairi za baiskeli yangu na magurudumu ya gari ni ya umbo la duara. Meza na mlango wetu una umbo la mstatili. Mayai nayo yana umbo la duaradufu. Baadhi ya pakiti za maziwa zina umbo la pembetatu. Nyota ambazo huonekana usiku zikimetameta huwa na pembe nyingi.

77

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **yanapendeza** ubaoni. Tamka sehemu za neno **ya na pendeza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **yanapendeza**. N/T/U: Endelea na maneno: **ya na staajabisha (yanastaajabisha), hu onekana (huonekana), ziki metameta (zikimetameta.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 76**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika nyakati mbalimbali.

| **Wakati uliopo** | | **Wakati uliopita** |
|---|---|---|
| Maumbo haya ya**na**pendeza | - | Maumbo yale ya**li**pendeza. |
| Maumbo haya ya**na**staajabisha | - | Maumbo yale ya**li**staajabisha. |
| Maumbo haya ya**na**patikana | - | Maumbo yale ya**li**patikana. |
| Maumbo haya ya**na**metameta | - | Maumbo yale ya**li**metameta. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 76**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mstatili, duaradufu** na **yanastaajabisha**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Maumbo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, sanduku la umbo la mraba linaweza kutumika kwa njia gani? (kuweka nguo na mavazi, vitabu n.k.)*
2. *Taja vitu vilivyo darasani ambavyo vina umbo la msatatili. (meza, mlango, dirisha, dawati n.k.)*
3. *Je, ni vitu gani unavyovijua ambavyo vina umbo la duara? (bakuli, sahani, tairi ya gari n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

1. **Maumbo haya yanapendeza - Maumbo yale yanapendeza.**
2. **Maumbo haya yanastaajabisha - Maumbo yale yalistaajabisha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 16: Siku ya 2*

Tarehe: ______________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 16: Siku ya 3

Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4 **Maumbo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m cho ro<br>**mchoro** | m ra ba<br>**mraba** | ke nge le<br>**kengele** |
| m vi ri ngo<br>**mviringo** | sa mbu sa<br>**sambusa** | sa ha ni<br>**sahani** |
| m s ta ti li<br>**mstatili** | wa cho re<br>**wachore** | mwa li mu<br>**mwalimu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa li vi kusanya<br>**walivikusanya** | a li wa ambia<br>**aliwaambia** |
| a li wa chorea<br>**aliwachorea** | a li tangulia<br>**alitangulia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita -li** | | **wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Wa**li**chora picha | - | Wa**ta**chora picha. |
| Wa**li**kuwa nyumbani | - | Wa**ta**kuwa nyumbani. |
| A**li**weka bakuli | - | A**ta**weka bakuli. |
| A**li**tangulia kanisani | - | A**ta**tangulia kanisani. |

78

Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4 **Maumbo**



**Kuchora maumbo**

Asubuhi, wanafunzi wa darasa la pili walichora maumbo. Mwalimu aliwaambia wachore sahani. Chini ya mchoro huu wakaandika neno mviringo. Tena aliwaambia wachore kitabu ambacho pande zote ni sawa kwa urefu. Chini ya mchoro huu waliandika neno mraba. Mchoro wa tatu ulikuwa wa meza. Chini ya mchoro huu mwalimu aliandika neno mstatili. Kisha aliwaambia wachore yai. Chini ya mchoro waliandika neno duaradufu. Mwishowe aliwaambia wanafunzi wachore sambusa. Wanafunzi walishangaa, "Sambusa?" Mwalimu aliwachorea sambusa kwenye ubao. Chini ya mchoro huu aliandika neno pembetatu.

79

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mchoro** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **m cho ro** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mchoro**. **[U]** Endelea na maneno: **mviringo, mraba, sambusa, kengele, sahani.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 78**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mviringo, samosa** na **amewaahidi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma shairi la "**Kuchora maumbo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mwalimu alikuwa amewaahidi wanafunzi nini? (aliwaahidi kuchora maumbo)*
2. *Wanafunzi walichora maumbo gani? (mviringo, mraba, mstatili, duaradufu na pembe tatu)*
3. *Yai lina umbo gani? (duara dufu)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mwalimu amesimama darasani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 16: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha umejiandaa vyema kabla ya kuenda darasani. Panga kadi za herufi utakapozitumia kwa mfuko wa herufi kabla ya kuanza kufunza. Hii itasaidia kukomboa wakati.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4** — **Maumbo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m cho ro<br>**mchoro** | m ra ba<br>**mraba** | ke nge le<br>**kengele** |
| m vi ri ngo<br>**mviringo** | sa mbu sa<br>**sambusa** | sa ha ni<br>**sahani** |
| m s ta ti li<br>**mstatili** | wa cho re<br>**wachore** | mwa li mu<br>**mwalimu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★ wa li vi kusanya — **walivikusanya**
a li wa ambia — **aliwaambia**
a li wa chorea — **aliwachorea**
a li tangulia — **alitangulia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita -li** | | **wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Wa**li**chora picha | - | Wa**ta**chora picha. |
| Wa**li**kuwa nyumbani | - | Wa**ta**kuwa nyumbani. |
| A**li**weka bakuli | - | A**ta**weka bakuli. |
| A**li**tangulia kanisani | - | A**ta**tangulia kanisani. |

78

**Wiki ya 16: Siku ya 3 na 4** — **Maumbo**



**Kuchora maumbo**

Asubuhi, wanafunzi wa darasa la pili walichora maumbo. Mwalimu aliwaambia wachore sahani. Chini ya mchoro huu wakaandika neno mviringo. Tena aliwaambia wachore kitabu ambacho pande zote ni sawa kwa urefu. Chini ya mchoro huu waliandika neno mraba. Mchoro wa tatu ulikuwa wa meza. Chini ya mchoro huu mwalimu aliandika neno mstatili. Kisha aliwaambia wachore yai. Chini ya mchoro waliandika neno duaradufu. Mwishowe aliwaambia wanafunzi wachore sambusa. Wanafunzi walishangaa, "Sambusa?" Mwalimu aliwachorea sambusa kwenye ubao. Chini ya mchoro huu aliandika neno pembetatu.

79

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **walivikusanya** ubaoni. N/T/U: Tamka sehemu za neno **wa li vi kusanya** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **walivikusanya** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **a li wa chorea (aliwachorea), a li wa ambia (aliwaambia), a li tangulia (alitangulia.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 78**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika nyakati mbalimbali.

| **Wakati uliopita -li** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Wa**li**chora picha | - | Wa**ta**chora picha. |
| Wa**li**kuwa nyumbani | - | Wa**ta**kuwa nyumbani. |
| A**li**weka bakuli | - | A**ta**weka bakuli. |
| A**li**tangulia kanisani | - | A**ta**tangulia kanisani. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 78**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mviringo, samosa** na **amewaahidi**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Kuchora Maumbo"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni vitu gani vingine ambavyo vina umbo la mviringo? (chini ya kikombe, sufuria n.k.)*
2. *Angalia darasani kisha utambue maumbo mbalimbali. (wanafunzi watambue maumbo mbalimbali)*
3. *Ni maumbo gani ambayo hukupendeza sana? (eleza jibu lako)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **walichora, watakuwa, aliweka, atatangulia**. Tumia neno **walichora** kuunda sentensi. Waulize wanafunzi kutumia maneno yaliyosalia kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 16: Siku ya 4*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 16: Siku ya 5 **Maumbo**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **du a ra - duara**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| m | a | ta | fu | pe |
| du | sta | ra | li | za |
| ka | mbe | ti | tu | du |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na-** | | **Wakati ujao -ta-** |
|---|---|---|
| Waimbaji wa**na**cheka | - | Waimbaji wa**ta**cheka. |
| Wavuvi wa**na**msalimia | - | Wavuvi wa**ta**msalimia. |
| Waumini wa**na**enda | - | Waumini wa**ta**enda. |

Vitendawili

1. Kafunua jicho jekundu.
2. Tunamsikia lakini hatumwoni.
3. Paarrrr hadi Meka.
4. Ndege wangu abembea mlingotini.
5. Mwanangu analia mwituni.
6. Popote niendapo hunifuata.
7. Dadangu akitoka kwao harudi tena.
8. Mchana yuko usiku simwoni.
9. Chang'aa chapendeza lakini hakifikiwi.
10. Kamba ndefu lakini haifungi kuni.
11. Mzee kobe akilia watu hufurahi.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kivuli | shoka | mvua | barabara | upepo | utelezi |
| kivuli | jua | upinde wa mvua | maji ya mvua | bendera | |

80

## Mada ya angani na mazingirani

1. Kafunua jicho jekundu. (jua)
2. Tunamsikia lakini hatumwoni. (upepo)
3. Paarrrr hadi Meka. (utelezi)
4. Ndege wangu abembea mlingotini. (bendera)
5. Mwanangu analia mwituni. (shoka)
6. Popote niendapo hunifuata. (kivuli)
7. Dadangu akitoka kwao harudi tena. (maji ya mvua)
8. Mchana yuko usiku simwoni. (kivuli)
9. Chang'aa chapendeza lakini hakifikiwi. (upinde wa mvua)
10. Kamba ndefu lakini haifungi kuni. (barabara)
11. Mzee kobe akilia watu hufurahi. (mvua)

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **du, a** na **ra** kuandika: neno **duara**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni kisha yasome na kueleza jinsi yanavyobadilika kulingana na wakati. N/T/U**:**

| **Wakati uliopo -na-** | | **Wakati ujao -ta-** |
|---|---|---|
| Waimbaji wa**na**cheka | - | Waimbaji wa**ta**cheka. |
| Wavuvi wa**na**msalimia | - | Wavuvi wa**ta**msalimia. |
| Waumini wa**na**enda | - | Waumini wa**ta**enda. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 80**.

### Vitendawili

**[N]** Sema neno **kitendawili** mara mbili huku wanafunzi wakijibu tega. Tega kitendawili. (Kwa mfano, **kuku wangu hutagia miibani**? Mwalimu achague mwanafunzi mmoja ategue kitendawili.

Mwanafunzi akitegua atumie hatua ya kwanza kutega kitendawili kingine. Wanafunzi wakishindwa kukitegua kitendawili, mwalimu awaombe mji. Akipewa mji aseme "niliendа (jina la mji) watoto wa mji huo wakanituma nije niwasalimie. Mmepokea salamu zao? jibu ni **nanasi.**

Mwalimu atege vitendawili vitano kutumia maagizo haya.

Wape wanafunzi nafasi ya kutega vitendawili vyao kwa kutumia mtindo huu.

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **maumbo, vipawa, yanastaajabisha, kuzidisha, kumsalimia, watachora, kusawazisha, alitangulia, vilivyozidisha**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 16: Siku ya 5*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza huu mwaka. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 — **Usafi na afya**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ha ta ri | ma tu mbo | m du du |
| **hatari** | **matumbo** | **mdudu** |
| ho ma | ki nga | u cha fu |
| **homa** | **kinga** | **uchafu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| a na po ishi | ki na po bakia |
| **anapoishi** | **kinapobakia** |
| ya na yo letwa | wa si ki chafue |
| **yanayoletwa** | **wasikichafue** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Ch**akula cha Ali ni **ki**chafu | - | **Vy**akula vya Ali ni **vi**chafu. |
| Nekesa ana **ch**akula safi | - | Nekesa ana **vy**akula safi. |
| Otieno anakula **ch**akula **ki**tamu | - | Otieno anakula **vy**akula **vi**tamu. |
| Juma alitupa **ch**akula **ki**baya | - | Juma alitupa **vy**akula **vi**baya. |

81

Wiki ya 17: Siku ya 1 na 2 — **Usafi na afya**



### Nzi

Nzi ni mdudu hatari sana kwa maisha ya binadamu. Mdudu huyu hupenda uchafu sana. Yeye husababisha magonjwa kama vile kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Kwa hivyo ni muhimu kila mtu ahakikishe kuwa mahali anapoishi ni safi. Kinga ni bora kuliko tiba. Kwa hivyo ni bora kujikinga kutokana na magonjwa yanayoletwa na nzi. Nyumbani na shuleni pia ni lazima kuwe safi. Chakula kinapobakia ni muhimu kifunikwe ili nzi wasikichafue.

82

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **hatari** ubaoni. Tamka silabi **ha ta** na **ri** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno upesi **hatari**. **[U]** Endelea na maneno: **homa, matumbo, kinga, mdudu, uchafu. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 81.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno: **hatari, husababisha, kinga**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **Nzi** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, nzi ni hatari sana kwa maisha ya nani? (mwanadamu)*
2. *Nzi hupenda nini? (uchafu, sehemu chafu)*
3. *Ni magonjwa gani huletwa na nzi? (kipindupindu na magonjwa ya kuhara)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **hatari, husababisha, kinga, ahakikishe, tiba.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 17: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kuandika herufi ubaoni, hakikisha usiandike hivi: **/e/** au **/sh/**, lakini uziandike hivi: **e** au **sh**.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ha ta ri | ma tu mbo | m du du |
| **hatari** | **matumbo** | **mdudu** |
| ho ma | ki nga | u cha fu |
| **homa** | **kinga** | **uchafu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| a na po ishi | ki na po bakia |
| **anapoishi** | **kinapobakia** |
| ya na yo letwa | wa si ki chafue |
| **yanayoletwa** | **wasikichafue** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Ch**akula cha Ali ni **ki**chafu | - | **Vy**akula vya Ali ni **vi**chafu. |
| Nekesa ana **ch**akula safi | - | Nekesa ana **vy**akula safi. |
| Otieno anakula **ch**akula **ki**tamu | - | Otieno anakula **vy**akula **vi**tamu. |
| Juma alitupa **ch**akula **ki**baya | - | Juma alitupa **vy**akula **vi**baya. |







Nzi

Nzi ni mdudu hatari sana kwa maisha ya binadamu. Mdudu huyu hupenda uchafu sana. Yeye husababisha magonjwa kama vile kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Kwa hivyo ni muhimu kila mtu ahakikishe kuwa mahali anapoishi ni safi. Kinga ni bora kuliko tiba. Kwa hivyo ni bora kujikinga kutokana na magonjwa yanayoletwa na nzi. Nyumbani na shuleni pia ni lazima kuwe safi. Chakula kinapobakia ni muhimu kifunikwe ili nzi wasikichafue.



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **anapoishi** ubaoni. Tamka sehemu za neno **a na po ishi** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **anapoishi** kwa upesi. **[U].** Endelea na maneno: **ya na yo letwa (yanayoletwa), ki na po bakia (kinapobakia), wa si ki chafue (wasikichafue.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 81**.

### ◆ Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U. Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Ch**akula cha Ali ni **ki**chafu | - | **Vya**kula vya Ali ni **vi**chafu |
| Nekesa ana **ch**akula safi | - | Nekesa ana **vya**kula safi |
| Otieno anakula **ch**akula **ki**tamu | - | Otieno anakula **vya**kula **vi**tamu |
| Juma alitupa **ch**akula **ki**baya | - | Juma alitupa **vya**kula **vi**baya |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 81**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno: **hatari, husababisha, ahakikishe, kinga, tiba**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Nzi** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, unafikiri nzi ni rafiki au adui? (wanafunzi wajibu na kueleza sababu zao)*
2. *Tunaweza kujikinga vipi kutoka kwa magonjwa yanayoletwa na nzi? (kudumisha usafi, kunawa mikono n.k.)*
3. *Je, unafikiri nzi hupatikana wapi? (chooni, nyumbani n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

| | | |
|---|---|---|
| 1. **Chakula changu ni chafu** | - | **Vyakula vyetu ni chafu.** |
| 2. **Hiki ni chakula kibaya** | - | **Hivi ni vyakula vibaya.** |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 17: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 — **Usafi na afya**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m sa la ni<br>**msalani** | ha ru fu<br>**harufu** | vi o shwe<br>**vioshwe** |
| u sa fi<br>**usafi** | ku du mi sha<br>**kudumisha** | vyo o<br>**vyoo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li tu tembelea<br>**alitutembelea** | wa li m tambua<br>**walimtambua** |
| tu li m karibisha<br>**tulimkaribisha** | ku wa shauri<br>**kuwashauri** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Kamau **ameketi** | - | Kamau **amesimama**. |
| **Kuja hapa** | - | **Enda pale**. |
| Kendi **amevaa** sweta | - | Kendi **amevua** sweta. |
| Kikombe kiko **chini ya** meza | - | Kikombe kiko **juu ya** meza. |
| Nyumba hii ni **safi** | - | Nyumba hii ni **chafu**. |
| Dengu hizi ni **chache** | - | Dengu hizi ni **nyingi**. |

83

Wiki ya 17: Siku ya 3 na 4 — **Usafi na afya**



**Mama Safi shuleni**

Mama Safi alitutembelea shuleni Bondeni. Tulimkaribisha kwa furaha. Alipoketi chini, sherehe ikaanza. Mama Safi alihisi furaha sana. Bila kusema jina lake, watu walimtambua kwa sababu ya mavazi yake. Alipopewa nafasi kuihutubia halaiki alisema, "Mwalimu Mkuu, Bwana Bakari, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nimekuja kuwashauri kuhusu usafi wa vyoo vyetu. Shuleni au nyumbani, vyoo ni lazima vioshwe vizuri kila siku. Njia moja ya kudumisha usafi ni kuhakikisha kwamba vyoo havina harufu wala wadudu wabaya." Mama Safi alimalizia kwa kusema, "Mnapoenda msalani, ni muhimu mvae viatu. Pia ni lazima mnawe mikono kwa sabuni baada ya kuutumia msala. Mkifanya hivyo bila shaka mtakuwa na afya njema."

84

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **msalani** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **m sa la** na **ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno kwa upesi **msalani**. **[U]** Endelea na maneno: **usafi, harufu, kudumisha, vioshwe, vyoo.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 83**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno: **alihisi, walimtambua, halaiki.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Mama Safi shuleni** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Nani alitembelea shule ya Bondeni? (mama safi)*
2. *Mama safi alimalizia kwa kusema nini? (wavae viatu wanapoenda msalani, wanawe mikono kwa sabuni)*
3. *Mama safi alikuja shuleni kufanya nini? (alikuja kushauri kuhusu usafi wa vyoo)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi wandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Mama safi anawazungumzia wanafunzi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 17: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kabla ya wanafunzi kutabiri, hakikisha wamesoma kichwa cha hadithi, na kueleza wanachokiona kwenye picha iliyo kwenye hadithi.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

## Usafi na afya

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m sa la ni<br>**msalani** | ha ru fu<br>**harufu** | vi o shwe<br>**vioshwe** |
| u sa fi<br>**usafi** | ku du mi sha<br>**kudumisha** | vyo o<br>**vyoo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li tu tembelea<br>**alitutembelea** | wa li m tambua<br>**walimtambua** |
| tu li m karibisha<br>**tulimkaribisha** | ku wa shauri<br>**kuwashauri** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Kamau **ameketi** | - | Kamau **amesimama**. |
| **Kuja hapa** | - | **Enda pale**. |
| Kendi **amevaa** sweta | - | Kendi **amevua** sweta. |
| Kikombe kiko **chini ya** meza | - | Kikombe kiko **juu ya** meza. |
| Nyumba hii ni **safi** | - | Nyumba hii ni **chafu**. |
| Dengu hizi ni **chache** | - | Dengu hizi ni **nyingi**. |





## Usafi na afya



**Mama Safi shuleni**

Mama Safi alitutembelea shuleni Bondeni. Tulimkaribisha kwa furaha. Alipoketi chini, sherehe ikaanza. Mama Safi alihisi furaha sana. Bila kusema jina lake, watu walimtambua kwa sababu ya mavazi yake. Alipopewa nafasi kuihutubia halaiki alisema, "Mwalimu Mkuu, Bwana Bakari, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nimekuja kuwashauri kuhusu usafi wa vyoo vyetu. Shuleni au nyumbani, vyoo ni lazima vioshwe vizuri kila siku. Njia moja ya kudumisha usafi ni kuhakikisha kwamba vyoo havina harufu wala wadudu wabaya." Mama Safi alimalizia kwa kusema, "Mnapoenda msalani, ni muhimu mvae viatu. Pia ni lazima mnawe mikono kwa sabuni baada ya kuutumia msala. Mkifanya hivyo bila shaka mtakuwa na afya njema."



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **alitutembelea** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **a li tu tembelea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **alitutembelea** kwa upesi. **[U].** Endelea na maneno: **tu li m karibisha (tulimkaribisha), wa li m tambua (walimtambua), ku wa shauri (kuwashauri.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 83**.

### ◆ Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. Soma sentensi hizi. Soma na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Kamau **ameketi** | - | Kamau **amesimama.** |
| **Kuja hapa** | - | **Enda pale.** |
| Kendi **amevaa** sweta | - | Kendi **amevua** sweta. |
| Kikombe kiko **chini ya** meza | - | Kikombe kiko **juu ya** meza. |
| Nyumba hii ni **safi** | - | Nyumba hii ni **chafu.** |
| Dengu hizi ni **chache** | - | Dengu hizi ni **nyingi.** |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 83**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **alihisi, walimtambua, halaiki.**

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mama Safi shuleni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, kwa nini mgeni akaitwa mama safi? (kwa sababu alipenda usafi, hufundisha watu kuhusu usafi)*
2. *Kwa nini vyoo vinastahili kuwa visafi? (vyoo vichafu huleta wadudu/magonjwa, vyoo huwa na harufu mbaya)*
3. *Taja njia nyingine za kudumisha usafi. (kufagia, kukata nyasi, n.k.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **keti, enda, chini, chafu**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia neno **keti** kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 17: Siku ya 4*

Wiki ya 17: Siku ya 5 **Ndege na wanyama**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nya ni - nyani**

★


| | | | |
|---|---|---|---|
| mbo | ge | nya | bu |
| i | te | mba | ka |
| nde | m | si | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** / **Wingi**

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hiki ni **ki**atu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**atu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**atu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**atu **vye**nu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**nu. |

**Tembo asaidiwa**



85

## Tembo asaidiwa

Tembo aliumwa na mguu. Ndege alimuuliza, “Mbona umekaa? Una shida gani?” Tembo alijibu, “Mguu umeumia. Siwezi kutembea. Lakini ningetaka kukutana na binamu yangu. Nifanye nini?” Ndege alijibu, “ningekuwa mimi, ningepaa hadi kwa binamu.” Naye alipaa na kwenda.

Buibui asiyekuwa na mguu mmoja akaja. Tembo alimuuliza swali lile lile. Tembo alijibu vile vile. Buibui alijibu, “Ningekuwa mimi, ningetembea na miguu saba iliyobaki hadi kwa binamu yangu.” Naye alitambaa na kwenda zake.

Wa tatu kuja alikuwa Nyani. Alimuuliza, “Unaumwa?” Tembo alimuambia shida yake. Naye aliruka kwa mkia na kwenda.

Simba akaja. Alimuuliza, “Mbona umekaa?” Tembo alijibu, “Mguu wangu umeumia. Siwezi kumuona binamu. Nifanyeje.” Simba alijibu, “Ningekuwa mimi, ningepiga mayowe wanyama waje kunisaidia.”

Simba alinguruma. Wanyama wote wakaja. Waliamua kumtafuta binamu wa Tembo. Akaja pale kumwona Tembo.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **nya** na **ni** kuandika neno **nyani**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U. Soma sentensi hizi. Soma na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hiki ni **ki**atu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**atu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**atu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**atu **vye**nu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**nu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 85**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **binamu, alipaa, mayowe, alinguruma.** Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi **"Tembo asaidiwa"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Tembo aliumia wapi? (aliumia mguu)*
2. *Simba alimsaidia tembo vipi? (simba alinguruma, simba aliwaita wanyama)*
3. *Kwa nini Ndege alimshauri Tembo kupaa? (kwa sababu alifikiri tembo kama ndege angeweza kupaa)*
4. *Ungekuwa pale, wewe ungemshauri Tembo afanye nini? (aone daktari, aende apumzike, alale, n.k.)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **matumbo, kinga, kifua, kichwa, msalani, alipaa, tembelea, karibisha, mwituni, dhiki.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 17: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 18: Siku ya 1

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 — **Kazi mbalimbali**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma fu mbo | ho s pi ta li ni |
| **mafumbo** | **hospitalini** |
| m ku li ma | sha mba ni |
| **mkulima** | **shambani** |
| da k ta ri | se re ma la |
| **daktari** | **seremala** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na zo fanywa | wa li furahia |
| **zinazofanywa** | **walifurahia** |
| hu wa hudumia | ku tengeneza |
| **huwahudumia** | **kutengeneza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**enda sokoni | - | **Siku**enda sokoni. |
| **Nili**tumia sabuni | - | **Siku**tumia sabuni. |
| **Nili**uza makaa | - | **Siku**uza makaa. |
| **Nili**fanya kazi ya ziada | - | **Siku**fanya kazi ya ziada. |

86

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 — **Kazi mbalimbali**



**Mafumbo ya Kazi**

Yusufu, Owalo na Linda walisema mafumbo kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na watu. Yusufu aliuliza, “Mimi hupanda mimea kama mahindi na mboga shambani. Je, mimi ni nani?” Linda alijibu, “Mkulima.” Owalo naye aliuliza, “Mimi huwahudumia wagonjwa hospitalini. Je, mimi ni nani?” Yusufu alijibu, “Daktari.” Linda pia aliuliza, “Mjomba wangu hufanya kazi ya kutengeneza vitu kwa kutumia mbao. Je, yeye ni nani?” Yusufu na Owalo walijibu pamoja, “Fundi!” Linda alisema, “Mmenoa. Nipeni mji nitawapa jibu sahihi.” Yusufu alimpa mji wa Mombasa. Linda alisema, “Nilienda Mombasa, watu wa Mombasa wakasema jibu ni seremala.” Wote walifurahishwa na mafumbo hayo.

87

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mafumbo** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ma fu mbo** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mafumbo**. **[U]** Endelea na maneno: **mkulima, daktari, hospitalini, shambani, seremala. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 86**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mafumbo, sahihi** na **seremala**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mafumbo ya kazi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Watoto walisema vitendawili kuhusu nini? (kazi mbalimbali)*
2. *Mtu ambaye hupanda mimea anaitwa nani? (mkulima)*
3. *Ni kazi gani zingine zilizotajwa katika hadithi hii? (daktari, fundi, seremala)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mpishi, mgonjwa, daktari, askari, mhunzi, hospitali.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 18: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha wanafunzi wameongea na wenzao kuhusu utabiri kabla ya kuuliza wachache waelezee kuhusu utabiri.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 18: Siku ya 2

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 **Kazi mbalimbali**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma fu mbo | ho s pi ta li ni |
| **mafumbo** | **hospitalini** |
| m ku li ma | sha mba ni |
| **mkulima** | **shambani** |
| da k ta ri | se re ma la |
| **daktari** | **seremala** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na zo fanywa | wa li furahia |
| **zinazofanywa** | **walifurahia** |
| hu wa hudumia | ku tengeneza |
| **huwahudumia** | **kutengeneza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**enda sokoni | - | **Siku**enda sokoni. |
| **Nili**tumia sabuni | - | **Siku**tumia sabuni. |
| **Nili**uza makaa | - | **Siku**uza makaa. |
| **Nili**fanya kazi ya ziada | - | **Siku**fanya kazi ya ziada. |

86

Wiki ya 18: Siku ya 1 na 2 **Kazi mbalimbali**



**Mafumbo ya Kazi**

Yusufu, Owalo na Linda walisema mafumbo kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na watu. Yusufu aliuliza, "Mimi hupanda mimea kama mahindi na mboga shambani. Je, mimi ni nani?" Linda alijibu, "Mkulima." Owalo naye aliuliza, "Mimi huwahudumia wagonjwa hospitalini. Je, mimi ni nani?" Yusufu alijibu, "Daktari." Linda pia aliuliza, "Mjomba wangu hufanya kazi ya kutengeneza vitu kwa kutumia mbao. Je, yeye ni nani?" Yusufu na Owalo walijibu pamoja, "Fundi!" Linda alisema, "Mmenoa. Nipeni mji nitawapa jibu sahihi." Yusufu alimpa mji wa Mombasa. Linda alisema, "Nilienda Mombasa, watu wa Mombasa wakasema jibu ni seremala." Wote walifurahishwa na mafumbo hayo.

87

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **zinazofanywa** ubaoni. Tamka sehemu za neno **zi na zo fanywa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **zinazofanywa**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **hu wa hudumia (huwahudumia), wa li furahia (walifurahia), ku tengeneza (kutengeneza.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 86**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma sentensi hizi.

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**enda sokoni | - | **Siku**enda sokoni. |
| **Nili**tumia sabuni | - | **Siku**tumia sabuni. |
| **Nili**uza makaa | - | **Siku**uza makaa. |
| **Nili**fanya kazi ya ziada | - | **Siku**fanya Kazi ya ziada |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 86**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **vitendawili, sahihi** na **seremala**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **Mafumbo ya Kazi** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni watoto wangapi waliosema mafumbo? (watoto watatu)*
2. *Taja kazi nyingine ambazo watu hufanya. (mwashi, mwanahabari, mwalimu)*
3. *Sema mafumbo ambayo unayajua. (ongoza wanafunzi kusema vitendawili sahihi)*

**Kuandika**

Wape wanafunzi muda waandike sentensi katika hali ya kukanusha.

1. **Sikuenda madukani - Nilienda madukani.**
2. **Sikufanya makosa - Nilifanya makosa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 18: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 18: Siku ya 3

**Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4** — **Kazi mbalimbali**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku u za | ma kaa | ge si |
| **kuuza** | **makaa** | **gesi** |
| po li si | f ri ji | su fu ri a |
| **polisi** | **friji** | **sufuria** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ni li li nunua | a li wa pigia |
| **nililinunua** | **aliwapigia** |
| ku m kamata | a li shtuka |
| **kumkamata** | **alishtuka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita -li** | **wakati uliopo -na** |
|---|---|
| Mteja a**li**fanya hesabu | - Mteja a**na**fanya hesabu. |
| Msafiri a**li**fika dukani | - Msafiri a**na**fika dukani. |
| Muuzaji a**li**ibiwa na wezi | - Muuzaji a**na**ibiwa na wezi. |
| Mwanamke a**li**wapigia simu polisi | - Mwanamke a**na**wapigia simu polisi. |

88

**Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4** — **Kazi mbalimbali**



**Swaleh ashikwa na polisi**

Swaleh alifanya kazi ya kuuza vitu dukani. Duka lake lilikuwa na bidhaa mbalimbali. Kati ya vitu alivyouza ni viti vya kukalia au sofa, sufuria, pasi, jiko la makaa na friji. Siku moja Atieno alifika kwenye duka la Swaleh. Alishtuka kuliona jiko lake la gesi ambalo lilikuwa limeibwa siku chache zilizopita. Bila kupoteza wakati Atieno aliwapigia polisi simu. Polisi walifika mara moja na kumkamata Swaleh. Swaleh akajitetea kwa kusema, "Mimi sina makosa. Jiko hili nililinunua kutoka kwa mtu nisiyemjua."

89

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **kuuza** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ku u za** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kuuza**. **[U]** Endelea na maneno: **polisi, makaa, friji, gesi, sufuria.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 88**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **bidhaa, friji** na **pasi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Swaleh ashikwa na polisi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Swaleh alifanya kazi gani? (kazi ya kuuza vitu mbalimbali, muuza dukani)*
2. *Taja vitu ambavyo Swaleh aliuza dukani. (sofa, sufuria, pasi, jiko, friji)*
3. *Kwa nini Swaleh alishikwa na polisi? (aliuza vitu vya kuibwa, aliuza jiko la gesi lililoibwa)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Swaleh ameshikwa na polisi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 18: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Je, unakumbuka mpangilio wa "Ninafanya", "Tunafanya", "Unafanya" wakati wa kufunza somo la kusoma?

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 — **Kazi mbalimbali**

Soma silabi na maneno.

| ku u za | ma kaa | ge si |
|---|---|---|
| **kuuza** | **makaa** | **gesi** |
| po li si | f ri ji | su fu ri a |
| **polisi** | **friji** | **sufuria** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| ni li li nunua | a li wa pigia |
|---|---|
| **nililinunua** | **aliwapigia** |
| ku m kamata | a li shtuka |
| **kumkamata** | **alishtuka** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **wakati uliopita -li** | **wakati uliopo -na** |
|---|---|
| Mteja a**li**fanya hesabu | - Mteja a**na**fanya hesabu. |
| Msafiri a**li**fika dukani | - Msafiri a**na**fika dukani. |
| Muuzaji a**li**ibiwa na wezi | - Muuzaji a**na**ibiwa na wezi. |
| Mwanamke a**li**wapigia simu polisi | - Mwanamke a**na**wapigia simu polisi. |

88

Wiki ya 18: Siku ya 3 na 4 — **Kazi mbalimbali**



Swaleh ashikwa na polisi

Swaleh alifanya kazi ya kuuza vitu dukani. Duka lake lilikuwa na bidhaa mbalimbali. Kati ya vitu alivyouza ni viti vya kukalia au sofa, sufuria, pasi, jiko la makaa na friji. Siku moja Atieno alifika kwenye duka la Swaleh. Alishtuka kuliona jiko lake la gesi ambalo lilikuwa limeibwa siku chache zilizopita. Bila kupoteza wakati Atieno aliwapigia polisi simu. Polisi walifika mara moja na kumkamata Swaleh. Swaleh akajitetea kwa kusema, "Mimi sina makosa. Jiko hili nililinunua kutoka kwa mtu nisiyemjua."

89

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **nilinunua** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **ni li nunua** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **nilinunua** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **ku m kamata (kumkamata), a li wa pigia (aliwapigia), a li shtuka (alishtuka.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 88**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopita -li** | | **Wakati uliopo -na** |
|---|---|---|
| Mteja a**li**fanya hesabu | - | Mteja a**na**fanya hesabu. |
| Msafiri a**li**fika dukani | - | Msafiri a**na**fika dukani. |
| Muuzaji a**li**ibiwa na wezi | - | Muuzaji a**na**ibiwa na wezi. |
| Mwanamke a**li**wapigia polisi | - | Mwanamke a**na**wapigia polisi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 88**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **bidhaa, friji** na **pasi**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Swaleh ashikwa na polisi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ukipata vitu ambavyo si vyako utafanya nini? (nitampelekea mwalimu, nitapeleka kwa chifu n.k.)*
2. *Je, polisi hufanya kazi gani? (kushika watu, kulinda watu n.k.)*
3. *Je, utakapokuwa mtu mzima, ungependa kufanya kazi gani? (waeleze kazi mbalimbali na sababu zao)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia maneno: **alifanya, anafika, aliibiwa, ananunua** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 18: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wanafunzi wanaposoma, tembea darasani ndio uweze kujua wale hawajui kusoma. Utawasaidia hawa wanafunzi kusoma.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 18: Siku ya 5 **Kazi mbalimbali**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **de re va - dereva**

★


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| la | ma | hu | si | nzi | se |
| ndi | na | re | pi | de | ku |
| fu | li | su | m | shi | va |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Sentensi** — **Kukanusha**

**Nili**fanya kazi zote - **Siku**fanya kazi zote.
**Nili**pika chai - **Siku**pika chai.
**Nili**wahudumia wagonjwa - **Siku**wahudumia wagonjwa.
**Nili**wapigia simu - **Siku**wapigia simu.

Fundi Mukundi



90

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **de, re** na **va** kuandika: neno **dereva**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome. N/T/U: Soma na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**fanya kazi zote | - | **Siku**fanya kazi zote. |
| **Nili**pika chai | - | **Siku**pika chai. |
| **Nili**wahudumia wagojwa | - | **Siku**wahudumia wagojwa. |
| **Nili**wapigia simu | - | **Siku**wapigia simu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 90**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **magurudumu, umbo** na **hodari**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Uliza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Fundi Mukundi"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Mukundi alitumia nini kutengeneza gari lake? (miti)*
2. *Taja maumbo ya gurudumu aliyotengeneza Mukundi. (pembetatu, mraba, duara)*
3. *Ni umbo gani lilimsaidia Mukundi? (duara)*
4. *Taja maumbo ambayo yanaonekana kwa vitu ambavyo viko darasani. (mlango- umbo la mstatili, ubao- umbo la mraba n.k..)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **polisi, jitu, malkia, sufuria, mwalimu, hospitali, vitendawili, mlinzi, daktari, mfalme.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 18: Siku ya 5*

## Fundi Mukundi

Siku moja fundi Mukundi alienda kubeba mawe akitumia  gari la kujitengenezea la miti. Akaweka mawe mengi sana kwenye gari. Aliamua kulifunga gari lile kwa kamba kisha akavuta, akavuta hadi kamba ikakatika.

Mara akaona kuwa gari lake halikuwa na magurudumu. Akachonga magurudumu mawili yenye umbo la pembe tatu na kuyafunga kwenye gari lake. Kisha akavuta na kuvuta lakini wapi, kamba ikakatika.

Akafikiria tena. Akachonga magurudumu mawili yenye umbo la mraba na kuyafunga kwenye gari lake. Kisha akavuta na kuvuta, lakini wapi, kamba ikakatika tena.

Akaamua kuchonga magurudumu mawili ya umbo la duara na kuyafunga kwenye gari lake. Akafunga kamba tena. Alipovuta, gari lake likaanza kwenda bila shida.

Wana Kijiji walipoona hivyo wakapendezwa sana. Tangu siku hiyo Fundi Mukundi akawa fundi hodari wa magari.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 **Miezi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| A go s ti | O k to ba | De se mba |
| **Agosti** | **Oktoba** | **Desemba** |
| Fe b ru a ri | Ja nu a ri | Se p te mba |
| **Februari** | **Januari** | **Septemba** |
| A p ri li | Ju ni | Ju la i |
| **Aprili** | **Juni** | **Julai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| hu tu karibisha | hu ni furahisha |
| **hutukaribisha** | **hunifurahisha** |
| tu na agana | hu zingatia |
| **tunaagana** | **huzingatia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **m**waka **m**moja | - | **mi**aka **mi**wili |
| **m**wezi **m**moja | - | **mi**ezi **mi**wili |
| **m**uhula **m**moja | - | **mi**hula **mi**wili |
| **m**tihani **m**moja | - | **mi**tihani **mi**wili |
| **m**wili **m**moja | - | **mi**ili **mi**wili |

91

Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2 **Miezi**



### Miezi ya mwaka

Mwaka mmoja huwa na miezi kumi na miwili. Januari hutukaribisha shuleni. Februari na Machi ni kucheza na kuendelea kujuana na wenzetu. Aprili hunitia woga kwani tunaagana na marafiki zangu. Mei, Juni na Julai hunifurahisha. Huwa ni miezi ya kukutana na marafiki zangu tena. Hadithi za likizo nazo huwa nyingi. Agosti mimi hurudi nyumbani kungojea Septemba. Oktoba mimi huzingatia masomo kwani Novemba mtihani waningojea. Desemba mimi hupungia darasa mkono wa buriani kwani nasonga mbele.

92

■ **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **Agosti** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **A go s ti** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Agosti**. **[U]** Endelea na maneno: **Februari, Oktoba, Januari, Desemba, Septemba, Juni, Julai, Aprili**.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 91**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hutukaribisha, woga, kuagana** na **mkono wa buriani**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Miezi ya mwaka"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mwaka mmoja huwa na miezi mingapi? (kumi na miwili)*
2. *Kwa nini Aprili hunitia woga? (kwa sababu tunaondoka na kuagana na marafiki)*
3. *Mimi hufanya kazi gani katika mwezi wa Novemba? (hufanya mtihani)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **Januari, Aprili, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 19: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kumbuka kufanya utabiri na wanafunzi Siku ya kwanza, ya tatu na ya tano pekee. Hakuna utabiri: Siku ya 2 na ya 4. Wanafunzi watarejelea msamiati.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2** **Miezi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| A go s ti | O k to ba | De se mba |
| **Agosti** | **Oktoba** | **Desemba** |
| Fe b ru a ri | Ja nu a ri | Se p te mba |
| **Februari** | **Januari** | **Septemba** |
| A p ri li | Ju ni | Ju la i |
| **Aprili** | **Juni** | **Julai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| hu tu karibisha | hu ni furahisha |
| **hutukaribisha** | **hunifurahisha** |
| tu na agana | hu zingatia |
| **tunaagana** | **huzingatia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **m**waka **m**moja | - | **mi**aka **mi**wili |
| **m**wezi **m**moja | - | **mi**ezi **mi**wili |
| **m**uhula **m**moja | - | **mi**hula **mi**wili |
| **m**tihani **m**moja | - | **mi**tihani **mi**wili |
| **m**wili **m**moja | - | **mi**ili **mi**wili |

91

**Wiki ya 19: Siku ya 1 na 2** **Miezi**



**Miezi ya mwaka**

Mwaka mmoja huwa na miezi kumi na miwili. Januari hutukaribisha shuleni. Februari na Machi ni kucheza na kuendelea kujuana na wenzetu. Aprili hunitia woga kwani tunaagana na marafiki zangu. Mei, Juni na Julai hunifurahisha. Huwa ni miezi ya kukutana na marafiki zangu tena. Hadithi za likizo nazo huwa nyingi. Agosti mimi hurudi nyumbani kungojea Septemba. Oktoba mimi huzingatia masomo kwani Novemba mtihani waningojea. Desemba mimi hupungia darasa mkono wa buriani kwani nasonga mbele.

92

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **hutukaribisha** ubaoni. Tamka sehemu za neno **hu tu karibisha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **hutukaribisha**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **tu na agana (tunaagana), hu ni furahisha (hunifurahisha), hu zingatia (huzingatia.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 91**.

◆ **Sarufi**

Andika maneno yafuatayo ubaoni. N/T/U: Soma maneno hayo.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **m**waka **m**moja | - | **mi**aka **mi**wili |
| **M**wezi **m**moja | - | **mi**ezi **mi**wili |
| **M**uhula **m**moja | - | **mi**hula **mi**wili |
| **M**tihani **m**moja | - | **mi**tihani **mi**wili |
| **m**wili **m**moja | - | **mi**ili **mi**wili |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 91**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **woga, tunaagana** na **mkono wa buriani**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Miezi ya mwaka"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Shule yetu hufungwa na kuelekea likizoni miezi ipi? (Aprili, Agosti na Desemba)*
2. *Eleza kazi ambazo unazifanya wakati wa likizo. (kulima, kusaidia wazazi, kuchunga mbuzi/ng'ombe n.k.)*
3. *Je, wewe ulizaliwa mwezi gani? (watoto wataje mwezi waliozaliwa)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

1. **Nimesoma darasa hili mwaka mmoja.**
2. **Baba alienda kazi miezi miwili.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 19: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 19: Siku ya 3

Wiki ya 19: Siku ya 3 na 4 **Miezi**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma va zi | vi nywa ji |
| **mavazi** | **vinywaji** |
| Wa k ri s to | ma chu ngwa |
| **Wakristo** | **machungwa** |
| i shi ri ni | she re he |
| **ishirini** | **sherehe** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu na po karibia | hu ni nunulia |
| **tunapokaribia** | **huninunulia** |
| hu kumbukwa | hu tu peleka |
| **hukumbukwa** | **hutupeleka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

**Kuakifisha**

Hiki ni kinywaji kitamu.

Kwa nini kinywaji ni kitamu?

Kwa nini kikombe kilivunjika?

Kikombe kilivunjika.

93

Wiki ya 19: Siku ya 3 na 4 **Miezi**



Mwezi wa Disemba

Naupenda mwezi wa Disemba. Mwezi huu hukumbukwa na Wakristo kote duniani. Ni mwezi wa kukumbuka siku ya Yesu Kristo kuzaliwa.Tunapokaribia Disemba wazazi wangu huninunulia mavazi mazuri. Baba hutupeleka kutembelea miji mbalimbali. Tarehe ishirini na tano, sisi hupika vyakula vitamu kama vile chapati, wali, kuku na nyama. Baada ya kuvila sisi huviteremsha kwa vinywaji kama soda na maji ya machungwa. Sherehe hizi huwa za kufana sana.

94

■ **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **mavazi** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ma va** na **zi** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mavazi**. **[U]** Endelea na maneno: **wakristo, ishirini, vinywaji, machungwa, sherehe.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 93**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wakristo, vinywaji** na **kufana**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Mwezi wa Desemba"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. N/T/U Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ninaupenda mwezi gani? (mwezi wa Desemba/mwezi wa kumi na mbili)*
2. *Kwa nini Wakristo hukumbuka mwezi wa Desemba? (ni mwezi wa Krismasi, ni mwezi aliozaliwa Yesu)*
3. *Ni mambo gani ambayo sisi hufanya tarehe ishirini na tano? (hupika vyakula, hula chakula, hunywa vinywaji)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Jiji la Mombasa lina pembe za ndovu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 19: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kabla ya kusoma hadithi mwalimu huzungumza kuhusu msamiati, husoma kichwa cha hadithi, huzungumza kuhusu picha na wanafunzi hatimaye hutoa utabiri.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ma va zi | vi nywa ji |
| **mavazi** | **vinywaji** |
| Wa k ri s to | ma chu ngwa |
| **Wakristo** | **machungwa** |
| i shi ri ni | she re he |
| **ishirini** | **sherehe** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ★ tu na po karibia | hu ni nunulia |
| **tunapokaribia** | **huninunulia** |
| hu kumbukwa | hu tu peleka |
| **hukumbukwa** | **hutupeleka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ **Kuakifisha**

Hiki ni kinywaji kitamu.


Kwa nini kinywaji ni kitamu?

Kwa nini kikombe kilivunjika?

Kikombe kilivunjika.








**Mwezi wa Disemba**

Naupenda mwezi wa Disemba. Mwezi huu hukumbukwa na Wakristo kote duniani. Ni mwezi wa kukumbuka siku ya Yesu Kristo kuzaliwa.Tunapokaribia Disemba wazazi wangu huninunulia mavazi mazuri. Baba hutupeleka kutembelea miji mbalimbali. Tarehe ishirini na tano, sisi hupika vyakula vitamu kama vile chapati, wali, kuku na nyama. Baada ya kuvila sisi huviteremsha kwa vinywaji kama soda na maji ya machungwa. Sherehe hizi huwa za kufana sana.



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **tunapokaribia** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **tu na po karibia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **tunapokaribia** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **hu kumbukwa (hukumbukwa), hu ni nunulia (huninunulia), hu tu peleka (hutupeleka.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 93**.

### ◆ Sarufi Kuafikisha (.?)

Andika sentensi ubaoni bila kuakifisha. N/T/U**:** Eleza wanafunzi jinsi ya kutumia alama hizi (.?.)

Hiki kinywaji kitamu

Kwa nini kinywaji ni kitamu

Kwa nini kikombe kilivunjika

Kikombe kilivunjika

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 93**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **wakristo, vinywaji** na **kufana**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mwezi wa Desemba"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, ni mambo gani ambayo wewe huyafanya mwezi wa Desemba? (hutembelea jamaa na marafiki/husaidia wazazi na walezi)*
2. *Je, ni mwezi gani unaoupenda sana? Eleza sababu ya jibu lako. (wanafunzi wajibu na kutoa sababu)*
3. *Ni vyakula gani ambavyo nyinyi hula wakati wa sherehe? (samaki, pilau, n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni wanafunzi waziakifishe.

Hiki kinywaji kitamu

Kwa nini kinywaji ni kitamu

Kwa nini kikombe kilivunjika

Kikombe kilivunjika

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 19: Siku ya 4*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 19: Siku ya 5

Wiki ya 19: Siku ya 5 **Miezi**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **Me i - Mei**

★


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ri | fe | sti | mba | ma |
| se | go | l | ua | ri |
| a | ju | de | la | chi |
| ni | ja | nu | me | br |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Wakati uliopo -na** — **Wakati ujao -ta**

Watoto wa**na**cheka - Watoto wa**ta**cheka.
Watu wa**na**enda - Watu wa**ta**enda.
Wazee wa**na**msalimia - Wazee wa**ta**msalimia.
Wakulima wa**na**pata - Wakulima wa**ta**pata.

Kibuyu cha ajabu



95

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **Me** na **i** kuandika: neno **Mei**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome. Zisome pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Wakati uliopo -na** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Watoto wa**na**cheka | - | Watoto wa**ta**cheka. |
| Watu wa**na**enda | - | Watu wa**ta**enda. |
| Wazee wa**na**msalimia | - | Wazee wa**ta**msalimia. |
| Wakulima wa**na**pata | - | Wakulima wa**ta**pata. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 95**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **kipawa, kuzidisha** na **kusawazisha**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Kibuyu cha ajabu"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Kibuyu cha ajabu

Zamani za kale paliishi kijana kwa jina Komoi. Alikuwa mkarimu sana. Siku moja katika mwezi wa Januari, mzee mmoja akaja kumuomba maji ya kunywa. Komoi alikuwa na kikombe kimoja cha maji akampa mzee. Baada ya kunywa maji, mzee alisema kuwa kile kiangazi hakingeisha hadi mwaka uishe. Akampa Komoi kibuyu na akatoweka.

Jua liliendelea, mwezi wa Februari na Machi jua liliwaka hata zaidi. Mimea ilikauka na mifugo wakaanza kufa. Komoi akakumbuka kibuyu alichopewa na mzee. Alipoangalia ndani, aliona maji. Alimimina maji kwenye kikombe halafu kwenye birika. Maji hayakwisha. Wanyama wote walikunywa maji. Maji mengine akanyunyizia mimea.

Komoi alienda kijijini na kutangazia kila mtu kuwa alikuwa na maji. Watu wote walikuja na vibuyu vyao kuchota maji. Wengine walikuja na mifugo yao.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Kijana Komoi alikuwa mwenye tabia gani? (mkarimu sana.)*
2. *Komoi alimpa mzee nini? (alimpa kikombe kimoja cha maji.)*
3. *Kutokana na kiangazi, ni nini kilichofanyika? (mimea iliharibika, maji yaliisha.)*
4. *Je, unafikiria hadithi hii ni ya ukweli au la? Eleza maoni yako. (la au ndio - watoe sababu zao.)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **woga, Machi, muhula, kuagana, Aprili, kinywaji, Oktoba, vyakula, hutukaribisha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 19: Siku ya 5*

# Wiki ya 20: Siku ya 1

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 **Alama za barabarani**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| mwa nga li fu<br>**mwangalifu** | wa nya ma<br>**wanyama** |
| ki vu ki o<br>**kivukio** | a ja li<br>**ajali** |
| de re va<br>**dereva** | ho s pi ta li<br>**hospitali** |




Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku wa fahamisha<br>**kuwafahamisha** | wa na o tumia<br>**wanaotumia** |
| i na yo onyesha<br>**inayoonyesha** | zi na po fuatwa<br>**zinapofuatwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Lile ni **ga**ri refu | - | Yale ni **ma**gari **ma**refu. |
| Lile ni **ga**ri kubwa | - | Yale ni **ma**gari **ma**kubwa. |
| Lile ni **ga**ri chafu | - | Yale ni **ma**gari chafu. |
| Lile ni **ga**ri safi | - | Yale ni **ma**gari safi. |

96

Wiki ya 20: Siku ya 1 na 2 **Alama za barabarani**




**Alama za barabarani**

Alama za barabarani ni muhimu kwa watu wote wanaotumia barabara. Watu wote wanaotembea kwa miguu, wale wanaoendesha baiskeli na madereva wa magari wanastahili kuzingatia alama hizo. Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule ili kuwafahamisha wanaotumia barabara kuwa waangalifu. Ni hatari watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi **H** inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo ni lazima awe mwangalifu. Vilevile, hapaswi kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama zingine ni kama kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa hupunguza ajali.

97

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mwangalifu** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **mwa nga li fu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mwangalifu**. **[U]** Endelea na maneno: **kivukio, dereva, wanyama, ajali, hospitali.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 96**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **waangalifu, kuzingatia** na **kivukio**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Alama za barabarani"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni akina nani wanaostahili kuzingatia alama za barabarani? (watu wote/madereva/walimu/watoto)*
2. *Taja alama moja ya barabarani. (alama ya kivukio)*
3. *Ni wapi mtu hapaswi kupiga honi ovyoovyo) (karibu na shule/karibu na hospitali)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **kivukio, madereva, msalaba, ajali, baiskeli**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 20: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufunza kwa utaratibu wiki ya kwanza. Sio haraka sana au polepole sana.

**Alama za barabarani**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| mwa nga li fu<br>**mwangalifu** | wa nya ma<br>**wanyama** |
| ki vu ki o<br>**kivukio** | a ja li<br>**ajali** |
| de re va<br>**dereva** | ho s pi ta li<br>**hospitali** |




Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ★ ku wa fahamisha<br>**kuwafahamisha** | wa na o tumia<br>**wanaotumia** |
| i na yo onyesha<br>**inayoonyesha** | zi na po fuatwa<br>**zinapofuatwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Lile ni **ga**ri refu | - | Yale ni **ma**gari **ma**refu. |
| Lile ni **ga**ri kubwa | - | Yale ni **ma**gari **ma**kubwa. |
| Lile ni **ga**ri chafu | - | Yale ni **ma**gari chafu. |
| Lile ni **ga**ri safi | - | Yale ni **ma**gari safi. |





**Alama za barabarani**




**Alama za barabarani**

Alama za barabarani ni muhimu kwa watu wote wanaotumia barabara. Watu wote wanaotembea kwa miguu, wale wanaoendesha baiskeli na madereva wa magari wanastahili kuzingatia alama hizo. Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule ili kuwafahamisha wanaotumia barabara kuwa waangalifu. Ni hatari watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi **H** inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo ni lazima awe mwangalifu. Vilevile, hapaswi kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama zingine ni kama kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa hupunguza ajali.



### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **kuwafahamisha** ubaoni. Tamka sehemu za neno **ku wa fahamisha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **kuwafahamisha**. N/T/U: Endelea na maneno: **i na yo onyesha (inayoonyesha); wa na o tumia (wanaotumia); zi na po fuatwa (zinapofuatwa.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 96**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Lile ni **ga**ri refu | - | Yale ni **ma**gari **ma**refu. |
| Lile ni **ga**ri kubwa | - | Yale ni **ma**gari **ma**kubwa. |
| Lile ni **ga**ri chafu | - | Yale ni **ma**gari chafu. |
| Lile ni **ga**ri safi | - | Yale ni **ma**gari safi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 96**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **waangalifu, kuzingatia** na **kivukio**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Alama ya barabarani** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni watu gani huvukia kwenye kivuko cha wanyama? (wachungaji, wachungaji wa wanyama)*
2. *Je unaweza kuchora mojawapo ya alama tatu za barabarani? (waongoze wanafunzi kuchora alama)*
3. *Kwa nini si vizuri kupiga honi karibu na shule? (kwa sababu watoto wanasoma, walimu wanafundisha, itawafanyia watoto kelele.)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi za sarufi za umoja na wingi katika vitabu vyao.

1. **Gari hili ni refu sana - Magari haya ni marefu sana.**
2. **Mbona gari lako ni chafu? - Mbona magari yenu ni chafu?**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 20: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 **Alama za barabarani**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| Ra shi di<br>**Rashidi** | de re va<br>**dereva** | t ra fi ki<br>**trafiki** |
| s ta di<br>**stadi** | m zu ngu ko<br>**mzunguko** | nye ku ndu<br>**nyekundu** |



Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ha ku hitimu<br>**hakuhitimu** | a li m danganya<br>**alimdanganya** |
| a li ji fundisha<br>**alijifundisha** | i li yo fuata<br>**iliyofuata** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na** | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|
| Dereva huyu a**na**hitimu | Dereva huyu a**ta**hitimu. |
| Rashidi a**na**julikana sana | Rashidi a**ta**julikana sana. |
| Mtu huyu a**na**mdanganya | Mtu huyu a**ta**mdanganya. |
| Roda a**na**shangaa sana | Roda a**ta**shangaa sana. |

98

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 **Alama za barabarani**



**Dereva Rashidi**

Rashidi alikuwa dereva ambaye hakuhitimu. Alijifundisha kuendesha gari kijijini. Siku moja Rashidi alimtembelea shangazi yake mjini Nairobi. Alipofika huko alimdanganya kwamba yeye ni dereva stadi. Shangazi yake alifurahi sana. Alijua sasa ingekuwa rahisi kwake yeye kwenda soko la Marikiti kila siku. Asubuhi iliyofuata shangazi aliamua kuenda sokoni. Rashidi aliruka kwenye gari harakaharaka ili kuliendesha. Walipofika kwenye mzunguko wa magari, Rashidi hakujua umuhimu wa taa za trafiki. Huyo! Alifululiza moja kwa moja japo aliiona taa nyekundu. Shangazi alishangaa! Kufumba na kufumbua macho, waliligonga gari lingine.

99

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **Rashidi** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **Ra shi di** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **Rashidi**. **[U]** Endelea na maneno: **stadi, dereva, mzunguko, trafiki** na **nyekundu**.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 98**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **hakuhitimu, stadi, trafiki**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma shairi ya **"Dereva Rashidi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja mji aliotembelea Rashidi. (mji wa Nairobi)*
2. *Rashidi alifanya makosa gani? (alimdanganya shangazi yake/aliendesha gari bila ujuzi)*
3. *Taa za trafiki zilikuwa wapi? (zilikuwa kwenye mzunguko wa magari)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii kuhusu picha ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha. Wanafunzi wachore alama nne za barabarani.

**Magari yamegongana barabarani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 20: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka hatua tatu muhimu kwenye mtindo wa kufunza somo. Mtindo huu ni: Ninafanya, Tunafanya na Unafanya.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 — **Alama za barabarani**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| Ra shi di<br>**Rashidi** | de re va<br>**dereva** | t ra fi ki<br>**trafiki** |
| s ta di<br>**stadi** | m zu ngu ko<br>**mzunguko** | nye ku ndu<br>**nyekundu** |



Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ha ku hitimu<br>**hakuhitimu** | a li m danganya<br>**alimdanganya** |
| a li ji fundisha<br>**alijifundisha** | i li yo fuata<br>**iliyofuata** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Dereva huyu a**na**hitimu | - | Dereva huyu a**ta**hitimu. |
| Rashidi a**na**julikana sana | - | Rashidi a**ta**julikana sana. |
| Mtu huyu a**na**mdanganya | - | Mtu huyu a**ta**mdanganya. |
| Roda a**na**shangaa sana | - | Roda a**ta**shangaa sana. |

98

Wiki ya 20: Siku ya 3 na 4 — **Alama za barabarani**



**Dereva Rashidi**

Rashidi alikuwa dereva ambaye hakuhitimu. Alijifundisha kuendesha gari kijijini. Siku moja Rashidi alimtembelea shangazi yake mjini Nairobi. Alipofika huko alimdanganya kwamba yeye ni dereva stadi. Shangazi yake alifurahi sana. Alijua sasa ingekuwa rahisi kwake yeye kwenda soko la Marikiti kila siku. Asubuhi iliyofuata shangazi aliamua kuenda sokoni. Rashidi aliruka kwenye gari harakaharaka ili kuliendesha. Walipofika kwenye mzunguko wa magari, Rashidi hakujua umuhimu wa taa za trafiki. Huyo! Alifululiza moja kwa moja japo aliiona taa nyekundu. Shangazi alishangaa! Kufumba na kufumbua macho, waliligonga gari lingine.

99

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **hakuhitimu** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **ha ku hitimu** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **hakuhitimu**. **[U]** Endelea na maneno: **a li ji fundisha (alijifundisha), a li m danganya (alimdanganya), i li yo fuata (iliyofuata.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 98**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Dereva huyu a**na**hitimu | - | Dereva huyu a**ta**hitimu. |
| Rashidi a**na**julikana sana | - | Rashidi a**ta**julikana sana. |
| Mtu huyu a**na**mdanganya | - | Mtu huyu a**ta**mdanganya. |
| Roda a**na**shangaa sana | - | Roda a**ta**shangaa sana. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 98**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **hakuhitimu, stadi, trafiki**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Dereva Rashidi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Rashidi alifanya makosa gani? (alipeleka gari bila ujuzi/ alidanganya.)*
2. *Unafikiri polisi walipofika walimfanya Rashidi nini? (walimuuliza maswali/walimshika na kumpeleka polisi nk.)*
3. *Je unajua rangi nyingine za trafiki? (nyekundu, kijani, manjano.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **anahitimu, atajulikana, anamdanganya, atashangaa**. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi. Tumia neno **anahitimu** kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 20: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kiswahili ni lugha ya kupendeza sana. Mwalimu lazima ajifunze kutamka maneno sawasawa ili aweze kuongoza wanafunzi kuyatamka vyema.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 20: Siku ya 5 — **Alama za barabarani**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma ta tu - matatu**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| la | ma | ri | si | ba | mo |
| ta | pi | ki | shi | tu | ga |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja -ako** — **Wingi -enu**

Hili ni gari **lako** - Haya ni **ma**gari **yenu**.
Hili ni koti **lako** - Haya ni **ma**koti **yenu**.
Hili ni basi **lako** - Haya ni **ma**basi **yenu**.
Hili ni pipa **lako** - Haya ni **ma**pipa **yenu**.

**Ufalme wa kobe**



100

## Ufalme wa Kobe

Zamani, mfalme wa wanyama alikuwa Kobe. Kila mnyama alikuwa na Siku yake ya kumpikia mfalme wao. Fisi alitengeneza orodha ya majina ya wanyama wa kupika. Punda hakupenda kazi ya upishi. Alisema, harufu ya moshi ilimfanya mgonjwa. Pundamilia alijitolea kumpikia Punda. Kila mara, Ngiri alimchochea Pundamilia asimpikie Punda.

Siku moja, Ndovu pia alijaribu kumuomba Nungunungu ampikie. Lakini Nungunungu aliogopa moto kwa sababu ya mishale yake. Alisema Ndovu angeomba Twiga ampikie kwa sababu Twiga alipenda kupika. Twiga naye alipenda kwenda safari kumtembelea shangazi yake, Kiboko.

Siku moja mfalme Kobe alikosa chakula. Akamwita Fisi ampe sababu. Fisi akamuuliza Ndovu kwa nini hakupika. Ndovu akasema alimuomba Twiga ampikie. Twiga akasema hakupika kwa sababu alienda kwa shangazi yake Kiboko. Mfalme Kobe alikasirika na kusema mpishi wake wa kila siku angekuwa Sungura. Tangu siku hiyo Sungura alimuandalia mfalme vyakula vitamu sana.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **ma ta** na **tu** kuandika neno **matatu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome. N/T/U**:** Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

**Umoja** — **Wingi**

Hili ni gari **lako** - Haya ni **ma**gari **yenu**.
Hili ni koti **lako** - Haya ni **ma**koti **yenu**.
Hili ni basi **lako** - Haya ni **ma**basi **yenu**.
Hili ni pipa **lako** - Haya ni **ma**pipa **yenu**.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 100**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **orodha, chochea/ alimchochea** na **nungunungu**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Ufalme wa Kobe"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni nani alitengeneza orodha ya majina ya kupika? (Fisi)*
2. *Kwa nini punda hakupenda kazi ya upishi? (Kwa sababu hakupenda moshi)*
3. *Kwa nini Kobe alimchagua sungura kuwa mpishi wake wa kila siku? (watoto waeleze sababu zao)*
4. *Je, unafikiri wanyama walikuwa wanasema ukweli? (Watoto wajibu na kutetea majibu yao)*

### ✍ Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **kivukio, madereva, msalaba, ajali, baiskeli, meli, mitumbwi, manowari, baiskeli, feri.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 20: Siku ya 5*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 21: Siku ya 1

**Wiki ya 21: Siku ya 1 na 2** **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mi tu mbwi | ba i s ke li | wa na ma ji |
| **mitumbwi** | **baiskeli** | **wanamaji** |
| e ro ple ni | ma no wa ri | u sa fi ri |
| **eropleni** | **manowari** | **usafiri** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li tumia | u me endelea |
| **walitumia** | **umeendelea** |
| wa li tembea | hu tumiwa |
| **walitembea** | **hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** (yako) | **Wingi** (zenu) |
|---|---|
| Meli **yako** imeenda | - Meli **zenu** zimeenda. |
| Feri **yako** imechafuka | - Feri **zenu** zimechafuka. |
| Manowari **yako** imezama | - Manowari **zenu** zimezama. |
| Baiskeli **yako** imeharibika | - Baiskeli **zenu** zimeharibika. |

101

**Wiki ya 21: Siku ya 1 na 2** **Marejeleo**



**Usafiri**

Zamani za kale, watu walitumia njia tofauti za usafiri. Watu wengi walitembea muda mrefu kwa miguu. Wengine walitumia wanyama kwa usafiri wao na wa mizigo pia. Watu walioishi karibu na mito, bahari na maziwa walitumia dau na mitumbwi. Mbali na kutembea, siku hizi watu wanatumia aina mbalimbali za magari, eropleni, baiskeli na pikipiki. Usafiri wa majini pia umeendelea sana. Siku hizi kuna meli, feri na manowari. Manowari hutumiwa sana na majeshi ya wanamaji vitani.

102

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mitumbwi** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **mi tu mbwi** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mitumbwi**. **[U]** Endelea na maneno: **eropleni, baiskeli, manowari, wanamaji, usafiri.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 101**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mitumbwi, manowari, maziwa**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha shairi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma taarifa:

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Usafiri"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni njia gani za usafiri zilizotumiwa zamani? (walitembea kwa miguu/wengine walitumia wanyama/ walitumia mitumbwi kuvuka mito)*
2. *Taja njia za usafiri wa kisasa. (magari, eropleni, baiskeli na meli)*
3. *Manowari hutumiwa sana na kina nani? (na majeshi,wanamaji)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mitumbwi, eropleni, baiskeli, manwari, wanamaji**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 21: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kumbuka kuwa kusoma hadithi kuna vipengele vitatu. Kusoma maneno vizuri, kwa mwendo mzuri na kuonyesha hisia na kuzingatia alama za uakifishaji.

# Wiki ya 21: Siku ya 2

**Wiki ya 21: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mi tu mbwi | ba i s ke li | wa na ma ji |
| **mitumbwi** | **baiskeli** | **wanamaji** |
| e ro ple ni | ma no wa ri | u sa fi ri |
| **eropleni** | **manowari** | **usafiri** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li tumia | u me endelea |
| **walitumia** | **umeendelea** |
| wa li tembea | hu tumiwa |
| **walitembea** | **hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (yako)** | | **Wingi (zenu)** |
|---|---|---|
| Meli **yako** imeenda | - | Meli **zenu** zimeenda. |
| Feri **yako** imechafuka | - | Feri **zenu** zimechafuka. |
| Manowari **yako** imezama | - | Manowari **zenu** zimezama. |
| Baiskeli **yako** imeharibika | - | Baiskeli **zenu** zimeharibika. |

101

**Wiki ya 21: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**



**Usafiri**

Zamani za kale, watu walitumia njia tofauti za usafiri. Watu wengi walitembea muda mrefu kwa miguu. Wengine walitumia wanyama kwa usafiri wao na wa mizigo pia. Watu walioishi karibu na mito, bahari na maziwa walitumia dau na mitumbwi. Mbali na kutembea, siku hizi watu wanatumia aina mbalimbali za magari, eropleni, baiskeli na pikipiki. Usafiri wa majini pia umeendelea sana. Siku hizi kuna meli, feri na manowari. Manowari hutumiwa sana na majeshi ya wanamaji vitani.

102

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **walitumia** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa li tumia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **walitumia**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **wa li tembea (walitembea), u me endelea (umeendelea), hu tumiwa (hutumiwa.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 101**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja (yako)** | | **Wingi (zenu)** |
|---|---|---|
| Meli **yako** imeenda | - | Meli **zenu** zimeenda. |
| Feri **yako** imechafuka | - | Feri **zenu** zimechafuka. |
| Manowari **yako** imezama | - | Manowari **zenu** zimezama. |
| Baiskeli **yako** imeharibika | - | Baiskeli **zenu** zimeharibika. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 101**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **mitumbwi, manowari, maziwa.**

### Kusoma taarifa:

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Usafiri"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni njia gani za usafiri huwa haraka zaidi? (ndege, gari)*
2. *Taja njia ya usafiri unayotamani kutumia zaidi. (ndege, n.k.)*
3. *Je, umewahi kusafiri kwa njia ya maji? (eleza ilivyokuwa kwako)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi hizi.

1. **Meli yako iko baharini - Meli yenu iko baharini.**
2. **Manowari yako imezama - Manowari yenu imezama.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 21: Siku ya 2*

Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4 **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| du me | bu ndi | ma pa mbo |
| **dume** | **bundi** | **mapambo** |
| ta u si | u shu ngi | chi ri ku |
| **tausi** | **ushungi** | **chiriku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ya na yo tumika | ku burudisha |
| **yanayotumika** | **kuburudisha** |
| hu tofautiana | ku pendeza |
| **hutofautiana** | **kupendeza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ndege huyu ana **m**domo mrefu | - Ndege hawa wana **mi**domo mirefu. |
| Anatuonyesha **m**fano mzuri | - Wanatuonyesha **mi**fano mizuri. |
| Chiriku huyu **ana** sauti nzuri | - Chiriku hawa **wana** sauti nzuri. |
| Nyuni huyu **ana** sauti nyororo | - Nyuni hawa **wana** sauti nyororo. |
| Tausi huyu **ana** rangi nzuri | - Tausi hawa **wana** rangi nzuri. |

103

Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4 **Marejeleo**



### Maumbile ya ndege

Ndege wengi hutofautiana kimaumbile. Utaona tofauti kati ya ndege mbalimbali hata baina ya dume na jike wa aina moja. Kwa mfano, tausi dume ana rangi nzuri kuliko jike. Njiwa jike huwa na mdomo mrefu kuliko njiwa dume. Bundi jike ana shingo nyembamba na dume ana shingo nene.

Baadhi ya ndege pia huwa na ushungi juu ya vichwa vyao na wengi hawana.

Ndege pia wana manyoya mazuri ya kupendeza. Kwa mfano, tausi na kanga wana manyoya yanayotumika kama mapambo. Ndege wana sauti tofauti za kuburudisha. Nyimbo za ndege huwa na ujumbe fulani. Watu wengi huamini kuwa chiriku ana sauti nzuri kuliko ndege wengine.

104

**Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **dume** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **du me** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **dume**. **[U]** Endelea na maneno: **tausi, bundi, ushungi, mapambo, chiriku.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 103**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **bundi, chiriku** na **ushungi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma taarifa:**

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Maumbile ya ndege"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni ndege gani waliotajwa kwenye hadithi hii. (tausi, njiwa)*
2. *Eleza tofauti ya kimaumbile baina ya ndege mbalimbali. (rangi tofauti, maumbile)*
3. *Ni ndege gani ambao manyoya yao hutumika kama mapambo? (tausi, kanga)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Tausi ni ndege maridadi sana.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 21: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapouliza maswali ya ufahamu yenye majibu kwenye hadithi, hakikisha kuwa wanafunzi wanaangalia jawabu kwenye hadithi kabla ya kujibu swali.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| du me | bu ndi | ma pa mbo |
| **dume** | **bundi** | **mapambo** |
| ta u si | u shu ngi | chi ri ku |
| **tausi** | **ushungi** | **chiriku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ★ ya na yo tumika | ku burudisha |
| **yanayotumika** | **kuburudisha** |
| hu tofautiana | ku pendeza |
| **hutofautiana** | **kupendeza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| ◆ **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ndege huyu ana **m**domo mrefu | - Ndege hawa wana **mi**domo mirefu. |
| Anatuonyesha **m**fano mzuri | - Wanatuonyesha **mi**fano mizuri. |
| Chiriku huyu **ana** sauti nzuri | - Chiriku hawa **wana** sauti nzuri. |
| Nyuni huyu **ana** sauti nyororo | - Nyuni hawa **wana** sauti nyororo. |
| Tausi huyu **ana** rangi nzuri | - Tausi hawa **wana** rangi nzuri. |

103

**Wiki ya 21: Siku ya 3 na 4** — **Marejeleo**



### Maumbile ya ndege

Ndege wengi hutofautiana kimaumbile. Utaona tofauti kati ya ndege mbalimbali hata baina ya dume na jike wa aina moja. Kwa mfano, tausi dume ana rangi nzuri kuliko jike. Njiwa jike huwa na mdomo mrefu kuliko njiwa dume. Bundi jike ana shingo nyembamba na dume ana shingo nene.

Baadhi ya ndege pia huwa na ushungi juu ya vichwa vyao na wengi hawana.

Ndege pia wana manyoya mazuri ya kupendeza. Kwa mfano, tausi na kanga wana manyoya yanayotumika kama mapambo. Ndege wana sauti tofauti za kuburudisha. Nyimbo za ndege huwa na ujumbe fulani. Watu wengi huamini kuwa chiriku ana sauti nzuri kuliko ndege wengine.

104

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **yanayotumika** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **ya na yo tumika** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **yanayotumika** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **hu tofautiana (hutofautiana), ku burudisha (kuburudisha), ku pendeza (kupendeza.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 103**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ndege huyu ana **m**domo mrefu | - | Ndege hawa wana **mi**domo mirefu. |
| Anatuonyesha **m**fano mzuri | - | Wanatuonyesha **mi**fano mizuri. |
| Chiriku **ana** sauti nzuri | - | Chiriku hawa **wana** sauti nzuri. |
| Nyuni huyu **ana** sauti nyororo | - | Nyuni hawa **wana** sauti nyororo. |
| Tausi huyu **ana** rangi nzuri | - | Tausi hawa **wana** rangi nzuri. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 103**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **bundi, chiriku na ushungi**.

### Kusoma taarifa:

**[N]** Soma taarifa kuhusu **"Maumbile ya ndege"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Taja majina ya ndege uwajuao. (wanafunzi wataje ndege mbalimbali)*
2. *Ni ndege gani anakupendeza zaidi? (kanga, tausi nk)*
3. *Kwa nini? (wanafunzi watoe sababu zao)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **mfano mzuri, sauti nyororo, rangi nzuri, midomo mirefu**. Tumia neno **tausi** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

**Tausi ni mfano mzuri wa ndege maridadi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 21: Siku ya 4*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 21: Siku ya 5 **Marejeleo**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **fe ri - feri**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| fe | da | li | ri |
| pi | nwa | mi | ma |
| me | gu | ga | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Sentensi** — **Hali ya kukanusha**

**Wali**tumia machela - **Hawa**kutumia machela.
**Wali**tembea kwa miguu - **Hawa**kutembea kwa miguu.
**Wali**ishi mjini - **Hawa**kuishi mjini.
**Wali**tofautiana - **Hawa**kutofautiana.

**Ugonjwa wa malaria**




105

### Ugonjwa wa malaria.

Tumaini aliamka akiwa anatetemeka mwili. Mwili wake ulikuwa na joto kali. Mama yake akaamua kumpeleka hospitali ya Shauri Moyo.

Hospitalini kulikuwa na wagonjwa wengi wenye maradhi tofauti tofauti. Magonjwa kama vile homa, kikohozi, upele na malaria. Wote walikuwa wameketi kwenye fomu wakingojea kumwona daktari.

Baada ya muda mfupi, daktari akamwita kwenye chumba cha kumfanyia uchunguzi. Hapo ndipo alimueleza kuwa alikuwa na ugonjwa wa malaria. Huu ni ugonjwa unaoletwa na mbu. Ili kujikinga na magonjwa haya, tunafaa kuhakikisha mbu hawazaani karibu na nyumba zetu. Pia mkitaka kuzuia malaria ni lazima mlale ndani ya chandarua kilichotibiwa. Malaria ni ugonjwa hatari sana na huua.

Tangu siku hiyo Tumaini na wenzake hufyeka nyasi nje ya nyumba yao. Pia wao hulala ndani ya chandarua kilichotibiwa na dawa.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **fe** na **ri** kuandika: neno **feri**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome na kueleza jinsi maneno yanavyobadilika katika kukanusha kwake. N/T/U:

| Sentensi | | Hali ya kukanusha |
|---|---|---|
| **Wali**tumia machela | - | **Hawa**kutumia machela. |
| **Wali**tembea kwa miguu | - | **Hawa**kutembea kwa miguu. |
| **Wali**ishi mjini | - | **Hawa**kuishi mjini. |
| **Wali**tofautiana | - | **Hawa**kutofautiana. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 105**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **maradhi, chandarua, uchunguzi**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Ugonjwa wa malaria"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Mama alimpeleka Tumaini hospitali wapi? (Shauri moyo)*
2. *Wagonjwa walikuwa wenye maradhi gani? (homa, upele, kikohozi)*
3. *Eleza jinsi unavyoweza kujikinga na malaria. (kuhakikisha mbu hawazaani karibu)*
4. *Je, umewahi patwa na ugonjwa? Ugonjwa gani? (wanafunzi waeleza)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **daktari, chiriku, maumbile, njiwa, dume, jike, eropleni, maradhi, uchunguzi, mitumbwi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 21: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 22: Siku ya 1

**Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2** **Rangi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ja wa bu | nye u si | wa ri di |
| **jawabu** | **nyeusi** | **waridi** |
| nye ku ndu | sa ma wa ti | u fu o ni |
| **nyekundu** | **samawati** | **ufuoni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u si staajabu | ku pendeza |
| **usistaajabu** | **kupendeza** |
| li ki chomoza | ni ta li jibu |
| **likichomoza** | **nitalijibu** |

Sarufi: Soma sentensi hizi

**Matumizi ya -angu na -etu**

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Hili ni kaa **langu** | - | Haya ni **ma**kaa **yetu**. |
| Hili ni swali **langu** | - | Haya ni **ma**swali **yetu**. |
| Hili ni ua **langu** | - | Haya ni **ma**ua **yetu**. |
| Hili ni jibu **langu** | - | Haya ni **ma**jibu **yetu**. |
| Hili ni pipa **langu** | - | Haya ni **ma**pipa **yetu**. |

106

**Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2** **Rangi**



**Rangi**

Rangi zote za ajabu, leo takupa jawabu,
Maswali yote nitajibu, nawe usistaajabu.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyekundu ni rangi gani? Ya maua natangaza,
Ua waridi la kupendeza, na jua likichomoza.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyeusi ni rangi pia, ambayo najivunia
Ni rangi ya nywele zangu, iliyo nyeusi pia.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Samawati ni rangi gani? Ndio rangi ya angani,
Na maji ya baharini, kuogelea ufuoni.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

107

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **jawabu** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **jawabu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **jawabu**. **[U]** Endelea na maneno: **nyekundu, nyeusi, samawati, waridi, ufuoni.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 106**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **jawabu, waridi, likichomoza**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha shairi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **"Rangi"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja majina ya rangi zilizotajwa kwenye shairi hili? (nyekundu, nyeusi, samawati)*
2. *Ua la waridi ni rangi gani? (nyekundu)*
3. *Taja vitu vilivyo na rangi ya samawati. (anga, maji ya bahari, wanafunzi wataje vitu vingine kutoka mazingira yao)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **jawabu, nyekundu, nyeusi, samawati, waridi**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 22: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Fuatilizia kwa kidole unaposoma sauti ili uunde silabi au wakati unasoma silabi zinazotengeneza neno. Baadaye pitisha kidole chini ya silabi au neno zima.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2 **Rangi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ja wa bu | nye u si | wa ri di |
| **jawabu** | **nyeusi** | **waridi** |
| nye ku ndu | sa ma wa ti | u fu o ni |
| **nyekundu** | **samawati** | **ufuoni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| u si staajabu | ku pendeza |
| **usistaajabu** | **kupendeza** |
| li ki chomoza | ni ta li jibu |
| **likichomoza** | **nitalijibu** |

Sarufi: Soma sentensi hizi

◆ **Matumizi ya -angu na -etu**

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Hili ni kaa **langu** | - | Haya ni **ma**kaa **yetu**. |
| Hili ni swali **langu** | - | Haya ni **ma**swali **yetu**. |
| Hili ni ua **langu** | - | Haya ni **ma**ua **yetu**. |
| Hili ni jibu **langu** | - | Haya ni **ma**jibu **yetu**. |
| Hili ni pipa **langu** | - | Haya ni **ma**pipa **yetu**. |

106

Wiki ya 22: Siku ya 1 na 2 **Rangi**



**Rangi**

Rangi zote za ajabu, leo takupa jawabu,
Maswali yote nitajibu, nawe usistaajabu.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyekundu ni rangi gani? Ya maua natangaza,
Ua waridi la kupendeza, na jua likichomoza.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyeusi ni rangi pia, ambayo najivunia
Ni rangi ya nywele zangu, iliyo nyeusi pia.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Samawati ni rangi gani? Ndio rangi ya angani,
Na maji ya baharini, kuogelea ufuoni.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

107

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **usistaajabu** ubaoni. Tamka sehemu za neno **u si staajabu** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **usistaajabu**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **ku pendeza (kupendeza), li ki chomoza (likichomoza), ni ta li jibu (nitalijibu.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 106**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja -angu** | | **Wingi -etu** |
|---|---|---|
| Hili ni kaa **langu** | - | Haya ni **ma**kaa **yetu**. |
| Hili ni swali **langu** | - | Haya ni **ma**swali **yetu**. |
| Hili ni ua **langu** | - | Haya ni **ma**ua **yetu**. |
| Hili ni jibu **langu** | - | Haya ni **ma**jibu **yetu**. |
| Hili ni pipa **langu** | - | Haya ni **ma**pipa **yetu**. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 106**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **jawabu, waridi, likichomoza.**

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **rangi** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja vitu vingine vilivyo na rangi nyekundu. (damu, matunda, maua, n.k.)*
2. *Ni rangi gani inakupendeza sana? Eleza jibu lako.*
3. *Taja rangi nyingine ambazo unajua.*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi katika umoja na wingi katika vitabu vyao.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Swali langu limejibiwa** | - | **Maswali yetu yamejibiwa.** |
| 2. | **Ua langu limekauka** | - | **Maua yetu yamekauka.** |
| 3. | **Pipa langu limechafuka** | - | **Mapipa yetu yamechafuka.** |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 22: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4** — **Rangi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | mwa nga za | ma to ne |
| **bendera** | **mwangaza** | **matone** |
| i ndi go | u ru ju a ni | ma nja no |
| **indigo** | **urujuani** | **manjano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| li na po mulika | hu onekana |
| **linapomulika** | **huonekana** |
| u na po kutana | hu tawanyika |
| **unapokutana** | **hutawanyika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Fulana **hii** ni nyekundu | - Fulana **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni ya samawati | - Nguo **hizi** ni za samawati. |
| Kalamu **hii** ni nyeupe | - Kalamu **hizi** ni nyeupe. |
| Penseli **hii** ni nyeusi | - Penseli **hizi** ni nyeusi. |

108

**Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4** — **Rangi**



**Rangi mbalimbali**

"Je, unajua rangi za bendera yetu?" Babu aliuliza. "Ndiyo," Kalu akajibu, "mwalimu wetu alituambia kuwa bendera yetu ina rangi nne. Juu huwa rangi ya urujuani kama shati langu. Katikati ni nyekundu kama damu na chini ni rangi ya kijani kibichi. Rangi hizo zimegawanywa kwa rangi ya manjano." Babu akasema, "Samahani Kalu. Rangi iliyo juu katika bendera yetu ni nyeusi. Nayo inayozigawanya ni nyeupe kama karatasi hii. Rangi kama indigo ambayo inafanana na koti hili langu haipatikani katika bendera yetu." "Asante babu. Sasa nimezifahamu rangi za bendera vyema," Kalu akasema.

109

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **bendera** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **be nde ra** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **bendera**. **[U]** Endelea na maneno: **indigo, mwangaza, urujuani, manjano, matone.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 108**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **indigo, urujuani, manjano**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Rangi mbalimbali"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja vitu vitatu vilivyo na rangi nyekundu. (Wanafunzi wataje vitu mbalimbali vya rangi nyekundu)*
2. *Rangi za bendera zimegawanywa kwa rangi gani. (nyeupe)*
3. *Je, unafikiri rangi nyekundu ilitumiwa katika bendera yetu kwa nini? Eleza maoni yako. (Wanafunzi waelezee sababu zao)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Bendera ya Kenya ina rangi nne.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 22: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kipindi cha somo la Kiswahili kina urefu wa dakika 30. Hakikisha unafunza kwa utaratibu ndio uweze kumaliza kufunza somo kwa muda uliopewa. Ukurasa wa (v) na (vi) una mpangilio wa kila sehemu na vile unavyostahili kufunza na muda wake.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — **Rangi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | mwa nga za | ma to ne |
| **bendera** | **mwangaza** | **matone** |
| i ndi go | u ru ju a ni | ma nja no |
| **indigo** | **urujuani** | **manjano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| li na po mulika | hu onekana |
| **linapomulika** | **huonekana** |
| u na po kutana | hu tawanyika |
| **unapokutana** | **hutawanyika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Fulana **hii** ni nyekundu | - Fulana **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni ya samawati | - Nguo **hizi** ni za samawati. |
| Kalamu **hii** ni nyeupe | - Kalamu **hizi** ni nyeupe. |
| Penseli **hii** ni nyeusi | - Penseli **hizi** ni nyeusi. |

108

Wiki ya 22: Siku ya 3 na 4 — **Rangi**



**Rangi mbalimbali**

"Je, unajua rangi za bendera yetu?" Babu aliuliza. "Ndiyo," Kalu akajibu, "mwalimu wetu alituambia kuwa bendera yetu ina rangi nne. Juu huwa rangi ya urujuani kama shati langu. Katikati ni nyekundu kama damu na chini ni rangi ya kijani kibichi. Rangi hizo zimegawanywa kwa rangi ya manjano." Babu akasema, "Samahani Kalu. Rangi iliyo juu katika bendera yetu ni nyeusi. Nayo inayozigawanya ni nyeupe kama karatasi hii. Rangi kama indigo ambayo inafanana na koti hili langu haipatikani katika bendera yetu." "Asante babu. Sasa nimezifahamu rangi za bendera vyema," Kalu akasema.

109

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **linapomulika** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **li na po mulika** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **linapomulika** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **u na po kutana (unapokutana), hu onekana (huonekana), hu tawanyika (hutawanyika.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 108**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno ubaoni. Soma katika umoja na wingi. N/T/U:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Fulana **hii** ni nyekundu | - Fulana **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni ya samawati | - Nguo **hizi** ni za samawati. |
| Kalamu **hii** ni nyeupe | - Kalamu **hizi** ni nyeupe. |
| Penseli **hii** ni nyeusi | - Penseli **hizi** ni nyeusi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 108**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **indigo, urujuani, manjano**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Rangi mbalimbali"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Bendera hupandishwa saa ngapi? (Ijumaa asubuhi)*
2. *Tazama vitu vilivyo darasani. Andika rangi nne ambazo unaweza kuzitambua.*
3. *Taja vitu vilivyo na rangi ya kijani kibichi. (miti, nyasi, n.k.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno darasa kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **bendera yetu**
2. **nyanja tatu**
3. **uwanja mmoja**
4. **rangi ya manjano**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 22: Siku ya 4*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 22: Siku ya 5

**Rangi**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **sa ma wa ti - samawati**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| sa | nye | ma | ku |
| wa | si | ti | ndu |
| ni | uki | pe | ja |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| Maji **yali**poteza rangi | - | Maji **hayaku**poteza rangi. |
| Maji **yali**tapakaa kote | - | Maji **hayaku**tapakaa kote. |
| Maji **yali**sababisha madhara | - | Maji **hayaku**sababisha madhara. |

Kwa nini mbingu ni samawati?



110

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **sa, ma, wa** na **ti** kuandika neno **samawati**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni kisha uzisome na kueleza jinsi zinavyobadilika.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| Maji **yali**poteza rangi | - | Maji **hayaku**poteza rangi. |
| Maji **yali**tapakaa kote | - | Maji **hayaku**tapakaa kote. |
| Maji **yali**sababisha madhara | - | Maji **hayaku**sababisha madhara. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 110**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **samawati, mafuriko** na **mashua**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Kwa nini mbingu ni samawati"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Baada ya kusoma**

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Eleza kwa ufupi kilichofanyika kwenye hadithi hii.*
2. *Ni watu gani waliopona? (wale waliojificha kwenye mashua maalumu)*
3. *Maji yana rangi gani? (hayana rangi)*
4. *Unafikiri hadithi hii ni ya kweli au la? (eleza jibu lako)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **nyekundu, nyeusi, samawati, waridi, indigo, urujuani, manjano**.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 22: Siku ya 5*

### Kwa nini mbingu ni samawati

Je, unajua kwa nini mbingu ni samawati? Hapo zamani za kale kulitokea mvua kubwa. Mvua hiyo ilinyesha kwa muda mrefu na kuleta mafuriko. Watu wengi walikufa. Waliopona ni wale waliojificha kwenye mashua maalum iitwayo safina.

Maji yalijaa kote hadi yakapita mawingu na kufikia mbingu. Siku hizo, maji yalikuwa na rangi ya samawati. Maji yaliposhikana na mbingu, mbingu zilipata rangi ya samawati. Wakati huo, maji yalipoteza rangi yake. Yaliporudi chini, hayakuwa na rangi ya samawati tena.

Nchi ilipokauka, watu waliokuwa wamejificha kwenye safina walitoka nje. Walipoangalia juu angani, waliona rangi ya mbingu imebadilika na kuwa samawati. Walipochota maji nyumbani, waliona hayana rangi yoyote. Lakini maji ya bahari huchukua rangi ya mbingu, kabla hayajachotwa.

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha kwamba umeangalia kazi ya ziada kabla ya kupeana kazi nyingine.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 23: Siku ya 1

**Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2** — **Saa na wakati**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| cho mbo | ki sa sa | ku fu ngwa |
| **chombo** | **kisasa** | **kufungwa** |
| ma u mbo | o fi si ni | shu ghu li |
| **maumbo** | **ofisini** | **shughuli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku wekwa | hu tofautiana |
| **kuwekwa** | **hutofautiana** |
| i ta ku saidia | hu tumiwa |
| **itakusaidia** | **hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Amesimama **karibu** na ukuta | - | Ameketi **mbali** na ukuta. |
| Kitabu kiko **juu** ya meza | - | Kitabu kiko **chini** ya meza. |
| Mlingoti uko **mbele** ya ofisi | - | Mlingoti uko **nyuma** ya ofisi. |
| Kitanda kiko **ndani** ya nyumba | - | Kitanda kiko **nje** ya nyumba. |

111

**Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2** — **Saa na wakati**



### Saa

Saa ni chombo cha kupimia muda au wakati. Kuna saa za kufungwa mkononi. Hizi huwa ndogo kiasi lakini hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Kuna saa za kuwekwa ukutani. Hizi nazo hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Pia kuna saa za kuwekwa mezani. Hizi pia hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Saa za mkono hutumiwa na mtu mmoja. Saa za ukutani na mezani mara nyingi hutumiwa na watu wengi. Saa ni muhimu shuleni, ofisini, nyumbani na hata hospitalini. Ni vizuri kuwa na saa. Itakusadia kufanya shughuli zako za kila siku kwa wakati unaofaa.

112

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **chombo** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **cho mbo** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **chombo**. **[U]** Endelea na maneno: **maumbo, kisasa, ofisini, kufungwa, shughuli.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 111**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **maumbo, chombo** na **shughuli**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Saa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Saa ni nini? (Saa ni chombo cha kupimia mda au wakati)*
2. *Eleza aina tofauti za saa. (Za kuvaliwa mkononi, za meza, za ukuta)*
3. *Saa hutumiwa wapi? (shuleni, ofisini, nyumbani na hospitalini)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika madaftari yao: **Umbo, daftari, mraba, shughuli, mstatili, yamefungwa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 23: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ni muhimu kutathmini kila mwanafunzi mara mbili kila muhula. Hii itakuwezesha kufahamu jinsi mwanafunzi anavyoendelea. Kusudi ni kuimarisha ufasaha wake wa kusoma na ufahamu. Kwa hivyo, ni bora kutathmini wanafunzi watatu kila siku.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 23: Siku ya 2

**Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2** — **Saa na wakati**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| cho mbo<br>**chombo** | ki sa sa<br>**kisasa** | ku fu ngwa<br>**kufungwa** |
| ma u mbo<br>**maumbo** | o fi si ni<br>**ofisini** | shu ghu li<br>**shughuli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| ku wekwa<br>**kuwekwa** | hu tofautiana<br>**hutofautiana** |
| i ta ku saidia<br>**itakusaidia** | hu tumiwa<br>**hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Amesimama **karibu** na ukuta | - | Ameketi **mbali** na ukuta. |
| Kitabu kiko **juu** ya meza | - | Kitabu kiko **chini** ya meza. |
| Mlingoti uko **mbele** ya ofisi | - | Mlingoti uko **nyuma** ya ofisi. |
| Kitanda kiko **ndani** ya nyumba | - | Kitanda kiko **nje** ya nyumba. |

111

**Wiki ya 23: Siku ya 1 na 2** — **Saa na wakati**



### Saa

Saa ni chombo cha kupimia muda au wakati. Kuna saa za kufungwa mkononi. Hizi huwa ndogo kiasi lakini hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Kuna saa za kuwekwa ukutani. Hizi nazo hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Pia kuna saa za kuwekwa mezani. Hizi pia hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Saa za mkono hutumiwa na mtu mmoja. Saa za ukutani na mezani mara nyingi hutumiwa na watu wengi. Saa ni muhimu shuleni, ofisini, nyumbani na hata hospitalini. Ni vizuri kuwa na saa. Itakusadia kufanya shughuli zako za kila siku kwa wakati unaofaa.

112

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **kutochelewa** ubaoni. Tamka sehemu za neno **ku to chelewa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **kutochelewa**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **I ta ku saidia (itakusaidia), hu to fautiana (hutofautiana), hu tumiwa (hutumiwa), ku wekwa (kuwekwa.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 111**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma peke yako. Soma na wanafunzi, wape nafasi wasome peke yao.

| Sentensi | | Kinyume |
|---|---|---|
| Amesimama **karibu** na ukuta | - | Ameketi **mbali** na ukuta. |
| Kitabu kiko **juu** ya meza | - | Kitabu kiko **chini** ya meza. |
| Mlingoti uko **mbele** ya ofisi | - | Mlingoti uko **nyuma** ya ofisi. |
| Kitanda kiko **ndani** ya nyumba | - | Kitanda kiko **nje** ya nyumba. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 111**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **maumbo, chombo** na **shughuli**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Saa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, saa inaweza kupatikana wapi hapa shuleni? (ofisini/darasani n.k.)*
2. *Saa inakusaidia vipi? (Inasaidia nisichelewe, kufuata vipindi vya masomo n.k.)*
3. *Taja umbo la saa ambalo unalijua. (mviringo n.k.)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi hizi katika vitabu vyao.

1. **Mti uko mbele ya ofisi** - **Mti uko nyuma ya ofisi.**
2. **Mto uko karibu na nyumba** - **Mti uko mbali na nyumba.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 23: Siku ya 2*

# Wiki ya 23: Siku ya 3

**Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4** — **Saa na wakati**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mwe ma | fo le ni | ma ra fiki |
| **mwema** | **foleni** | **marafiki** |
| wa ka ti | pa re di | a su bu hi |
| **wakati** | **paredi** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| hu wa ongoza | hu ji tayarisha |
| **huwaongoza** | **hujitayarisha** |
| i na po wadia | i ta ku saidia |
| **inapowadia** | **itakusaidia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja (hii) | Wingi (hizi) |
|---|---|
| Saa **hii** ni ya **mwa**nafunzi | - Saa **hizi** ni za **wa**nafunzi. |
| Ofisi **hii** ni ya **mwa**limu | - Ofisi **hizi** ni za **wa**limu. |
| Nyumba **hii** ni ya **m**zazi wangu | - Nyumba **hizi** ni za **wa**zazi wetu. |
| Shule **hii** ni ya msingi | - Shule **hizi** ni za msingi. |

113

**Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4** — **Saa na wakati**



Mwema

Mwema huishi karibu na shule yake. Kila siku, yeye huamka saa kumi na mbili asubuhi. Bila kupoteza wakati, yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja inapowadia, Mwema hupata kiamshakinywa. Yeye huanza safari yake kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni kwenda paredi. Baada ya paredi wanafunzi hurudi darasani kuanza masomo. Mwalimu wao huwasalimia, "M hali gani wanafunzi?" Wao hujibu, "Njema." Saa nne kamili wao huenda kucheza nje na marafiki zao. Saa sita kamili, Mwema hurudi nyumbani. Kabla ya kwenda, mwalimu wao huwaongoza kuimba wimbo mtamu wa "**Nasikia Sauti**."

114

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **mwema** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **mwe ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **mwema**. **[U]** Endelea na maneno: **wakati, foleni, paredi, marafiki, asubuhi.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 113**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **foleni, inapowadia** na **paredi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mwema"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mwema huamka saa ngapi? (Mwema huamka saa kumi na mbili asubuhi.)*
2. *Eleza vitu ambavyo Mwema hufanya kwa wakati wake? (saa moja - kiamsha kinywa, saa mbili - paredi, saa nne - kucheza, saa sita - nyumbani)*
3. *Ni wimbo gani ambao Mwema huimba? (Nasikia sauti).*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi wandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Wanafunzi wameketi darasani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 23: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kufunza msamiati, unaweza kutumia lugha inayoeleweka na wanafunzi. Pia vitu halisi, picha na maelezo pamoja na kutumia neno kwenye sentensi ni mbinu itakayowasaidia wanafunzi kuelewa vyema.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4** — **Saa na wakati**

Soma silabi na maneno.

| mwe ma | fo le ni | ma ra fiki |
|---|---|---|
| **mwema** | **foleni** | **marafiki** |
| wa ka ti | pa re di | a su bu hi |
| **wakati** | **paredi** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| hu wa ongoza | hu ji tayarisha |
|---|---|
| **huwaongoza** | **hujitayarisha** |
| i na po wadia | i ta ku saidia |
| **inapowadia** | **itakusaidia** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja (hii)** | **Wingi (hizi)** |
|---|---|
| Saa **hii** ni ya **mwa**nafunzi | - Saa **hizi** ni za **wa**nafunzi. |
| Ofisi **hii** ni ya **mwa**limu | - Ofisi **hizi** ni za **wa**limu. |
| Nyumba **hii** ni ya **m**zazi wangu | - Nyumba **hizi** ni za **wa**zazi wetu. |
| Shule **hii** ni ya msingi | - Shule **hizi** ni za msingi. |

113

**Wiki ya 23: Siku ya 3 na 4** — **Saa na wakati**



**Mwema**

Mwema huishi karibu na shule yake. Kila siku, yeye huamka saa kumi na mbili asubuhi. Bila kupoteza wakati, yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja inapowadia, Mwema hupata kiamshakinywa. Yeye huanza safari yake kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni kwenda paredi. Baada ya paredi wanafunzi hurudi darasani kuanza masomo. Mwalimu wao huwasalimia, "M hali gani wanafunzi?" Wao hujibu, "Njema." Saa nne kamili wao huenda kucheza nje na marafiki zao. Saa sita kamili, Mwema hurudi nyumbani. Kabla ya kwenda, mwalimu wao huwaongoza kuimba wimbo mtamu wa "**Nasikia Sauti**."

114

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **huwaongoza** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **hu wa ongoza** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **huwaongoza** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **i na po wadia (inapowadia), hu ji tayarisha (hujitayarisha), i ta ku saidia (itakusaidia.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 113**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma katika umoja na wingi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Saa **hii** ni ya mwanafunzi | - | Saa **hizi** ni za **wa**nafunzi. |
| Ofisi **hii** ni ya mwalimu | - | Ofisi **hizi** ni za **wa**limu. |
| Nyumba **hii** ni ya mzazi wangu | - | Nyumba **hizi** ni za **wa**zazi wetu. |
| Shule **hii** ni ya msingi | - | Shule **hizi** ni za msingi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 113**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **foleni, inapowadia** na **paredi**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu "**Mwema"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Je, wewe huamka saa ngapi? (wanafunzi waeleze masaa yao ya kuamka)*
2. *Eleza mambo unayofanya shuleni kutoka asubuhi mpaka saa saba huku ukizingatia saa. (kusoma, kucheza, n.k.)*
3. *Baada ya masomo shuleni, wewe hurudi nyumbani saa ngapi? (saa saba, saa sita na nusu n.k.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno **saa hii** kuunda sentensi. Waulize wanafunzi kutumia maneno yaliyosalia kuunda sentensi.

1. **ofisi hii**
2. **nyumba hizi**
3. **shule hii**
4. **nguo hizi**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 23: Siku ya 4*

Wiki ya 23: Siku ya 5 **Saa na wakati**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **a su bu hi - asubuhi**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ma | na | su | ni | cha |
| a | cho | ku | bu | pe |
| ke | u | mi | o | si |
| ro | sa | ji | m | hi |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Nguo **hii** ni nzuri | - | Nguo **hizi** ni nzuri. |
| Hospitali **hii** ni kubwa | - | Hospitali **hizi** ni kubwa. |
| Meza **hii** ni pana | - | Meza **hizi** ni pana. |
| Hadithi **hii** ni ndefu | - | Hadithi **hizi** ni ndefu. |

Obura na saa yake



115

**Oburu, Saa na Kasuku.**

Oburu ana ndege wake aina ya Kasuku ambaye anampenda sana. Jumamosi moja, baba yake alimpa zawadi. Ilikuwa saa ya dhahabu. Oburu alifurahi sana.

Baada ya kumsaidia mama kufanya kazi za nyumbani, Oburu alivaa saa yake na kupanda mwembe. Alipenda kukaa kule juu na kusoma vitabu vyake vya hadithi.

Muda mchache baadaye aliangalia saa yake na kusema, "Ala! Ni saa sita!" Kasuku wake aliyekuwa pale mtini alirudia, "Ala! Ni saa sita!" Oburu alicheka na kuendelea kusoma.

Saa saba ilipofika mamake aliita, "Oburu! Shuka mtini. Sasa ni saa saba." Kasuku aliyekuwa bado yuko pale mtini alirudia, "Oburu! Shuka mtini. Sasa ni saa saba."

Oburu alipokuwa akishuka, kasuku naye aliruka na kutua kichwani pake.

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote na wanafunzi. Tumia silabi **a,su, bu** na **hi** kuandika: neno **asubuhi**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Nguo **hii** ni nzuri | - | Nguo **hizi** ni nzuri. |
| Hospitali **hii** ni kubwa | - | Hospitali **hizi** ni kubwa. |
| Meza **hii** ni pana | - | Meza **hizi** ni pana. |
| Hadithi **hii** ni ndefu | - | Hadithi **hizi** ni ndefu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 115**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **kipawa, kuzidisha** na **kusawazisha**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Oburu, Saa na Kasuku"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Hadithi hii ilitokea siku gani? (ilikuwa Siku ya Jumamosi)*
2. *Baba alimpa Oburu zawadi gani? (saa ya dhahabu)*
3. *Kasuku alirudia maneno gani? (Ala! ni saa sita!/Oburu, shuka chini, sasa ni saa saba)*
4. *Unafikiria ni sababu gani ilimfanya kasuku kuruka na kutua kichwani mwake Oburu? (walikuwa marafiki n.k.)*

**Kuandika - Imla**

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **ofisi, saa, foleni, shule, daftari, paredi, mstatili, shughuli, kiangazi, kiamshakinywa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 23: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku pe nde za | ma zi ngi ra | wa na ri a dha |
| **kupendeza** | **mazingira** | **wanariadha** |
| mbu ga | ma a ja bu | u li mwe ngu |
| **mbuga** | **maajabu** | **ulimwengu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa me tu letea | ku tafuta |
| **wametuletea** | **kutafuta** |
| hu furahia | wa na hitaji |
| **hufurahia** | **wanahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| Wanariadha **wetu** wameshinda | - | Wanariadha **wenu** wameshinda. |
| Wanyama **wetu** ni muhimu sana | - | Wanyama **wenu** ni muhimu sana. |
| Watu **wetu** ni wazuri | - | Watu **wenu** ni wazuri. |
| Wachezaji **wetu** ni mashuhuri | - | Wachezaji **wenu** ni mashuhuri. |







**Nchi ya Kenya**

Kenya ni nchi ya kupendeza sana. Wanariadha wetu wametuletea sifa ulimwenguni kwa ushindi wao katika mbio za masafa marefu. Watu wengi hufurahia kuzuru nchi ya Kenya.Watu kutoka mabara mengine huja kuwaona wanyama pori kwenye mbuga zetu. Jiji la Nairobi ni jiji la kipekee ulimwenguni. Jiji hili lina mbuga ya wanyama. Mlima Kenya ni wa pili kwa urefu katika milima yote barani Afrika. Mbuga ya Masai Mara ni mojawapo ya maajabu ya ulimwengu. Hii ni kwa sababu ya kongoni ambao huvuka mto Mara katika msimu wao kila mwaka. Ni desturi kwa wanyama hawa kuvuka kuja upande wa Kenya kutafuta malisho. Wanyama wanahitaji mazingira mema. Ili tupate faida kutokana na utalii, ni lazima tuyalinde mazingira yetu.



## ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **kupendeza** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ku pe nde za** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kupendeza**. **[U]** Endelea na maneno: **mbuga, mazingira, maajabu, wanariadha, ulimwengu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 116**.

## Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wanariadha, masafa marefu** na **mbuga**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Nchi ya Kenya"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

## Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Wanariadha wamefanya nini ili kuletea Kenya sifa?* *(wameshinda/wameshinda mbio za masafa marefu)*
2. *Watu kutoka bara zingine huja Kenya kufanya nini?* *(kuona wanyama pori/kuzuru sehemu mbalimbali za Kenya.)*
3. *Ni sababu gani inafanya Masai Mara kuwa ya ajabu?* *(Kwa sababu ya nyumbu/nyumbu wanaporuka mto Mara)*

## Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **ulimwengu, mazingira, maajabu, Afrika, mji, wanariadha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 24: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Sauti za herufi ni muhimu kwa kusaidia mwanafunzi kusoma kwa haraka. Ni wajibu wako kuhakikisha umefanya mazoezi ya kusema sauti za herufi kabla ya kuzifunza na kuzisema darasani.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 24: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku pe nde za | ma zi ngi ra | wa na ri a dha |
| **kupendeza** | **mazingira** | **wanariadha** |
| mbu ga | ma a ja bu | u li mwe ngu |
| **mbuga** | **maajabu** | **ulimwengu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa me tu letea | ku tafuta |
| **wametuletea** | **kutafuta** |
| hu furahia | wa na hitaji |
| **hufurahia** | **wanahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| Wanariadha **wetu** wameshinda | - | Wanariadha **wenu** wameshinda. |
| Wanyama **wetu** ni muhimu sana | - | Wanyama **wenu** ni muhimu sana. |
| Watu **wetu** ni wazuri | - | Watu **wenu** ni wazuri. |
| Wachezaji **wetu** ni mashuhuri | - | Wachezaji **wenu** ni mashuhuri. |

116

Wiki ya 24: Siku ya 1 na 2 **Mazingira**



Nchi ya Kenya

Kenya ni nchi ya kupendeza sana. Wanariadha wetu wametuletea sifa ulimwenguni kwa ushindi wao katika mbio za masafa marefu. Watu wengi hufurahia kuzuru nchi ya Kenya.Watu kutoka mabara mengine huja kuwaona wanyama pori kwenye mbuga zetu. Jiji la Nairobi ni jiji la kipekee ulimwenguni. Jiji hili lina mbuga ya wanyama. Mlima Kenya ni wa pili kwa urefu katika milima yote barani Afrika. Mbuga ya Masai Mara ni mojawapo ya maajabu ya ulimwengu. Hii ni kwa sababu ya kongoni ambao huvuka mto Mara katika msimu wao kila mwaka. Ni desturi kwa wanyama hawa kuvuka kuja upande wa Kenya kutafuta malisho. Wanyama wanahitaji mazingira mema. Ili tupate faida kutokana na utalii, ni lazima tuyalinde mazingira yetu.

117

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **wametuletea** ubaoni. NTU Tamka sehemu za neno **wa me tu letea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **wametuletea**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **hu furahia (hufurahia), ku tafuta (kutafuta), wa na hitaji (wanahitaji.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 116**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. Soma katika umoja na wingi. N/T/U:

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| Wanariadha **wetu** wameshinda | - | Wanariadha **wenu** wameshinda. |
| Wanyama **wetu** ni muhimu sana | - | Wanyama **wenu** ni muhimu sana. |
| Watu **wetu** ni wazuri | - | Watu **wenu** ni wazuri. |
| Wachezaji **wetu** ni mashuhuri | - | Wachezaji **wenu** ni mashuhuri. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 116**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **wanariadha, masafa marefu** na **mbuga.**

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Nchi ya Kenya** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Tunaweza kulinda mazingira yetu vipi? (kutokata miti, kutunza mito n.k.)*
2. *Taja miji iliyoko nchini Kenya ambayo unaijua. (Mombasa, Kisumu n.k.)*
3. *Taja wanyama wanaoishi nchini Kenya. (simba, ndovu, nyati, n.k.)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika madaftari yao:

1. **Watoto wetu wameenda shule - Watoto wenu wameenda shule.**
2. **Watu wetu wana nidhamu - Watu wenu wana nidhamu**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 24: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| vyu ma | m mo mo nyo ko |
| **vyuma** | **mmomonyoko** |
| cha nga mo to | mba o |
| **changamoto** | **mbao** |
| p la s ti ki | ka ra ta si |
| **plastiki** | **karatasi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| tu na vyo tumia | vi na po tupwa |
| **tunavyotumia** | **vinapotupwa** |
| hu tengenezwa | vi li vyo tengenezwa |
| **hutengenezwa** | **vilivyotengenezwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | Kukanusha |
|---|---|
| Vitu hivi **vina**oza | - Vitu hivi **havi**ozi. |
| Vyuma vile **vina**tupwa | - Vyuma vile **havi**tupwi. |
| Vizazi vya sasa **vina**lindwa | - Vizazi vya sasa **havi**lindwi. |
| Vitabu vyetu **vina**tumiwa | - Vitabu vyetu **havi**tumiwi. |

118





**Linda mazingira**

Vitu vingi tunavyotumia kila siku hutengenezwa kwa vyuma, mbao, plastiki au hata chupa. Vitu hivi vinapotupwa, haviozi kwa urahisi. Hivyo basi changamoto kubwa tuliyo nayo ni kuepukana na kuharibu mazingira yetu. Ni muhimu kutupa takataka mahali panapofaa. Ni vyema pia kutumia vitu ambavyo vimetengenezwa kwa chupa, karatasi au chuma. Tujaribu kuepuka kutumia vitu vilivyotengenezwa kwa plastiki. Tuvitumie vitu hivi kwa muda mrefu kabla ya kuvitupa. Ni lazima pia tupande miti mingi tunavyoweza. Miti huboresha hewa, hupunguza mmomonyoko wa udongo na kuleta mvua. Kazi yetu ni kuyalinda mazingira yetu kwa vizazi vijavyo.

119

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **vyuma** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **vyu ma** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **vyuma**. **[U]** Endelea na maneno: **changamoto, plastiki, mmomonyoko, mbao , karatasi.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 118**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **changamoto, kuboresha** na **mazingira**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma taarifa:

**[N]** Soma taarifa ya **"Mazingira yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Vitu vingi tunavyo tumia hutengenezwa kwa nini? (vyuma, mbao, plastiki na chupa)*
2. *Mwandishi anatueleza tukome kufanya nini? (kurusha takataka/kutupa takataka ovyo)*
3. *Eleza umuhimu wa miti. (huboresha/husafisha hewa/ hupunguza mmonyoko wa udongo/pia huleta mvua)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Tunalinda mazingira kwa kupanda miti.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 24: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wa kusoma hadithi (zamu yangu), hakikisha kuwa unasoma kwa mwendo wako na sio mwendo wa wanafunzi ili waweze kuelewa. Ni kwa njia hii pia wanafunzi watajua jinsi ya kusoma kwa haraka.

**Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4** — **Mazingira**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| vyu ma | m mo mo nyo ko |
| **vyuma** | **mmomonyoko** |
| cha nga mo to | mba o |
| **changamoto** | **mbao** |
| p la s ti ki | ka ra ta si |
| **plastiki** | **karatasi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| tu na vyo tumia | vi na po tupwa |
| **tunavyotumia** | **vinapotupwa** |
| hu tengenezwa | vi li vyo tengenezwa |
| **hutengenezwa** | **vilivyotengenezwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | Kukanusha |
|---|---|
| Vitu hivi **vina**oza | - Vitu hivi **havi**ozi. |
| Vyuma vile **vina**tupwa | - Vyuma vile **havi**tupwi. |
| Vizazi vya sasa **vina**lindwa | - Vizazi vya sasa **havi**lindwi. |
| Vitabu vyetu **vina**tumiwa | - Vitabu vyetu **havi**tumiwi. |

118

**Wiki ya 24: Siku ya 3 na 4** — **Mazingira**



**Linda mazingira**

Vitu vingi tunavyotumia kila siku hutengenezwa kwa vyuma, mbao, plastiki au hata chupa. Vitu hivi vinapotupwa, haviozi kwa urahisi. Hivyo basi changamoto kubwa tuliyo nayo ni kuepukana na kuharibu mazingira yetu. Ni muhimu kutupa takataka mahali panapofaa. Ni vyema pia kutumia vitu ambavyo vimetengenezwa kwa chupa, karatasi au chuma. Tujaribu kuepuka kutumia vitu vilivyotengenezwa kwa plastiki. Tuvitumie vitu hivi kwa muda mrefu kabla ya kuvitupa. Ni lazima pia tupande miti mingi tunavyoweza. Miti huboresha hewa, hupunguza mmomonyoko wa udongo na kuleta mvua. Kazi yetu ni kuyalinda mazingira yetu kwa vizazi vijavyo.

119

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **tunavyotumia** ubaoni. Tamka sehemu za neno **tu na vyo tumia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **tunavyotumia** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **hu tengenezwa (hutengenezwa), vi na po tupwa (vinapotupwa), vi li vyo tengenezwa (vilivyotengenezwa.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 118**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| Vitu hivi **vina**oza | - | Vitu hivi **havi**ozi. |
| Vyuma vile **vina**tupwa | - | Vyuma vile **havi**tupwi. |
| Vizazi vya sasa **vina**lindwa | - | Vizazi vya sasa **havi**lindwi. |
| Vitabu vyetu **vina**tumiwa | - | Vitabu vyetu **havi**tumiwi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 118**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **changamoto, kutoathiri** na **mazingira**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mazingira yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Taja vyombo vya plastiki vinavyotumiwa nyumbani. (chupa, mikebe, mabirika n.k.)*
2. *Je, wanafunzi wanaweza kufanya nini ili kulinda mazingira yao? (kuyaweka safi, kufyeka nyasi, kufagia n.k.)*
3. *Kuna manufaa gani katika kulinda mazingira yetu? (afya nzuri n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hizi ubaoni. Tumia maneno **vitu vinaoza** kutunga sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **vitu vinaoza**
2. **vyuma havitupwi**
3. **vizazi vinalindwa**
4. **vitabu havitumiwi**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 24: Siku ya 4*

**Wiki ya 24: Siku ya 5** **Mazingira**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: m li ma - mlima

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| to | ti | nya | ki |
| m | di | mbu | ju |
| sa | mi | ma | ga |
| a | li | vu | ra |

Sarufi: Soma maneno haya.

● -etu -enu

watoto **wetu** - watoto **wenu**
wanyama **wetu** - wanyama **wenu**
wazazi **wetu** - wazazi **wenu**
walimu **wetu** - walimu **wenu**
ndege **wetu** - ndege **wenu**

Mwezi



120

## Mwezi

Hapo zamani za kale Mwezi alikuwa na watoto wawili. Watoto hao walikuwa Jua na Upepo. Wote waliishi pamoja angani.

Mwezi alimpenda Jua kuliko Upepo. Kwa sababu hiyo, Upepo hakumpenda Jua hata kidogo.

Siku moja, Mwezi alienda kuokota kuni na kuwaacha watoto wake nyumbani. Upepo alitafuta kiboko na kumfukuza Jua.

Jua alipokuwa akitoroka, alianguka kwa ngurumo na radi. Alilia kwa uchungu. Machozi yake yalianguka ardhini. Hapo ndipo mvua ikanyesha kwa mara ya kwanza.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **m, li** na **ma** na kuandika: neno **mlima. [T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U: Soma maneno haya.

| -etu | | -enu |
|---|---|---|
| watoto **wetu** | - | watoto **wenu** |
| wanyama **wetu** | - | wanyama **wenu** |
| wazazi **wetu** | - | wazazi **wenu** |
| walimu **wetu** | - | walimu **wenu** |
| ndege **wetu** | - | ndege **wenu** |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 120**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **angani** na **ardhi**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mwezi"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Watoto waliotajwa kwenye hadithi waliitwa nani?* *(Jua na Upepo)*
2. *Kwa nini Upepo alimfukuza Jua? (kwa sababu Upepo hakumpenda)*
3. *Ngurumo na radi zilisababishwa na nini?* *(zilisababishwa na Jua kuanguka)*
4. *Je, unafikiria hadithi hii ni ya ukweli au la? Eleza maoni yako. (wanafunzi wajibu na kueleza sababu zao)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **mvua, mbuga, udongo, mnyama, plastiki, ulimwengu, mmomonyoko, wanariadha, mazingira, vyuma.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 24: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — **Haki za jinsia**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa na ngu | ku cho ta | Ma ri a |
| **wanangu** | **kuchota** | **Maria** |
| ta fa dha li | na a mi ni | Ma ta no |
| **tafadhali** | **naamini** | **Matano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu si achwe | a ta ni peleka |
| **tusiachwe** | **atanipeleka** |
| tu ki kamilisha | tu na shukuru |
| **tukikamilisha** | **tunashukuru** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nina**umwa sana | - | **Si**umwi sana. |
| **Nina**baki hapa nyumbani | - | **Si**baki hapa nyumbani. |
| **Nina**msaidia mama yako | - | **Si**msaidii mama yako. |
| **Nina**piga simu kazini | - | **Si**pigi simu kazini. |
| **Nina**mpeleka mama hospitalini | - | **Si**mpeleki mama hospitalini. |

121

Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2 — **Haki za jinsia**



Mchezo wa kuigiza: Mama augua

**Mama**: Wanangu, naumwa sana. Sijiwezi sijitambui. Inabidi niende kumwona daktari mara moja. Baba yenu atanipeleka.

**Baba**: Sijui kama nitapewa ruhusa kazini. Hebu nimpigie simu mkubwa wangu. Na wewe Maria tafadhali ukitoka shuleni leo, usaidie hapa nyumbani. Unaweza kusaidiana na Matano kuchota maji na kupika chakula.

**Maria**: Naam baba. Tunashukuru. Tukikamilisha kazi nyumbani tutasoma vitabu vyetu ili tusiachwe nyuma.

**Baba**: Ninaona mnapenda kusoma sana wanangu. Haya basi, nendeni.

**Matano**: Asante baba. Naamini mama atapata nafuu.

122

## Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **wanangu** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **wa na ngu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **wanangu**.

**[U]** Endelea na maneno: **kuchota, tafadhali, naamini, Maria, matano.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 121**.

## Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya vifungu hivi vya maneno **sijiwezi sijitambui, kuchota maji** na **tutaachwa nyuma**.
Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma mchezo wa kuigiza:

**[N]** Soma mchezo kuhusu **"Mama augua"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

## Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni nani alikuwa mgonjwa? (mama alikuwa mgonjwa.)*
2. *Maria alisemaje? (wanafunzi waseme vitu mbalimbali alivyosema Maria.)*
3. *Matano alisemaje (wanafunzi waseme maneno aliyosema Matano.)*

## Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **kuchota, tafadhali, tutaachwa, kutafuta, mamako**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 25: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha anawapongeza wanafunzi kila wakati wanapojibu maswali sahihi. Pia ni muhimu kusaidia wale wanaokosa kutoa jibu sahihi na kuwatia moyo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

**Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2** **Haki za jinsia**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa na ngu | ku cho ta | Ma ri a |
| **wanangu** | **kuchota** | **Maria** |
| ta fa dha li | na a mi ni | Ma ta no |
| **tafadhali** | **naamini** | **Matano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu si achwe | a ta ni peleka |
| **tusiachwe** | **atanipeleka** |
| tu ki kamilisha | tu na shukuru |
| **tukikamilisha** | **tunashukuru** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nina**umwa sana | - | **Si**umwi sana. |
| **Nina**baki hapa nyumbani | - | **Si**baki hapa nyumbani. |
| **Nina**msaidia mama yako | - | **Si**msaidii mama yako. |
| **Nina**pigа simu kazini | - | **Si**pigi simu kazini. |
| **Nina**mpeleka mama hospitalini | - | **Si**mpeleki mama hospitalini. |

121

**Wiki ya 25: Siku ya 1 na 2** **Haki za jinsia**



**Mchezo wa kuigiza: Mama augua**

**Mama**: Wanangu, naumwa sana. Sijiwezi sijitambui. Inabidi niende kumwona daktari mara moja. Baba yenu atanipeleka.
**Baba**: Sijui kama nitapewa ruhusa kazini. Hebu nimpigie simu mkubwa wangu. Na wewe Maria tafadhali ukitoka shuleni leo, usaidie hapa nyumbani. Unaweza kusaidiana na Matano kuchota maji na kupika chakula.
**Maria**: Naam baba. Tunashukuru. Tukikamilisha kazi nyumbani tutasoma vitabu vyetu ili tusiachwe nyuma.
**Baba**: Ninaona mnapenda kusoma sana wanangu. Haya basi, nendeni.
**Matano**: Asante baba. Naamini mama atapata nafuu.

122

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **tusiachwe** ubaoni. Tamka sehemu za neno **tu si achwe** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **mwanitegemea**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **a ta ni peleka (atanipeleka), tu ki kamilisha (tukikamilisha), tu na shukuru (tunashukuru.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 121**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nina**umwa sana | - | **Si**umwi sana. |
| **Nina**baki hapa nyumbani | - | **Si**baki hapa nyumbani. |
| **Nina**msaidia mama yako | - | **Si**msaidii mama yako. |
| **Nina**piga simu kazini | - | **Si**pigi simu kazini. |
| **Nina**mpeleka mama hospitalini | - | **Si**mpeleki mama hospitalini. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 121**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **sijiwezi sijitambui, kuchota maji** na **tutaachwa nyuma**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mama augua"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Kwa nini mama alihitaji kumwona daktari haraka? (mama alikuwa mgonjwa/alikuwa anaumwa.)*
2. *Kutia bidii katika masomo kuna manufaa gani kwa wanafunzi? ( atapita mtihani na kwenda shule ya sekondari nk.)*

*Mwalimu: (Ongoza wanafunzi kuigiza mchezo huu.)*

**Kuandika**

Wape wanafunzi muda waandike sentensi za sarufi za umoja na wingi katika vitabu vyao.

1. **Sibaki nyumbani peke yangu - Ninabaki nyumbani peke yangu.**
2. **Sipigi simu kazini - Ninapiga simu kazini.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 25: Siku ya 2*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 25: Siku ya 3 na 4 — **Haki za jinsia**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ka ti ba | ma e nde le o | u ta ma du ni |
| **katiba** | **maendeleo** | **utamaduni** |
| po to vu | dhu lu ma | ma dha ra |
| **potovu** | **dhuluma** | **madhara** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na zo tokana | ku wa saidia |
| **zinazotokana** | **kuwasaidia** |
| i na pinga | ku faidi |
| **inapinga** | **kufaidi** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | Kinyume |
|---|---|
| Mila hizi ni **nzuri** | - Mila hizi ni **mbaya.** |
| Jamii hii ni **kubwa** | - Jamii hii ni **ndogo.** |
| Katiba hii ni ya **sasa** | - Katiba hii ni ya **zamani.** |
| Madhara haya ni **makubwa** | - Madhara haya ni **madogo.** |

123

Wiki ya 25: Siku ya 3 na 4 — **Haki za jinsia**



**Mila na tamaduni**

Kila jamii kote duniani ina utamaduni wake. Kuna baadhi ya mambo katika utamaduni ambayo ni potovu. Utamaduni mzuri hujenga na kufaidi jamii na watu binafsi. Utamaduni potovu huleta madhara katika maisha na maendeleo ya jamii. Baadhi ya mambo mazuri katika jamii ni kama vile watoto kutii wazazi wao na kuwasaidia kazi za nyumbani. Baadhi ya mambo potovu ni kama ndoa za mapema, tabia ya kuiba ng'ombe na vita kati ya jamii. Katiba ya Kenya inalinda kila mkenya. Inapinga utamaduni mbaya pamoja na dhuluma zinazotokana na utamaduni huo.

124

### ■ Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **katiba** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ka ti ba** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **katiba**. **[U]** Endelea na maneno: **potovu, dhuluma, utamaduni, madhara, maendeleo. Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** 123.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mila, potovu** na **binafsi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mila na tamaduni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja mila nzuri kulingana na hadithi hii? (kutii wazazi/ kusaidia wazazi kazi)*
2. *Ni zipi mila potovu? (kutahiri wasichana/ndoa za mapema/kuiba ng'ombe/vita vya kijamii)*
3. *Ni nini inamlinda kila mkenya kutokana na mila potovu? (Katiba mpya ya Kenya)*

### Kuandika

Andika sentensi hii kuhusu picha ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Watoto wanasaidia kazi za nyumbani.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 25: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Ufahamu wa fonimu huzingatia kufunza sauti za herufi. Wakati wa kufunza sauti, mwalimu hapaswi kuziandika herufi hizi ubaoni. Kipindi hiki ni cha mazungumzo pekee.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ka ti ba | ma e nde le o | u ta ma du ni |
| **katiba** | **maendeleo** | **utamaduni** |
| po to vu | dhu lu ma | ma dha ra |
| **potovu** | **dhuluma** | **madhara** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na zo tokana | ku wa saidia |
| **zinazotokana** | **kuwasaidia** |
| i na pinga | ku faidi |
| **inapinga** | **kufaidi** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | **Kinyume** |
|---|---|
| Mila hizi ni **nzuri** | - Mila hizi ni **mbaya.** |
| Jamii hii ni **kubwa** | - Jamii hii ni **ndogo.** |
| Katiba hii ni ya **sasa** | - Katiba hii ni ya **zamani.** |
| Madhara haya ni **makubwa** | - Madhara haya ni **madogo.** |







### Mila na tamaduni

Kila jamii kote duniani ina utamaduni wake. Kuna baadhi ya mambo katika utamaduni ambayo ni potovu. Utamaduni mzuri hujenga na kufaidi jamii na watu binafsi. Utamaduni potovu huleta madhara katika maisha na maendeleo ya jamii. Baadhi ya mambo mazuri katika jamii ni kama vile watoto kutii wazazi wao na kuwasaidia kazi za nyumbani. Baadhi ya mambo potovu ni kama ndoa za mapema, tabia ya kuiba ng'ombe na vita kati ya jamii. Katiba ya Kenya inalinda kila mkenya. Inapinga utamaduni mbaya pamoja na dhuluma zinazotokana na utamaduni huo.



★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **zinazotokana** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **zi na zo tokana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **zinazotokana** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **ku wa saidia (kuwasaidia), i na pinga (inapinga), ku faidi (kufaidi.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 123**.

◆ **Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma katika umoja na wingi.

| **Sentensi** | **Kinyume** |
|---|---|
| Mila hizi ni **nzuri** | - Mila hizi ni **mbaya.** |
| Jamii hii ni **kubwa** | - Jamii hii ni **ndogo.** |
| Katiba hii ni ya **sasa** | - Katiba hii ni ya **zamani.** |
| Madhara haya ni **makubwa** | - Madhara haya ni **madogo.** |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 123**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **utamaduni, potovu** na **binafsi**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mila na tamaduni"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

**Maswali**

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni tamaduni gani unazozijua kuwa ni mbaya/potovu mbali na zile tulizozitaja kipindi kilichopita? (kudharau wanawake/wasichana, n.k.)*
2. *Taja baadhi ya tamaduni nzuri katika jamii yenu. (kuheshimu wazee/wazazi, n.k.)*
3. *Haki gani nyingine ambazo katiba imekupatia kama mtoto? (haki ya kupata elimu, matibabu n.k.)*

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni. Tumia maneno **tamaduni nzuri** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **mila nzuri**
2. **bahati mbaya**
3. **jamii kubwa**
4. **madhara madogo**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 25: Siku ya 4*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 25: Siku ya 5 **Haki za jinsia**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ka ti ba - katiba**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | ti | la | ka | mi | dhu |
| ba | cho | po | ba | mwe | ri |
| to | tu | ku | zi | che | vu |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **ni**nacheka | - | **si**cheki |
| **ni**nalia | - | **si**lii |
| **ni**naimba | - | **si**imbi |
| **ni**nabeba | - | **si**bebi |
| **ni**nakata | - | **si**kati |

Mavazi



125

## Mavazi

Jana ilikuwa Ijumaa. Niliamka mapema sana. Nje kulikuwa na baridi. Nilivaa kofia na kaptula. Mama alisema nivae fulana kwa sababu kulikuwa na mvua. Mama alikuwa amevaa rinda jekundu. Alifunga kanga kiunoni na kitambaa kichwani.

Baada ya kunywa uji, tulichukua jembe na kwenda shambani. Nilimsaidia mama kupanda mbegu za mahindi.

Adhuhuri jua liliwaka. Nilitoa fulana na kofia. Tuliketi na kupata chakula cha mchana. Jioni, mvua ilinyesha.

Tulirudi nyumbani tukiwa tumelowa na kuchoka sana.

Baada ya kuoga, nilivaa koti, vesti na suruali ndefu. Mama alivaa buibui. Baba, alivaa kanzu. Sote tulielekea msikitini kusali.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **ka, ti** na **ba** na kuandika neno **katiba. [T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi

### ● Sarufi

Andika maneno haya ubaoni kisha uyasome. N/T/U: Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **ni**nacheka | - | **si**cheki |
| **ni**nalia | - | **si**lii |
| **ni**naimba | - | **si**imbi |
| **ni**nabeba | - | **si**bebi |
| **ni**nakata | - | **si**kati |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 125**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **fulana, kaptula** na **adhuhuri**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Mavazi"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ni mavazi gani yametajwa kwenye hadithi hii. (kofia, kaptula, fulana, rinda, kitambaa n.k.)*
2. *Eleza alichovaa anayezungumza. (kofia na kaptula)*
3. *Kwa nini aliambiwa avae fulana? (kulikuwa kunanyesha)*
4. *Kwa nini baba alivaa kanzu? (alikuwa akienda msikitini kusali)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **kuchota, tafadhali, tutaachwa, mamako, katiba, potovu, kabambe, dhuluma, utamaduni, madhara**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 25: Siku ya 5*

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u ta ma du ni | ma bu i bu i | wa ta wa |
| **utamaduni** | **mabuibui** | **watawa** |
| ki i sla mu | ma ri nda | wa ka to li ki |
| **kiislamu** | **marinda** | **wakatoliki** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu tofautiana | hu tumiwa |
| **hutofautiana** | **hutumiwa** |
| hu valiwa | hu patikana |
| **huvaliwa** | **hupatikana** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Hili** ni vazi fupi | - | **Haya** ni **ma**vazi **ma**fupi. |
| **Hili** ni rinda zuri | - | **Haya** ni **ma**rinda **ma**zuri. |
| **Hili** ni buibui refu | - | **Haya** ni **ma**buibui **ma**refu. |
| **Hili** ni shati dogo | - | **Haya** ni **ma**shati **ma**dogo. |

126

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**



**Mavazi mbalimbali**

Kuna mavazi mbalimbali ambayo huvaliwa na wanadamu. Mavazi haya hutofautiana kwa sababu ya utamaduni, dini, sherehe, kazi na hata hali ya anga. Kwa mfano, kanzu huvaliwa na wanaume wa dini ya kiislamu. Nao wanawake waislamu huvalia mabuibui. Watawa wa kikatoliki huvaa veli na marinda marefu. Kanga na shuka hutumiwa kama mavazi ya kitamaduni. Jina lingine la kanga ni leso na hupatikana katika rangi mbalimbali. Leso huwa na maandishi yenye ujumbe spesheli.

127

### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **utamaduni** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **u ta ma du ni** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **utamaduni**. **[U]** Endelea na maneno: **kiislamu, mabuibui, marinda, watawa, wakatoliki.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 126**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mabuibui, kanga** na **spesheli**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mavazi mbalimbali"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mavazi hutofautiana kwa sababu zipi? (utamaduni, dini, sherehe, kazi, anga n.k.)*
2. *Eleza mavazi wanayovaa wanawake waislamu/ watawa wa kikatoliki. (mabuibui/veli na marinda marefu)*
3. *Mavazi ya kitamaduni ni yapi? (kanga, shuka)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **kiislamu, mabuibui, marinda, kuwabana, kanga** na **spesheli.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 26: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha umejiandaa vyema kabla ya kuenda darasani. Panga kadi za herufi utakapozitumia kwa mfuko wa herufi kabla ya kuanza kufunza. Hii itasaidia kuokoa wakati.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u ta ma du ni | ma bu i bu i | wa ta wa |
| **utamaduni** | **mabuibui** | **watawa** |
| ki i sla mu | ma ri nda | wa ka to li ki |
| **kiislamu** | **marinda** | **wakatoliki** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ★ hu tofautiana | hu tumiwa |
| **hutofautiana** | **hutumiwa** |
| hu valiwa | hu patikana |
| **huvaliwa** | **hupatikana** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| ◆ Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Hili** ni vazi fupi | - | **Haya** ni **ma**vazi **ma**fupi. |
| **Hili** ni rinda zuri | - | **Haya** ni **ma**rinda **ma**zuri. |
| **Hili** ni buibui refu | - | **Haya** ni **ma**buibui **ma**refu. |
| **Hili** ni shati dogo | - | **Haya** ni **ma**shati **ma**dogo. |

126

Wiki ya 26: Siku ya 1 na 2 **Mavazi**



**Mavazi mbalimbali**

Kuna mavazi mbalimbali ambayo huvaliwa na wanadamu. Mavazi haya hutofautiana kwa sababu ya utamaduni, dini, sherehe, kazi na hata hali ya anga. Kwa mfano, kanzu huvaliwa na wanaume wa dini ya kiislamu. Nao wanawake waislamu huvalia mabuibui. Watawa wa kikatoliki huvaa veli na marinda marefu. Kanga na shuka hutumiwa kama mavazi ya kitamaduni. Jina lingine la kanga ni leso na hupatikana katika rangi mbalimbali. Leso huwa na maandishi yenye ujumbe spesheli.

127

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **hutofautiana** ubaoni. Tamka sehemu za neno **hu tofautiana** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **hutofautiana**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **hu tumiwa (hutumiwa), hu valiwa (huvaliwa), hu patikana (hupatikana.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 126**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Hili** ni vazi fupi | - | **Haya** ni **ma**vazi **ma**fupi. |
| **Hili** ni rinda zuri | - | **Haya** ni **ma**rinda **ma**zuri. |
| **Hili** ni buibui refu | - | **Haya** ni **ma**buibui **ma**refu. |
| **Hili** ni shati dogo | - | **Haya** ni **ma**shati **ma**dogo. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 126**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya haya maneno **mabuibui, kanga** na **spesheli**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mavazi mbalimbali"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja aina zingine za mavazi. (sare za shule, kanzu, kofia, vibaragashia n.k.)*
2. *Wakati wa baridi, watu huvaa mavazi gani? (koti, sweta, jaketi, n.k.)*
3. *(Beba leso au maleso. Wape nafasi wanafunzi wasome misemo mbalimbali. Waagize waandike misemo hiyo kwenye madaftari.)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi hizi kwa umoja na wingi katika vitabu vyao.

1. **Vazi lako ni fupi sana.**
2. **Wasichana wamevaa marinda mazuri.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 26: Siku ya 2*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

**Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4** — **Mavazi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa me vaa | ki le mba | nye u pe |
| **wamevaa** | **kilemba** | **nyeupe** |
| ka nzu | shu ka | vye u si |
| **kanzu** | **shuka** | **vye usi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| i li po wadia | a li ji funga |
| **ilipowadia** | **alijifunga** |
| a li mu uliza | wa li agana |
| **alimuuliza** | **waliagana** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Nipatie **ki**lemba **che**upe | - | Tupatie **vi**lemba **vye**upe. |
| Ninataka **ki**atu **che**kundu | - | Tunataka **vi**atu **vye**kundu. |
| Ninapenda **ko**ti **je**usi | - | Tunapenda **ma**koti **me**usi. |
| Ninavaa **ri**nda **je**usi | - | Tunavaa **ma**rinda **me**usi. |

128

**Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4** — **Mavazi**



### Siku ya ibada

Siku ya Jumapili ilipowadia Mzee Okelo alivalia koti jeusi. Alijifunga kilemba chake kichwani na kuvalia viatu vyeusi. Alianza safari kuelekea kanisani. Njiani alikutana na rafiki yake Mzee Sakuda. Mzee Sakuda alikuwa amevaa kanzu nyeupe pepepe. “Mbona huendi kanisani leo?” Okelo alimuuliza rafiki yake. “Ninaenda kumwona shangazi yangu ambaye ameugua kwa muda mrefu,” alijibu Mzee Sakuda. Basi waliagana na Mzee Okelo akashika njia moja kwa moja hadi kanisani. Huko watu walikuwa wamevaa nguo za aina mbalimbali.

129

■ **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **wamevaa** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **wa me vaa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **wamevaa**. **[U]** Endelea na maneno: **kanzu, kilemba, shuka, nyeupe, vyeusi.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 128**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **nyeupe pepepe, ameugua** na **kilemba**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi ya **"Siku ya Ibada"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Eleza mavazi ambayo Mzee Okello alikuwa amevaa. (koti jeusi, kilemba, viatu vyeusi)*
2. *Mzee Sakuda alikuwa amevaa mavazi yapi? (kanzu nyeupe)*
3. *Baada ya kuagana mzee Okelo alielekea wapi? (kanisani)*

**Kuandika**

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Kwaya imesimama mbele ya kanisa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 26: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Wakati wa kuunda maneno kutoka kwa jedwali, kumbusha wanafunzi kuwa wanaweza tu kutengeneza haya maneno wakitumia sauti au silabi zilizo kwenye jedwali. Maneno hayo ni sharti yawe maneno halisi yenye maana.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4 — **Mavazi**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa me vaa | ki le mba | nye u pe |
| **wamevaa** | **kilemba** | **nyeupe** |
| ka nzu | shu ka | vye u si |
| **kanzu** | **shuka** | **vye usi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ★ i li po wadia | a li ji funga |
| **ilipowadia** | **alijifunga** |
| a li mu uliza | wa li agana |
| **alimuuliza** | **waliagana** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Nipatie **ki**lemba **che**upe | - | Tupatie **vi**lemba **vye**upe. |
| Ninataka **ki**atu **che**kundu | - | Tunataka **vi**atu **vye**kundu. |
| Ninapenda **ko**ti **je**usi | - | Tunapenda **ma**koti **me**usi. |
| Ninavaa **ri**nda **je**usi | - | Tunavaa **ma**rinda **me**usi. |

128

Wiki ya 26: Siku ya 3 na 4 — **Mavazi**



**Siku ya ibada**

Siku ya Jumapili ilipowadia Mzee Okelo alivalia koti jeusi. Alijifunga kilemba chake kichwani na kuvalia viatu vyeusi. Alianza safari kuelekea kanisani. Njiani alikutana na rafiki yake Mzee Sakuda. Mzee Sakuda alikuwa amevaa kanzu nyeupe pepepe. “Mbona huendi kanisani leo?” Okelo alimuuliza rafiki yake. “Ninaenda kumwona shangazi yangu ambaye ameugua kwa muda mrefu,” alijibu Mzee Sakuda. Basi waliagana na Mzee Okelo akashika njia moja kwa moja hadi kanisani. Huko watu walikuwa wamevaa nguo za aina mbalimbali.

129

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **ilipowadia** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **i li po wadia** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **ilipowadia** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **wa li agana (waliagana), a li mu uliza (alimuuliza), a li ji funga (alijifunga.**)

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 128**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Nipatie **ki**lemba **che**upe | - | Tupatie **vi**lemba **vye**upe. |
| Ninataka **ki**atu **che**kundu | - | Tunataka **vi**atu **vye**kundu. |
| Ninapenda **ko**ti **je**usi | - | Tunapenda **ma**koti **me**usi. |
| Ninavaa **ri**nda **je**usi | - | Tunavaa **ma**rinda **me**usi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 128**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **nyeupe pepepe, ameugua** na **kilemba**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Siku ya ibada"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Kwa nini watu hupenda kuvalia nadhifu wakati wanaenda sehemu za ibada? (huwa wanaenda kuabudu, kuonyesha heshima, n.k.)*
2. *Taja mavazi ambayo unafikiri Mzee Okelo aliyaona kanisani. (rinda, koti, fulana, n.k.)*
3. *Rangi ya sare ya shule yenu ni gani? (wanafunzi wajibu)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **kanzu, shuka, vyeusi, kufaidi**. Tumia neno **kanzu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 26: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Iwapo kuna wanafunzi wasioweza kujibu maswali ya ufahamu, waelekeze kwenye mbinu zitakazowapatia jibu kwa urahisi. Usiwapatie jibu papo hapo.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 26: Siku ya 5 **Mavazi**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **sha ti - shati**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| mba | nda | ri | sha | bui | a |
| li | re | ti | le | sa | rua |
| i | ke | su | nga | ki | bui |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** — **Wingi**

Buibui **hili** ni chafu - **Ma**buibui **haya** ni **ma**chafu.
Shati **hili** ni refu - **Ma**shati **haya** ni **ma**refu.
Vazi **hili** ni zuri - **Ma**vazi **haya** ni **ma**zuri.
Rinda **hili** ni fupi - **Ma**rinda **haya** ni **ma**fupi.

Mama afua nguo



130

## Mama afua nguo

Mama anafua nguo na kuzianika kwenye kamba. Maria anamtazama huku akitambua kila nguo inayoanikwa. Maria anasema, “Hii ni sare yangu ya shule.”

Mama anaanika nguo zingine kwenye kamba. Maria anasema, “Hii ni suruali ya kaka, Musa. Siku ya Ijumaa, yeye alivaa suruali nyeusi na shati hili jeupe tukaenda shuleni. Naye mama alivaa buibui na baba akavaa kanzu wakaelekea msikitini kusali.”

Mama anatabasamu huku akiendelea kuanika nguo. Maria anaendelea kusema, “Shati hili la mikono mirefu na kaptula ni za baba. Yeye huzivaa tunapoenda matembezi.”

“Nacho hiki kilemba na kanga hii ni ya mama.” Mama anamalizia kwa kuanika blausi na fulana mbili ndogo. Maria anampigia mama makofi na kusema, “Asante mama kwa kutufulia nguo. Tutang’ara kwelikweli.”

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **sha** na **ti** kuandika: neno **shati**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentesi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Buibui **hili** ni chafu | - | **Ma**buibui **haya** ni **ma**chafu. |
| Shati **hili** ni refu | - | **Ma**shati **haya** ni **ma**refu. |
| Vazi **hili** ni zuri | - | **Ma**vazi **haya** ni **ma**zuri. |
| Rinda **hili** ni fupi | - | **Ma**rinda **haya** ni **ma**fupi. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 130**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **kaptura, kung'ara, kufulia, kusali**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Mama afua nguo"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Maswali**

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Maria alitambua nguo gani kwanza? (sare ya shule/ sare yake)*
2. *Suruali ilikuwa ya nani? (suruali ilikuwa ya kaka Musa)*
3. *Kilemba huvaliwa wapi? (kichwani)*
4. *Unahitaji nini kufua nguo? (maji safi, sabuni, n.k.)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika madaftari yao: **utamaduni, mabuibui, kuwabana, kanzu, vyeusi, kiatu, kilemba, blausi, fulana, suruali.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 26: Siku ya 5*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kitu cha muhimu zaidi katika mradi wa KUSOMA ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaweza kusoma vizuri wakimaliza huu mwaka. Je, umeweza kuwasaidia wasome vilivyo?

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — Alama za hesabu

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a li pa za | mbu zi | ma pa cha |
| **alipaza** | **mbuzi** | **mapacha** |
| wa li o sa li a | m si tu | O jwa ng' |
| **waliosalia** | **msitu** | **Ojwang'** |

Tarakimu

| | | |
|---|---|---|
| 10 - **kumi** | 20 - **ishirini** | 30 - **thelathini** |
| 50 - **hamsini** | 80 - **themanini** | 100 - **mia moja** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa li po kuwa | wa me beba |
| **walipokuwa** | **wamebeba** |
| ku wa rudisha | a li wa peleka |
| **kuwarudisha** | **aliwapeleka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Huyu** | | **Yule** |
|---|---|---|
| Mbuzi **huyu** anakimbia | - | Mbuzi **yule** anakimbia. |
| Ndege **huyu** anapendeza | - | Ndege **yule** anapendeza. |
| Fisi **huyu** ni mlafi | - | Fisi **yule** ni mlafi. |
| Ng'ombe **huyu** ametulia | - | Ng'ombe **yule** ametulia. |

131

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — Alama za hesabu



**Mzee Ojwang'**

Mzee Ojwang alikuwa na mbuzi kumi. Aliwapeleka malishoni karibu na msitu mkubwa. Walipokuwa wakila nyasi, fisi akaja na kumla mmoja. Mzee Ojwang alipaza sauti na kuita, "Wooiii! Nisaidie. Fisi! Mbuzi wangu! Wooooiii! Fisi! Mbuzi wangu!" Wanakijiji wakaja haraka kumsaidia Mzee Ojwang. Wengi walijaribu kumfukuza fisi. Wengine wakapiga simu kwa idara ya ulinzi wa wanyama pori. Lakini fisi tayari alikuwa amerudi kwenye msitu mkubwa. Wanakijiji walimsaidia Mzee Ojwang kuwarudisha nyumbani mbuzi waliosalia. Kesho yake, Mzee Ojwang alijawa na furaha alipopata mbuzi wake wawili wamezaa mapacha.

132

■ **Kusoma maneno kutumia silabi**

N/T/U Andika neno **alipaza** ubaoni. Tamka silabi **a li pa za** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **alipaza**. **[U]** Endelea na maneno: **waliosalia, mbuzi, msitu, mapacha, Ojwang.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 131**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **malishoni, alipaza** na **mapacha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mzee Ojwang"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Mzee Ojwang alikuwa na mbuzi wangapi mwanzoni? (alikuwa na mbuzi kumi)*
2. *Eleza kilichotendeka baada ya kuenda malishoni. (mbuzi walipokuwa wakila nyasi, fisi akaja na kumla)*
3. *Kwa nini mzee Ojwang' alifurahi sana? (mbuzi wake walizaa mapacha)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **waliosalia, mbuzi, msitu, malishoni, idara** na **mapacha, ng'ombe, thelathini, hamsini, themanini.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 27: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Hakikisha kuwasaidia watoto ambao hawajui kusoma. Wape mazoezi ya kusoma sauti, silabi na maneno mepesi. Baada ya muda mfupi wataanza kusoma kama wengine.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 27: Siku ya 2

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — **Alama za hesabu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a li pa za | mbu zi | ma pa cha |
| **alipaza** | **mbuzi** | **mapacha** |
| wa li o sa li a | m si tu | O jwa ng’ |
| **waliosalia** | **msitu** | **Ojwang’** |

Tarakimu

| | | |
|---|---|---|
| 10 - **kumi** | 20 - **ishirini** | 30 - **thelathini** |
| 50 - **hamsini** | 80 - **themanini** | 100 - **mia moja** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| ★ wa li po kuwa | wa me beba |
| **walipokuwa** | **wamebeba** |
| ku wa rudisha | a li wa peleka |
| **kuwarudisha** | **aliwapeleka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Huyu** | | **Yule** |
|---|---|---|
| Mbuzi **huyu** anakimbia | - | Mbuzi **yule** anakimbia. |
| Ndege **huyu** anapendeza | - | Ndege **yule** anapendeza. |
| Fisi **huyu** ni mlafi | - | Fisi **yule** ni mlafi. |
| Ng’ombe **huyu** ametulia | - | Ng’ombe **yule** ametulia. |

131

Wiki ya 27: Siku ya 1 na 2 — **Alama za hesabu**



**Mzee Ojwang’**

Mzee Ojwang alikuwa na mbuzi kumi. Aliwapeleka malishoni karibu na msitu mkubwa. Walipokuwa wakila nyasi, fisi akaja na kumla mmoja. Mzee Ojwang alipaza sauti na kuita, “Wooiii! Nisaidie. Fisi! Mbuzi wangu! Wooooiii! Fisi! Mbuzi wangu!” Wanakijiji wakaja haraka kumsaidia Mzee Ojwang. Wengi walijaribu kumfukuza fisi. Wengine wakapiga simu kwa idara ya ulinzi wa wanyama pori. Lakini fisi tayari alikuwa amerudi kwenye msitu mkubwa. Wanakijiji walimsaidia Mzee Ojwang kuwarudisha nyumbani mbuzi waliosalia. Kesho yake, Mzee Ojwang alijawa na furaha alipopata mbuzi wake wawili wamezaa mapacha.

132

**★ Kusoma maneno marefu**

Andika neno **walipokuwa** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa li po kuwa** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **walipokuwa**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **ku wa rudisha (kuwarudisha), wa me beba (wamebeba), a li wa peleka (aliwapeleka.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 131**.

**◆ Sarufi**

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| | | |
|---|---|---|
| Mbuzi **huyu** anakimbia | - | Mbuzi **yule** anakimbia. |
| Ndege **huyu** anapendeza | - | Ndege **yule** anapendeza. |
| Fisi **huyu** ni mlafi | - | Fisi **yule** ni mlafi. |
| Ng'ombe **huyu** ametulia | - | Ng'ombe **yule** ametulia. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 131**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **malishoni, alipaza** na **mapacha**.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Mzee Ojwang"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

**Maswali**

Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Baada ya kisa kilichotendeka mzee Ojwang alibaki na mbuzi wangapi? (alibaki na mbuzi tisa: 10 – 1 = 9)*
2. *Baada ya mbuzi wawili kuzaa mapacha alikuwa na mbuzi wangapi pamoja? (2 x 2 = 4, 4 + 9 = 13 kumi na watatu)*
3. *Ni wanyama gani wengine ambao hula wanyama wengine? (simba, chui, n.k.)*

**Kuandika**

Wape wanafunzi muda waandike sentensi za sarufi hizi katika madaftari yao.

1. **Mbuzi huyu ni mdogo - Mbuzi hawa ni wadogo.**
2. **Fisi huyu anakula nyama - Fisi hawa wanakula nyama.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 27: Siku ya 2*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 **Alama za hesabu**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ku o nge za | ku zi di sha |
| **kuongeza** | **kuzidisha** |
| ku to a | ku fa u lu |
| **kutoa** | **kufaulu** |
| ku ga wa nya | ku sa wa zi sha |
| **kugawanya** | **kusawazisha** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na vyo dhani | hu ku elekeza |
| **wanavyodhani** | **hukuelekeza** |
| ku vi elewa | ya na yo husisha |
| **kuvielewa** | **yanayohusisha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Alama **ya** hesabu | - | Alama **za** hesabu. |
| Alama **ya** kuongeza | - | Alama **za** kuongeza. |
| Alama **ya** kutoa | - | Alama **za** kutoa. |
| Alama **ya** kuzidisha | - | Alama **za** kuzidisha. |
| Alama **ya** kujumlisha | - | Alama **za** kujumlisha. |

133

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 **Alama za hesabu**



Alama za hesabu

Wanafunzi wengi hudhani kuwa somo la hesabu ni gumu. Ukweli ni kwamba somo hili sio gumu kama wanavyodhani. Kuna vitu kadhaa ambavyo ukivijua na kuvielewa basi hesabu huwa rahisi sana. La kwanza ni kujua alama za hesabu kama vile: alama ya kuongeza (+), alama ya kutoa (-), alama ya kugawanya (÷), alama ya kuzidisha (×) na alama ya kusawazisha (=). Alama hizi hukuelekeza kutatua matatizo mbalimbali yanayohusu hesabu. Somo la hesabu hukupa ujuzi wa kuweza kufanya kazi mbalimbali. Kwa hivyo tunasoma hesabu ili kufaulu katika mitihani yetu na pia kwa ajili ya manufaa ya maisha ya baadaye. Ukitaka kufaulu ni lazima upende na kufanya bidii kwenye somo hili la hesabu.

134

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **kuongeza** ubaoni. Tamka silabi **ku o nge za** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kuongeza**. **[U]** Endelea na maneno: **kutoa, kugawanya, kuzidisha, kuongeza, kusawazisha, kufaulu.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 133**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **alama ya kutoa, alama ya kugawanya,** na **alama ya kuzidisha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma taarifa ya **"Alama za hesabu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni somo lipi hudhaniwa kuwa gumu? (Ni somo la hesabu)*
2. *Orodhesha alama za hesabu zilizotajwa kwenye hadithi hii? (+ alama ya kuongeza, –, ÷, x, =)*
3. *Kwa nini tunasoma somo la hesabu? (ili tupite mtihani/ kufaulu mtihani kwa manufaa ya maisha ya baadaye)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**i. Mama ana ndizi mbili.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 27: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapojitayarisha kwa somo, ni muhimu kusoma na kutafakari kuhusu vidokezo vya mwalimu kwenye mwongozo.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 — **Alama za hesabu**

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ku o nge za | ku zi di sha |
| **kuongeza** | **kuzidisha** |
| ku to a | ku fa u lu |
| **kutoa** | **kufaulu** |
| ku ga wa nya | ku sa wa zi sha |
| **kugawanya** | **kusawazisha** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na vyo dhani | hu ku elekeza |
| **wanavyodhani** | **hukuelekeza** |
| ku vi elewa | ya na yo husisha |
| **kuvielewa** | **yanayohusisha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Alama **ya** hesabu | - | Alama **za** hesabu. |
| Alama **ya** kuongeza | - | Alama **za** kuongeza. |
| Alama **ya** kutoa | - | Alama **za** kutoa. |
| Alama **ya** kuzidisha | - | Alama **za** kuzidisha. |
| Alama **ya** kujumlisha | - | Alama **za** kujumlisha. |

133

Wiki ya 27: Siku ya 3 na 4 — **Alama za hesabu**



Alama za hesabu

Wanafunzi wengi hudhani kuwa somo la hesabu ni gumu. Ukweli ni kwamba somo hili sio gumu kama wanavyodhani. Kuna vitu kadhaa ambavyo ukivijua na kuvielewa basi hesabu huwa rahisi sana. La kwanza ni kujua alama za hesabu kama vile: alama ya kuongeza (+), alama ya kutoa (-), alama ya kugawanya (÷), alama ya kuzidisha (×) na alama ya kusawazisha (=). Alama hizi hukuelekeza kutatua matatizo mbalimbali yanayohusu hesabu. Somo la hesabu hukupa ujuzi wa kuweza kufanya kazi mbalimbali. Kwa hivyo tunasoma hesabu ili kufaulu katika mitihani yetu na pia kwa ajili ya manufaa ya maisha ya baadaye. Ukitaka kufaulu ni lazima upende na kufanya bidii kwenye somo hili la hesabu.

134

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **wanavyodhani** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa na vyo dhani** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanavyodhani**. **[U]** Endelea na maneno: **ku vi elewa (kuvielewa), hu ku elekeza (hukuelekeza), ya na yo husisha (yanayohusisha.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 133**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U**:** Soma katika umoja na wingi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Alama **ya** hesabu | - | Alama **za** hesabu. |
| Alama **ya** kuongeza | - | Alama **za** kuongeza. |
| Alama **ya** kutoa | - | Alama **za** kutoa. |
| Alama **ya** kuzidisha | - | Alama **za** kuzidisha. |
| Alama **ya** kujumlisha | - | Alama **za** kujumlisha. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 133**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **alama ya kutoa, alama ya kugawanya,** na **alama ya kuzidisha**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Alama za hesabu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Eleza umuhimu wa hesabu maishani? (wanafunzi waeleze majibu yao)*
2. *Somo unalolipenda zaidi ni lipi? Eleza jibu lako. (waeleze masomo haya kwa Kiswahili)*
3. *Ni masomo gani mengine unayoyasoma? (wanafunzi waeleze majina ya masomo mengine kwa Kiswahili)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni. Tumia maneno **alama ya hesabu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **alama ya hesabu**
2. **alama za kuongeza**
3. **alama ya kutoa**
4. **alama za kujumlisha**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 27: Siku ya 4*

Wiki ya 27: Siku ya 5 — Alama za hesabu

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ku ga wa nya - kugawanya**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| nya | za | ku | di | ga | to |
| nge | zi | a | sha | o | wa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** — **Wingi**

**M**kuki huu ni mdogo - **Mi**kuki hii ni midogo.
**M**ti huu ni mkubwa - **Mi**ti hii ni mikubwa.
**M**situ huu ni mzuri - **Mi**situ hii ni mizuri.
**M**nazi huu ni mrefu - **Mi**nazi hii ni mirefu.

Mafumbo



135

★ **Jedwali la silabi**

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ku ga wa nya** kuandika neno **kugawanya**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

● **Sarufi**

Andika sentesi hizi ubaoni. Soma katika umoja na wingi. Soma na wanafunzi wape nafasi wanafunzi wasome peke yao.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kuki huu ni mdogo | - | **Mi**kuki hii ni midogo. |
| **M**ti huu ni mkubwa | - | **Mi**ti hii ni mikubwa. |
| **M**situ huu ni mzuri | - | **Mi**situ hii ni mizuri. |
| **M**nazi huu ni mrefu | - | **Mi**nazi hii ni mirefu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 135**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **hitaji, mwanga, kivuli**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi **"Mafumbo"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

**Baada ya kusoma**

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Mtu wa kwanza ni nani? (maji)*
2. *Mtu wa pili ni nani? (jua)*
3. *Mtu wa kwanza hutoka wapi? (angani/mvua)*
4. *Jina la mtu wa nne ni nani? (simba)*

**Kuandika - Imla**

Soma maneno haya huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **alipaza, mapacha, msitu, mbuzi, mkuki, kuzidisha, kutoa, kujumlisha, kusawazisha.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 27: Siku ya 5*

## Mafumbo

Mimi ni muhimu. Kila mtu ananihitaji. Ninamaliza kiu. Ninatumika kwa usafi. Mimi ni nani?

Mimi ni mkubwa. Ninaishi angani. Natoa mwangaza duniani kote. Nikilala giza huingia. Mimi ni nani?

Mimi ni rafiki wa kila kiumbe. Ninasafisha hewa. Nazaa matunda. Nawapatia binadamu kivuli. Mimi ni nani?

Mimi huishi msituni. Nina miguu minne. Mimi hula nyama. Wengine huniita mfalme. Mimi ni nani?

### Majibu

| | |
|---|---|
| maji | jua |
| simba | angani/mvua |

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufunza kwa utaratibu wiki ya kwanza. Sio haraka sana au polepole sana.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ta ra ki mu | i shi ri ni | the la thi ni |
| **tarakimu** | **ishirini** | **thelathini** |
| i da di | ha m si ni | ti si ni |
| **idadi** | **hamsini** | **tisini** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na i penda | wana funzi |
| **wanaipenda** | **wanafunzi** |
| wa wili | wavu lana |
| **wawili** | **wavulana** |

Sarufi: Soma maneno haya na tarakimu.

| Majina | | Tarakimu |
|---|---|---|
| Mia moja na hamsini | - | 150 |
| Mia mbili | - | 200 |
| Mia mbili na hamsini | - | 250 |
| Mia tatu | - | 300 |
| Mia tatu na hamsini | - | 350 |
| Mia nne | - | 400 |
| Mia tano | - | 500 |







### Tarakimu

Shule ya msingi ya Pomoni ina wanafunzi wengi. Jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza ni mia mbili. Idadi ya wasichana wa darasa la kwanza ni mia moja na wawili. Idadi ya wavulana ni tisini na wanane. Jumla ya wanafunzi wa darasa la pili ni mia nne na ishirini. Wasichana wa darasa la pili ni mia tatu na wavulana ni mia moja ishirini. Jumla ya wanafunzi wa darasa la tatu ni mia tatu hamsini na saba. Idadi ya wasichana wa darasa la tatu ni mia mbili na ishirini na ya wavulana ni mia moja thelathini na saba. Jumla ya wanafunzi wa shule ya Pomoni ni mia tisa sabini na saba.



## Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **tarakimu** ubaoni. Tamka silabi **ta ra ki mu** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno upesi **tarakimu**. **[U]** Endelea na maneno: **idadi, ishirini, hamsini, thelathini, tisini.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 136**.

## Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **jumla** na **idadi**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Tarakimu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

## Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Je, shule ya Pomoni ina wanafunzi wangapi katika darasa la kwanza? (mia mbili)*
2. *Wasichana wa darasa la pili ni wangapi? (mia tatu)*
3. *Shule hii ina jumla ya wanafunzi wangapi? (mia tisa sabini na saba)*

## Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **mia mbili, mia tatu, tisini na wanne, mia mbili na ishirini.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 28: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Mwalimu mzuri ni yule anayechukua muda kujiyatarisha kabla ya somo. Ni vizuri kuliangalia somo kabla ya kulifunza. Kujitayarisha vyema kunafanya somo liwe zuri na la kupendeza.

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 — **Tarakimu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ta ra ki mu | i shi ri ni | the la thi ni |
| **tarakimu** | **ishirini** | **thelathini** |
| i da di | ha m si ni | ti si ni |
| **idadi** | **hamsini** | **tisini** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa na i penda | wana funzi |
| **wanaipenda** | **wanafunzi** |
| wa wili | wavu lana |
| **wawili** | **wavulana** |

Sarufi: Soma maneno haya na tarakimu.

| **Majina** | | **Tarakimu** |
|---|---|---|
| Mia moja na hamsini | - | 150 |
| Mia mbili | - | 200 |
| Mia mbili na hamsini | - | 250 |
| Mia tatu | - | 300 |
| Mia tatu na hamsini | - | 350 |
| Mia nne | - | 400 |
| Mia tano | - | 500 |

136

Wiki ya 28: Siku ya 1 na 2 — **Tarakimu**



### Tarakimu

Shule ya msingi ya Pomoni ina wanafunzi wengi. Jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza ni mia mbili. Idadi ya wasichana wa darasa la kwanza ni mia moja na wawili. Idadi ya wavulana ni tisini na wanane. Jumla ya wanafunzi wa darasa la pili ni mia nne na ishirini. Wasichana wa darasa la pili ni mia tatu na wavulana ni mia moja ishirini. Jumla ya wanafunzi wa darasa la tatu ni mia tatu hamsini na saba. Idadi ya wasichana wa darasa la tatu ni mia mbili na ishirini na ya wavulana ni mia moja thelathini na saba. Jumla ya wanafunzi wa shule ya Pomoni ni mia tisa sabini na saba.

137

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **wanaipenda** ubaoni. Tamka sehemu za neno **wa na i penda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **wanaipenda** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **wa na funzi – wanafunzi; wa wili – wawili; wavulana [T].**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 136**.

### ◆ Sarufi

**[N]** Andika tarakimu na majina yake ubaoni. Soma tarakimu hizi. Soma na wanafunzi **[U]** uwape nafasi wasome peke yao.

| **Majina** | | **Tarakimu** |
|---|---|---|
| Mia moja hamsini | - | 150 |
| Mia mbili | - | 200 |
| Mia mbili hamsini | - | 250 |
| Mia tatu | - | 300 |
| Mia tatu hamsini | - | 350 |
| Mia nne | - | 400 |
| Mia tano | - | 500 |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 136**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **jumla** na **idadi**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Tarakimu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Unafikiri wanafunzi wasichana wa darasa la kwanza ni wangapi? (mia moja n.k.)*
2. *Je, unafikiri shule hii ina walimu wengi au wachache? (wengi kwa sababu ina wanafunzi na madarasa mengi)*
3. *Je, unafikiri kwa nini watu wanaipenda shule hii? (Pengine ina madarasa mazuri, walimu wazuri, n.k.)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike tarakimu katika vitabu vyao.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mia moja | – | 100 | Mia tatu na hamsimi | – | 350 |
| Mia mbili | – | 200 | Mia moja na sabini | – | 170 |
| Mia moja na hamsini | – | 150 | | | |

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 28: Siku ya 2*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 28: Siku ya 3

**Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4** — Tarakimu

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ha ba ri | m mo ja | wa wi li |
| **habari** | **mmoja** | **wawili** |
| shu le ni | njo o ni | ra fi ki |
| **shuleni** | **njooni** | **rafiki** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ye potea | tu m rudishe |
| **aliyepotea** | **tumrudishe** |
| tu ki m pata | tu wa rudishe |
| **tukimpata** | **tuwarudishe** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|
| Mtoto mmoja | 1 | Watoto wawili | 2 |
| Paka mmoja | 1 | Paka watano | 5 |
| Rafiki mmoja | 1 | Marafiki wanne | 4 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu watatu | 3 |
| Samaki mmoja | 1 | Samaki saba | 7 |
| Ndovu mmoja | 1 | Ndovu kumi | 10 |
| Msichana mmoja | 1 | Wasichana sita | 6 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu kumi | 10 |

138

**Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4** — Tarakimu



**Wimbo wa kuhesabu**

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Kuna mtoto mmoja aliyepotea na tukimpata tumrudishe shule.
Rafiki yangu njoo, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto wawili waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto watatu waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

139

■ **Kusoma maneno kutumia silabi**

Andika neno **habari** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ha ba ri** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno kwa upesi **habari**. **[U]** Endelea na maneno: **shuleni, mmoja, njooni, wawili, rafiki.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 138**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno: **rafiki, kupotea na kurudisha.** Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma au imba **"Wimbo wa kuhesabu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni namba gani huja baada ya sita? (saba)*
2. *Wakimpata mtoto watamfanya nini? (watampeleka shule/watampeleka shuleni)*
3. *Mwimbaji anamwambiaje rafiki yake? (anamwambia, "rafiki yangu njoo tuende shule leo")*

**Kusoma:**

Andika sentensi hii ubaoni kuhusu picha kisha wanafunzi waandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Watoto wanacheza mpira.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 28: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati wanafunzi wanaposoma, tembea kwa darasa ndio uweze kujua wale hawajui kusoma. Utawasaidia hawa wanafunzi kusoma.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 28: Siku ya 4

**Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4** — **Tarakimu**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ha ba ri | m mo ja | wa wi li |
| **habari** | **mmoja** | **wawili** |
| shu le ni | njo o ni | ra fi ki |
| **shuleni** | **njooni** | **rafiki** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ye potea | tu m rudishe |
| **aliyepotea** | **tumrudishe** |
| tu ki m pata | tu wa rudishe |
| **tukimpata** | **tuwarudishe** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|
| Mtoto mmoja | 1 | Watoto wawili | 2 |
| Paka mmoja | 1 | Paka watano | 5 |
| Rafiki mmoja | 1 | Marafiki wanne | 4 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu watatu | 3 |
| Samaki mmoja | 1 | Samaki saba | 7 |
| Ndovu mmoja | 1 | Ndovu kumi | 10 |
| Msichana mmoja | 1 | Wasichana sita | 6 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu kumi | 10 |

138

**Wiki ya 28: Siku ya 3 na 4** — **Tarakimu**



**Wimbo wa kuhesabu**

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Kuna mtoto mmoja aliyepotea na tukimpata tumrudishe shule.
Rafiki yangu njoo, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto wawili waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto watatu waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

139

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **aliyepotea** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **a li ye potea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **aliyepotea** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **tu ki m pata (tukimpata), tu m rudishe (tumrudishe), tu wa rudishe (tuwarudishe.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 138**.

◆ **Sarufi**

Andika maneno na tarakimu hizi ubaoni. Soma peke yako. Soma na wanafunzi kisha wanafunzi wasome peke yao.

| Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|
| mtoto mmoja | 1 | watoto wawili | 2 |
| paka mmoja | 1 | paka watano | 5 |
| rafiki mmoja | 1 | marafiki wanne | 4 |
| mwalimu mmoja | 1 | walimu watatu | 3 |
| samaki mmoja | 1 | samaki saba | 7 |
| ndovu mmoja | 1 | ndovu kumi | 10 |
| msichana mmoja | 1 | wasichana sita | 6 |
| mwalimu mmoja | 1 | walimu kumi | 10 |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 138**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **rafiki, kupotea na kurudisha.**

**Kusoma hadithi**

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Wimbo wa kuhesabu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya wawili wawili**.**

**Maswali**

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Hesabu kutoka kumi hadi mia moja kwa makumi? (wape mfano, kisha watoto wahesabu 10, 20, 30, 40, 50, 60, 70, 80, 90, 100)*
2. *Umuhimu wa kwenda shule ni nini? (tunajifundisha mambo mengi/tunapata marafiki/tunajitayarisha kwa maisha ya baadaye)*
3. *Tuimbe wimbo mwingine wenye namba. (wanafunzi na mwalimu waimbe wimbo wa tarakimu)*

**Kuandika**

Andika maneno haya ubaoni. Tumia neno **ndugu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

1. **Halima ana ndugu wawili.**
2. **Mbwa watatu.**
3. **Samaki tisa.**
4. **Sungura tisa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 28: Siku ya 4*

Tarehe: ______________________ Muda: _______________ Idadi: _______________

Wiki ya 28: Siku ya 5 **Tarakimu**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ta no - tano**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | n | fu | ku | ba | e |
| ni | no | n | l | li | o |
| sa | ya | ne | tu | ti | mi |

Sarufi: Soma maneno na tarakimu.

●

| **Majina** | **Tarakimu** |
|---|---|
| Mia moja | 100 |
| Mia moja hamsini | 150 |
| Mia mbili | 200 |
| Mia mbili sabini | 270 |
| Mia tatu | 300 |

**Gazeti la baba**



140

## Gazeti la baba

Paliondokea kijana mmoja aliyeitwa Romeo. Siku moja baba yake alimtuma amletee gazeti la tarehe nane.

Romeo alichukua shilingi mia moja na kuelekea dukani. Alipofika kule alimuuliza mwenye duka, "Una gazeti la tarehe nane?" Mwenye duka alijibu, "Sina." Romeo aliuliza tena, "Je, unalo la tarehe nne?" Mwenye duka aliitikia. Romeo aliagiza magazeti mawili ya tarehe nne na kuelekea nyumbani.

Alipofika nyumbani, alimpatia babake yale magazeti mawili. Baba alipoona tarehe ni tofauti aliuliza, "Nani alikutuma magazeti mawili ya tarehe nne?" Romeo alisema, "Baba, nilikosa gazeti la tarehe nane. Lakini nikakumbuka kuwa nne mara mbili ni nane. Hivyo basi niliitisha magazeti mawili ya tarehe nne ili tupate tarehe nane."

Badala ya baba kukasirika, alicheka na kusema, "Mwanangu, haiwi hivyo kwenye gazeti. Ukiwa mkubwa, utaelewa kuwa kila siku ina gazeti lake."

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Soma silabi zote pamoja na wanafunzi. Tumia silabi **ta** na **no** kuandika neno **tano**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

**[N]** Andika maneno haya na tarakimu ubaoni. **[T]** Soma mstari wa kwanza. **[T]** Soma mstari wa pili pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape nafasi wanafunzi wasome mistari iliyobaki.

| **Majina** | | **Tarakimu** |
|---|---|---|
| Mia moja | - | 100 |
| Mia moja hamsini | - | 150 |
| Mia mbili | - | 200 |
| Mia mbili sabini | - | 270 |
| Mia tatu | - | 300 |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 140**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno **tarehe, kuelekea, aliagiza**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi **"Gazeti la baba"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Baada ya kusoma

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Baba alimtuma Romeo anunue nini (anunue gazeti la tarehe nane)*
2. *Romeo aliagiza apewe nini? (magazeti mawili ya tarehe nane)*
3. *Unafikiri Romeo alikuwa mtoto mwerevu? (Eleza jibu lako)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **ishirini, thelethini, hamsini, mia mbili, dukani, nyumbani, kumi na nne, mia tano, mia tatu, tisini.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 28: Siku ya 5*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Wiki ya 29: Siku ya 1

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 — **Rangi za bendera**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nye u pe | ki ja ni | nye ku ndu |
| **nyeupe** | **kijani** | **nyekundu** |
| nye u si | ki bi chi | dhi ha ka |
| **nyeusi** | **kibichi** | **dhihaka** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | | |
|---|---|---|
| i me ni lea | tu li yo pigania | wa me ni sinya |
| **imenilea** | **tuliyopigania** | **wamenisinya** |
| twa ji vunia | tu si pendane | i ki pepea |
| **twajivunia** | **tusipendane** | **ikipepea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| nchi **ya**ngu | - | nchi **ze**tu |
| bendera **ya**ngu | - | bendera **ze**tu |
| rangi **ya**ngu | - | rangi **ze**tu |
| taifa **la**ngu | - | mataifa **ye**tu |
| gari **la**ngu | - | magari **ye**tu |
| koti **la**ngu | - | makoti **ye**tu |

141

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 — **Rangi za bendera**



**Rangi za bendera yetu**

Nchi yangu imenilea, Taifa langu la Kenya,
Nchi yangu taitetea, wabaya wamenisinya,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Rangi nne za bendera, ni muhimu nakwambia,
Nyeusi ya mwanadamu, uhuru kapigania,
**Bendera ikipepea, wakenya** twajivunia.

Nyekundu ni ya damu, ilomwagika vitani,
Mashujaa kahitimu, mjini na vijijini,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Kijani rangi ya nchi, twaitetea hakika,
Tuipende hii nchi, sisi sote bila dhihaka,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia**

Rangi nyeupe ya amani, kwa nini tusipendane?
Kumpenda wako jirani, hakuna hata jingine,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

142

### Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **nyeupe** ubaoni. Tamka silabi **nye u pe** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **nyeupe**. **[U]** Endelea na maneno **nyeusi, kijani, kibichi, nyekundu, dhihaka.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 141**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **wamenisinya, twajivunia** na **dhihaka**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **"Rangi za bendera yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**.** **[U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Bendera ya Kenya ina rangi ngapi? Hebu zitaje rangi hizo. (nne: nyeusi, nyeupe, nyekundu na kijani kibichi)*
2. *Rangi nyekundu inasimamia nini? (ni damu ya mkenya)*
3. *Rangi nyeupe ni ya nini? (amani)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **nyeupe, nyeusi, kijani kibichi na nyekundu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 29: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka hatua tatu muhimu kwenye mtindo wa kufunza somo. Mtindo huu ni: Ninafanya, Tunafanya na Unafanya.

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 — **Rangi za bendera**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nye u pe | ki ja ni | nye ku ndu |
| **nyeupe** | **kijani** | **nyekundu** |
| nye u si | ki bi chi | dhi ha ka |
| **nyeusi** | **kibichi** | **dhihaka** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | | |
|---|---|---|
| i me ni lea | tu li yo pigania | wa me ni sinya |
| **imenilea** | **tuliyopigania** | **wamenisinya** |
| twa ji vunia | tu si pendane | i ki pepea |
| **twajivunia** | **tusipendane** | **ikipepea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| nchi **ya**ngu | - | nchi **ze**tu |
| bendera **ya**ngu | - | bendera **ze**tu |
| rangi **ya**ngu | - | rangi **ze**tu |
| taifa **la**ngu | - | mataifa **ye**tu |
| gari **la**ngu | - | magari **ye**tu |
| koti **la**ngu | - | makoti **ye**tu |

141

Wiki ya 29: Siku ya 1 na 2 — **Rangi za bendera**



Rangi za bendera yetu

Nchi yangu imenilea, Taifa langu la Kenya,
Nchi yangu taitetea, wabaya wamenisinya,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Rangi nne za bendera, ni muhimu nakwambia,
Nyeusi ya mwanadamu, uhuru kapigania,
**Bendera ikipepea, wakenya** twajivunia.

Nyekundu ni ya damu, ilomwagika vitani,
Mashujaa kahitimu, mjini na vijijini,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Kijani rangi ya nchi, twaitetea hakika,
Tuipende hii nchi, sisi sote bila dhihaka,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia**

Rangi nyeupe ya amani, kwa nini tusipendane?
Kumpenda wako jirani, hakuna hata jingine,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

142

★ **Kusoma maneno marefu**

Andika neno **imenilea** ubaoni. Tamka sehemu za neno **i me ni lea** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **imenilea**. N/T/U**:** Endelea na maneno: **wa me ni sinya (wamenisinya), twa ji vunia (twajivunia), tu si pendane (tusipendane), i ki pepea (ikipepea.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 141**.

◆ **Sarufi**

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U: Soma maneno haya.

| **Umoja -angu** | | **Wingi -etu** |
|---|---|---|
| nchi **ya**ngu | - | nchi **ze**tu |
| bendera **ya**ngu | - | bendera **ze**tu |
| rangi **ya**ngu | - | rangi **ze**tu |
| taifa **la**ngu | - | mataifa **ye**tu |
| gari **la**ngu | - | magari **ye**tu |
| koti **la**ngu | - | makoti **ye**tu |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 141**.

**Kabla ya kusoma:**

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **wamenisinya, twajivunia** na **dhihaka**.

**Kusoma shairi**

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **"Rangi za bendera yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili.

**Maswali**

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Rangi gani hukupendeza sana kati ya zile nne za bendera ya kenya?. (wanafunzi wataje rangi mbalimbali)*
2. *Je, unajua rangi ya bendera ya Tanzania au Uganda? Eleza darasa.*
   *(Tanzania ni: ________________________________)*
   *(Uganda ni: ________________________________)*
3. *Kwa nini unaipenda nchi ya Kenya? (Wanafunzi waeleze mambo yanayowafanya kuipenda Kenya.)*

**Kuandika**

Andika sentensi hizi ubaoni. Wanafunzi waziandike katika vitabu vyao:

1. **Nchi yangu naipenda - Nchi zetu tunazipenda.**
2. **Gari langu ni maridadi - Magari yetu ni maridadi.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 29: Siku ya 2*

# Wiki ya 29: Siku ya 3



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | ma ri da di | nye ku ndu |
| **bendera** | **maridadi** | **nyekundu** |
| wa za le ndo | hu s ta wi sha | A f ri ka |
| **wazalendo** | **hustawisha** | **Afrika** |



Bendera ya Kenya



Bendera ya Tanzania



Bendera ya Uganda

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| i na wakilisha | i li yo mwagika |
| **inawakilisha** | **iliyomwagika** |
| tu ki pigania | wa li o pigania |
| **tukipigania** | **waliopigania** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| -etu | | -enu |
|---|---|---|
| Uhuru **wetu** | - | Uhuru **wenu** |
| Uchumi **wetu** | - | Uchumi **wenu** |
| Ushujaa **wetu** | - | Ushujaa **wenu** |







### Bendera yetu

Kila taifa ulimwenguni lina bendera yake ya kipekee. Taifa letu la Kenya lina bendera iliyo na rangi nne. Kila rangi ina maana yake. Rangi nyeusi inawakilisha rangi ya watu wa Kenya. Wengi wa wakenya, kama watu wengine barani Afrika, ni watu weusi. Rangi nyekundu inawakilisha ushujaa wa wazalendo waliopigania uhuru wetu. Pia inawakilisha damu iliyomwagika wakati wa kupigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi inawakilisha ukulima kwenye nchi yetu. Mimea huwa na rangi ya kijani kibichi. Rangi ya mwisho ni nyeupe. Rangi hii inawakilisha amani ya nchi yetu. Kwa kweli bendera yetu ni maridadi sana.



## ■ Kusoma maneno kutumia silabi

N/T/U Andika neno **bendera** ubaoni. Tamka silabi **be nde ra** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **bendera**.
**[U]** Endelea na maneno: **maridadi, nyekundu, wazalendo, hustawisha, Afrika.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 143**.

## Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **maridadi, wazalendo** na **inawakilisha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

## Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi ya **"Bendera yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

## Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Ni kitu gani kilichotajwa kwenye hadithi ambacho hupatikana kila nchi ulimwenguni? (bendera)*
2. *Rangi ya kijani kibichi huwakilisha nini? (uchumi na nchi yetu)*
3. *Rangi nyeusi ni ya nini? (rangi ya watu/wanadamu/ watu waliopigania uhuru wetu)*

## Kuandika

Andika sentensi hii kuhusu picha ubaoni kisha wanafunzi wandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

**Wanafunzi wanaimba wimbo wa taifa.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 29: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Wakati unapouliza maswali ya ufahamu yenye majibu kwenye hadithi, hakikisha kuwa wanafunzi wanaangalia jawabu kwenye hadithi kabla ya kujibu swali.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 29: Siku ya 3 na 4 **Rangi za bendera**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | ma ri da di | nye ku ndu |
| **bendera** | **maridadi** | **nyekundu** |
| wa za le ndo | hu s ta wi sha | A f ri ka |
| **wazalendo** | **hustawisha** | **Afrika** |



Bendera ya Kenya



Bendera ya Tanzania



Bendera ya Uganda

Soma sehemu za neno na neno lote.


★ i na wakilisha — **inawakilisha**
i li yo mwagika — **iliyomwagika**
tu ki pigania — **tukipigania**
wa li o pigania — **waliopigania**

Sarufi: Soma maneno haya.

| -etu | | -enu |
|---|---|---|
| Uhuru **wetu** | - | Uhuru **wenu** |
| Uchumi **wetu** | - | Uchumi **wenu** |
| Ushujaa **wetu** | - | Ushujaa **wenu** |

143

Wiki ya 29: Siku ya 3 na 4 **Rangi za bendera**



**Bendera yetu**

Kila taifa ulimwenguni lina bendera yake ya kipekee. Taifa letu la Kenya lina bendera iliyo na rangi nne. Kila rangi ina maana yake. Rangi nyeusi inawakilisha rangi ya watu wa Kenya. Wengi wa wakenya, kama watu wengine barani Afrika, ni watu weusi. Rangi nyekundu inawakilisha ushujaa wa wazalendo waliopigania uhuru wetu. Pia inawakilisha damu iliyomwagika wakati wa kupigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi inawakilisha ukulima kwenye nchi yetu. Mimea huwa na rangi ya kijani kibichi. Rangi ya mwisho ni nyeupe. Rangi hii inawakilisha amani ya nchi yetu. Kwa kweli bendera yetu ni maridadi sana.

144

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **inawakilisha** ubaoni. Tamka sehemu za neno **I na wakilisha** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **inawakilisha** kwa upesi. **[U]** Endelea na maneno: **tu ki pigania (tukipigania), i li vyo mwagika (ilivyomwagika), wa li o pigania (waliopigania.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 143**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U: Soma maneno haya:

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| uhuru **we**tu | - | uhuru **we**nu |
| uchumi **we**tu | - | uchumi **we**nu |
| ushujaa **we**tu | - | ushujaa **we**nu |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa** *143.*

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya maneno **maridadi, wazalendo** na **inawakilisha**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **"Bendera yetu"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili. Wachague wanafunzi wachache wasimulie hadithi waliyoisoma.

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Watu hufanya nini wakati bendera inapopandishwa kwenye mlingoti? (husimana wima, huimba wimbo wa taifa)*
2. *Ni wimbo gani huimbwa wakati wa bendera kuteremshwa? (wimbo wa taifa)*
3. *Taja mashujaa unaowajua. (Mzee Jomo Kenyatta, Kung'u Karumba, Wangari Maathai, Mekatilili wa Menza, Ochieng' Oneko)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **uhuru wetu, uchumi wenu, ushujaa wetu**. Tumia maneno **uhuru wetu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 29: Siku ya 4*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Fuatilizia kwa kidole unaposoma sauti ili uunde silabi au wakati unasoma silabi zinazotengeneza neno. Baadaye pitisha kidole chini ya silabi au neno zima.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 29: Siku ya 5

## Rangi za bendera

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nye ku ndu - nyekundu**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| the | ki | ni | ndu | ma |
| ji | nye | ku | si | lu |
| kaa | u | ja | pe | mbi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● Nyekundu kama damu.
Nyeusi kama makaa.
Nyeupe kama theluji.
Kijani kama nyasi mbichi.

### Wimbo wa taifa

1 Ee Mungu nguvu yetu,
Ilete baraka kwetu,
Haki iwe ngao na mlinzi,
Natukae na undugu,
Amani na uhuru,
Raha tupate na ustawi.

2 Amkeni ndugu zetu,
Tufanye sote bidii,
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

3 Natujenge taifa letu,
Ee ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima,
Tuungane mikono,
Pamoja kazini,
Kila siku tuwe na shukrani.

145

**Vidokezo vya Mwalimu**
Hakikisha wanafunzi wameongea na wenzao kuhusu utabiri kabla ya kuuliza wachache waelezee kuhusu utabiri.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **nye ku ndu** kuandika: neno **nyekundu**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi wakitumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika sentesi hizi ubaoni. Soma sentensi hizi. Soma pamoja na wanafunzi. Wape nafasi wasome peke yao.

i. Nyekundu kama damu.
ii. Nyeusi kama makaa.
iii. Nyuepe kama theluji.
iv. Kijani kama nyasi mbichi.

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 145**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno **baraka, uhuru** na **istahili**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi **"Wimbo wa Taifa"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Baada ya kusoma

[N/T/U] Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Ubeti wa kwanza unaomba Mungu afanye nini? (Mungu alete baraka n.k.)*
2. *Katika wimbo wa taifa, watu wanahimizwa kufanya nini? (waamke na kufanya bidii, n.k.)*
3. *Tufanye mazoezi ya kuimba wimbo wa taifa pamoja. (waongoze wanafunzi kuimba wimbo wa taifa)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **nyeupe, nyekundu, kijani kibichi, nchi, bendera, koti, taifa, wazalendo, kilimo.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 29: Siku ya 5*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku fu a ta | m shi ndo | ma zi ngi ra |
| **kufuata** | **mshindo** | **mazingira** |
| so ko ni | ma ga nda | shi mo ni |
| **sokoni** | **maganda** | **shimoni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li m fuata | wa li po fika |
| **walimfuata** | **walipofika** |
| ya li yo m fanya | a ka wa ambia |
| **yaliyomfanya** | **akawaambia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ganda hili ni kubwa | - **Ma**ganda haya ni **ma**kubwa. |
| Ganda hili ni dogo | - **Ma**ganda haya ni **ma**dogo. |
| Ganda hili ni tamu | - **Ma**ganda haya ni **ma**tamu. |







**Mazingira**

Watoto wengi hupenda kufuata wazazi au walezi wao wanapoenda sokoni. Siku moja Diba na Habona walimfuata mama yao sokoni. Walipofika sokoni waliona watu wengi wakila ndizi na kutupa maganda njiani. Mara Diba na Habona wakasikia mshindo mkuu. Walipoangalia wakaona mama yao ameanguka chini. Wakamwambia, "Pole mama." Walipotazama zaidi wakaona ganda la ndizi lililokuwa limetupwa. Ni ganda hilo lililomfanya mama akateleza na kuanguka chini.
Hapo ndipo mama akawaambia wanawe kwamba ni muhimu watu watunze mazingira. Mbali na hatari ya kuanguka kwa sababu ya kutupa taka ovyo, mazingira pia huchafuka. Aliwaeleza kuwa takataka zote zinafaa kutupwa mahali panapofaa. Takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa la taka au kwenye shimo, bali si barabarani.



### Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **kufuata** ubaoni. N/T/U Tamka silabi **ku fua ta** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **kufwata**. **[U]** Endelea na maneno: **sokoni, mshindo, maganda, mazingira, shimoni.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 146**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya maneno **mshindo, maganda** na **akateleza**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi kuhusu **Mazingira** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Diba na Habona walienda wapi? (sokoni)*
2. *Eleza jambo lililofanyika walipofika sokoni. (wanafunzi waeleze hadithi kwa ufupi)*
3. *Hatari ya kutupa takataka ovyo ni ipi? (kuanguka, kuchafua mazingira, n.k.)*

### Kuandika - Imla

Soma maneno haya mara mbili huku wanafunzi wakiyaandika katika vitabu vyao: **sokoni, mshindo, maganda, mazingira, shimoni.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 30: Siku ya 1*

**Vidokezo vya Mwalimu**
Kumbuka kufanya utabiri na wanafunzi Siku ya kwanza, ya tatu na ya tano pekee. Hakuna utabiri: Siku ya 2 na ya 4. Wanafunzi watarejelea msamiati.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 30: Siku ya 2

**Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku fu a ta | m shi ndo | ma zi ngi ra |
| **kufuata** | **mshindo** | **mazingira** |
| so ko ni | ma ga nda | shi mo ni |
| **sokoni** | **maganda** | **shimoni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


| | |
|---|---|
| wa li m fuata | wa li po fika |
| **walimfuata** | **walipofika** |
| ya li yo m fanya | a ka wa ambia |
| **yaliyomfanya** | **akawaambia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ganda hili ni kubwa | - | **Ma**ganda haya ni **ma**kubwa. |
| Ganda hili ni dogo | - | **Ma**ganda haya ni **ma**dogo. |
| Ganda hili ni tamu | - | **Ma**ganda haya ni **ma**tamu. |

146

**Wiki ya 30: Siku ya 1 na 2** — **Marejeleo**



**Mazingira**

Watoto wengi hupenda kufuata wazazi au walezi wao wanapoenda sokoni. Siku moja Diba na Habona walimfuata mama yao sokoni. Walipofika sokoni waliona watu wengi wakila ndizi na kutupa maganda njiani. Mara Diba na Habona wakasikia mshindo mkuu. Walipoangalia wakaona mama yao ameanguka chini. Wakamwambia, "Pole mama." Walipotazama zaidi wakaona ganda la ndizi lililokuwa limetupwa. Ni ganda hilo lililomfanya mama akateleza na kuanguka chini.

Hapo ndipo mama akawaambia wanawe kwamba ni muhimu watu watunze mazingira. Mbali na hatari ya kuanguka kwa sababu ya kutupa taka ovyo, mazingira pia huchafuka. Aliwaeleza kuwa takataka zote zinafaa kutupwa mahali panapofaa. Takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa la taka au kwenye shimo, bali si barabarani.

147

### ★ Kusoma maneno marefu

Andika neno **walimfuata** ubaoni. N/T/U Tamka sehemu za neno **wa li m fuata** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno lote **walimfuata**. Endelea na maneno: **wa li po fika (walipofika), ya li yo m fanya (yaliyomfanya), a ka wa ambia (akawaambia.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 146**.

### ◆ Sarufi

Andika sentensi hizi ubaoni. N/T/U: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ganda hili ni kubwa | - | **Ma**ganda haya ni **ma**kubwa. |
| Ganda hili ni dogo | - | **Ma**ganda haya ni **ma**dogo. |
| Ganda hili ni tamu | - | **Ma**ganda haya ni **ma**tamu. |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 146**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **mshindo, maganda** na **akateleza**.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma shairi kuhusu **"Mazingira"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome katika vikundi vya watu wawili wawili**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Unafikiri ni vitu gani viliuzwa sokoni? (wanafunzi wataje bidhaa mbalimbali)*
2. *Ni vitu gani husababisha takataka hapa shule? (karatasi, mabaki ya chakula n.k.)*
3. *Wewe hutupa takataka hizo wapi? (wanafunzi waeleze wanapotupa takataka)*

### Kuandika

Wape wanafunzi muda waandike sentensi za sarufi za umoja na wingi katika vitabu vyao.

1. **Hili ni ganda kubwa sana - Haya ni maganda makubwa sana.**
2. **Hili ni ganda tamu - Haya ni maganda matamu.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 30: Siku ya 2*

Tarehe: ______________ Muda: ______________ Idadi: ______________

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| da wa | m za zi | u go njwa |
| **dawa** | **mzazi** | **ugonjwa** |
| si nda no | da k ta ri | u nge dha ni |
| **sindano** | **daktari** | **ungedhani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na tu shinda | zi na tu linda |
| **zinatushinda** | **zinatulinda** |
| u ta hatarisha | u si sherehekee |
| **utahatarisha** | **usisherehekee** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Maneno | | Kinyume |
|---|---|---|
| dawa **tamu** | - | dawa **chungu** |
| dawa **nyingi** | - | dawa **chache** |
| dawa **kubwa** | - | dawa **ndogo** |
| dawa **mbaya** | - | dawa **nzuri** |
| dawa **ghali** | - | dawa **rahisi** |

148

Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4 — **Marejeleo**



**Dawa**

Dawa za kila aina, naomba usichezee,
Ugonjwa wa kila namna, daktari muelezee,
Kuna chungu na tamu sana, mtoto sisherehekee,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa za maji twapenda, ni tamu kama asali,
Za tembe zinatushinda, ungedhani ni pilipili,
Sindano zinatulinda, kutoka kwa homa kali,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa usiweke ovyo, ni hatari kwa maisha,
Mtoto akila sivyo, uzima huenda kwisha,
Dawa ukiacha hivyo, maisha utahatarisha,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

149

## Kusoma maneno kutumia silabi

Andika neno **dawa** ubaoni. N/T/U: Tamka silabi **da wa** kisha uunganishe silabi hizo na useme neno **dawa**. **[U]** Endelea na maneno: **ugonjwa, Daktari, mzazi, sindano, ungedhani.**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 148**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wanafunzi waeleze maana ya vifungu hivi vya maneno **mtoto sisherehekee, ungedhani ni pilipili, dawa usiwache ovyo** na **uzima huenda kwisha**. Eleza wanafunzi maana ya maneno hayo. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Waulize wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi la **"Dawa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole. **[T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape wanafunzi nafasi wasome peke yao**.**

### Maswali

Waulize wanafunzi kama utabiri wao ulitimia. Wape nafasi wajibu maswali yafuatayo:

1. *Taja aina za dawa zilizotajwa kwenye shairi hili. (dawa za maji, dawa za tembe, dawa tamu, dawa chungu, dawa za sindano)*
2. *Shairi hili linatuelezea kwamba tunywe dawa vipi? (tunywe wakati mzazi yuko)*
3. *Ukinywa dawa ovyo, nini kitafanyika? (unaweza kufa n.k.)*

### Kuandika

Andika sentensi hii ubaoni kisha wanafunzi wandike sentensi zingine mbili kuhusu picha.

i. **Dawa ziko juu ya kabati.**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 30: Siku ya 3*

**Vidokezo vya Mwalimu**

Kumbuka kuwa kusoma hadithi kuna vipengele vitatu. Kusoma maneno vizuri, kwa mwendo mzuri na kuonyesha hisia na kuzingatia alama za uafikishaji.

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

# Wiki ya 30: Siku ya 4

**Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4** — **Marejeleo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| da wa | m za zi | u go njwa |
| **dawa** | **mzazi** | **ugonjwa** |
| si nda no | da k ta ri | u nge dha ni |
| **sindano** | **daktari** | **ungedhani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na tu shinda | zi na tu linda |
| **zinatushinda** | **zinatulinda** |
| u ta hatarisha | u si sherehekee |
| **utahatarisha** | **usisherehekee** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Maneno | | Kinyume |
|---|---|---|
| dawa **tamu** | - | dawa **chungu** |
| dawa **nyingi** | - | dawa **chache** |
| dawa **kubwa** | - | dawa **ndogo** |
| dawa **mbaya** | - | dawa **nzuri** |
| dawa **ghali** | - | dawa **rahisi** |

148

**Wiki ya 30: Siku ya 3 na 4** — **Marejeleo**



**Dawa**

Dawa za kila aina, naomba usichezee,
Ugonjwa wa kila namna, daktari muelezee,
Kuna chungu na tamu sana, mtoto sisherehekee,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa za maji twapenda, ni tamu kama asali,
Za tembe zinatushinda, ungedhani ni pilipili,
Sindano zinatulinda, kutoka kwa homa kali,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa usiweke ovyo, ni hatari kwa maisha,
Mtoto akila sivyo, uzima huenda kwisha,
Dawa ukiacha hivyo, maisha utahatarisha,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

149

### ★ Kusoma maneno marefu

N/T/U Andika neno **zinatushinda** ubaoni. Tamka sehemu za neno **zi na tu shinda** kisha uunganishe sehemu hizo na useme neno **zinatushinda**. **[U]** Endelea na maneno: **u ta hatarisha (utahatarisha), zi na tu linda (zinatulinda), si sherehekee (sisherehekee.)**

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 148**.

### ◆ Sarufi

Andika maneno ubaoni. N/T/U: Soma maneno haya.

| Maneno | | Kinyume |
|---|---|---|
| Dawa tamu | - | Dawa chungu |
| Dawa nyingi | - | Dawa chache |
| Dawa kubwa | - | Dawa ndogo |
| Dawa mbaya | - | Dawa nzuri |
| Dawa ghali | - | Dawa rahisi |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 148**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Wakumbushe wanafunzi maana ya vifungu hivi vya maneno **mtoto sisherehekee, ungedhani ni pilipili, dawa usiwache ovyo** na **uzima huenda kwisha**.

### Kusoma shairi

**[N]** Soma au kariri shairi kuhusu **"Dawa"** huku wanafunzi wakifuatilia kwa kidole**. [T]** Soma pamoja na wanafunzi**. [U]** Wape nafasi wanafunzi wasome kwa vikundi vya watu wawili**.**

### Maswali

Waulize maswali yafuatayo:

1. *Kati ya aina za dawa zilizotajwa kwenye shairi ni ipi unapenda sana? (wanafunzi wataje huku wakitoa sababu)*
2. *Taja jina moja la dawa ambayo umewahi kuitumia? (wanafunzi wataje dawa mbalimbali)*
3. *Umewahi kudungwa sindano? (Eleza ulichohisi)*

*Mwalimu: (Wape nafasi wanafunzi wakariri au kuimba shairi hili kwa pamoja.)*

### Kuandika

Andika maneno haya ubaoni: **dawa tamu, dawa chache, dawa ndogo, dawa nzuri**. Tumia maneno **dawa tamu** kuunda sentensi. Eleza wanafunzi watumie maneno haya kuunda sentensi: dawa chache, dawa ndogo, dawa nzuri.

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 30: Siku ya 4*

Tarehe: ____________ Muda: ____________ Idadi: ____________

Wiki ya 30: Siku ya 5 **Marejeleo**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma zi ngi ra - mazingira**

★


| | | | |
|---|---|---|---|
| ra | ma | wa | da |
| zi | si | za | nda |
| no | m | ngi | ga |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Neno | | Kinyume | Neno | | Kinyume |
|---|---|---|---|---|---|
| ghali | — | rahisi | simama | — | keti |
| panda | — | shuka | lia | — | cheka |
| jenga | — | bomoa | juu | — | chini |

Majumba ya Nairobi



150

## Majumba ya Nairobi

Siku moja Katini na wenzake wa kikundi cha kwaya walienda kuimba jijini Nairobi. Kabla ya kuimba, waliona ni heri watembelee jumba la mikutano la Kenyatta.

Mwalimu akawapeleka mahali kwenye lifti. Watu wakatoka na bikizee akaingia. Muda si muda akatokea msichana mrembo sana. Katini akamuuliza mwalimu, "Kwani Nairobi wanabadilisha wazee kuwa vijana?" Mwalimu akamuelezea kuwa walikuwa watu wawili tofauti.

Katini, mwalimu na wanafunzi wenzake wakaingia kwenye lifti hadi ghorofa ya ishirini na nane. Mlango ukafunguka na wote wakatoka. Waliona majumba mengi ya kila aina. Waliona ghorofa ndefu zenye ofisi nyingi. Upande wa pili waliona eneo la makazi likiwa na nyumba zisizokuwa za ghorofa.

Alipotazama upande mwingine akaona nyumba za mabati kwenye mtaa wa mabanda. Baadaye walienda kwenye ukumbi kuimba na kuwatumbuiza watu.

### ★ Jedwali la silabi

**[N]** Chora jedwali la silabi. Tumia silabi **ma, zi, ngi** na **ra** kuandika: neno **mazingira**. **[T]** Soma neno pamoja na wanafunzi. **[U]** Wape wanafunzi nafasi ya kuunda maneno halisi kutumia jedwali la silabi.

### ● Sarufi

Andika maneno haya ubaoni. N/T/U. Soma maneno hayo.

| Neno | | Kinyume |
|---|---|---|
| ghali | - | rahisi |
| panda | - | shuka |
| jenga | - | bomoa |
| simama | - | keti |
| lia | - | cheka |
| juu | - | chini |

**Eleza wanafunzi wasome kwenye vitabu vyao ukurasa wa 150**.

### Kabla ya kusoma:

**[N]** Eleza wanafunzi maana ya maneno: **lifti, ukumbi** na **kutumbuiza**. Soma kichwa cha hadithi. Waonyeshe wanafunzi picha. **[U]** Eleza wanafunzi wazungumze kuhusu picha kisha watoe utabiri wao.

### Kusoma hadithi

**[N]** Soma hadithi **"Majumba ya Nairobi"** kwa wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini.

### Maswali

Uliza kama utabiri wa wanafunzi umetimia. Waulize maswali yafuatayo:

1. *Katini na wenzake walienda Nairobi kufanya nini? (walienda Nairobi kuimba)*
2. *Taja aina ya majumba waliyoyaona walipokuwa juu ya jumba la Kenyatta? (ghorofa, ofisi, n.k.)*
3. *Je, unafikiri ni kwa nini Katini anafikiria Nairobi wanabadilisha wazee kuwa vijana? (kwa sababu ya wale aliowaona wakiingia na kutoka kwenye lifti)*
4. *Eleza jambo lililokufurahisha kutoka kwa hadithi hii. (wanafunzi waeleze walichokifurahia)*

### Kuandika - Imla

Wasomee wanafunzi maneno haya mara mbili huku wakiyaandika katika vitabu vyao: **sokoni, mshindo, maganda, mazingira, shimoni, ugonjwa, daktari, mzazi, sindano, ungedhani**

Hakikisha wanafunzi wanaandika kwa hati nadhifu wanapofanya mazoezi ya kuandika.

**Kitabu cha Kazi ya Ziada** - *Wiki ya 30: Siku ya 5*

Tarehe: ____________________ Muda: ______________ Idadi: ______________

# Kiswahili 2

## Mwongozo wa Mwalimu

Kitabu hiki cha Kiswahili kimetayarishwa na kuchapishwa chini ya mradi wa TUSOME. Kimeandikwa kufuatia mwongozo wa mawanda na mfuatano uliofanyiwa utafiti wa hali ya juu kwa miaka mitatu katika mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini. Utafiti huu uliegemea kubuni njia mwafaka za kufunza usomaji na ufahamu.

Vipengele muhimu na vya kipekee kuhusu hiki kitabu ni:

- Kitabu hiki kinafuata mtaala wa taifa la Kenya.
- Mazoezi ya somo yamefuata mpangilio wa mantiki kutokana na utafiti wa njia bora za kufunza Kiswahili katika darasa la kwanza na la pili.
- Kitabu hiki kina michoro ya kupendeza ambayo hufanya somo la Kiswahili liwe la kuvutia.
- Masomo katika kitabu hiki hujumuisha vijenzi vyote vya lugha ambavyo ni; kusikiza, kuongea, kusoma na kuandika.
- Mpangilio wa kitabu hiki umekusudia kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa uzoefu kwa sababu kinawapatia nafasi ya kukumbana na vijenzi vyote vya kusoma.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

**Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.**

**Januari 2016**